**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Thelathini na Nne – Tarehe 22 Mei, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile leo ni mara yangu ya kwanza kukaa kwenye Bunge hili la Kumi na Mbili basi natumia fursa hii kuwashukuru tena na kuwaomba ushirikiano wetu nikiamini kwamba Mwenyezi Mungu atakuwa pamoja nasi. Ahsanteni sana.

Katibu tuendelee.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**MWENYEKITI:** Hati za kuwasilisha Mezani Waziri wa Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Taasisi zake kwa mwaka fedha wa 2021/ 2022.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Waziri wa Viwanda na Biashara.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Bisahara mwaka 2021/2022.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira. Karibu Mwenyekiti, kwa niaba.

**MHE. MARTHA N. GWAU - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu na Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile leo kama ilivyo kwenye *Order Paper* zetu hatuna maswali, kwa hiyo, Katibu naomba tuendelee.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA VIWANDA NA BISHARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, namkaribisha Waziri wa Wiwanda na Biashara ili aweze kuja kuleta Hotuba yake ya Bajeti, karibu sana.

**WAZIRI WA WIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambayo ilichambua bajeti ya Viwanda na Biashara Fungu Namba 44 na Fungu Namba 60 naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kujadili na kupitisha makadirio ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili kumbukumbu sahihi za Bunge lako Tukufu ninaomba hotuba yangu yote ya bajeti itumike kama Kumbukumbu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeaswa kila tunapopata fursa hatuna budi kumshukuru Mungu na kuwashukuru watu ambao wameleta tofauti katika maisha yetu. Ninamshukuru Mungu kwa wingi wa rehema, baraka na fadhili zake kwangu ambazo zimeniwezesha kuwa hapa nilipo leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima kubwa, ninamshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Ninamuahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania kwa ujumla kuwa mimi na viongozi wenzangu na watumishi wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara tutafanya kazi kwa bidii, maarifa, uaminifu na utiifu katika kuhakikisha kuwa sekta ya viwanda na biashara inachangia kikamilifu katika kufikia malengo ya kitaifa kama yalivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa utulivu na hekima za uongozi ambazo Mwenyezi Mungu amemjalia hata akaweza kutuongoza vizuri na nchi ikapita salama katika kipindi kigumu cha mpito kufuatia msiba mkubwa uliolikumba Taifa letu kutoka na kifo cha Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Nami naungana na Bunge lako Tukufu na Watanzania wote kumpa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan pole kwa msiba huo

na namuombea nakumtakia baraka za Mwenyezi Mungu katika kuongoza Awamu ya Sita ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu kwa Imani kubwa ambayo Mheshimiwa Rais ameonesha kwao na kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuongoza nchi yetu. Ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri walionitangulia kwa kuwasilisha bajeti zao na kupata ridhaa ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha nawapongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge hili Tukufu na kwa uongozi wao mahiri wa chombo hiki kwa Taifa letu na kwa malezi mema kwa Wabunge wote. Nina wapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao na ushauri ambao wamekuwa wakitoa kwa Serikali tangu Bunge hili na mtandao huu uanze. Kwa kipekee ninawashukuru sana kwa kukubali jana kuhudhuria kikao hiki leo namie kupata nafasi ya kuwasilisha bajeti yangu siku hii ya Jumamosi. Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana pia na Bunge lako Tukufu kutoa pole kwa watanzania kufuatia kifo cha viongozi wetu wengine wa kitaifa, Hayati Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Hayati Balozi Mhandisi John William Kijazi aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Aidha, natoa pole kwa Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote, familia, ndugu na jamaa kwa kuondokewa na Wabunge wenzetu Mheshimiwa Martha J. Umbulla aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara; Mheshimiwa Mhandisi Ataashasta Nditiye aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambwe na hivi karibuni Mheshimiwa Khatib Said Haji aliyekuwa Mbunge Jimbo la Konde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nifanye mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya

Viwanda na Biashara kwa mwaka 2020/2021. Katika mwaka 2020/2021 Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Fungu Namba 44 na Fungu Namba 60 iliidhinishiwa matumizi ya jumla ya shilingi 81,366,902,000; kati ya fedha hizo shilingi 29,687,886,000 ni matumizi ya maendeleo na shilingi 51,679,016,000 ni matumizi ya kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2021 Wizara ilikuwa imepokea na kutumia jumla ya shilingi 45,512,707,118.7, sawa asilimia 55.9 ya Bajeti iliyoidhinishwa. Kwa kutumia bajeti hii Wizara imeweza kutekeleza programu, miradi na kazi mbalimbali zilizopangwa kama ilivyoanishwa katika kitabu changu cha bajeti kuanzia ukurasa wa 11 – 59. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nifanye rejea baadhi ya programu, miradi na kazi zilizotekelezwa katika mwaka 2020/2021. Ili kuendeana na mazingira ya sasa na yajayo; Wizara ilianza mchakato wa kuzipitia sera na kutunga sera mpya katika kuongoza sekta ya viwanda na biashara nchini. Sera hizi ni pamoja na Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda, Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biarashara Ndogo, Sera ya Taifa ya Biashara ya mwaka 2003 na Sera ya Taifa ya Ubora ambayo ni sera mpya inayopendekezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliendelea na utekelezaji wa miradi ya kielelezo na ya kimkakati kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Moja ya miradi hii ni uendelezaji wa kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools,* kiwanda hiki kinazaalisha vipuri vya aina mbalimbali kwa ajili ya viwanda hususan katika sekta ya kilimo, madini, nishati na usafirishaji. Wizara kupitia Shirika la Maendeleo ya Tafia - *NDC* imeanza uboreshaji na upanuzi wa kiwanda cha *KMTC* ambapo Serikali imetoa kiasi cha shilingi milioni 760 kwa ajili ya ukarabati wa mitambo katika kiwanda hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, *NDC* imeingia mkataba wa awali na *TANESCO* kwa nia ya kuzalisha minara ya kusambaza umeme kwa ajili ya umeme utakaozalishwa katika Bwawa la Mwalimu Nyerere. Hatua hii itasaidia Serikali

kuokoa zaidi ya shilingi bilioni 71 ambazo zimekuwa zikitumika kuagiza minara kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliendelea na utekelezaji wa mkakati wa kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji wa sekta binafsi katika maeneo maalum ya kiuchumi kupitia Mamlaka ya *EPZA*. Hadi kufikia mwezi Machi, 2021 miradi 176 yenye thamani ya dola za Kimarekani bilioni 2.5 imesajiliwa. Na jumla ya watu 58,198 wameajiriwa katika viwanda vilivyowekezwa katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliendelea kuimarisha sekta ya viwanda vidogo inayosimamiwa na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo - *SIDO*. Moja ya mkakati uliotekelezwa kupitia shirika hili ni kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa wajasiriamali wadogo kupitia Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali Wadogo yaani *National Entrepreneurship Development Fund* ulioanzishwa mwaka 1994. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 Mfuko huu ulikuwa na mtaji wa jumla ya shilingi bilioni 9.6 na umeshatoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 82.6. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 Mfuko ulitoa jumla ya mikopo 1,498 yenye thamani shilingi bilioni 3.1. Moja ya mafanikio makubwa ya mfuko huu ni kiwango kizuri cha mikopo inayorejeshwa na wajasiriamali ambacho sasa kimefikia asilimia 91. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania hufanya biashara nchi mbalimbali duniani. Nchi hizi zimegawanyika katika makundi makubwa matano ambayo ni Asia, hususan nchi za China, India na Japan, Jumuiya ya Ulaya, Marekani, Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika SADC na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa ujumla wake, biashara kati ya Tanzania na nchi hizi imeendele kuimarika. Hata hivyo, bado Tanzania inauza zaidi bidhaa za mazao ambayo hayajachakatwa na kusindikwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini ikiwemo

kuratibu utekelezaji wa mpango wa kuboresha mazingira ya biashara ya uwekezaji nchini maarufu kama *Blue Print for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment.* Pamoja na hatua zingine ada na tozo 232 ambazo zilikuwa kero na kikwazo kwa biashara zilifutwa. Aidha, Serikali inaendelea kurekebisha sheria mbalimbali kwa lengo la kuboresha mazingira ya kisera na kisheria kama ilivyopendekezwa katika mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha ushindani wa haki wa kibiashara nchini, Serikali kupitia Tume ya Ushindani - *FCC* imeendelea kushughulikia mashauri mbalimbali ya kibiashara. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 Tume ya Ushindani imeshughulikia mashauri 17 yanayohusu makubaliano yanayofifisha ushindani, miunganiko ya kampuni yaliyofanyika bila idhini ya *FCC*, makubaliano ya siri na matumizi mabaya ya nguvu ya soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kuwasilisha mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo Kuu la Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 ni kuleta mapinduzi ya uchumi Kwa maendeleo ya watu. Moja ya nyenzo ya kuleta mapinduzi ya uchumi iliyoanishwa katika Ilani hii ni kujenga Tanzania ya uchumi wa viwanda na kukuza biashahra. Aidha, sekta ya viwanda na biashara imebainishwa katika mpango huu, kuwa na mchango wa kipekee katika kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano yaani mwaka 2021/2022 – 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wake katika uchumi wa Taifa mchango wa sekta ya viwanda na biashara katika upande wa Taifa bado hauridhishi sana. Kwa mfano; kwa mujibu wa taarifa ya uchumi wa Wizara ya Fedha na Mipango ya mwaka 2020, mchango wa sekta ya viwanda katika pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.5 pekee. Aidha,

kiwango cha kusindika mazao ya kilimo bado ni kidogo na hivyo kusababisha mazao mengi kuuzwa kama mali ghafi bila kuongezwa thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hali hii na kwa kuzingatia malengo mapana ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 lengo kuu litakalo ongoza mpango wa bajeti wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2021 na Taasisi zake ni kuongeza mchango wa sekta ya viwanda na biashara katika pato la Taifa na katika kuzalisha ajira nchini kwa kuchochea tija katika uzalishaji wa ndani na sekta zinazozalisha, zinazorudisha viwanda kama vile kilimo, mifugo, misitu na madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi mama wa ujenzi wa sekta ya viwanda umezingatia kuwa maisha ya binadamu hapa duniani, yametawaliwa na shughuli kubwa mbili; yaani kula na kutumia. Hivyo basi, msisitizo wa kipekee utawekwa katika kujenga na kuendeleza viwanda vya uzalishaji. Vinavyolenga kutosheleza mahitaji ya bidhaa ya soko la ndani kuwania kuhakikisha kuwa tunaanza kula na kutumia tunavyozalisha na kuzalisha tunavyokula na kutumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia malengo la kiuchumi yaliyoanishwa katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, pamoja maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 hususan aya za 13, 14 na 18; uchaguzi wa programu, miradi na kazi ya sekta ya viwanda na biashara katika mwaka ujao wa fedha umezingatia vipaumbele 10 vifuatavyo:-

Kipaumbele cha kwanza ni kuendeleza na kulinda viwanda vya kuchakata na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha pili, ni kuendeleza na kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya ngozi, nguo na mavazi. *(Makofi)*

Kipaumbele cha tatu, ni kuhamasisha, kuendeleza na kulinda viwanda vya kuzalisha chuma na bidhaa za chuma. *(Makofi)*

Kipaumbele cha nne, ni kuweka msukumu na mazingira mazuri kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vya kuunganisha vifaa vya ki-elektroniki na magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha tano, ni kuhamasisha viwanda vinavyozalisha vifaa vya ujenzi. *(Makofi)*

Kipaumbele cha sita, ni kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kutengeneza betri na umeme wa magari kwa kutumia rasilimali asili za nchi kama vile madini ya Rithium, Vanadium na Titanium. *(Makofi)*

Kipengele cha saba, nikuweka mazingira wezeshi, kisera na kisheria ya kufanya biashara. *(Makofi)*

Kipaumbele cha nane, ni kujiunga au kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya za Kiuchumi na Kimasoko za Kikanda kwa ajili ya kupanua fursa za kibiashara kwa bidhaa za Tanzania. *(Makofi)*

Kipaumbele cha tisa, ni kuimarisha upatikanaji wa mitaji kwa wajasiliamali na wafanyabiashara wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kipaumbele cha kumi, ni kuweka mazingira bora, kisera, kisheria na kiutendaji kwa ajili ya kuchochea na kulinda ukuaji wa sekta binasfi kama *engine* na msingi wa ujenzi wa uchumi kwa viwanda na ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia vipaumbele hivi kumi na kwa kuzingatia maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassani aliyoyatoa kupitia hotuba yake kwa Taifa aliyotoa hapa Bungeni tarehe 22 Aprili, 2021; Wizara imepanga

kutekeleza programu, miradi na kazi 15 zifuatazo katika mwaka ujao wa fedha.

Kazi ya kwanza, ni kukamilisha mapitio ya sera na sheria zinazoongoza sekta ya viwanda na biashara; kazi ya pili, ni kujenga mitaa ya viwanda vya kitaifa yaani *National Industrial Parks* na kuhamasisha ushiriki wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika kujenga mitaa ya viwanda katika maeneo yao kwa kushirikiana na shirika la Viwanda Vidogo - *SIDO;* hii ni pamoja na kuanza ujenzi wa Mtaa wa Viwanda wa Kurasini, wenye kujumuisha Kongano ya viwanda vya kuchakata na kusindika mazao, viwanda vya kuunganisha vifaa vya elektroniki na ukanda maalum wa kibiashara ya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya tatu ni kusimamia utekelezaji wa miradi ya kielelezo na kimkakati ikiwemo miradi ya mikaa ya mawe wa Mchuchuma na chuma cha Liganga. Mradi wa Magadi Soda katika Bonde la Engaruka, mradi wa *Kilimanjaro Machine Tools*, Mradi wa Viwanda katika Ukanda Maalum wa Kiuchumi wa Bagamoyo na Mradi wa Ujenzi wa Mtaa na Viwanda - *TAMCO* kule Kibaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya nne, ni kufanya tathmini ya kina kuhusu mafanikio na changamoto za utekelezaji wa miradi ya maeneo ya ukanda maalum wa kiuchumi ili kuyaweka maeneo haya katika mukhtadha wa Tanzania ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya tano ni kuendelea kuratibu utekelezaji wa mpango wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini; kazi ya sita, kukamilisha taratibu za kuwapata wawekezaji wapya wa viwanda vilivyobinafsishwa na baadaye kurudishwa Serikalini; kazi ya saba ni kukamilisha kanzidata ya viwanda na biashara nchini na kazi ya nane kuimarisha mfumo wa usajili wa makampuni na leseni za biashara kupitia wakala wa usajili na leseni za biashara nchini *(BRELLA)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya tisa, kuimarisha Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali wadogo kwa kupanua wigo wa mtaji wa mfuko huu; kazi ya kumi, kuratibu na kusimamia uanzishwaji wa maeneo maalum ya kibiashara *(trading hubs)* kwa lengo la kuchochea masoko kwa bidhaa za ndani na biashara ya Kimataifa nchini na kazi ya kumi na moja, kuimarisha na kukuza matumizi ya utafiti na maendeleo, teknolojia na ubunifu katika sekta ya viwanda na biashara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kumi na mbili, kuendelea kusimamia viwango vya ubora na kubuni viwango vipya kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa na kuingizwa Tanzania kupitia Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* na Wakala wa Vipimo nchini; kazi ya kumi na tatu ni kukamilisha majadiliano na hatimaye kuridhia mkataba wa eneo huru la biashara Afrika *(Africa Continental Free Trade Area- AfCFTA). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kumi na nne, kukuza na kuimarisha majadiliano na wamiliki wa viwanda na wafanyabiashara kama msingi muhimu wa kujengana imani kati yao na Serikali na hatua muhimu ya kutambua na kutatua changamoto zinazowakabili katika shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kumi na tano, kuendelea kutafuta masoko ya bidhaa kwa kutekeleza mkakati wa kukuza masoko ya nje *(National Export Strategy). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuongeza uzalishaji wa sukari kwa kupanua na kuongeza uwezo wa viwanda vikubwa vilivyopo ikiwemo Kiwanda cha Sukari cha Kilombero pamoja na kuanzisha viwanda vikubwa vipya. Sambamba na hatua hizi, katika jitihada za kuongeza uzalishaji wa sukari nchini ili kukidhi mahitaji ya bidhaa hii, Serikali imeiagiza Taasisi ya *TEMDO* kufanya usanifu na kuanza kutengeneza mitambo midogo kwa lengo la kuwezesha wajasiriamali wadogo waanze kuchakata miwa ili kupata sukari. Hatua hii itaweza

kuongeza uzalishaji wa sukari na kuhakikisha kuwa wakulima wadogo *(out growers)* wanaweza kuchakata miwa yao wenyewe bila kuwa tegemezi kwa viwanda vikubwa vilivyopo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kwamba jitihada zote hizi ambazo nimezieleza katika kueneza sekta ya viwanda na biashara nchini zitazaa matunda tarajiwa ikiwa pamoja na mambo mengine kutakuwa na ushindani wa haki wa kibiashara na wazalishaji halisi na kwamba walaji wanalindwa dhidi ya bidhaa bandia na mienendo hadaifu sokoni. Kwa hivyo, Serikali kupitia Tume ya Ushindani itaendelea kudhibiti bidhaa bandia, kuimarisha ushindani wa haki wa kibiashara na kumlinda mlaji kwa kudhibiti mienendo inayofifisha ushindani na kuhadaa walaji ili kuwa na ukuaji jumuishi na endelevu wa kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kutekeleza kikamilifu vipaumbele ambavyo nimevieleza pamoja na programu, miradi na kazi hizo hapo juu ambazo nimezieleza katika hotuba yangu, ninaomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara ya jumla ya shilingi 105,670,459; kati ya fedha hizi shilingi 52,582,573 ni matumizi ya kawaida na shilingi 53,087,886 ni matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani; napenda kuwashukuru sana viongozi wenzangu na watumishi wenzangu wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa ushirikiano walionipa katika kutimiza majukumu yetu. Kipekee ninamshukuru sana Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara kwa usaidizi mwema na uhodari wakujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge hapa Bungeni. Ninawapongeza sana wananchi wa Jimbo la Mufindi Kaskazini kwa kupata Mbunge hodari, mchapakazi na kiongozi makini. *(Makofi)*

Ninamshukuru Ndugu Dotto Mgosha James, Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Hashim Twalib Abdallah na Menejimenti yote ya

Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Wakuu wa Taasisi zake kwa weledi na bidii yao katika kutekeleza majukumu ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana viongozi wa sekta binafsi wanaoendesha sekta ya viwanda na biashara nchini kwa upendo na ushirikiano wao mkubwa ambao wananipa tangu niteuliwe katika nafasi hii ya Waziri wa Viwanda na Biashara. Naomba niwataje angalau wachache kuwakilisha wenzao wengi; Bi. Angelina Ngalula Mwenyekiti wa *TPSF,* pamoja na Mtendaji wake Mkuu Ndugu Francis Nanai, Ndugu Paul Makanza, Rais wa Shirikisho la wenye Viwanda Tanzania, pamoja na Mtendaji wake Mkuu Ndugu Leodgar Tenga ambaye pia amewahi kuwa kiongozi mahiri wa michezo hapa nchini. Ndugu Paul Koi, Rais wa Chama cha Wafanyabiasara, Viwanda na Kilimo Tanzania. Kupitia kwao ninawashukuru wenye viwanda na wafanyabisahara wote nchini kwa heshima kubwa wanayoipa nchi yetu kupitia ajira wanazotengeneza na mchango wao mkubwa katika kujenga uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza kwa dhati kabisa Wenyeviti wa Bunge waliochaguliwa hivi karibuni nikianza na wewe mwenyewe Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mjini Magharibi. *(Makofi)*

Nampongeza pia Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini. *(Makofi)*

Aidha, nampongeza sana Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile na Mheshimiwa Erick James Shigongo na Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara na Mazingira kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuendesha sekta ya viwanda na biashara nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Ubungo kwa heshima na ridhaa

waliyonipa ya kuwawakilisha hapa Bungeni na kwa ushirikiano walionipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, nawashukuru sana viongozi wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Ubungo na Mkoa wa Dar es Salaam kwa malezi na ushirikiano tulionao katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Ninawashukuru pia Madiwani wenzangu wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ambao leo kwa heshima kubwa wamekuja hapa kuniunga mkono katika hotuba yangu hii ya bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa kipekee, ninamshukuru sana mke wangu Prosista Laswai kwa urafiki mwema, mapenzi ya dhati ya malezi bora kwa watoto wetu watatu Tandu, Calvin na Nsungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; Has Jo Chan Profesa maarufu wa uchumi wa Korea ya Kusini na ambaye amekuwa mshauri wa uchumi wa Benki ya Dunia kwa miaka mingi amewahi kusema na nakuu; *"History has repeatedly shown that the single most important thing that distinguishes rich countries from poor countries is basically their higher capabilities in manufacturing."*

Aidha, Hayati Ali Mufuruki na wenzake katika kitabu chao cha *Tanzania's Industrialization Journey 2015/2056* wameeleza kuwa; jina lingine la nchi iliyoendelea ni nchi yenye viwanda. Hii inamaanisha kuwa ili nchi yetu iweze kuwa nchi iliyoendelea, lazima iwe ni nchi yenye viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhima tuliyoweka kama Taifa kupitia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 hadi 2025/2026 na kwa uimara wa Chama cha Mapinduzi katika kuongoza nchi hii na kwa unyenyekevu, ushupavu, uzalendo na weledi na uchapakazi wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na kwa mapenzi mema ambayo Mungu anayo juu ya Taifa hili la Tanzania na kwa umahiri mkubwa wa Bunge lako hili chini ya uongozi shupavu sana wa Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Spika na Mbunge

wa Kongwa na Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, Naibu Spika na Mbunge wa Mbeya Mjini, tuna imani kubwa kuwa tutaenda kuleta mapinduzi ya kiuchumi kupitia sekta imara ya viwanda na *Inshaallah* nchi yetu itakuwa nchi iliyoendelea katika uhai wetu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawasalimu katika jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kazi iendelee. Hotuna yangu yote hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Viwanda na Biashara yenye anwani ifuatayo www.mit.go.tz katika lugha zote mbili yaani kiswahili na kiingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## HOTUBA YA BAJETI YA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 - KAMA ILIVYOWSILISHWA MEZANI

### *1.* UTANGULIZI

***1. Mheshimiwa Spika;*** Kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara Fungu 44 (Viwanda) na Fungu 60 (Biashara) tarehe 28 Machi, 2021 Jijini Dodoma, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mipango na Bajeti kwa Mwaka 2020/2021. Aidha, naliomba Bunge lako tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2021/2022.

***2. Mheshimiwa Spika;*** Naomba kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, baraka na fadhila zake kwangu na kwa kuniwezesha kuwa sehemu ya Bunge hili nikiwa buheri wa afya na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kutekeleza jukumu la kuwasilisha na kujadili Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2021/2022.

***3. Mheshimiwa Spika;*** Kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara. Ninamshukuru pia kwa kuendelea kumwamini Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, Mbunge wa Jimbo la Mufundi Kaskazini kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara. Tunamuahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania kuwa tutafanya kazi kwa bidii, weledi, ubunifu, uaminifu na utiifu katika jitihada za ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini ikiwemo usimamizi makini wa rasilimali zilizopo katika Wizara ya Viwanda na Biashara na Taasisi zake.

***4. Mheshimiwa Spika;*** Naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushika nafasi ya kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu kumuombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa nguvu, ulinzi na afya katika kuwatumikia Watanzania.

***5. Mheshimiwa Spika;*** Naomba nitumie nafasi hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge lako Tukufu, wanafamilia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa ujumla kwa kumpoteza Kiongozi wetu mpendwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyeaga dunia tarehe 17 Machi, 2021. Kiongozi huyo alikuwa mtu dhahiri na asiyeteteleka katika kuchukua maamuzi magumu na kuyasimamia kwa umakini na hivyo kuleta matokeo yaliyokusudiwa. Wizara ya Viwanda na Biashara itaendelea kuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa inaenzi juhudi za Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

***6. Mheshimiwa Spika;*** Pia, napenda kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondokewa na Hayati Benjamini William Mkapa, aliyekuwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu ya Serikali ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania; Hayati Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; na Hayati Balozi Mhandisi John William Herbert Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Matukio hayo yasiyozoeleka yalifululiza na kutuacha na majonzi makubwa. Tunaomba Mwenyezi Mungu awarehemu viongozi wetu hao wapendwa, Amina.

***7. Mheshimiwa Spika;*** Aidha, katika mwaka 2020/2021, Bunge liliondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara na Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Justus Nditiye, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambwe. Naomba nitoe pole kwako Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote, familia, ndugu na jamaa wa marehemu. Tunaomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwa mfariji kamili katika kadhia hizo.

***8. Mheshimiwa Spika;*** Napenda kuchukua nafasi hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Othman Masoud; Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa umoja wao wanavyoweka mbele na kuyatetea maslahi ya Taifa. Dhamira hiyo imejidhihirisha kwa kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa ili kuhakikisha Zanzibar inaendelea kuwa na umoja kwa lengo la kuleta maendeleo kwa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

***9. Mheshimiwa Spika;*** Napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango (Mb.) kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na Chama cha Mapinduzi na baadaye kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, nampongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuaminiwa kuendelea kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika hii siyo zawadi kwake, bali

ni heshima ya kutambua uwezo wake katika kusimamia shughuli za Serikali kwa umahiri mkubwa.

***10. Mheshimiwa Spika;*** Nitumie fursa hii pia kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansansu, kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuongoza Mhimili wa Bunge. Aidha, naipongeza na kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini, Makamu wake Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Buchosa na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati. Ushauri na maelekezo yao yamezingatiwa kikamilifu katika maandalizi ya Mpango na Bajeti hii. Tunawaahidi kuwapa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu ya ujenzi wa Taifa letu.

***11. Mheshimiwa Spika;*** Naomba kutumia fursa hii pia kulishukuru Baraza la Taifa la Biashara (Tanzania National Business Council – TNBC) kwa kufanikisha uratibu ushirikiano na mashauriano yenye tija kati ya Serikali na Sekta Binafsi. Vilevile, nazishukuru Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (Tanzania Private Sector Foundation – TPSF); Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (Confederation of Tanzania Industries – CTI); Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (Tanzania Chambers of Commerce, Industry and Agriculture – TCCIA); na Baraza la Kilimo Tanzania (Agriculture Council of Tanzania – ACT) kwa michango yao katika kuendeleza Sekta za Viwanda, Biashara, Masoko, Viwanda Vidogo, na Biashara Ndogo. Tunaendelea kuwategemea kama nguzo na mihimili muhimu ya kushirikiana nayo katika kutekeleza kwa vitendo sera na mipango ya kisekta katika kuendeleza viwanda na biashara na uchumi wetu kwa ujumla.

***12. Mheshimiwa Spika;*** Hotuba hii ya Bajeti ninayoiwasilisha leo ni matokeo ya uratibu na ushirikiano mzuri wa viongozi wenzangu katika Wizara, akiwemo mtangulizi wangu, Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe (Mb.) ambaye sasa ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Uwekezaji; Naibu Waziri Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, Mbunge wa Mufindi Kaskazini; Katibu Mkuu Bw. Doto Mgosha James;

Naibu Katibu Mkuu Dkt. Hashil Twaibu Abdallah; aliyekuwa Katibu Mkuu Prof. Riziki Silas Shemdoe na Naibu wake Bw. Ludovick James Nduhiye, Wakuu wa Idara, Vitengo, Taasisi na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi. Napenda kuwashukuru na kuwaomba kuendelea kuongeza jitihada ili kuleta matokeo bora zaidi na uendelevu.

***13. Mheshimiwa Spika;*** Napenda kuwapongeza na kuwashukuru wananchi na wapiga kura wa Jimbo langu la Ubungo kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa uhakika katika kutekeleza majukumu kwa manufaa ya Jimbo na Taifa kwa ujumla. Kipekee namshukuru mke wangu mpendwa Bi. Prosista, watoto na familia yangu kwa ujumla kwa upendo wao, uvumilivu na sala zao wakati wote ninapotekeleza majukumu haya ya kitaifa.

***14. Mheshimiwa Spika;*** Baada ya maelezo hayo ya utangulizi, ninaomba sasa niwasilishe Mpango na Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2021/2022, unaojumuisha Umuhimu wa Viwanda na Biashara na Mchango wa Sekta ya Viwanda na Biashara katika uchumi wa Taifa; Tathmini ya Utekelezaji wa Malengo ya Bajeti kwa mwaka 2020/2021; Mipango na Bajeti kwa Mwaka 2021/2022; Malengo ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka 2021/2022; na kisha kuwasilisha maombi ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa kipindi cha mwaka 2021/2022.

## 2. UMUHIMU WA VIWANDA NA BIASHARA KATIKA UCHUMI WA TAIFA

***15. Mheshimiwa Spika;*** Kama tunavyofahamu, Serikali inatekeleza azma ya ujenzi wa uchumi wa viwanda. Tunapozungumzia ujenzi wa uchumi wa viwanda tunamaanisha shughuli zinazolenga maendeleo ya watu na vitu wakati maendeleo ya watu yakipewa kipaumbele. Katika ujenzi wa uchumi wa viwanda, Sekta ya Viwanda inakuwa kiungo muhimu cha kuchochea na kuhamasisha maendeleo ya sekta wezeshi na tegemezi katika uchumi wa viwanda zikiwemo kilimo, uvuvi, mifugo, misitu na madini kwa uzalishaji wa malighafi za viwanda. Kwa upande mwingine, ustawi wa

viwanda hutegemea miundombinu ya barabara, reli, usafiri wa anga, nishati, mawasiliano na maji. Aidha, uchumi wa viwanda unahitaji rasilimali watu ambayo ni muhimu katika mnyororo mzima kuanzia uzalishaji malighafi, uzalishaji wa bidhaa viwandani na usambazaji wa bidhaa hadi mikononi mwa walaji.

***16. Mheshimiwa Spika;*** Dira yetu ya Maendeleo ya Mwaka 2025 inalenga kuona kuwa Tanzania inahitimu na kuondokana kuwa Nchi Maskini na kuwa Nchi ya Uchumi wa Kati ifikapo Mwaka 2025. Kimsingi kwa kiasi kikubwa lengo hilo limekwisha kufikiwa kabla ya muda uliopangwa. Wizara ya Viwanda na Biashara katika kazi yake ya kuhakikisha ujenzi wa viwanda unaendelea nchini, itaendelea kuhakikisha kwamba haturudi tulikotoka na kwamba tunapanda zaidi kuelekea na Uchumi wa Kati wa Juu ifikapo 2025. Katika kufikia uchumi wa kati, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 inalenga kuona kuwa uchumi wetu unabadilika kutoka ule unaotegemea kilimo chenye uzalishaji duni kwenda kuwa uchumi wa viwanda vya kati (semi-industrialised economy) unaoendeshwa na kilimo cha kisasa chenye uzalishaji mkubwa na wenye tija, na ambao umefungamanishwa na viwanda na huduma zinazopatikana vijijini na mijini.

***17. Mheshimiwa Spika;*** Katika kujenga uchumi wa viwanda ambao lengo lake kubwa ni kufanya mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo inaendelea kuwa chachu muhimu sana. Sekta hiyo inahitaji ujuzi, maeneo yaliyotengwa na kuwekewa miundombinu wezeshi, teknolojia za kisasa zinazopatikana kwa bei rahisi na mitaji ambayo Watanzania walio wengi wanaweza kuimudu. Sekta hiyo ni shule kwani kupitia viwanda vidogo na biashara ndogo, wajasiriamali hupata ujuzi na uzoefu wa shughuli za uzalishaji na kuweza kuhitimu kuwa wawekezaji na wafanyabiashara wa kati na wakubwa. Katika jitihada za kuhamasisha ujenzi wa viwanda kwa msambao nchi nzima, ni viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati vinavyoweza kujengwa na kuendeshwa kwa tija nchi nzima. Ni dhahiri kuwa Sekta hiyo ni muhimu sana katika kushiriki na kuchochea ujenzi wa uchumi jumuishi kutokana

na kutegemea malighafi inayozalishwa nchini na hususan wakulima walio wengi, hutumia teknolojia rahisi na hutoa ajira kwa wingi.

***18. Mheshimiwa Spika;*** Pamoja na umuhimu huo wa viwanda vidogo, viwanda vikubwa pia ni vya msingi katika kuchochea ujenzi na uendelevu wa viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati. Kwa upande mmoja, viwanda hivyo huzalisha bidhaa ambazo ndiyo msingi wa viwanda vingine na kuzalisha bidhaa za kati ambazo hutumiwa na viwanda vya kati, vidogo na vidogo sana katika kuzalisha bidhaa. Vilevile, viwanda hivyo hupokea bidhaa kutoka viwanda vidogo au malighafi kutoka kwa wazalishaji ili kuzalisha bidhaa nyingine. Hivyo, Wizara kupitia Mpango na Bajeti ya mwaka 2021/2022 itaendeleza jitihada za kuunganisha nguvu na viwanda vikubwa kwa kuwa uwepo wa viwanda vya aina hizo zote ni muhimu. Hii itawezesha kukamilisha mnyororo wa uzalishaji wa viwanda ambao ni endelevu na unganishi kwa sekta za uzalishaji malighafi hususan zitokanazo na kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini.

***19. Mheshimiwa Spika;*** Ni dhahiri kuwa ustawi wa shughuli za viwanda unategemea kwa kiasi kikubwa ushiriki wa wadau mbalimbali. Ujenzi wa viwanda unaanza kwa kutambua eneo la kujenga viwanda ambalo ubainishwaji wake na uwekaji wa miundombinu wezeshi na saidizi unahusisha mamlaka mbalimbali ikiwemo Sekta Binafsi. Ili Sekta ya Viwanda iwe endelevu, suala la utunzaji wa mazingira ni muhimu sana. Aidha, uendeshaji wa viwanda na sekta wezeshi na saidizi zinahitaji nguvu kazi zenye ujuzi na weledi. Kwa misingi hiyo, mafanikio ya azma ya ujenzi wa uchumi wa viwanda ni matokeo ya ushirikiano na jitihada za Wizara zote na Serikali kwa upande mmoja na Sekta Binafsi na Wadau wa Maendeleo kwa upande mwingine.

## 3. MCHANGO WA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA KATIKA UCHUMI

### *3.1.Sekta ya Viwanda*

***20. Mheshimiwa Spika;*** Mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa kwa mwaka 2020 ulikuwa asilimia 8.4

ikilinganishwa na asilimia 8.5 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 0.1 ***(Kiambatisho Na.1)***. Vilevile, Sekta ya Viwanda ilikua kwa kiwango cha asilimia 4.5 mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 5.8 mwaka 2019 ***(Kiambatisho Na. 2)***. Upungufu huo ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na athari za janga la UVIKO - 19. Kwa upande mwingine, Sekta ya Viwanda imeongeza ajira kutoka 336,797 mwaka 2019 hadi ajira 370,485 mwaka 2020 ***(Kiambatisho Na. 3)***.

***21. Mheshimiwa Spika;*** Mchango wa Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo katika Pato la Taifa ni asilimia 35. Sekta hiyo imeajiri zaidi ya Watanzania milioni nane (8), ikiwa ni ya pili katika sekta za kiuchumi katika kutoa ajira ikifuatia Sekta ya Kilimo.

### ***3.2.*** **Sekta ya Biashara**

***22. Mheshimiwa Spika;*** Mchango wa Sekta ya Biashara katika Pato la Taifa kwa mwaka 2020 ulikuwa asilimia 8.7 ikilinganishwa na asilimia 8.8 mwaka 2019 sawa na upungufu wa asilimia 0.1. Vilevile, Sekta ya Biashara ilikua kwa kiwango cha asilimia 2.1 mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 5.5 mwaka 2019. Upungufu huo umechangiwa na athari za UVIKO – 19.

***23. Mheshimiwa Spika;*** Sekta ya Biashara imewezesha uuzaji nje wa bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani Bilioni 6.06 kwa mwaka 2020 ukilinganisha na Dola za Marekani Bilioni 5.00 kwa mwaka 2019, ikiwa ni ongezeko la Dola za Marekani Bilioni 1.06. Ongezeko hilo limetokana na kuimarika kwa uzalishaji nchini na kutumika kwa fursa mbalimbali za masoko.

## **4. *TATHMINI YA* MPANGO *NA* UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2020/2021**

### **Bajeti Iliyoidhinishwa na Kupokelewa kwa Mwaka 2020/2021**

***24. Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Fungu 44 na 60 iliidhinishiwa matumizi ya jumla ya Shilingi 81,366,902,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi

29,687,886,000 ni za Matumizi ya Maendeleo na Shilingi 51,679,016,000 ni za Matumizi ya Kawaida. Aidha, hadi kufikia mwezi Machi 2021, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi 45,512,707,118.72, sawa asilimia 55.94 ya Bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi 38,629,551,706.20 sawa na asilimia 74.75 ni za Matumizi ya Kawaida na Shilingi 6,883,155,412.52 sawa asilimia 23.19 ni za Matumizi ya Maendeleo.

### *4.1. Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2020/2021*

#### *4.1.1. Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara - BLUEPRINT*

***25. Mheshimiwa Spika;*** Serikali ilianzisha na kupitisha Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara kwa lengo la kuimarisha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji nchini na hivyo kushughulikia masuala yaliyokuwa yakilalamikiwa na wadau wa sekta mbalimbali. Aidha, Serikali iliandaa Mpango Kazi (BLUEPRINT Action Plan) wa kutekeleza mapendekezo ya kushughulikia changamoto zilizoainishwa katika BLUEPRINT. Mpango Kazi umejielekeza katika kuboresha mazingira ya biashara hasa kurekebisha Sheria, kanuni na tozo katika mamlaka za udhibiti ambazo zinakinzana; Kuunganisha majukumu ya taasisi ambayo yanaingiliana; Kuweka mifumo ya kielektroniki ya kutoa huduma mbalimbali ikiwemo leseni, vibali na tozo; Kuweka taratibu bayana na miongozo ili kuwawezesha watumia huduma kukidhi matakwa ya kisheria; Kuwezesha kuanzisha vituo vya huduma vya pamoja katika Mamlaka za Halmashauri na maeneo mengine ya uwekezaji na biashara; na Kuwezesha kuunganisha mifumo ya utoaji leseni na vibali kati ya Mamlaka za Udhibiti na maeneo mengine. Utekelezaji wa Mpango Kazi ulianza rasmi Julai mosi, 2019.

***26. Mheshimiwa Spika;*** Hadi hivi sasa, Serikali imefuta au kupunguza viwango vya kodi, tozo na ada mbalimbali zipatazo 232 zilizokuwa kero kwa wafanyabiashara na wawekezaji. Hatua hizo zililenga kupunguza muda na gharama za kupata leseni na vibali vingine vya kufanya biashara nchini hasa kwa wajasiriamali wadogo na wa kati.

***27. Mheshimiwa Spika;*** Katika kuhakikisha Mpango kazi wa BLUEPRINT unatekelezwa ipasavyo, Serikali iliandaa Mradi wa *Support for Business Environment, Growth and Innovation* (BEGIN) ambao umefadhiliwa na Umoja wa Ulaya kwa kiasi cha Euro milioni 10 kwa ajili ya kuhakikisha kuwa Mpango kazi huo unatekelezwa ipasavyo. Hivi sasa Wizara inakamilisha uandishi wa mchanganuo wa matumiz ili kuanza utekelezajii. Aidha, Wizara ikiwa ndiye Mratibu wa Mpango wa *Blueprint* inaendelea kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa BLUEPRINT kutokana na taarifa za kisekta zinazotekeleza Mpango huo.

### *4.1.2. Mapitio na Utungaji wa Sera na Marekebisho ya Sheria na Kanuni*

#### *a) Mapitio na Utungaji wa Sera*

#### *i) Mapitio ya Sera Endelevu ya Maendeleo ya Viwanda (SIDP, 1996 - 2020)*

***28. Mheshimiwa Spika;*** Tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (SIDP, 19962020) imefanyika na kuonesha umuhimu wa kufanya marejeo ya sera hiyo. Umuhimu huo unatokana na uwepo wa masuala mapya yaliyojitokeza (*emerging issues)* kama vile masuala ya matumizi ya rasilimali za majini (blue economy) na mwelekeo wa kukuza uchumi shindani unaotegemea maarifa mapya. Wizara tayari imekamilisha uchambuzi wa utekelezaji wa Sera na kuandaa andiko la awali na rasimu ya sera hiyo. Hatua hiyo itafuatiwa na kukamilisha maandalizi ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera, Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini pamoja na Mkakati wa Mawasiliano ndani ya mwaka 2021/2022.

#### *ii) Mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo (SME Policy, 2003)*

***29. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekamilisha hatua zote za awali za marejeo ya Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ambapo rasimu ya Sera na Mkakati wa Utekelezaji

wa Sera umekamilika. Aidha, maoni toka kwa wadau wa Sekta ya Umma yamekusanywa. Vilevile, Wizara imeandaa rasimu ya Mkakati wa Mawasiliano kwa ajili ya Sera hiyo. Hatua hizo zitawezesha kukamilisha sera hiyo kabla ya Mwezi Desemba 2021.

***iii) Mapitio ya Sera ya Taifa ya Biashara ya Mwaka 2003***

***30. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imekamilisha hatua zote za awali za mapitio ya Sera ya Taifa ya Biashara ya mwaka 2003 zikiwemo kukamilisha Andiko la Tafiti ya Sera (Policy Background Research Paper), Rasimu ya Sera, Mkakati wa Utekelezaji na Mkakati wa Mawasiliano. Hatua inayofuata ni kupata maoni ya mwisho ya wadau ambayo yatawezesha hatua zinazofuata za kukamilisha Sera hiyo ndani ya mwaka 2021.

***iv) Utungaji wa Sera ya Taifa ya Ubora***

***31. Mheshimiwa Spika;*** Wizara inaendelea kukamilisha utunzi wa Sera ya Taifa ya Ubora (National Quality Policy - NQP). Sera hiyo inalenga kuondoa changamoto mbalimbali zilizopo katika Taasisi za Udhibiti Ubora ambazo zinahusika na miundombinu ya ubora, masuala ya vifaa katika maabara pamoja na kufungamanisha na Taasisi za kimataifa zinazoratibu masuala ya ubora. Kwa sasa, Wizara imekamilisha rasimu ya Sera, Mkakati wa Utekelezaji na tayari imewashirikisha wadau wote muhimu kuhusiana na Sera hiyo kwa hatua zinazofuata.

***v) Mkakati wa Kukuza Mauzo ya Nje***

***32. Mheshimiwa Spika;*** Wizara inaendelea na maandalizi ya Mkakati wa Kukuza Mauzo ya Nje (National Export Strategy - NES) unaolenga kuhakikisha kuwa Nchi inaongeza wigo wa mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi hususan mazao ya kilimo na bidhaa za viwandani. Mkakati huo pia unalenga kutumia ipasavyo fursa za masoko nje ya nchi. Wizara inaendelea kukusanya maoni ya wadau kwa lengo la kuuboresha na kuukamilisha.

***b) Marekebisho ya Sheria Mbalimbali***

***33. Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2020/2021, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanya marekebisho ya Sheria mbili za Wizara kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020. Sheria hizo ni Sheria ya Makampuni Sura 212 ambapo marekebisho yalilenga kuwezesha upatikanaji wa taarifa za wanufaika wa mwisho katika kampuni ili ikodi, kudhibiti utakatishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi. Sheria ya Ushindani Sura 285 ilirekebishwa ili adhabu kwa kosa chini ya Sheria hiyo iwe kampuni iliyosajiliwa Tanzania na sio kugusa hesabu za kampuni hiyo nje ya nchi. Lengo la marekebisho hayo ni kutimiza azma kuu ya Serikali ya kuwa na Tanzania inayovutia uwekezaji wa viwanda na kujenga mazingira mazuri ya biashara.

***34. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imewasilisha marekebisho ya sheria mbalimbali ambayo tayari yamesomwa Bungeni kwa mara ya kwanza. Marekebisho hayo yamezigusa Sheria ya Majina ya Biashara, Sura 213, Sheria ya Alama za Biashara na Huduma Sura 326 na Sheria ya Makampuni, Sura 212.

***35. Mheshimiwa Spika;*** Wizara inakusudia kutunga Sheria ya Kujilinda Dhidi ya Athari za Kibiashara ya mwaka, 2021 (Trade Remedies Act, 2021) ili kufuta Sheria ya *Anti Dumping and Counterveilling Measures* ya 2004 ili kulinda biashara na viwanda vya ndani, kuzuia uingizwaji wa bidhaa kwa wingi; bidhaa kuuzwa kwa bei ya chini ikilinganishwa na bei kwenye nchi zinazotoka; na bidhaa zenye ruzuku zilikotoka hivyo kuathiri bidhaa za ndani ya nchi zisizo na ruzuku. Mapendekezo ya Sheria hiyo yamewasilishwa katika ngazi ya maamuzi Serikalini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaendelea kufanya mapitio ya Sheria Ishirini na Mbili (22) zinazosimamiwa na Wizara ili kuboresha mazingira ya biashara hapa nchini na kuwezesha utekelezaji wa *BLUEPRINT* kupitia Wizara na Marekebisho ya sheria mbalimbali chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

***36. Mheshimiwa Spika;*** Pia, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaandaa na kutangaza katika Gazeti la Serikali Kanuni mbalimbali ili kuwezesha utekelezaji wa Sheria Kuu. Wizara iliongeza muda wa mwaka mmoja kuwasilisha Taarifa za Wanufaika wa Mwisho wa Makampuni kwa Tangazo la Serikali Na.189/2021 na tayari imeandaa Kanuni chini ya Sheria ya Makampuni, Sura 212 ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa za wanufaika wa mwisho wa Makampuni kufuatia marekebisho ya Sheria ya Makampuni kupitia Sheria ya Fedha 2020. Aidha, Kanuni saba (7) za kutekeleza Sheria ya Viwango Sura 130 na moja chini ya Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania Sura 155 zinakamilishwa. Wizara inaendelea kupitia upya Kanuni zote zilizopo ili kuona hitaji la kurekebisha au kuwa na Kanuni mpya zinazoendana na mabadiliko ya maendeleo ya sayansi na teknolojia hapa nchini na duniani kote. Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaendelea kupitia na kutoa ushauri wa awali kwenye mikataba ya kimataifa inayogusa Sekta ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Wizara kwa mwongozo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inatoa ushauri wa kisheria na kuendesha mashauri ya Wizara na Taasisi zake.

***37. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na TBS ilifanya kikao cha marekebisho ya Sheria ya Viwango Tanzania sura Na. 30 na kufanya maboresho ya Kanuni za Sheria ya TBS. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na (FCC) na (FCT) imekamilisha Andiko la mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Ushindani Na. 8 ya Mwaka 2003 na tayari limewasilishwa katika hatua mbalimbali za maamuzi serikalini.

### *4.1.3. Sekta ya Viwanda*

#### *a) Utekelezaji wa Mikakati ya Kisekta ya Kuendeleza Viwanda*

***38. Mheshimiwa Spika;*** Mkakati Unganishi wa Sekta ya Viwanda umejikita katika kutengeneza mazingira ya uwekezaji wa viwanda ulio shindani kupitia Ujenzi wa kongano za viwanda, ujenzi wa miundombinu wezeshi ya viwanda,

uhamishaji wa ushindani wa bidhaa kimataifa na uwezeshaji wa taasisi za viwanda (institutional support). Aidha, Mkakati ulilenga kufanya Sekta ya Viwanda kuwa ni mhimili wa maendeleo ya uchumi. Sekta za kipaumbele zilizoanishwa katika Mkakati ni pamoja na Sekta Ndogo za: Ngozi; Nguo na Mavazi; Chuma na Bidhaa za Chuma; Mbolea na Kemikali za Viwandani; na Uchakataji wa bidhaa zinazotokana na kilimo kama vile mafuta ya kula, korosho, matunda, maziwa na bidhaa za maziwa.

***39. Mheshimiwa Spika****;* Baadhi ya sekta ndogo za kipaumbele zilizoainishwa katika Mkakati huo zinatekelezwa kupitia mikakati mahsusi ya sekta husika. Mafanikio ya utekelezaji wa Mikakati hiyo ya kisekta ni kama ifuatavyo:

**(i) *Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Ngozi na Bidhaa za Ngozi***

***40. Mheshimiwa Spika;*** Serikali imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Ngozi na Bidhaa za Ngozi unaohusisha kuwahamasisha wawekezaji kujenga viwanda vya kisasa vya kusindika ngozi kufikia hatua ya mwisho yaani *Finished Leather*. Mkakatii pia unalenga kujenga viwanda vya kisasa vya kutengeneza bidhaa za ngozi kwa kutumia teknolojia zinazokubalika katika soko la dunia. Kutokana na jitihada hizo:

- Kiwanda cha *ACELeather* cha Morogoro kilichokuwa hakifanyi kazi kimefunga mashine za kisasa na mwaka 2021 kimeanza kuchakata ngozi hadi hatua ya mwisho. Kiwanda hicho kina uwezo wa kusindika vipande vya ngozi za ng'ombe 5,000 na ngozi za mbuzi 12,000 kwa siku;

- Kiwanda cha *Kilimanjaro International Leather Industries Company Ltd* kilichokuwa kinaitwa *Karanga Leather Industry* kimefunga (install) mashine za kisasa zenye uwezo wa kutengeneza jozi milioni 1.2 za viatu kwa mwaka. Kiwanda hicho tayari kimekamilika kwa asilimia 100 na kimeanza uzalishaji;

- Wizara imeanza kuendeleza Eneo la Zuzu kwa ajili ya kujenga Kongano la Ngozi katika Mkoa wa Dodoma (Leather

Cluster) lenye jumla ya ekari 107. Ujenzi wa jengo la kiwanda (Industrial shed) moja kati ya majengo matatu tayari umeanza na unatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka 2021. Aidha, michoro ya majengo mawili yatakayofuata kujengwa inakamilishwa;

• Katika kuvutia uwekezaji na kuvilinda viwanda vya ndani, Serikali imeweka vivutio vya uwekezaji kwenye Sekta Ndogo ya Ngozi kwa kuweka msamaha wa kodi kwenye mashine na malighafi zinazotoka nje ya nchi ambazo zinatumika katika uzalishaji wa ngozi na bidhaa zake; na

• Wizara kupitia TIRDO na kwa ufadhili wa COSTECH inatekeleza Mradi wa Uongezaji wa Thamani wa Ngozi katika Wilaya ya Meru, Monduli na Arusha mjini. Kupitia Mradi huo, zaidi ya wafugaji 419 wamejengewa uwezo wa kutunza ngozi kwa kutumia malighafi rahisi na zinazopatikana katika maeneo yao, uchunaji sanifu pamoja na kugawiwa visu mahsusi kwa ajili ya kuchunia.

**(ii) Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Nguo na Mavazi**

***41. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Sekta ya Nguo na Mavazi (Cotton to Cloth - C2C) kwa kuweka mazingira mazuri katika viwanda vya nguo ikiwa ni pamoja na kudhibiti uingizwaji holela wa vitenge na khanga kutoka nje ya nchi. Baadhi ya viwanda vimeanza kuwekeza vikiwemo Kiwanda cha *MWATEX (2000) Ltd* kilichopo katika Mkoa wa Mwanza ambacho kimeanza kufunga mashine mpya za kuzalisha vitenge vya WAX chenye uwezo wa kuzalisha mita 500,000 kwa mwezi; na Kiwanda cha *NIDA Textiles Ltd* kilichopo jijini Dar es Salaam ambacho kipo katika hatua za kufunga mitambo mipya ya kuzalisha khanga na vitenge. Aidha, Vinu viwili (2) vya kuchambua pamba (ginneries) vinavyomilikiwa na Vyama vya Ushirika katika Wilaya ya Kahama na Chato ambavyo vilikuwa vimesimamisha uzalishaji kwa muda mrefu vimefufuliwa. Mafanikio hayo yanatokana na uwekezaji mkubwa unaotokana na mkopo wa jumla ya Shilingi Bilioni 18 kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).

**(iii) *Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mbogamboga na Matunda***

***42. Mheshimiwa Spika;*** Katika kuhakikisha kuwa Sekta Ndogo ya Mboga Mboga na Matunda inakuwa na tija kwa ajili ya kuongeza soko la mazao hayo nje ya nchi, Wizara kwa kushirikiana na Sekretariati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) imeandaa Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mbogamboga na Matunda na Mpango Kazi wa utekelezaji (*Action Plan*) wa Afrika Mashariki (2021-2031). Mkakati na Mpango huo utatoa mwongozo wa namna bora ya kusindika mazao hayo kufikia viwango na ubora unaotakiwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na nje ya Jumuiya. Wizara pia itaendelea kutoa elimu kwa wadau juu ya mkakati huo ili kuhakikisha wanakuwa na taarifa sahihi kuhusu eneo hilo.

**b) Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani**
**1) Uzalishaji wa Dawa na Vifaa Tiba**

***43. Mheshimiwa Spika;*** Sekta inatarajiwa kuongeza uzalishaji sambamba na kutengeneza dawa za aina mbalimbali ili kufikia malengo ya asilimia 60 ya uzalishaji wa Dawa na Vifaa Tiba Nchini ifikapo Mwaka 2025. Pia Wizara imeendelea kuchukua hatua za makusudi kushawishi na kuhakikisha kuwa sekta inaongeza uwekezaji wa viwanda vipya pamoja na kuweka mitambo ya kisasa katika viwanda vya zamani na kuongeza ufanisi wa viwanda hivyo. Hatua hizo ni pamoja na:-

i) Kuandaa Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Utengenezaji Dawa za Binadamu na Vifaa Tiba (*Pharmaceutical Sector Development Strategy*);

ii)Wizara imeshirikiana na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kuainisha aina za dawa zinazotengenezwa na viwanda vya ndani na kutosheleza mahitaji ya nchi kwa lengo la kuzifanya bidhaa hizo kuwa na ushindani katika soko;

iii) Wizara kupitia Shirika la Utafiti wa Viwanda (TIRDO) ilifanya tathmini ya uzalishaji katika viwanda vya kusindika nyuzi za

pamba ili kuhakiki uwezo wa uzalishaji na kubaini iwapo viwanda hivyo vinaweza kuzalisha malighafi ya kutosha kwa Kiwanda cha Vifaa Tiba kinachokusudiwa kujengwa katika Mkoa wa Simiyu;

iv) Kuendeleza mapambano dhidi ya Ugonjwa wa Virusi vya Korona (UVIKO-19) ambapo Wizara ya Viwanda na Biashara imeendelea kusimamia uzalishaji wa malighafi na vifaa kinga ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa kutosha wa vitakasa mikono na barakoa za makundi maalum *(surgical masks*); na

v) Kuhamasisha ujenzi wa viwanda uliwezesha mwitikio wa kuanza ujenzi wa Kiwanda cha Dawa cha Kairuki.

**2) Uzalishaji wa Sukari**

***44. Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ina jumla ya viwanda vikubwa vitano vya kuzalisha sukari ambavyo ni: *Kilombero Sugar - I, Kilombero Sugar – II,* na *Mtibwa Sugar Ltd* vilivyopo Mkoa wa Morogoro; *Kagera Sugar Ltd* kilichopo Mkoa wa Kagera, na Kiwanda cha TPC - Moshi kilichopo Mkoa wa Kilimanjaro. Aidha, kuna Kiwanda cha *Manyara Sugar Co. Ltd* kilichopo Mkoa wa Manyara chenye ukubwa wa kati. Viwanda vyote hivyo vina uwezo wa kuzalisha (installed capacity) wa jumla ya tani 462,863 za sukari kwa mwaka. Uwezo huo wa uzalishaji ni pungufu ya mahitaji ya sukari nchini ambayo ni wastani wa tani 635,000 kwa mwaka (inayojumuisha tani 470,000 za matumizi ya kawaida na tani 165,000 za matumizi ya viwandani).

***45. Mheshimiwa Spika;*** Ili kuziba pengo la uzalishaji wa sukari nchini, Wizara imeendelea kuvihamasisha viwanda vilivyopo kupanua zaidi uwezo wake wa uzalishaji. Mfano, Kiwanda cha *Kilombero Sugar* kimeanza maandalizi ya ujenzi wa kiwanda kipya ambao unatarajiwa kuanza mwaka 2021/2022 na kukamilika ndani ya kipindi cha miaka mitatu kwa gharama za Dola za Marekani Milioni 239. Kiwanda hicho kitaongeza uzalishaji wa sukari kutoka tani 125,000 kwa mwaka hadi tani 271,000 kwa mwaka. Aidha, upanuzi wa

kiwanda hicho utaongeza matumizi ya miwa ya wakulima wadogo kutoka tani 600,000 hadi tani 1,450,000 kwa mwaka. Vilevile, Kiwanda cha Sukari Manyara kimeongeza uwezo wa kuchakata miwa kutoka tani 50 kwa siku hadi kufikia tani 750 kwa siku.

***46. Mheshimiwa Spika;*** Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuwavutia wawekezaji wapya na kuna maendeleo mazuri katika baadhi ya miradi. Katika Mradi wa Mkulazi II (eneo la Mbigiri), ujenzi wa majengo ya kiwanda cha sukari unatarajiwa kuanza rasmi mwezi Mei, 2021 na uzalishaji wa sukari kuanza mwezi Desemba, 2021. Kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 50,000 za sukari kwa mwaka. Vile vile, Kiwanda cha Sukari cha Bagamoyo (*Bagamoyo Sugar)* kinatarajia kuanza uzalishaji wake ifikapo mwezi Juni 2021. Kiwanda hicho, kinatarajia kuzalisha sukari kwa kuanza na tani 30,000 hadi kufikia tani 70,000 za sukari kwa mwaka.

***3) Uzalishaji wa Bidhaa za Chuma Viwandani***

***47. Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia mwezi Desemba 2020, Nchi yetu ilikuwa na viwanda 25 vya kuzalisha chuma na bidhaa za chuma. Viwanda hivyo huzalisha nondo, mabati, mabomba, misumari, senyenge na bidhaa nyinginezo. Kati ya hivyo, Viwanda vya kuzalisha nondo vipo 16 vyenye uwezo wa kuzalisha tani 1,082,700 kwa mwaka, wakati uzalishaji halisi ni tani 240,336 kwa mwaka, sawa na asilimia 22 ya uwezo wake. Mahitaji ya nondo nchini kwa mwaka ni tani 440,336, hivyo uzalishaji huo wa ndani hutosheleza asilimia 55 ya mahitaji yote na asilimia 45 inayobaki huagizwa kutoka nje ya nchi. Aidha, Nchi yetu ina viwanda vipatavyo saba (7) vya kutegeneza mabomba ya chuma vyenye uwezo wa kuzalisha tani 223,200 kwa mwaka. Uzalishaji halisi kwa sasa ni tani 99,100 sawa na asilimia 44 ya uwezo wa uzalishaji. Mabomba yanayozalishwa katika viwanda hivyo hutumika kwa shughuli mbalimbali za usambazaji maji na pia hutumika kama malighafi katika viwanda vya ujenzi na ufundi.

***48. Mheshimiwa Spika;*** Nchi yetu ina viwanda viwili vikubwa vinavyozalisha mabati kuanzia hatua ya awali (intergrated)

ambavyo ni ALAF na *MMI Steel*. Viwanda hivyo vina uwezo wa kuzalisha tani 158,000 kwa mwaka wakati uzalishaji halisi kwa sasa ni tani 58,189 kwa mwaka, sawa na asilimia 37 ya uwezo halisi. Sambamba na hilo, pia kuna viwanda vya kukunja mabati zaidi ya 60 nchini ambavyo hununua mabati kutoka nje ya nchi, kukunja migongo na kukata.

***49. Mheshimiwa Spika;*** Malighafi muhimu ya kuzalisha nondo hapa nchini ni chuma chakavu (scrap metals). Katika siku za hivi karibuni, upatikanaji wake umekuwa hautoshelezi mahitaji ya viwanda vya nondo na hivyo viwanda kulazimika kuagiza malighafi (billets) kutoka nje ya nchi. Wizara inaendelea na majadiliano na mwekezaji atakayeweza kuzalisha chuma ghafi kwa kutumia madini ya chuma cha Liganga ili kutosheleza mahitaji ya chuma ghafi nchini kikiwemo chuma safi (billets) na hivyo kuondokana na utegemezi wa kuingiza chuma toka nje.

***C) Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati***

**(i) *Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma cha Liganga***

***50. Mheshimiwa Spika;*** Miradi ya chuma cha Liganga na makaa ya mawe ya Mchuchuma ni Mradi Unganishi na ipo katika wilaya ya Ludewa, Mkoa wa Njombe. Makaa ya mawe ya Mchuchuma yaligunduliwa mwaka 1860 wakati chuma cha Liganga kiligunduliwa mwaka 1898. Tokea kipindi hicho pamekuwepo na tafiti nyingi pamoja na juhudi mbalimbali za kuanzisha kiwanda cha chuma. Juhudi hizo zilikabiliwa na changamoto za mtaji na teknolojia ya kuchenjua chuma.

***51. Mheshimiwa Spika***; Katika Miradi ya Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma cha Liganga, zoezi la uhakiki wa mali za wananchi watakaopisha ujenzi wa miradi hiyo limekamilika. Aidha, Shilingi Bilioni 11.04 zinatarajiwa kulipwa kama fidia kwa wananchi 1,145 kwa maeneo yote ya miradi. Vilevile, upitiaji na ufanyaji wa majadiliano ya mikataba kati ya Shirika la Taifa la Maendeleo - NDC na mwekezaji unaendelea pamoja na kurejea Sheria za Kuendeleza Mradi

Unganishi wa Mchuchuma na Liganga kwa kuzingatia Sheria za Madini ya Mwaka 2010 na Sheria Na. 6 na Na. 7 za Mwaka 2017 na kulipwa kwa ada za leseni za kuchimba madini (Special Mining Licence - SML) katika eneo la Mradi. Majadiliano hayo yatakapokamilika yatafungua njia kwa mwekezaji kuanza utekelezaji wa Mradi ikiwa ni pamoja na kulipa fidia. Aidha, uboreshaji wa barabara kutoka Itoni (Njombe) kuelekea maeneo ya miradi Liganga na Mchuchuma za kiliomita 250 kwa kiwango cha changarawe ulifanywa na Serikali. Kwa sasa, kilomita 50 za kipande korofi cha barabara kutoka Lusitu hadi Mawengi kinatengenezwa kwa kiwango cha zege.

### (ii) *Mradi wa Kilimanjaro Machine Tools (KMTC)*

***52. Mheshimiwa Spika;*** Mradi wa Kiwanda cha KMTC unamilikiwa na NDC na Kiwanda kilijengwa mwaka 1984 kwa madhumuni ya kuendeleza utaalam wa ufuaji chuma kwa ajili ya kutengeneza mashine na vipuli vya mitambo mbalimbali. Tangu Kiwanda cha KMTC kianze uzalishaji upya mwaka 2014/2015, kimefanikiwa kuzalisha na kuuza mashine 50 za mbao (wood working machines), mashine tano (5) za kusagia mahindi (maize milling machines) na mashine mbili (2) za kupukuchilia mahindi (maize huller). Vilevile, Kiwanda kinazalisha vipuri vya aina mbalimbali kwa ajili ya viwanda, hususan katika Sekta ya Kilimo, Madini na Usafirishaji. Wizara kupitia NDC inaendelea na uboreshaji wa Kiwanda cha KMTC ambapo imeanza kukarabati mitambo ya kuyeyusha bidhaa za chuma (Galvanizing Plant). Pia, Wizara imepanga kujenga Tanuru la Kuyeyushia Chuma (Foundry) na kuanzisha karakana ya kuchomelea vyuma (Fabrication Workshop). Vilevile, NDC imeingia mkataba wa awali (MoU) na TANESCO kwa nia ya kuzalisha minara ya kusambaza Umeme katika Mradi wa *Julius Nyerere Hydropower Plant* kutoka kwenye bwawa hilo jipya kwenda Kinyerezi, Dar es Salaam ambayo ilitarajiwa kuagizwa kutoka nje ya nchi.

**(iii)** ***Mradi wa Magadi Soda katika Bonde la Engaruka***

***53. Mheshimiwa Spika;*** Magadi Soda ni moja ya rasimali kubwa zilizopo katika Bonde la Engaruka lilipo katika Wilaya ya Monduli, Mkoa wa Arusha. Uchorongaji uliofanyika mwaka 2011 – 2013 ulibaini kiasi cha Mita za ujazo Bilioni 4.68 za magadi soda na kiasi hicho huongezeka kwa Mita za ujazo Milioni 1.9 kila mwaka. Upembuzi yakinifu ambao unafanywa na TIRDO unalenga kuanzisha kiwanda cha kuzalisha magadi kwa kiwango cha Tani Milioni 10 kwa mwaka kwa ajili ya matumizi ya viwanda vya ndani na kuuza nje.

***54. Mheshimiwa Spika***; Katika kukamilisha tafiti za Mradi wa Magadi Soda – Engaruka na kujenga kiwanda – Engaruka, kazi ya upembuzi yakinifu (TechnoEconomic Study) imekamilika na ripoti ya utafiti huo imekwishafanyiwa mapitio ya mwisho na kurudishwa TIRDO kwa ajili ya hatua ya ukamilishwaji na uchapaji mwishoni. Uzalishaji wa Magadi Soda umepangwa kuwa tani laki tano (5) kwa mwaka na kiwanda kitakapoanza uzalishaji utakuwa unaongezeka mpaka kufikia tani milioni moja (1) kwa mwaka kulingana na mahitaji kwa ajili ya matumizi ya viwanda vya kemikali nchini na kuuza nje ya nchi kupitia Bandari ya Tanga. Zoezi la uthaminishaji na uhakiki wa ardhi na mali za wananchi umekamilika na utagharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 14.63.

**(iv)** ***Mradi wa Kiwanda cha Matairi Arusha***

***55. Mheshimiwa Spika;*** Katika juhudi za kufufua na kuendesha Kiwanda cha Matairi cha Arusha, Wizara kupitia Shirika la NDC inaendelea kutafuta mwekezaji mpya baada ya kutofikia muafaka na mwekezaji aliyejitokeza *"Sayinvest Overseas Ltd."* Mwekezaji huyo alionesha nia ya kuwekeza kiwanda cha kuzalisha matairi chenye uwezo wa kuzalisha wastani wa matairi yasiyopungua milioni kumi (10) kwa mwaka. Hata hivyo, Mwekezaji huyo hakuweza kutimiza matakwa ya mkataba ulioingiwa baina yake na NDC. Aidha, Wizara imejipanga kufanya tathmini nyingine ya kina ili kuja na mapendekezo bora zaidi ya namna ya kuendeleza mradi huo katika eneo hilo au vinginevyo.

**(v) *Mradi wa Matrekta ya URSUS***

***Mheshimiwa Spika;*** Mradi wa Matrekta wa URSUS unatokana na Mkataba wa Ushirikiano wa Kiuchumi baina ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Poland, uliosainiwa tarehe 28 Septemba, 2015. Serikali ya Jamhuri ya Poland iliiteua Kampuni ya URSUS na Serikali ya Tanzania ikateua SUMA JKT kama watekelezaji na baadae Mradi huo ukahamishiwa NDC kwa utekelezaji. Katika Mkataba huo, Serikali ya Poland ilitoa Mkopo nafuu wa Dola za Marekani Milioni 110 wenye riba ya asilimia 0.3 (0.3%) kwa mwaka, ukiwa na *grace period* ya miaka mitano na utarudishwa katika kipindi cha miaka 30. Fedha ya Mradi zinagharamia ujenzi wa Kiwanda cha Kuunganisha Matrekta, kununua matrekta 2,400 na zana zake vikiwa katika vipande vipande (Semi Knocked Down - SKD), kuviunganisha na kuvisambaza kwa wateja, kujenga vituo nane (8) vya kuhudumia wateja (service centres), kutoa mafunzo; na ujenzi wa maghala ya kuhifadhi nafaka ambao uko chini ya Wizara ya Kilimo na Ushirika, ambapo kila moja utagharimu Dola za Marekani Milioni 55.

***56. Mheshimiwa Spika;*** Ujenzi wa kiwanda kipya cha kuunganisha matrekta umekamilika kwa asilimia 80. Aidha, hadi mwezi Mei 2021, matrekta 764, majembe 511 ya kulimia na majembe 233 ya kusawazisha yameunganishwa na kuuzwa kwa fedha taslimu na kwa njia ya mikopo. Matrekta yaliyoletwa nchini ya aina sita (6) yenye uwezo wa 50HP 2WD, 65HP 2WD, 75HP 2WD, 75HP 4WD, 85HP 2WD na 85HP 4WD. Kwa sasa, Mradi umeajiri wafanyakazi 15. Utekelezaji wa mradi huo umesimama kutokana na matatizo ya Kampuni ya URSUS ya Poland kushindwa kijiendesha. Hali hiyo imesababisha Kampuni hiyo kushindwa kukamilisha Mradi, ambapo kati ya matrekta 2,400 yaliyotakiwa kuletwa nchini, ni matrekta 822 tu yameletwa.

***57. Mheshimiwa Spika;*** Serikali imeunda Timu ya Majadiliano (Government Negotiation Team - GNT) kwa ajili ya kujadiliana na Serikali ya Poland ili kufikia muafaka wa mradi huo. Hatua hiyo ni pamoja na Serikali ya Poland kuteua kampuni nyingine itakayokamilisha Mradi ili lengo la Serikali la kuongeza tija

katika kilimo kwa kutumia zana bora na kuongeza uzalishaji wa malighafi za viwanda litimie. Wakati huo huo, baada ya GNT kukamilisha kazi yake, Serikali inakusudia kuendelea kutoa matrekta na zana bora kwa njia ya mikopo isiyo na riba kwa wakulima kama inavyofanya sasa.

**(vi) *Mradi wa Makaa ya Mawe Katewaka***

***58. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia NDC inakusudia kuanzisha mgodi wa makaa ya mawe katika eneo la Muhumbi lililopo Wilaya ya Ludewa Mkoa wa Njombe kwa kushirikana na Mwekezaji Binafsi. Upembuzi yakinifu na Mpango kazi wa uchimbaji kwa ajili ya Mradi huo umekamilika. NDC inaendelea kufanya majadiliano na mwekezaji ili kukamilisha makubaliano ya utekelezaji wa mradi.

**(vii) *Mradi wa Maganga Matitu Sponge Iron - Ludewa***

***59. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia NDC inalenga kuanzisha mgodi wa chuma na kiwanda cha kufua chuma. Majadiliano na mwekezaji aliyepatikana yanaendelea. Wakati huo huo, mwekezaji huyo amekamilisha uhakiki wa kiwango cha mashapo ambao unaonesha kuwepo kwa tani milioni 103. Wizara inakusudia kutumia taasisi za ndani kuhakiki kiwango cha mashapo kilichooneshwa katika taarifa ya mwekezaji ili mradi uweze kuanza kutekelezwa kwa kuzingatia ripoti ya uhakiki wa mashapo itakayofanywa na taasisi ya ndani.

**(viii) *Mradi wa Makaa ya Mawe – Ngaka***

***60. Mheshimiwa Spika;*** Mradi huo unatekelezwa na Kampuni ya *TANCOAL Energy Limited* ambayo ni ya Ubia kati ya NDC (30%) na *Intra Energy (Tanzania) Limited (70%)*. Mradi ulilenga kuanzisha mgodi wa makaa ya mawe, kituo cha kufua umeme cha Megawati 200 kwa kuanzia hadi kufikia megawati 400 na msongo wa umeme wa Kilovoti 220 kutoka Ngaka mpaka Songea. Hata hivyo, kwa sasa Mradi huo unazalisha makaa ya mawe peke yake. Aidha, Mradi huo umesaidia kutoa kwa uhakika nishati ya makaa ya mawe

kwa viwanda 49 nchini. Pia, Mgodi umeajiri wafanyakazi 500 zikiwemo ajira 191 za kudumu, ajira 228 za muda pamoja na ajira 81 zisizo za moja kwa moja.

***61. Mheshimiwa Spika;*** Mradi huo ulikua na jumla ya leseni za uchimbaji nne (4), ambapo leseni mbili (2) zimeisha muda wake na kurudishwa Wizara ya Madini. Wizara kupitia NDC inaendelea na taratibu za kuomba upya leseni za vitalu hivyo vilivyopo eneo la Mbuyura Mkapa (North Ngaka) ili uchimbaji wa makaa ya mawe uanze kwa kushirikiana na mbia mwingine. Hivi sasa viwanda vya saruji vya Tanga, Dangote na Mbeya vinaendelea kutumia makaa ya mawe ya Ngaka. Hapo awali viwanda hivyo vilikuwa vinaagiza makaa ya mawe kutoka Afrika ya Kusini, Msumbiji na Malawi. Makaa mengine yameuzwa Malawi, Kenya, Uganda, Rwanda na Zambia.

**(ix) *Mradi wa Kongane la Viwanda TAMCO -Kibaha***

***62. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia NDC inaendeleza Kongane la Viwanda la TAMCO lenye ukubwa wa ekari 201 lililopo Kibaha, Mkoa wa Pwani. Eneo hilo limegawanyika katika sekta tatu ambazo ni: Viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba (Pharmaceutical and Medical Facilities Industries); Viwanda vya Kuunganisha Magari na Mitambo (Motor Vehicles and Equipment Assembly); na Viwanda vya Nguo na Mavazi (Textiles and Apparel Industries). Mpaka sasa, kuna viwanda vitatu (3) ambavyo vinafanya uzalishaji ambavyo ni Kiwanda cha Viuadudu (Tanzania Biotech Product Ltd), Kiwanda cha Kuunganisha Magari (*GF Trucks* Assembling Ltd) na Kiwanda cha Chanjo za Wanyama cha *Hester Bioscience Africa*. Serikali inaendelea kuboresha na kujenga miundombinu ya msingi ili kuhakikisha eneo hilo linawavutia wawekezaji zaidi na kuongeza tija katika sekta ya viwanda nchini.

***63. Mheshimiwa Spika;*** Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, viwanda hivyo vimeingizia Serikali zaidi ya Shilingi Bilioni tano (5) ikiwa ni kodi na tozo mbalimbali. Jambo hilo linaashiria kwamba Eneo la TAMCO litakapokuwa limejengwa

viwanda vyote litakuwa na manufaa makubwa ya kiuchumi kwa Taifa.

**Kiwanda cha Kuzalisha Viuadudu vya Kuua Viluilui vya Mbu (Tanzania Biotech Products Ltd - TBPL)**

***64. Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda hicho ambacho kinamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 kilianzishwa kwa lengo la kutokomeza ugonjwa wa malaria hapa nchini. Kiwanda kina uwezo wa kuzalisha lita milioni sita za viuadudu kwa mwaka na kinasimamiwa na kampuni tanzu ya NDC *Tanzania Biotech Products Ltd.* Uzalishaji wa Viuadudu kibiashara ulianza rasmi Januari, 2017 ambapo hadi kufikia Mwezi Aprili 2021, lita 724,000 zilikuwa zimezalishwa. Hadi kufikia mwezi Mei 2021, kiasi cha lita 714,124 kimeuzwa katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Kati ya hizo, lita 319,780 zimeuzwa katika soko la ndani kupitia Halmashauri za Wilaya pamoja na Taasisi mbalimbali na soko la nje lita 394,344 katika nchi za Angola, Niger, Msumbiji na Kenya. Serikali imeziagiza Halmashauri zote nchini kutenga bajeti halisi kwa ajili ya manunuzi ya viuadudu ili kutokomeza Malaria nchini ifikapo 2030. Aidha, Kiwanda kimeanza kuzalisha viatilifu kwa ajili ya mazao ya pamba, mahindi na mbogamboga ambapo uzalishaji wa majaribio lita 600 umekwishafanyika. Bidhaa hiyo iko katika hatua za mwisho za majaribio katika Taasisi ya *Tanzania Agricultural Research Institute* (TARI). Mipango ya baadae ya kiwanda ni kuzalisha bidhaa nyingine kama vile *biofertilizer* na *food suppliments.*

**Kiwanda cha Kuzalisha Vifaa Tiba na Chanjo za Wanyama (*Animal Vaccines)***

***65. Mheshimiwa Spika;*** Kampuni ya *Hester Bioscience Africa* ya India iliingia mkataba na NDC wa upangishaji wa eneo la ujenzi wa kiwanda hicho cha kuzalisha chanjo za wanyama mwaka 2017. Ujenzi wa kiwanda hicho ulianza mwezi Januari 2019 kwa gharama ya Dola za Marekani Milioni 18 sawa na Shilingi Bilioni Arobaini na Moja. Kiwanda kitazalisha ajira za moja kwa moja zipatazo 200 na zisizo za moja kwa moja zaidi

ya 1,000. Kiwanda hicho ni cha kipekee katika Afrika na uzalishaji unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Mei 2021.

**(x) *Mradi wa Mashamba ya Mpira ya Kalunga na Kihuhwi***

***66. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia NDC inamiliki Shamba la Mpira la Kihuhwi lenye ukubwa wa hekta 789.2 lililopo Muheza pamoja na Shamba la Mpira Kalunga lenye ukubwa wa hekta 754.4 lililopo Kilombero. Mashamba hayo ambayo ni sehemu ya Kiwanda cha Matairi Arusha yalihamishiwa rasmi NDC kupitia Tangazo katika Gazeti la Serikali (Government Notice – GN) Na. 266 Toleo Namba 29 la tarehe 17/07/2017. Uzalishaji wa mashamba hayo ni takribani tani thelathini (30) za mpira kwa mwezi wenye thamani ya zaidi ya Shilingi Milion 72. Mpira unaozalishwa unauzwa katika viwanda vya ndani na hasa Kiwanda cha Viatu Bora. NDC ina lengo la kuongeza uzalishaji ili kukidhi mahitaji ya viwanda vya ndani ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba MSD itaweza kupata malighafi ya mpira kwa ajili ya kutengeneza *cloves* na bidhaa nyingine zinazozalishwa. Hii imepunguza kiasi cha mpira uliokuwa unaagizwa nje ya nchi na hivyo kupunguza matumizi ya fedha za kigeni.

***67. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia NDC inaendeleza jitihada za kuboresha mitambo ya kuchakata utomvu, kupanda miti mipya na kuboresha miundombinu ili kuongeza uzalishaji. Usimamizi na uendelezaji wa mashamba umeimarishwa na kufanya uzalishaji kuongezeka kutoka tani 50 mpaka tani 259 kwa mwaka.

***d) Ulinzi wa Viwanda Nchini***

***68. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango imeendelea na juhudi ya kutekeleza hatua za makusudi za kuvikuza, kuviendeleza na kuvilinda viwanda nchini. Wizara imefanya utafiti ili kupata taarifa stahiki zitakazosaidia kufikia maamuzi sahihi wakati wa maandalizi ya Bajeti ya Mwaka 2021/2022 na kuziwasilisha taarifa hizo kwenye Kikosi Kazi cha Maboresho ya Mfumo wa Kodi (Task Force on Tax Reforms). Maeneo yaliyofanyiwa utafiti

ni uzalishaji wa *clinker*, *LABSA,* bidhaa za chuma na mabati, ngozi na bidhaa za ngozi, karatasi na bidhaa za karatasi, magunia ya katani, *leaf springs* na uunganishaji wa trela.

***69. Mheshimiwa Spika;*** Utafiti umeonesha kuwa maombi yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali ambayo yalihusu kuongeza ushuru kwa bidhaa za viwandani zinazoingizwa nchini, utekelezaji wake umekuwa mgumu kwa sasa kwa kuwa viwanda (vilivyotembelewa) vimeonekana vinazalisha chini ya uwezo wake. Jambo hilo linaathiri soko la ndani na hivyo kulazimika kuendelea kuagiza toka nje. Vilevile, Wizara imeendelea kusimamia jitihada za kuvikuza, kuviendeleza na kuvilinda viwanda vya ndani kwa kuendelea kuruhusu kutoza kodi kwa mafuta yanayotoka nje kwa asilimia 10 kwa mafuta ghafi, asilimia 25 kwa mafuta yaliyosafishwa kwa kiwango cha kati na asilimia 35 kwa mafuta yaliyosafishwa hadi kiwango cha mwisho (refined).

***70. Mheshimiwa Spika;*** Katika Sekta ya Bidhaa za Chuma na Mabati, Ngozi na Bidhaa za Ngozi, wadau walipendekeza kuongeza ushuru kwa bidhaa za aina hiyo zinatoka nje ya nchi. Baada ya Tafiti kufanyika ilibainika uzalishaji wa bidhaa hizo ndani ya nchi hautoshelezi mahitaji hivyo ilishauriwa kuendelea kutoza viwango vya ushuru vilivyopo.

***e) Kuhamasisha Uwekezaji wa Sekta Binafsi katika Maeneo Maalum ya EPZ/SEZ***

***71. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Mamlaka ya EPZ imekuwa ikihamasisha uwekezaji katika maeneo maalum ya EPZ/SEZ ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uwekezaji kutoka sekta binafsi. Hadi kufikia Mwezi Machi 2021, miradi 176 imesajiliwa kwenye maeneo ya EPZ/SEZ. Katika kipindi hicho, mitaji iliyowekezwa inakadiriwa kufikia Dola za Marekani Bilioni 2.4719; na ajira za viwandani zinazotarajiwa kuzalishwa ni takriban ajira 58,198 **(Kiambatisho Na. 4)**.

***f) Kuhamasisha Uendelezaji wa Sekta ya Mafuta ya Kula***

***72. Mheshimiwa Spika;*** Mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni takriban tani 570,000 (MT) kwa mwaka wakati uwezo wa

ndani wa uzalishaji ni tani 210,000 (MT) kwa mwaka. Hivyo, kuna uhaba wa tani 365,000 (MT) kwa mwaka unaojaziwa na mafuta yanayoagizwa kutoka nje.

***73. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TANTRADE, SIDO na TBS inaendelea kutoa elimu kwa wasindikaji wa mafuta ya kula katika mikoa yote nchini ili kukidhi viwango vya ubora unaotakiwa kitaifa na kimataifa ili kuhimili ushindani na kuyafikia masoko ya nje. Kwa mwaka 2020/2021, jumla ya wajasiriamali 2,296 walipatiwe mafunzo kuhusu usindikaji wa mafuta ya kula.

***i) Kueneza Falsafa ya KAIZEN Nchini***

***74. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Japan, imekuwa ikitekeleza Mradi wa KAIZEN kwenye Sekta ya Viwanda. Lengo la Mradi huo ni kukuza Sekta ya Viwanda ili kuiwezesha kuongeza mchango wake kwenye Pato la Taifa na ukuaji wa uchumi kwa ujumla. Mradi unahusisha vipengele vinne ambavyo ni Kujenga uwezo wa kitaasisi na kuimarisha muundo wa uratibu wa KAIZEN; Kuandaa wakufunzi wa KAIZEN; Kuwezesha viwanda kufikiwa na huduma za KAIZEN; na Kuweka Mfumo thabiti wa kueneza falsafa ya KAIZEN.

***75. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imefanikiwa kukamilisha Mpango wa Kitaifa wa Uongezaji Endelevu wa Ubora na Tija katika Sekta ya Uzalishaji Viwandani (FKM 2020 – 2030) kupitia program ya KAIZEN na uzinduzi wa FKM 2020 - 2030 na maadhimisho ya siku ya KAIZEN katika Mkoa wa Dodoma, mwezi Agosti 2020. Aidha, mafunzo ya kuoanisha KAIZEN kwenye uendelezaji wa kongano za viwanda yanaendelea kufanyika kwa majaribio katika mikoa ya Dodoma, Kagera, Mbeya na Morogoro ambapo zaidi ya kongano saba (7) zimenufaika.

***76. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kushiriki katika maandalizi ya Mkakati wa Kueneza Falsafa ya KAIZEN Barani Afrika (Africa KAIZEN Annual Conference Initiative Action Plan – AKIAP 2021 – 2025). Inatarajiwa kuwa, Mkakati huo utaweka malengo mapana ya muda mrefu wa kutumia kwa ufanisi rasilimali za Afrika na mbinu bunifu katika kuongeza tija, ubora

na ushindani endelevu wa ukuaji uchumi wa Afrika. Aidha, Mkakati huo utakapokamilika unatarajiwa kuzinduliwa hapa Tanzania mwishoni mwa Mwaka 2021.

***4.1.4. Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo' a) Kuimarisha/Kuboresha Upatikanaji wa Huduma za Kifedha kwa Wajasiriamali***

***77. Mheshimiwa Spika,*** Katika juhudi za kuboresha na kuimarisha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wajasiriamali, Wizara imeongeza kiasi cha Shilingi Bilioni 1.59 ili kutunisha mtaji wa Mfuko wa Kuendeleza Wajasiriamali Wananchi (National Entepreneurship Development Fund - NEDF). Lengo ni kuhakikisha kuwa huduma inayotolewa na Mfuko huo inawafikia wajasiriamali wengi zaidi na kuongeza fursa za ajira na kipato kwa wananchi. Mfuko huo kwa sasa una mtaji uliofikia kiasi cha Shilingi 9,690,398,910 na umeweza kutoa mikopo yenye thamani ya Shilingi 82,635,982,000 kwa wajasiriamali 96,375.

***78. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya mikopo 1,498 yenye thamani ya Shilingi 3,141,700,000 ilitolewa kwa wajasiriamali mbalimbali kote nchini. Kati ya mikopo hiyo, asilimia 47.8 ilitolewa kwa wanawake, asilimia 52.2 ilitolewa kwa wanaume. Aidha, asilimia 30 ilitolewa kwa miradi mbalimbali ya wajasiriamali maeneo ya vijijini. Mikopo hiyo iliwezesha kupatikana kwa ajira 4,295 ambapo asilimia 49.2 ya ajira hizo zilikwenda kwa wanawake. Wizara itaendelea kufanya tathmini za mara kwa mara kuhusiana na uendeshwaji wa Mfuko huo ili kubaini changamoto zinazoukabili na kuchukua hatua kwa lengo la kuboresha huduma zinazotolewa na Mfuko huo.

***b)Kuhamasisha Urasimishaji wa Shughuli za Wajasiriamali Wasio Rasmi***

***79. Mheshimiwa Spika,*** Wizara pamoja na Taasisi zake imeendelea kuhamasisha wajasiriamali wote nchini kusajili/ kurasimisha shughuli zao za kiuchumi kwenye mamlaka husika. Aidha, Wizara imekamilisha ujenzi wa majengo viwanda 15

katika mikoa ya Dodoma, Manyara, Kagera, Mtwara Kigoma na Geita katika maeneo ya SIDO yenye lengo la kupunguza tatizo la upatikanaji wa maeneo rasmi ya kufanyia shughuli za uzalishaji kwa wajasiriamali. Majengo hayo yatahamasisha urasimishaji wa shughuli za wajasiriamali katika maeneo hayo na kurahisisha uwekezaji. Pia, Wizara imeshiriki kwenye uhamasishaji wa utengaji wa maeneo ya kufanyia shughuli za wajasiriamali kwa kila Halmashauri ya Wilaya ambayo yatasaidia kurahisisha urasimishaji wa shughuli za wajasiriamali nchini.

***c) Kuendeleza Mitaa ya Viwanda ya SIDO na Kutengeneza Mfumo Unganishi wa Shughuli za TEHAMA za Shirika***

***80. Mheshimiwa Spika,*** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia SIDO ilipanga kujenga majengo viwanda (industrial sheds) katika mikoa ya Mwanza, Arusha, Dar es Salaam, Katavi, Simiyu, Ruvuma, Singida, Njombe, Shinyanga, Mara, Kigoma na Morogoro. Hadi kufikia mwezi Machi, 2021 ujenzi wa majengo matano (5) ulikuwa umefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo: Mkoa wa Mwanza unajenga jengo moja ambalo lipo katika hatua ya umaliziaji na Mikoa ya Katavi na Morogoro inajenga majengo mawili kila mmoja ambapo ujenzi upo katika hatua ya boma. Kazi ya ujenzi huo inatarajiwa kukamilika ifikapo Juni 2021.

***81. Mheshimiwa Spika,*** Aidha, Wizara kupitia SIDO imeendelea na ujenzi wa miundombinu muhimu (barabara mifumo ya maji, umeme, mitaro ya maji taka na uzio) kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za umma kama TARURA na TANESCO katika mitaa ya viwanda. Katika mwaka 2020/2021, Wizara ilipanga kujenga miundombinu hiyo katika mikoa ya Mbeya, Rukwa, Kagera, Geita, Manyara, Tabora, Simiyu, Pwani, Mtwara, Mara, Kigoma, Shinyanga, Morogoro, Lindi, Mwanza, Tanga na Ruvuma. Hadi kufikia Machi 2021, kazi za ujenzi wa miundombinu zimefanyika katika Mkoa wa Kigoma ambapo ujenzi wa barabara kwa kiwango cha changarawe umekamilika na ujenzi wa mitaro unaendelea. Kwa upande wa Mkoa wa Kagera, ujenzi wa uzio umekamilika na mtaro unaendelea kujengwa na kuwekwa karavati; na Mkoa wa

Geita ujenzi wa uzio, mitaro na barabara unaendelea. Wizara itaendelea kujenga miundombinu muhimu kwa ajili ya mitaa ya viwanda ya SIDO kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha. Kwa upande wa utengenezaji wa Mfumo Unganishi wa Shughuli za TEHAMA za SIDO, kiasi cha Shilingi 300,000,000 kilitumika kwa ajili ya kuunganisha mikoa 10 katika Mkongo wa Taifa na mikoa 10 katika mtandao wa Shirika. Mikoa mitano (5) ya Singida, Shinyanga, Geita, Rukwa na Iringa imeunganishwa na Mkongo wa Taifa pia utekelezaji unaendelea kwa mikoa mingine iliyobaki.

***d) Kujenga Ofisi za Kutolea Huduma katika Mikoa ya Morogoro, Njombe na Songwe***

***82. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na juhudi za kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kujenga Ofisi za SIDO katika mikoa ya Morogoro, Njombe na Songwe**.** Katika mwaka 2020/2021, SIDO imeanisha maeneo ya ujenzi wa majengo husika pamoja na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi (land use plans), michoro ya kihandisi (architectural drawings) na gharama za ujenzi.

***e) Kuimarisha Vituo vya Kuendeleza Teknolojia vya (Technology Development Centres -TDC) vya SIDO***

***83. Mheshimiwa Spika,*** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kwa kushirikiana na SIDO ilipanga kuimarisha Vituo vya Kuendeleza Teknolojia kwa kuweka mashine na mitambo ya kisasa katika kituo cha kuendeleza teknolojia kilichopo katika Mkoa wa Iringa. Mahitaji ya mashine, vipimo (specifications), gharama zake vimeainishwa na taratibu za manunuzi za kumpata mzabuni zimefanyika, tenda imefunguliwa na mkataba unatarajiwa kusainiwa mwezi Mei 2021. Aidha, kwa kutumia mashine/mitambo iliyopo katika vituo saba (7) vya kuendeleza teknolojia (TDCs) vilivyopo katika mikoa ya Arusha, Kigoma, Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, Lindi na Shinyanga, kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya mashine 563 na vipuri 810 viliweza kuzalishwa na kuuzwa kwa wajasiriamali. Vituo hivyo pia vinajihusisha na uendelezaji wa teknolojia na kutoa huduma za kiufundi kwa wajasiriamali

wadogo na kati wa mjini na vijijini kwa kuzingatia Mkakati wa Wilaya Moja Bidhaa Moja na fursa zinazojitokeza katika maeneo yao.

***f) Kutoa Mafunzo ya Ujasiriamali na Usimamizi wa Biashara***

***84. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia SIDO hutoa mafunzo ya ujasiriamali yanayolenga kutoa ujuzi maalum wa kiufundi katika uzalishaji mali kama vile usindikaji wa vyakula, ngozi, chaki, ubanguaji korosho, vyakula vya mifugo, mianzi, ufinyanzi na vibuyu. Aidha, mafunzo mengine yanayotolewa hulenga kujenga na kuimarisha mbinu za kibiashara na uendeshaji wa miradi ya kiuchumi kwa walengwa hasa menejimenti, masoko, ubora wa bidhaa, mbinu za uzalishaji mali, utunzaji wa vitabu na mafunzo ya mashine, uongozi wa vikundi/vyama hutolewa. Katika Mwaka 2020/2021, jumla ya kozi 576 ziliendeshwa mikoani kote na kuhusisha jumla ya wajasiriamali 17,494.

***g) Kutambua/Kutafuta/Kutengeneza na Kusambaza Teknolojia Mpya kwa Ajili ya Matumizi ya Viwanda Vidogo na vya Kati***

***85. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia SIDO imeendelea kutambua/kutafuta/kutengeneza na kusambaza teknolojia mpya kwa ajili ya matumizi ya viwanda vidogo na vya kati. Hii imesaidia matumizi ya teknolojia muafaka, kuongeza ufanisi, tija na kuhakikisha kuwa bidhaa zinazozalishwa zinakuwa na viwango na ubora unaotakiwa. Kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi 2021, jumla ya teknolojia 73 zilitambuliwa na kusambazwa katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Katavi, Kilimanjaro, Morogoro, Mbeya, Mtwara, Mwanza, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Singida, Tabora na Tanga. Mashine na zana hizo ziliwezesha kuanzishwa na kuimarisha shughuli za viwanda na miradi ya uzalishaji kwa wajasiriamali. Teknolojia zilizotambuliwa na kusambazwa zinahusu usindikaji wa vyakula, ufungashaji wa vyakula vilivyosindikwa, utengenezaji wa vifaa vya ujenzi hasa matofali, utengenezaji wa chokaa, chaki na batiki, utengenezaji wa sabuni, mashine za kupasulia miamba ya mawe (Stone crusher processing machine) pamoja na

mashine za uchambuzi na upangaji mazao (sorting and grading machine).

### *h) Kuendeleza Ubunifu wa Teknolojia na Mawazo ya Bidhaa Mpya Chini ya Programu ya Kiatamizi*

***86. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia SIDO huwasaidia wajasiriamali wenye ubunifu wa teknolojia na mawazo ya bidhaa mpya kwa kuwaendeleza kwa kuwapatia huduma mbalimbali kama vile maeneo ya kufanyia kazi, ushauri wa kiufundi na mitaji ili wakue na kufikia viwango vya kujitegemea. Katika kipindi cha Julai 2020, hadi Machi 2021, jumla ya teknolojia na mawazo ya bidhaa 13 yalihudumiwa katika mikoa ya Mtwara, Singida, Dar es Salaam, Mwanza na Morogoro. Miongoni mwa teknolojia hizo zilihusu kutengeneza kuni/mkaa kutokana na pumba za mpunga (rice husk briquettes machine), utengenezaji juice (concentrated juice making machine), bidhaa za nyama, bidhaa za matangazo na mapambo (branding products), *fencing wire,* uchakataji bidhaa za mafuta ya nazi na korosho pamoja na teknolojia za vichochezi katika mabwawa ya samaki, majiko ya kupikia (stove cooker) na utengenezaji wa bidhaa za kiutamaduni (cultural products).

### *i) Kutoa Mafunzo na Huduma za Ugani kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati*

***87. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia SIDO hutoa huduma za ushauri na ugani kwa wajasiriamali katika nyanja za ufundi, uchumi, uongozi, masoko, ubora wa bidhaa, teknolojia, kubuni, kusanifu na kutayarisha uchambuzi yakinifu wa miradi ya viwanda na biashara kwa vikundi/vyama vya wajasiriamali ukiwa unalenga kuviimarisha na kuviwezesha kujenga msingi wa kujitegemea katika sekta ya viwanda na biashara ndogo. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 jumla ya wajasiriamali wahitaji 11,789 walipatiwa huduma za ushauri katika maeneo mbalimbali yanayohusiana na uendelezaji wa biashara na shughuli za uzalishaji.

### *4.1.5. Sekta ya Biashara*

**Kuendeleza kutafuta fursa nafuu za biashara kati ya Nchi na Nchi (Bilateral), Kikanda (Regional) na Kimataifa (Multilateral)**

***a) Majadiliano ya Fursa Mbalimbali za Masoko Baina ya Nchi na Nchi***

***88. Mheshimiwa Spika;*** Katika kuimarisha mahusiano ya kibiashara baina ya nchi na nchi pamoja na kutafuta fursa nafuu za biashara na masoko ya uhakika, Wizara ilifanikiwa kuanzisha majadiliano ya Hati za Makubaliano (Memorundum of Undrestanding-MOU) na nchi mbalimbali za kimkakati ambazo ni pamoja na nchi za Afrika Kusini, Namibia, Angola, Urusi, Burundi, Madagascar na Mauritius. Kukamilika kwa hati hizo za makubaliano kutasaidia katika kupanua wigo wa masoko ya uhakika kwa kuondoa vikwazo vya kibiashara visivyokuwa vya kiushuru, kuimarisha ushirikiano kwenye maeneo ya biashara, viwanda na SMEs na hivyo kukuza biashara kati ya Tanzania na mataifa hayo.

***b) Majadiliano ya Fursa Mbalimbali za Masoko Kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki***

***89. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeshiriki katika zoezi la kuboresha na kukuza biashara ya huduma nchini na ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye sekta saba za kipaumbele ambazo ni Elimu, Usambazaji, Uchukuzi, Utalii, Mawasiliano, Fedha na sekta ya Huduma za Biashara. Kupitia zoezi hilo, Wizara kwa kushirikiana na Sekretariati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imefanikiwa kubainisha vikwazo vya kisheria, kanuni na taratibu vinavyozuia ufanyaji biashara ya huduma na watoa huduma, pamoja na kuandaa mfumo wa kuondoa vikwazo hivyo kwenye sekta husika. Katika kufanikisha utekelezaji huo, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeanzisha Kamati ya Kikanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ajili ya kuratibu biashara ya huduma.

***90.***

***Mheshimiwa Spika;*** Katika kuwezesha na kukuza biashara ya bidhaa nchini na ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wizara kwa kushirikiana na Sekretarieti ya EAC imeendelea na

uondoaji wa Vikwazo vya Biashara Visivyokuwa vya Kiushuru (NTBs). Katika mwaka 2020/2021, jumla ya NTBs 10 ziliondolewa. Aidha, vikwazo 17 ambavyo havijaondolewa vipo kwenye hatua mbalimbali za utatuzi.

***91. Mheshimiwa Spika;*** Kupitia Kamati ya Kitaifa ya Kushughulikia Vikwazo vya Biashara Visivyokuwa vya Kiushuru, Wizara ilishirikiana na sekta binafsi kuandaa mafunzo kwa wadau wa Zanzibar (Unguja na Pemba) yaliyofanyika mwezi Septemba 2020. Mafunzo hayo pia yalifanyika katika Kanda ya Kaskazini Manispaa ya Moshi, Arusha na mipaka ya Holili, Tarakea na Namanga mwezi Desemba, 2020. Mafunzo hayo yalikuwa na lengo la kuwawezesha wadau ikiwa ni pamoja na watendaji wa taasisi za umma na wafanyabiashara kuelewa maana ya vikwazo (NTBs) na jinsi ya kutoa taarifa mara wanapokutana na vikwazo hivyo katika kusafirisha bidhaa zao hapa nchini na nje ya mipaka ya Tanzania. Wadau walielimishwa jinsi ya kutoa taarifa kwa njia ya ujumbe mfupi (SMS), kupitia Kamati ya NMC, barua pepe kwa mratibu au kuorodhesha katika mfumo wa kieletroniki (Online Mechanism) wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wadau takriban 150 walipatiwa mafunzo hayo kwa lengo la kuwajengea uelewa wa NTBs na madhara yake, kuepuka kusababisha vikwazo na kutoa taarifa ya vikwazo wanavyokumbana navyo.

***92. Mheshimiwa Spika;*** Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Pamoja wa Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa inayopakana na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kujadili changamoto za biashara katika mipaka ya Tanzania na nchi za Kenya na Rwanda uliofanyika kuanzia tarehe 27-30 Juni, 2020 jijini Arusha. Kupitia mkutano huo, nchi za Tanzania, Kenya na Rwanda zilikubaliana hatua za kufuata ili kupitisha mizigo hususan kwa madereva na malori.

***93. Mheshimiwa Spika;*** Wizara iliratibu na kushiriki kwenye kikao cha maandalizi na kikao cha majadiliano ya kuanzishwa kwa Mkataba wa Biashara kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Uingereza. Kikao hicho kiliangalia na

kujadili namna bora ya kuanza kwa majadiliano ya Mkataba wa Biashara hasa ukizingatia kwamba Uingereza imejitoa rasmi katika Umoja wa Ulaya tarehe 1 Januari, 2021. Katika Kikao cha Ngazi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Ngazi ya EAC na UK, nchi za EAC isipokuwa Kenya ziliomba kupelekwa mbele kwa majadiliano hayo ili ziweze kupata muda wa kufanya mashauriano zaidi na kujiandaa na majadiliano husika.

***94. Mheshimiwa Spika;*** Sekretarieti ya EAC ilitakiwa kuandaa pendekezo kwenda Uingereza kwa ajili ya kuahirisha muda wa majadiliano kwa mwaka mmoja. Vilevile, Maafisa Waandamizi wa EAC walitakiwa kuwashirikisha Maafisa wa Uingereza kuandaa utaratibu wa mpito ili kuwezesha nchi ya Kenya kulifikia soko la Uingereza kwa masharti ya upendeleo baada ya tarehe 31 Desemba, 2020. Ili kujiandaa na majadiliano hayo, Wizara imeunda Kikosi Kazi cha Kitaifa cha Majadiliano ambacho kitafanya uchambuzi na kuainisha faida na hasara ambazo nchi inaweza kuzipata katika Mkataba husika.

***c) Majadiliano ya Fursa Mbalimbali za Masoko katika Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA)***

***95. Mheshimiwa Spika,*** Katika kutafuta fursa nafuu za biashara na masoko ya uhakika ya Kikanda, Wizara inaendelea kukamilisha majadiliano ya Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA) lenye watu takribani bilioni 1.3. Mkataba huo unajumuisha Itifaki ya Biashara ya Bidhaa, Biashara ya Huduma, Ushindani, Uwekezaji na Itifaki ya Utatuzi wa Migogoro. Hadi kufikia Desemba 2020, Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika kupitia Mkutano wa Dharura wa 13 ulipitisha Maazimio ya Kisera na Kisheria kuwezesha kuanza kwa biashara chini ya Mkataba wa AfCFTA tarehe 1 Januari, 2021. Soko hilo litafungua fursa za biashara ya bidhaa na huduma kwa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika. Sekta tano (5) za kipaumbele kwenye Biashara ya Huduma ni pamoja na Sekta ya Biashara, Fedha, Mawasiliano, Utalii na Uchukuzi. Aidha, Tanzania inaendelea kukamilisha taratibu

za ndani kwa ajili ya kuridhia utekelezaji wa Mkataba huo ili kunufaika na fursa zilizopo kwenye Mkataba huo.

***d)Majadiliano ya Fursa Mbalimbali za Masoko katika Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC)***

***96. Mheshimiwa Spika,*** Katika kuboresha mazingira ya biashara ndani ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), Tanzania kupitia SADC inaendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa kuanzisha Mfumo wa Uombaji na Utoaji Vyeti vya Utambuzi wa Uasili wa Bidhaa kwa Njia ya Mtandao (e-certificate on Rules of Origin - RoO). Mfumo huo, uliidhinishwa katika Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC. Aidha, Mfumo huo utaanza kwa kushirikisha nchi sita (6) ambazo ni Botswana, Eswatini, Malawi, Namibia, Tanzania na Zambia na utarahisisha ufanyaji biashara mipakani hususan kwa wafanyabiashara wadogo. Sambamba na hilo, Sekretarieti ya SADC imeanzisha *SADC Business Directory* ambayo inasaidia kutoa taarifa za ufanyaji biashara, kutoa fursa kwa wafanyabiashara na makampuni mbalimbali kutoka nchi wanachama kujitangaza ndani ya SADC.

***97. Mheshimiwa Spika,*** Majadiliano ya awamu ya pili kwenye Biashara ya Huduma yatahusisha sekta sita (6) zilizobakia ambazo ni Sekta ya Huduma za Biashara, Elimu, Afya, Usambazaji, Mazingira na Burudani, Utamaduni na Michezo. Sekta hizo zilikubaliwa na Mkutano wa 40 wa SADC wa *Trade Negotiating ForumService* uliofanyika Mwezi Oktoba 2020.

***98. Mheshimiwa Spika;*** Kupitia Mpango Mkakati wa Maendeleo wa Kanda 2020 – 2030 (Regional Indicative Strategic Development Plan - RISDP 202- -2030) wa SADC, Tanzania imeweza kutumia mwongozo huo katika mipango na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na mikakati ya kisekta hususan maandalizi ya Sera ya Biashara, Viwanda na Viwanda Vidogo. Aidha, Mkakati huo unawezesha kuwa na maandalizi yanayoanzia katika sekta ya chini kabisa ya wazalishaji hadi kufikia sekta ya juu

kabisa ya uzalishaji ambao unazingatia viwango na ubora wa kikanda na kimataifa.

***99. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Mkutano wa Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi ulioandaliwa na kuratibiwa na Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi zinazopakana na Bahari ya Hindi (IORA) umeweza kuwasaidia wanawake wajasiriamali namna ambavyo wanaweza kufufua biashara na uchumi wao kufuatia athari za mlipuko wa virusi vya Korona katika Kanda, ikiwa ni pamoja na namna ya kukabiliana na janga hilo.

***e) Majadiliano ya Fursa Mbalimbali za Masoko katika Eneo Huru la Biashara la Utatu (COMESAEAC NA SADC)***

***100. Mheshimiwa Spika;*** Katika kuimarisha mahusiano ya kibiashara kikanda na kutafuta fursa za masoko nafuu, Serikali ipo mbioni kukamilisha uchambuzi kwa ajili ya kujiunga na Eneo Huru la Biashara la Utatu (COMESA-EAC NA SADC). Tarehe 8 Januari, 2021 Wizara iliwasilisha rasimu ya Waraka wa kuridhia Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Utatu (COMESA, EAC na SADC) Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri (CS) ukajadiliwa na kutolewa maoni/mapendekezo ambayo yanaendelea kufanyiwa kazi kwa kushirikiana na wadau.

***101. Mheshimiwa Spika***; Mkataba ambao ulisainiwa na nchi 22 kati ya nchi 26 ikiwemo Tanzania unaweza kuanza kutekelezwa endapo utaridhiwa na nchi kumi na nne (14). Mpaka sasa nchi kumi (10) tayari zimeridhia Mkataba huo ambazo ni: Afrika Kusini, Botswana, Burundi, Eswatini, Kenya, Misri, Namibia, Rwanda, Uganda na Zambia. Aidha, Mkataba huo unatakiwa uwe umeridhiwa ifikapo Juni 2021. Faida ya kujiunga na Jumuiya hiyo kubwa kwanza ni kuongeza wigo wa masoko ya bidhaa zetu hususan zile zinazotokana na kilimo, kuongezeka kwa uzalishaji pamoja na kutoa ajira kwa Watanzania walio wengi.

***f) Majadiliano ya Fursa Mbalimbali za Masoko katika Nchi za Afrika, Karibeani na Pasifiki (ACP) na Umoja wa Ulaya (EU)***

***102. Mheshimiwa Spika;*** Katika kuhakikisha kuwa, biashara kati ya nchi za Afrika, Karibeani na Pasifiki (ACP) na Umoja wa Ulaya (EU) inaendelea kufanyika, Wizara ilishiriki kwenye majadiliano ya Mkataba mpya wa ubia wa ushirikiano kati ya nchi za ACP na EU. Majadiliano ya Mkataba huo yalianza kwa kuwa Mkataba wa awali (Cotonou Agreement) ulikuwa ufikie ukomo tarehe 31 Desemba, 2020. Hata hivyo, Mkataba huo uliongezwa muda hadi tarehe 30 Novemba 2021 ili kutoa muda wa kutosha kukamilisha majadiliano ya Mkataba mpya. Aidha, majadiliano ya Mkataba mpya yamekwishakamilika na Mkataba huo mpya ulitiwa saini (initialing) tarehe 15 Aprili 2021. Mkataba mpya umejumuisha masuala yote muhimu ya ushirikiano ikiwa ni pamoja na masuala ya biashara, uchumi na siasa.

***g)Majadiliano ya Fursa Mbalimbali za Masoko Kimataifa***

***103. Mheshimiwa Spika;*** Katika kulinda rasilimali za bahari, hususan samaki, Wizara imeshiriki katika Majadiliano ya Mkataba wa Kudhibiti Ruzuku kwenye Sekta ya Uvuvi katika Shirika la Biashara Duniani (WTO Fisheries Subsidies Agreement). Mkataba huo ni kwa ajili ya kudhibiti uvuvi usiotolewa taarifa na kuratibiwa/kusimamiwa (Illegal, Unregulated and Unreported (IUU) Fishing); Uwezo Uliopita Kiasi na Uvuvi uliopitiliza (Overcapacity and Overfishing); na Uvuvi wa Samaki Walio Hatarini Kupotea (Over Fished Stocks). Majadiliano hayo yalitarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2020 lakini kutokana na uwepo wa vipengele ambavyo nchi wanachama zinatofautiana mitazamo, majadiliano yanaendelea. Mkataba huo ukikamilika, utasaidia kupunguza Uvamizi wa Uvuvi katika Maeneo ya Nchi Wanachama (Exclusive Economic Zones - EEZ) na kutachangia kupunguza uvuvi haramu baharini hasa unaofanywa na wavuvi wakubwa kutoka mataifa yanayotoa ruzuku.

***104. Mheshimiwa Spika;*** Katika kuendelea kulinda maslahi ya nchi, Wizara kwa kushirikiana na Ubalozi wetu uliopo Uswisi

Geneva, imeshiriki kikamilifu katika majadiliano yanayoendelea ndani ya Shirika la Biashara Duniani yanayohusu pendekezo la kukataza nchi wanachama kuweka vikwazo au vizuizi kwenye manunuzi ya chakula yanayofanywa na Programu ya Umoja wa Mataifa ya Chakula Duniani (World Food Programme). Msimamo ambao tumeendelea kusimamia ni ule wa kuhakikisha kuwa manunuzi hayo yanayofuata taratibu za ndani ya nchi husika na kwamba kwa namna yoyote ile yasiathiri usalama wa chakula nchini. Mataifa yaliyoendelea na yanayoendelea yanapinga msimamo huu, kwani wao wanataka manunuzi ya WFP yasiwekewe vikwazo vyovyote. Tanzania bado imeendelea kusimamia msimamo wake kwa sababu sera ya kuzuia mauzo ya mazao ya chakula ni muhimu na inatumiwa na nchi kadhaa, hususan nchi zinazoendelea kwa ajili ya kulinda usalama wa chakula na pia katika kuhakikisha mazao yanaongezwa thamani ndani ya nchi kabla ya kuuzwa nje kwa lengo la kuongeza ajira katika mnyororo wa thamani.

***105. Mheshimiwa Spika;*** Katika utafutaji wa vyanzo mbadala vya fedha, Wizara ipo kwenye hatua za mwisho za majadiliano na Sekreterieti ya COMESA kuhusu utekelezaji wa programu za COMESA za Uwezeshaji Biashara (Trade Facilitation) na Masoko ya Mipakani (Small Cross Border Markets). Programu hizo zinafadhiliwa na Umoja wa Ulaya kupitia Mfuko wa Umoja wa Ulaya wa Maendeleo (European Development Fund - EDF 11). Programu hizo zinatekelezwa katika mipaka mbalimbali ya nchi za COMESA na mipaka ya nchi zilizoko katika Kanda ya Utatu (Tripartite) inayojumuisha SADC-EAC-COMESA.

***106. Mheshimiwa Spika;*** Kupitia Programu hizo, Tanzania itanufaika kupitia mpaka wa Tunduma/Nakonde ambao unaunganisha Tanzania na Zambia. Kwa upande wa Programu ya Uwezeshaji Biashara, majadiliano yako katika hatua nzuri. Tunategemea kupata ufadhili wa utekelezaji wa shughuli zenye kiasi cha Dola za Marekani 2,220,670 katika mpaka wa Tunduma. Aidha, kwa upande wa Programu ya Masoko ya Mipakani, majadiliano bado yanaendelea na kazi kubwa itakuwa ni ujenzi wa soko la wajasiriamali katika eneo

la Majengo, Tunduma. Majadiliano hayo yanafanyika kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji wa Tunduma.

***107. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na Kituo cha Biashara cha Kimataifa (International Trade Centre – ITC) imefanya utafiti wa pili wa Vikwazo vya Biashara Visivyo vya Kiushuru (NonTariff Measures Survey). Dhumuni kuu la tafiti hizo ni kubaini changamoto zisizo za kiushuru zinazowakabili wafanyabiashara wanapouza nje na ndani ya nchi pamoja na juhudi zilizofanywa na Serikali katika kutatua changamoto hizo. Tafiti hizo hufanywa kwa kufanya majadiliano na makampuni na wafanyabiashara wengine katika Sekta Binafsi. Hivyo, tafiti hizo hubeba mtazamo wa Sekta Binafsi (Business Perspectives). Kikao cha wadau cha kuboresha utafiti huo kilifanyika tarehe 10 -11 Machi, 2021 Dar es Salaam ambapo maoni na mapendekezo kadhaa yalitolewa.

***108. Mheshimiwa Spika;*** Uelewa mzuri wa mtazamo wa wafanyabiashara kuhusu NTMs ni muhimu kwa Serikali kwani husaidia Serikali kujua vikwazo ambavyo wafanyabiashara wake wanakumbana navyo wakati wa kufanya biashara ndani na nje ya nchi na kuweka mikakati thabiti ya kuzishughulikia. Utafiti huo, pia hutoa fursa kwa Serikali kufafanua mikakati na sera zake na namna zinavyosaidia katika kuondoa vikwazo vya kibiashara visivyo vya kiushuru.

***109. Mheshimiwa Spika;*** Kutokana na umuhimu wa masuala ya uwezeshaji biashara nchini na kikanda, Wizara ilifanya maandalizi na hatimaye kushiriki kwenye mkutano wa Kamati Ndogo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Uwezeshaji Biashara (EAC SubCommittee on Trade Facilitation) uliofanyika tarehe 2021 Aprili, 2021 kwa njia ya mtandao. Katika mkutano huo, nchi wanachama zilikubaliana masuala kadhaa ya uwezeshaji biashara ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na urahisishaji wa hatua na taratibu (simplification of processes) za ufanyaji wa biashara pamoja na kuendelea kuboresha mifumo ya taarifa za biashara.

***110. Mheshimiwa Spika;*** Kwa kuzingatia kuwa dunia kwa sasa inahamia kwenye ufanyaji biashara kwa njia ya kielektroniki

na hali hiyo inachagizwa na maendeleo makubwa na ya haraka ya TEHAMA yanayoendelea kutokea duniani, Wizara kwa kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (United Nations Conference on Trade and Development - UNCTAD) ilifanya tathmini za utayari wa ufanyaji biashara kwa njia ya kieletroniki. Tathmini hizo kwa kiasi kikubwa zimesaidia katika kujua uwezo (strength) na mapungufu/ changamoto zilizopo pamoja na mapendekezo ya kisera na ya kimkakati ambayo nchi inapaswa kuzingatia ili kuweza kushiriki kikamilifu na kunufaika na ufanyaji biashara kwa njia ya mtandao (e-commerce).

***111. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Kamati ya Kitaifa ya Uwezeshaji biashara, iliandaa na kushiriki kwenye Kikao cha Kamati ya Uongozi ya Uwezeshaji Biashara (NCTF Steering Committee). Kupitia kikao hicho, masuala mbalimbali yalijadiliwa na kufanyiwa maamuzi ikiwa ni pamoja na kuidhinisha Hadidu za Rejea (TORs) za Kamati ya Kitaifa ya Uwezeshaji Biashara, Kuidhinisha Mpango Mwelekeo (Roadmap) wa Miaka Mitano (2020/21-2024/25) na Kuidhinisha Maeneo ya Kundi A, B na C ya utekelezaji wa Mkataba wa Uwezeshaji Biashara wa Shirika la Biashara Duniani (WTO TFA) ambayo baada ya kupata idhini yaliwasilishwa Sekretariati ya WTO Septemba 2020.

***112. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (United Nations Conference on Trade and Development - UNCTAD) ilifanikiwa kuanzisha Mfumo wa Utoaji Taarifa za Biashara Mtandaoni (Trade Information Module) unaowawezesha wafanyabiashara kujua taratibu za kuingiza bidhaa nchini, kuuza bidhaa nje ya nchi, nyaraka zinazohitajika, zinakopatikana nyaraka na kwa muda wa kupatikana. Hii imewasaidia wafanyabiashara kuwa na taarifa za awali na kufanya maamuzi sahihi bila kupoteza muda mwingi. Mfumo huo kwa sasa unaratibiwa na BRELA na unakusudiwa kuhamishiwa Taasisi ya TanTrade.

***113. Mheshimiwa Spika;*** Katika kutumia Mfumo huo, wafanyabiashara na wadau wanaweza kuona kwa uwazi

Taasisi husika inayotoa leseni au kibali, muda atakaotumia kupata leseni na vibali, nyaraka za kuwasilisha, gharama na sheria zinazosimia taratibu husika. Aidha, Mfumo unatoa fursa kwa mfanyabiashara kuwasilisha malalamiko na maoni pindi anapokuwa hajaridhika na huduma iliyotolewa kwa kupitia mawasiliano ya Taasisi husika yaliyoainishwa kwenye mfumo. Hatua inayofuata ni uzinduzi wa Mfumo huo kuufanya rasmi kwani ndiyo Mfumo unaotembelewa zaidi kuliko mifumo mingine kama hiyo ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**h)** ***Kuimarisha na Kuweka Uhakika Fursa za Biashara Kimataifa na Kupata Misaada ya Kifedha na Kiufundi***

***114. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kushiriki kwenye majadiliano yanayoendelea ya biashara ya kimataifa katika Shirika la Biashara Duniani (WTO). Majadiliano yanayoendelea hivi sasa yanafahamika kama majadiliano ya Duru la Maendeleo la Doha (Doha Development Agenda-DDA). Majadiliano ya DDA yanalenga kufikia makubaliano yanayozingatia maslahi, hususan ya nchi zinazoendelea na nchi maskini ikiwemo Tanzania. Katika majadiliano hayo yanayofanyika kila siku katika Shirika hilo, Tanzania huwakilishwa na Ubalozi wake wa kudumu ulioko mjini Geneva, Uswisi. Pamoja na Ubalozi, washiriki kutoka nyumbani (capital based officials) huhudhuria baadhi ya mikutano ambayo mara nyingi huhitaji ujuzi maalum. Kupitia majadiliano hayo fursa kadhaa hupatikana katika biashara ya kimataifa.

***115. Mheshimiwa Spika;*** Wizara na wadau wengine nchini wameendelea kufaidika na fursa mbalimbali za kujenga uwezo wa uchambuzi wa masuala ya kibiashara. Fursa hizo ni pamoja na kushiriki mafunzo yanayofadhiliwa na WTO kila mwaka. Mafunzo hayo ni kama vile: Mafunzo ya sera za biashara kikanda (Regional Trade Policy) ngazi ya Diploma; Mafunzo ya Diploma ya Juu ya Sera za Biashara (Advanced Trade Policy Course); na Mafunzo katika maeneo maalum (specialized courses) yanayofanyika kwa njia ya mtandao (online courses). Mafunzo mengine yanayoendeshwa na WTO ni yale ya vitendo kwa muda mrefu (Internships). Mafunzo

hayo yamekuwa na manufaa makubwa katika kuwajengea uwezo na ujuzi kwa wataalam wetu.

***116. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia WTO imekuwa pia ikipata msaada wa kifedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali nchini. Kwa mwaka 2020/2021, Wizara imepata ufadhili wa kiasi cha Dola za Marekani Milioni 2.6 kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Kuwajengea Uwezo Wajasiriamali Wadogo na wa Kati (Strengthen MSMEs Capacity to Improve Competitiveness in Domestic, Regional and International Markets for Selected Value Chains). Lengo la Mradi huo ni kuwawezesha wajasiriamali kushiriki kikamilifu katika soko la ndani, kikanda na kimataifa. Mradi huo unatekelezwa katika pande zote za Muungano (Bara na Zanzibar) na umelenga wajasiriamali wanaojishughulisha katika mnyororo wa thamani (value chains) katika bidhaa za asali, mbogamboga (Horticulture) na mafuta ya mawese (Palm Oil) kwa upande wa Tanzania Bara na dagaa aina ya *Anchovies* na mwani (Seaweed) kwa upande wa Zanzibar. Kupitia Mradi huo, wajasiriamali watapewa mafunzo na mashine za kuchakata bidhaa wanazozalisha.

***117. Mheshimiwa Spika;*** Tanzania inaendelea kufaidika na fursa za upendeleo maalum wa biashara (preferential market access) kutokana na majadiliano ya biashara ya kimataifa kupitia Shirika la Biashara Duniani (World Trade Organization – WTO). Fursa hizo za upendeleo hutolewa kwa nchi zilizo katika kundi la nchi zinazoendelea na LDCs ambazo ni wanachama wa WTO. Bidhaa kutoka nchi zinazoendelea huingia katika masoko ya nchi zilizoendelea na baadhi ya zinazoendelea bila kutozwa ushuru wa forodha na wala kuwekewa ukomo wa kiasi cha kuuza *(Duty Free Quota Free market access– DFQF)* au kuwekewa tozo ndogo za ushuru wa forodha.

***118. Mheshimiwa Spika;*** Tanzania imeendelea kunufaika na Mpango wa AGOA kwa kuruhusiwa kupeleka zaidi ya bidhaa 6,400 bila kulipa ushuru wa forodha. Aidha, katika kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa AGOA (AGOA National stratergy), Wizara inaendelea kuhamisisha wafanyabiashara wa

Tanzania kuweza kutumia ipasavyo fursa ya soko la AGOA ili kukuza mauzo ya bidhaa zetu, kuongeza fedha za kigeni, kuchochea ukuaji wa viwanda pamoja na kukuza ajira nchini.

**i) *Mwenendo wa Biashara Baina ya Nchi na Nchi, Kikanda na Kimataifa.***

***119. Mheshimiwa Spika*;** Mauzo ya bidhaa kwenye masoko ya upendeleo ya **China** yaliongezeka kutoka Dola za Marekani Milioni 233.60 mwaka 2019 hadi Dola za Marekani Milioni 238.80 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 2.2. Ongezeko hilo linatokana na uzalishaji na uuzaji kwa wingi mbegu za ufuta. Bidhaa zingine zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na tumbaku, pamba, *jute*, *manila* (coconut, abaca) na nguo na mavazi. Manunuzi ya Tanzania kutoka China yalikuwa Dola za Marekani Milioni 1,987.60 mwaka 2019 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 2,155.80 mwaka 2020, sawa na asilimia 8.5. Ongezeko hilo limetokana na uagizaji kwa wingi bidhaa zenye thamani kubwa ambazo zinatumika katika uzalishaji na ujenzi wa miundombinu. Bidhaa hizo ni matrekta, matairi ya magari, *gas oil* na vifaa vinavyotumika katika ujenzi wa reli (tramway track construction material of iron and steel). Urari wa biashara unaonesha nakisi ya Dola za Marekani Milioni 1,917.00. (**Kiambatisho Na. 5**)

***120. Mheshimiwa Spika*;** Mauzo katika Soko la **India** yalipungua kutoka Dola za Marekani Milioni 867.70 mwaka 2019 hadi Dola za Marekani Milioni 528.60 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 39.1. Upungufu huo ulitokana na kupungua kwa uuzaji wa bidhaa za maua, kahawa, alizeti, madini na ufuta. Bidhaa zilizoongozwa kuuzwa kwa wingi mwaka 2020 ni korosho na mbaazi. Aidha, manunuzi ya Tanzania kutoka India yalipungua kutoka Dola za Marekani Milioni 1,258.40 mwaka 2019 hadi Dola za Marekani Milioni 1,089.50 mwaka 2020, sawa na asilimia 13.4. Kupungua kwa biashara baini ya nchi hizo mbili kumeathiriwa na uwepo wa janga la ugonjwa wa Covid-19 duniani. Pamoja na upungufu huo wa biashara, urari wa biashara unaonesha nakisi ya Dola za Marekani Milioni 560.90. (**Kiambatisho Na. 6**).

***121. Mheshimiwa Spika***; Mauzo katika soko la **Japan** yalipungua kutoka Dola za Marekani Milioni 64.10 mwaka 2019 hadi Dola za Marekani Milioni 55.80 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 12.9. Manunuzi ya bidhaa kutoka Japan yalikuwa na thamani ya Dola za Marekani Milioni 485.10 mwaka 2019 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 375.90 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 22.5. Bidhaa zilizoagizwa kwa wingi ni zile zinazotumika kwenye uzalishaji viwandani kama vile mashine, mitambo na kemikali. Urari wa biashara umeonesha nakisi ya Dola za Marekani Milioni 320.10. (**Kiambatisho Na. 7**)

### j) JUMUIYA YA UMOJA WA ULAYA- EU

***122. Mheshimiwa Spika***; Bidhaa zilizonunuliwa na Tanzania kutoka Jumuiya ya Ulaya zilikuwa na thamani ya Dola za Marekani milioni 909.01 mwaka 2019 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 1029.00 kwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 13.2. Bidhaa zilizoagizwa kwa wingi ni pamoja na; vifaa vya mitambo, mashine mbalimbali, vipuri vya magari, magari, nguo, vyombo vya majini (marine vessels), gesi na mafuta, vifaa vya madawa (medical apparatus), *paper board, fittings, gas tubes, mineral/ chemical fertilizers, data processing machines,* vifaa vya mawasiliano na vifaa vya uchunguzi wa kimaabara. Pia, mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Jumuiya ya Ulaya yaliongezeka kutoka Dola za Marekani Milioni 399.30 kwa mwaka 2019 hadi kufikia Dola za Marekani Milioni 605.20 mwaka 2020, ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 34. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni bidhaa za tumbaku, madini, kahawa, maharage ya soya, alizeti, pamba na maua. Kutokana na hali hiyo urari wa biashara umeonesha nakisi ya Dola za Marekani Milioni 423.80. Nakisi hiyo inatokana na Tanzania kuuza zaidi malighafi katika soko la Jumuiya ya Ulaya wakati Tanzania inaagiza bidhaa za viwandani (finished products). (**Kiambatisho Na. 8**)

***123. Mheshimiwa Spika***; Mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda **Marekani** kupitia Mpango wa AGOA kwa mwaka 2019 yaliongezeka na kufikia Dola za Marekani Milioni 51,971

ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 42,432 kwa mwaka 2018. Mauzo hayo kwa kiasi kikubwa yalichangiwa na Sekta ya Nguo na Mavazi. Aidha, ili kuongeza mauzo zaidi katika soko hilo, Wizara imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza Mauzo ya Tanzania katika soko la Marekani kupitia Mpango wa AGOA. (**Kiambatisho Na. 9**)

### k) JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)

***124. Mheshimiwa Spika***; Katika kutumia fursa za masoko ya kikanda, mauzo ya Tanzania katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2020 yalikuwa Dola za Marekani Milioni 812.50 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 674.40 mwaka 2019 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 16.99. Ongezeko hilo limetokana na mauzo ya bidhaa za chai, mahindi, ngano, alizeti, mchele, bidhaa za karatasi, mabati, vigae, vyandarua, kemikali (methyl bromide), saruji na mafuta ya kupaka. Aidha, bidhaa za Tanzania zilizouzwa kwa wingi katika soko hilo ni pamoja na mbogamboga, chai, matunda, magunia, mifuko ya plastiki, wanyama hai, viazi, samaki, udongo asilia, kahawa, mahindi, mchele, unga wa nafaka, karanga, mawese, ufuta, pamba na makaa ya mawe. Mauzo hayo kwa kiasi kikubwa yanaenda katika nchi ya Kenya ikifuatiwa na Rwanda. Kwa upande mwingine, uagizaji wa Tanzania kutoka nchi za Jumuiya hiyo ulipungua kutoka Dola za Marekani Milioni 329.10 mwaka 2019 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 324.30 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 1.6. Upungufu huo unatokana na kuimarika kwa uzalishaji viwandani hususan bidhaa zinazotumiwa kwa wingi nchini (consumable goods). (**Kiambatisho Na. 10**)

### l) JUMUIYA YA MAENDELEO YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC)

***125. Mheshimiwa Spika***; Mauzo ya Tanzania kwenda katika soko la nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), mwaka 2020 yalikuwa Dola za Marekani Milioni 1,458.3 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 1,330.90 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 9.6. Ongezeko hilo linatokana uuzaji kwa wingi bidhaa za madini, pamba,

chai, kahawa, vigae, vyandarua, kemikali (methyl bromide), *petroleum coke*, saruji, sabuni na mafuta ya kupaka. Aidha, bidhaa hizo ziliuzwa katika nchi za Afrika Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia na Malawi. Uagizaji wa Tanzania kutoka katika soko hilo uliongezeka kutoka Dola za Marekani Milioni 155.10 mwaka 2019 hadi Dola za Marekani Milioni 470.30 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 203.2. Ongezeko hilo lilitokana na uagizaji kwa wingi bidhaa za magari ya kusafirishia mizigo, malighafi za chuma (semi-finished products of iron) na sukari ya viwandani. (**Kiambatisho Na. 11**)

### *4.1.6. Sekta ya Masoko*

#### a) Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara Nchini

***126. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na BRELA ilianzisha Mifumo ya *Online Registration System* (ORS) na *National Business Portal* (NBS) ambayo hutumika kutoa huduma za kusajili Makampuni, Majina ya Biashara, Alama za Biashara na Huduma, kutoa Hataza na kutoa Leseni za Viwanda na Biashara. Ili kusogeza huduma hiyo karibu na wananchi, Wizara iliwajengea uwezo Maafisa Biashara na Maafisa TEHAMA walioko katika Halmashauri ili waweze kutoa huduma kwa Wafanyabiashara wanaohitaji huduma zinazotolewa na BRELA katika maeneo yao. Wizara ilitoa Mafunzo kwa Maafisa Biashara na Maafisa TEHAMA 57 na kufanya ukaguzi wa viwanda 16 katika Kanda ya Pwani (Mikoa ya Pwani, Lindi na Mtwara) Mkoani Pwani; Kanda ya Ziwa Tanganyika (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora); na Kanda ya Kaskazini (Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga).

***127. Mheshimiwa Spika;*** Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya Makampuni 7,148, Majina ya Biashara 15,282 na Alama za Biashara na Huduma 1,699 yamesajiliwa. Aidha, BRELA imetoa Leseni za Biashara za Daraja A 8,404, Leseni za Viwanda 160 na Hataza 22 **(Kiambatisho Na. 12)**.

***128. Mheshimiwa Spika;*** Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha marekebisho ya Sheria ya Makampuni, Sura ya 212 kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha, 2020. Lengo la marekebisho hayo ni kuwezesha upatikanaji wa taarifa za wanufaika wa mwisho katika kampuni. Taarifa hizo ni muhimu kwa sababu za kikodi, kudhibiti utakatishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi. Kutokana na marekebisho hayo, Wizara iliandaa Kanuni chini ya Sheria ya Makampuni, zitakazowezesha upatikanaji wa taarifa za wanufaika wa mwisho ikiwa ni pamoja na kuandaa Daftari la Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners Register).

***129. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) imesaini Hati ya Makubaliano kati ya TBS na ZFDA ili bidhaa kutoka pande mbili za Muungano ziweze kusafirishwa na wafanyabiashara katika mazingira rahisi ya biashara. Hatua hiyo ni mwendelezo wa kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara kwa wafanyabiashara katika pande mbili za Muungano (Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar). Hivyo, kupitia makubaliano hayo, bidhaa za chakula na vipodozi kutoka pande mbili za Muungano zitasafirishwa pasipo usumbufu endapo zitakuwa zimesajiliwa na Mamlaka husika katika upande zinakotokea. Hali hiyo inapunguza kero za Muungano katika Sekta ya Viwanda na Biashara.

***130. Mheshimiwa Spika;*** Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Februari 2021, Wizara kupitia TBS imekamilisha maandalizi ya viwango muhimu katika kilimo, chakula, uhandisi na viwango vya vifungashio mbalimbali. Jumla ya viwango 209 ambavyo ni sawa na asilimia 41.8 ya lengo la kutayarisha viwango 500 kwa mwaka vimeandaliwa. Aidha, kati ya viwango 209 vilivyokamilika, viwango 21 ni vya uhandisi mitambo (mechanical), 39 ni vya kemikali (chemical), 14 ni vya uhandisi umeme (electro technical), vine (4) ni vya sekta mtambuka (general techniques), 27 ni vya madini (mining and minerals), 10 ni vya mazingira (environmental), 11 ni vya ujenzi (building) na 83 ni vya Sekta ya Kilimo na Chakula (food and agriculture).

***131.*** **Mheshimiwa *Spika*;** Wizara kupitia TBS imepata Mshauri Mwelekezi (*Consultant*) kwa ajili ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuanza ujenzi wa *Viwango House* Dodoma ili kubaini gharama halisi ya ujenzi wa jengo, mpango wa matumizi ya kiwanja (*master plan*), mchoro wa jengo pamoja na taratibu nyingine za ujenzi. Lengo ni kuendelea kusogeza huduma karibu na mwananchi na kuwapunguzia gharama.

**b) Utatuzi wa Malalamiko/Kero za Wadau wa Biashara**

***132. Mheshimiwa Spika;*** Mnamo tarehe 27 Septemba hadi 1 Oktoba, 2020 Wizara ilifanya ufuatiliaji kuhusu malalamiko ya wafanyabiashara juu ya ukiukwaji wa Sheria na Kanuni za utozaji ushuru wa mazao katika Mkoa wa Mbeya (Halmashauri ya Kyela na Rungwe). Katika kuchukua hatua za kutatua changamoto hizo, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI iliratibu vikao na Halmashauri husika kujadili changamoto ya utozaji ushuru wa mazao hususan ndizi na kutatua suala hilo kwa makubaliano ya kutekeleza Sheria na Kanuni zinazosimamia uuzaji na usafirishaji wa mazao ndani ya Halmashauri na kupitia Halmashauri nyingine.

***133. Mheshimiwa Spika;*** Wizara iliratibu kikao cha Umoja wa Wafanyabiashara Tanzania mnamo tarehe 05 Septemba, 2020 Jijini Dar-es Salaam. Lengo kuu la kikao lilikuwa ni kusikiliza changamoto zinazowakabili wadau wa usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi (TANEXA) na kuzipatia ufumbuzi. Changamoto hizo ni pamoja na upatikanaji wa vibali vya kuuza mazao nje ya nchi na masuala ya tozo na kodi mbalimbali za biashara. Wizara imewasiliana na Mamlaka mbalimbali zinazohusika ikiwa ni pamoja na Wizara ya Kilimo ili kurahisisha upatikanaji wa vibali kwa wakati. Aidha, Wizara imeendelea kushirikiana na Sekta Binafsi kuainisha changamoto na kuzitafutia suluhisho kwa nia ya kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini kupitia utekelezaji wa BLUEPRINT.

***134. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeshughulikia malalamiko ya wafanyabiashara wanaolalamikia taasisi za udhibiti kama vile:- Tume ya Ushindani (FCC), Shirika la Viwango Tanzania

(TBS) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Malalamiko hayo ni pamoja na:-

i. Tarehe 05 Mei, 2021 Wizara iliratibu kikao cha Taasisi zinazohusika na upangaji wa ratiba husika (Tanker Line up) ambazo ni Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Wakala wa Uingizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA). Kupitia kikao hicho imesisitizwa vikao vya Wadau vinavyofanyika mara moja kwa wiki kila siku ya Ijumaa viendelee na kila mdau ashiriki kwa lengo la kupata ratiba inayokubalika na wadau wote kwa maslahi mapana ya uchumi wa Taifa na wananchi wake. Kampuni hizo zimekuwa zikiingiza mafuta ya kula nchini ili kukidhi upungufu pamoja 365,000 MT kwa mwaka ya mahitaji halisi ya mafuta hayo ya tani 570,000 MT kwa mwaka wakati kiasi kinachozalishwa nchini pamoja ni 205,000 MT kwa mwaka (TARI-2020).

ii. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imeendelea kusimamia na kuwezesha ushushaji mapema wa mafuta ya kula yanayoingia kutoka nje ili kuongeza ugavi sokoni hivyo kuwezesha upatikanaji wake kwa wananchi na kupunguza kupanda kwa bei.

iii. Malalamiko kutoka Chama cha Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC) kuhusu gharama kubwa za viwango vya ubora wa bidhaa kwa wajasiriamali wadogo baada ya kumalizika kwa muda wa miaka mitatu wanaopewa na SIDO kuwa kubwa sana, tozo na kodi mbalimbali ambazo hutozwa wakati wa kufanya biashara zao, uondoaji wa bidhaa ambazo hazina nembo ya ubora sokoni kuwapa hasara wajasiriamali, ucheleweshwaji wa majibu ya kupima viwango vya ubora wa bidhaa, wajasiriamali ambao bidhaa zao zilikuwa zimesajiliwa TFDA kabla ya kuwa TMDA kutotambuliwa na TBS.

iv. Taasisi za Wizara zilizoguswa katika changamoto hizo ni pamoja na TBS na FCC ambapo tayari Wizara kupitia taasisi hizo imetoa ufafanuzi na mwongozo kwa TWCC ya namna ya kutatua changamoto. Aidha, Wizara imeelekeza Shirika

la Viwango Tanzania (TBS) kuweka utaratibu rafiki wa kuwahudumia wajasiriamali wadogo kwa fedha za Serikali, TBS kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa bidhaa kwa mujibu wa mifumo inayotumika ili kujiridhisha kwamba bidhaa zilizoko sokoni zinaendelea kukidhi matakwa ya viwango, TBS kutumia mifumo ya kielektroniki katika kutoa huduma zake za ukaguzi na utoaji wa ithibati, TBS kuwagawia wakaguzi wote tarakilishi ndogo (ipads) ambazo hutumika kuwasajili wakiwa katika maeneo yao ya kazi, TBS kutambua usajili wa bidhaa na majengo uliokuwa umekwishafanywa na iliyokuwa TFDA .

***135.*** **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia TanTrade ilifanikiwa kuratibu huduma ya Kliniki ya Biashara ambapo jumla ya wadau wa biashara 566 walinufaika na huduma hiyo. Aidha, changamoto za kibiashara zipatazo 161 zilitatuliwa papo kwa papo na 332 zinaendelea kufanyiwa kazi na taasisi wezeshi. Huduma hiyo ilitolewa katika Maonesho yaliyoratibiwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Simiyu, Geita na Zanzibar. Mafanikio ya utekelezaji huo ni pamoja na: -

i. Kuwezesha jumla ya wafanyabiashara 34 kupata mitaji yenye thamani ya milioni 700 kutoka kwa Benki ya NBC kwa ajili ya kuendeleza biashara mbalimbali ikiwemo ununuzi wa mashine za kuongezea thamani mazao ya kilimo, kuanzisha kiwanda cha maji, na kuimarisha taratibu mbalimbali za biashara;

ii. Kuwezesha wadau 20 kupata alama ya ubora na usajili wa jengo la biashara na kupata alama ya Msimbomilia (Bar code), na

iii. Kutoa na kujenga uelewa kwa wafanyabiashara 56 kuhusu usajili wa biashara, taratibu za ulipaji wa kodi, namna ya kupata cheti cha uthibitisho wa mlipa kodi na uandaaji wa mahesabu sahihi.

**c) Kuwaunganisha Wazalishaji, Wasindikaji na Wafanyabiashara na Masoko ya Ndani na Nje ya Nchi**

***136. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TanTrade iliratibu na kufanya Mikutano ya Biashara (B2B) na Makongamano ya

Biashara kwa njia ya Mtandao wa *Zoom* kwa lengo la kutangaza bidhaa mbalimbali zinazozalishwa nchini na kuwaunganisha wazalishaji na wanunuzi ambapo jumla ya wafanyabiashara 1,436 walipata fursa ya kushiriki mikutano hiyo. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:-

i. Wanunuzi saba (7) wa Muhogo na bidhaa zake walionesha nia ya kununua muhogo mkavu tani 325,000 kwa mwaka, muhogo mbichi tani 35 kwa wiki na unga wa muhogo tani 3,000 kwa mwezi kutoka kwa wakulima wa Mikoa ya Tanga, Lindi na Mtwara;

ii. Kuwaunganisha wajasiriamali 43 na wanunuzi wa ndani na nje ya nchi wa bidhaa za nafaka, matunda, kahawa, chai na viungo;

iii. Kampuni ya *Lise Food* kutoka Uholanzi imeingia makubaliano na kampuni za *Ottimale na Triven Farm Ltd* kununua tani 16 za parachichi na nanasi kwa wiki wakati wa msimu; na kampuni ya *Widike Ltd* kununua tani 4 za Pilipili Kichaa (Africa bird eye chill) na tani 50 za Tangawizi kwa mwezi;

iv. Umoja wa Wafanyabiashara wa Soko la Mwanakwerekwe Zanzibar waliingia makubaliano ya kununua mazao mbalimbali ya mbogamboga ikiwemo vitunguu, nyanya, viazi mviringo, nyanya chungu na magimbi;

v. Kampuni ya *Kilolo Farm* iliyo Mkoani Iringa kuingia makubaliano na Kampuni ya *Olivado Tanzania* kununua parachichi tani 50 kwa mwezi;

vi. Kampuni ya *Otimale Limited* ya Dar es Salaam kupata oda ya kuuza tani 10 za iliki kutoka Kampuni ya *China Ltd* ya nchini India, kuanzia Mwezi Agosti, 2021; na
vii. Kuwezesha vikundi vya Wakulima vinavyosimamiwa na Kampuni ya *Sustainable Agriculture Trust* (SAT), kupata oda za kuuza tani 100 za Binzari manjano, tani 100 za Pilipili Mtama na tani 150 za Karafuu kwa Kampuni ya *Mahashree Agro processing* ya Morogoro.

***137. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TBS imetoa mafunzo kwa wazalishaji, wasindikaji, wasambazaji na wauzaji wa mafuta ya kula kuhusu viwango, ubora, uhifadhi, utunzaji, ufungashaji na lebo za mafuta ya kula. Mafunzo hayo yalifanyika katika mikoa ya Kanda ya Kati kwenye wilaya za mikoa ya Singida, Tabora na Dodoma. Jumla ya wadau walioshiriki kwenye mafunzo hayo kwa Kanda ya Kati ni 1,722. Vilevile, mafunzo ya aina hiyo yamefanyika katika mikoa ya Nyanda za juu Kusini (Iringa na Mbeya) ambapo jumla ya wadau 985 walishiriki kwenye mafunzo hayo.

***138. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imefanya kazi ya kuchambua na kuainisha Makampuni ya Tanzania yaliyopewa vibali vya kuuza mazao ya kilimo kupitia Wizara ya Kilimo kwa lengo la kutambua bidhaa, kiasi, thamani na mahali bidhaa hizo zilipouzwa. Aidha, Wizara imefanikisha kutoa ushauri na kuwezesha upatikanaji wa soko na uuzaji wa mahindi meupe kiasi cha *Metric Tonne* (MT) 1,000 kati ya Kampuni ya *Jerusalem Victory Green Co. Ltd* ya Njombe na Kampuni ya *Mwendanayo Investments* ya Lilongwe, Malawi. Kampuni hizo ziliingia mkataba tarehe 19 Desemba, 2020. Aidha, jumla ya makampuni 13 kutoka Dar es Salaam, Arusha, Kigoma, Kagera, Singida, Mara, na Dodoma yameunganishwa na fursa ya soko la Mahindi nchini Msumbiji. Vilevile, Wizara ilishiriki katika kikao cha tarehe 30 Desemba, 2020 kuhusu majadiliano ya fursa ya biashara ya mboga mboga na maua kati ya Tanzania na Qatar.

***139. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na TanTrade imefanya tathmini ya hali ya mwenendo wa biashara ya Mpunga na Mchele katika Manispaa ya Kahama – Shinyanga kuanzia tarehe 03-09 Februari, 2021. Aidha, kutokana na tathmini hiyo iliyofanyika imebainika kuwa Mchele umekuwa ukiuzwa zaidi katika nchi za jirani kama vile Kenya, Uganda na Rwanda. Hata hivyo, Tanzania inaweza kupanua wigo wa biashara ya kuuza mchele katika masoko mengine yanayoibukia (emerging markets) ambayo yanaweza kufikika kirahisi kama vile Sudani Kusini, DRC, Madagascar, Visiwa vya Comoro, Msumbiji na Afrika ya Kusini. Kupitia taarifa hizo, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na

Ushirikiano wa Afrika Mashiriki kupitia Balozi zetu inaendelea na mkakati wa kuwaunganisha wafanyabiashara wa Tanzania na wafanyabiashara wa nchi hizo ili kupata masoko ya mchele kwenye nchi hizo.

***140. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TanTrade imeanzisha majadiliano ya ushirikiano na Shirika la Posta ili kuwezesha wafanyabiashara kuuza katika mfumo wa soko mtandao (*e-posta*) ili kunufaika na fursa za masoko ya mtandao. Kwa kipindi husika, jumla ya kampuni 150 zimesajiliwa na zinafanya biashara katika mfumo huo.

***141. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na TanTrade imeanza hatua za awali za uanzishaji wa dawati la waambata wa biashara katika Ofisi za Balozi sita (6) katika nchi sita za kipaumbele zikiwemo China, India, Afrika ya Kusini, Kenya, Ubelgiji na Uholanzi. Mapendekezo ya nchi hizo yamezingatia wingi wa biashara inayofanyika katika nchi hizo pamoja na kupanua wigo kwa bidhaa zinazozalishwa nchini.

**d) Kuhamasisha na Kuendeleza Matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na Kutekeleza "BLUEPRINT" kuhusu Uratibu wa Ghala zote Nchini**

***142. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia uratibu wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) inashirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) pamoja na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX), TAMISEMI kupitia Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Bodi za Mazao zinazosimamia mazao ya kimkakati na mazao mengine ikiwa ni pamoja na ufuta, mbaazi, choroko na dengu kuendeleza na kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Kupitia Mfumo huo, mazao hukusanywa, kuhifadhiwa na kuuzwa kupitia Soko la Bidhaa Tanzania. Katika msimu wa mwaka 2020/2021, tani 19,867.811 za korosho na tani 5,200.367 za choroko zimeuzwa kupitia Soko la Bidhaa Tanzania.

***143.* Mheshimiwa Spika;** Wizara imeendelea kuhamasisha na kusimamia matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwenye mazao kumi ya kilimo ambayo yameingizwa katika

Mfumo huo. Mazao hayo ni Mbaazi, Dengu, Soya, Mpunga, Ufuta, Kakao, Kahawa, Alizeti, Korosho na Mahindi. Katika msimu wa mwaka 2020/21, uhamasishaji wa matumizi ya Mfumo umefanyika katika mikoa ya Simiyu na Geita kwa mazao ya choroko na dengu; Mkoa wa Kagera kwenye zao la Kahawa, na Mkoa wa Ruvuma kwenye zao la Soya, Mkoa wa Singida, Lindi, Iringa, Songwe pamoja na Katavi kwa zao la ufuta. Hata hivyo, Serikali itaendelea kuhamasisha matumizi ya Mfumo huo kwenye mazao ya sasa pamoja na kuongeza idadi.

***144.* Mheshimiwa *Spika*;** Katika kipindi cha Julai 2020, hadi Machi 2021, jumla ya tani 346,457.90 za mazao zilikusanywa kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala, ambapo zao la Korosho liliongoza kwa kukusanya tani 204,567.65, zao la Ufuta tani 98,904.50, zao la Mbaazi 10,143.42, zao la Kahawa tani 11,649.43, zao la Kakao tani 6,607.95, zao la Soya tani 1,693.44, Choroko tani 12,781.82 na zao la Dengu tani 109.7.

***145.* Mheshimiwa Spika:** Serikali kupitia Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala inaendelea kutekeleza "BLUEPRINT" ambapo inakamilisha mapitio ya sheria na kanuni zinazosimamia uendeshaji wa Ghala zote. Aidha, Bodi inaendelea na maboresho ya Mfumo wa Kielektroniki utakaokuwa na kanzidata ya Ghala zote zinazotumia Mfumo wa Stakabadhi na zisizotumia Mfumo wa Stakabadhi ili kuweza kuzitambua, kuzidarajisha na kuwa na taarifa muhimu kuhusu ghala hizo.

**e) Kuhamasisha na Kurahisisha Biashara Mipakani**

***146. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kuhamasisha na kuboresha mazingira ya biashara mipakani kwa kutembelea mipaka ya Mutukula na Rusumo mkoani Kagera na mpaka wa Namanga (OSBP) kwa lengo la kutambua hali ya ufanyaji biashara, athari za COVID-19 katika biashara kupitia mipaka hiyo, aina za bidhaa na takwimu ya bidhaa husika zinazoingia na kuuzwa nje kupitia mipaka husika. Tathmini hiyo ililenga kubaini changamoto wanazokabiliana nazo na kuzitafutia ufumbuzi.

***147. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na *Trade Mark East Africa (*TMEA*)* imeandaa Andiko la Ujenzi wa Masoko ya Mipakani (Cross Border MarketsCBM) kwenye mipaka ya Holili, Tunduma na Mtukula. Wizara imetembelea na kukusanya maoni ya wadau katika mipaka hiyo kwa lengo la kujua uhitaji wa masoko hayo kwenye mipaka hiyo. Lengo ni kuhakikisha ujenzi wa masoko hayo unakuwa wenye tija kwa wafanyabishara na Taifa kwa ujumla.

***148. Mheshimiwa Spika;*** Vilevile, Wizara ilishiriki katika mkutano wa kupitia taarifa ya awali *(*inception report*)* ya usanifu wa jengo la Kituo cha Huduma kwa Pamoja Mpakani (OSBP) Manyovu/Mugina tarehe 09 Desemba, 2020. Katika mkutano huo, Wizara ilipewa jukumu la kuratibu na kusimamia uanzishwaji wa Dawati la Biashara (*Trade Information desk*) kwa ajili ya kupokea na kutoa taarifa za kibiashara na uwekezaji nchini.

**f) Kuhamasisha na kuwezesha wananchi kutangaza bidhaa na huduma za Tanzania**

***149. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake, iliratibu na kushiriki Maonesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) yaliyofanyika kuanzia tarehe 01 Julai hadi 13 Julai, 2020 katika Viwanja vya Mwalimu J. K. Nyerere barabara ya Kilwa. Jumla ya makampuni 2,837 yalishiriki katika Maonesho ya 44 ya DITF, 2020 ukilinganisha na makampuni 3,250 yaliyoshiriki katika Maonesho ya 43 ya DITF 2019 ambayo ni upungufu wa asilimia 12. Kati ya kampuni zilizoshiriki maonesho mwaka 2020, kampuni 43 zilitoka nje ya nchi ambapo nchi 5 zilishiriki ikilinganishwa na kampuni 520 kutoka nchi 35 zilizoshiriki mwaka 2019. Aidha, kupungua kwa washiriki wa Maonesho hayo ulisababishwa na uwepo wa Homa Kali ya Mapafu unaosababishwa na virusi vya Korona (COVID-19) ambapo nchi nyingi duniani zilifunga mipaka yao.

***150. Mheshimiwa Spika;*** Jumla ya Watembeleaji 60,000 walinufaika na huduma ya vitambulisho vya Taifa; leseni za biashara 109; vitambulisho vya wajasiriamali wadogo 7; leseni za vileo 7; ada ya huduma (Service Levy) 62; wananchi 2050

walipata huduma za afya kati yao 170 walipewa rufaa kwa ajili ya uchunguzi zaidi; Upatikanaji wa ajira za muda zipatazo 15,912; na fursa ya kutangaza mazao 9 kupitia Banda Maalum kwa ajili ya Bodi zote ikiwemo Korosho, Kahawa, Pareto, Mkonge, Pamba, Tumbaku, Nafaka, Chai na Sukari.

***151. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake, ilishiriki katika Maonesho ya Nane Nane 2020 katika Viwanja vya Nyakabindi, Bariadi katika Mkoa wa Simiyu. Jumla ya wajasiriamali 49 waliokidhi vigezo vya usindikaji wa bidhaa za kilimo kutoka Mikoa ya Simiyu, Kagera, Mwanza, Shinyanga na Dar es Salaam waliwezeshwa kushiriki moja kwa moja katika banda la Wizara na kupata fursa za kutangaza bidhaa zao, kujifunza teknolojia za uzalishaji pamoja na mbinu bora za biashara.

***152. Mheshimiwa Spika;*** Wakati wa Maonesho hayo huduma mbalimbali zilitolewa na Wizara pamoja na taasisi zake ikiwemo: Usajili wa Makampuni na Majina ya Biashara ulikuwa unatolewa na BRELA; na Mafunzo kwa wastaafu yalitolewa na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE). Wizara kwa kushirikiana na TANTRADE waliendesha kongamano la Wanawake-*Tanzania Business Women Association* (TABWA) kwa lengo la kutoa mafunzo ya biashara na kuwezesha Wanawake na Vijana kiuchumi; Darasa la mafunzo (Kliniki ya Biashara) kwa wajasiriamali kuhusu masoko,;usindikaji na vifungashio; Matumizi ya Vipimo sahihi na Mafunzo ya kutumia zana mbalimbali zinazotengenezwa na SIDO na CAMARTEC.

***153. Mheshimiwa Spika;*** Wizara ilishiriki katika Maonesho ya Tatu ya Teknolojia na Uwekezaji katika Sekta ya Madini, 2020 yaliyofanyika tarehe 17 – 27 Septemba, 2020 katika Uwanja wa Bombambili Kalangalala Mjini Geita. Lengo kuu la Maonesho lilikuwa ni kukuza na kuboresha shughuli za Wachimbaji, Wachenjuaji na Wachomaji wa dhahabu sambamba na kuwaunganisha wadau hao na Wasambazaji wa Teknolojia za Uchimbaji na Uongezaji thamani Madini. Wanunuzi, Wauzaji wa Madini, Wizara na Taasisi za Kisekta, Taasisi za Udhibiti na Usalama, Makampuni, Mashirika ya Bima, Taasisi pamoja na Wadau wengine walishiriki.

***154. Mheshimiwa Spika;*** Maonesho hayo yalibeba Kauli mbiu "Madini ni Uchumi, 2020 Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo ya Taifa", ikilenga kutoa hamasa kwa wadau pamoja na kutambua teknolojia ya uchimbaji, uchenjuaji na uongezaji thamani wa madini ya dhahabu katika kukuza Sekta ya Madini na Uwekezaji nchini, pia waweze kushiriki kikamilifu katika zoezi la kuchagua viongozi bora katika Uchaguzi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliofanyika mwezi Oktoba, 2020.

***155. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TanTrade iliratibu na kuandaa Maonesho ya Tano ya Bidhaa za Viwanda vya Tanzania ambapo kwa mwaka 2020 jumla ya wadau 596 wa viwanda walishiriki ikilinganishwa na wadau 542 mwaka 2019 Washiriki hao ni pamoja na Viwanda vidogo, vya kati na vikubwa na Taasisi za Serikali ambazo zilitangaza bidhaa na teknolojia wanazozalisha na kuhamasisha uwekezaji katika viwanda hapa nchini pamoja na kujadili changamoto mbalimbali zinazokabili Sekta ya Viwanda na Biashara. Lengo la uratibu wa Maonesho hayo ni kuongeza uelewa wa Watanzania juu ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya Tanzania na kuongeza hamasa ya kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini ambapo kupitia Maonesho hayo watembeleaji waliweza kuziona bidhaa hizo na kutambua thamani na ubora wake kwa lengo la kuzitumia.

***156. Mheshimiwa Spika;*** Katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Wizara kwa kushirikiana na TanTrade imefanya vikao mbalimbali vya maandalizi ya ushiriki wa Tanzania kwenye Maonesho ya Dunia ya Expo- Dubai, 2020. Maonesho hayo sasa yamesogezwa mbele kwa mwaka mmoja kutokana na Janga la Ugonjwa wa Homa ya Mapafu (COVID -19) na hivyo yamepangwa kufanyika tarehe 01 Oktoba, 2021 hadi tarehe 31 Machi, 2022. Wizara kupitia TanTrade inaendelea na maandalizi ikiwa ni pamoja na kuandaa "documentary" za Miradi saba (7) kutoka Taasisi za TPA, TRC, COSTECH, TPDC, TCAA, TANESCO, *Institute of Marine Science* (IMS) ambazo zinaendana na kauli mbiu ndogo ya maonesho *"Innovation, Opportunity and Sustainability"*.

### g) Uimarishaji Ushindani katika Soko na Biashara ya Ndani

***157. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Wakala wa Vipimo (WMA) imeendelea kufanya uhakiki na huduma za usahihi wa vipimo na mifumo ya upimaji katika Sekta ya Biashara, Afya, Usalama na Mazingira kwa lengo la kumlinda mlaji. Hadi kufikia mwezi Machi 2021, Wakala wa Vipimo imekagua na kuhakiki vipimo 621,515 sawa na asilimia 112.4 ya lengo la kukagua vipimo 552,973 vilivyokadiriwa. Wakala imetoa elimu kuhusu matumizi sahihi ya vipimo kwa watumiaji wa vipimo kama vile waendesha pikipiki, wajasiriamali wadogo na viziwi kwenye mikoa ya Dar es Salaam na Tabora. Pia, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo imeendelea na zoezi la ukaguzi wa kawaida na wa kushtukiza wa vipimo mbalimbali vitumikavyo kwenye biashara, afya, usalama na mazingira. Vipimo vilivyokaguliwa kwa wingi ni mizani, pampu za kuuzia mafuta, dira za maji, malori ya kubebea mchanga/kokoto na magari ya kubebea mafuta.

### Mwenendo wa Bei za Baadhi ya Mazao

***158. Mheshimiwa Spika;*** Mwenendo wa ugavi na bei za mazao, bidhaa na huduma muhimu nchini imeendelea kuimarika. Ugavi wa mazao ya chakula umeimarika kutokana na mavuno makubwa ya mazao ya chakula katika msimu wa kilimo wa mwaka 2019/2020 hivyo kufanya bei za mazao mbalimbali kuwa stahimilivu. Wastani wa bei ya baadhi ya mazao ya chakula umepanda ikilinganishwa kwa robo ya tatu ya mwaka 2019/2020 na robo ya tatu ya mwaka 2020/2021. Bei ya gunia la kilo 100 la mahindi imeshuka kwa asilimia 34.7; maharage yameshuka kwa asilimia 7.2; mchele umeshuka kwa asilimia 27.4; wakati viazi mviringo na ulezi bei imepanda kwa asilimia 1.6 na 8.8 mtawalia **(Kiambatisho Na. 13)**.

***159. Mheshimiwa Spika;*** Hali ya ugavi wa mafuta ya kula katika soko la ndani takriban katika mikoa yote hapa nchini inaendelea kuimarika kwa kasi kidogo. Hali hiyo inafanya bei ziendelee kuwa juu ikilinganishwa na kipindi kama hiki mwaka 2020. Bei ya chini kwa sasa ya Shilingi 5,500 kwa lita ni ya

mafuta ya kula ya mawese na bei ya juu ni Shilingi 6,500 kwa mafuta ya kula ya alizeti ambapo bei ya chini imeonesha kuwa ni Shilingi 6,000 na bei ya juu ni Shilingi 7,000 kwa lita.

***160. Mheshimiwa*** **Spika;** Wastani wa bei ya jumla ya Sukari kwa wafanyabiashara na wasambazaji wakubwa ni kati ya Shilingi 2,300 na Shilingi 2,533 kwa kilo moja na kwa upande wa bei ya rejareja katika maeneo mengi nchini ni kati ya Shilingi 2,500 na Shilingi 2,900 kwa kilo na baadhi ya maeneo bei imefikia Shilingi 3,000.

***161. Mheshimiwa*** **Spika;** Bei ya bidhaa zingine muhimu za viwandani hususan saruji, mabati, na nondo zimeendelea kuwa stahimilivu kutokana na uzalishaji wa kuridhisha katika viwanda vya ndani vya bidhaa hizo **(Kiambatisho Na. 14)**.

***162. Mheshimiwa Spika;*** Katika kipindi cha mwezi Machi, 2021, wastani wa bei kwa gunia la kilo 100 nchini ni Shilingi 48,341 kwa mahindi, Shilingi 177,340 kwa maharage, Shilingi 139,212 kwa mchele, Shilingi 100,688 kwa mtama, Shilingi 123,461 kwa ngano, Shilingi 142,081 kwa ulezi, Shilingi 103,214 kwa uwele na Shilingi 70,835 kwa viazi mviringo **(Kiambatisho Na. 15)**.

***163.*** **Mheshimiwa *Spika*;** Hadi kufikia tarehe 9 Aprili, 2021 wastani wa bei ya jumla ya Sukari kwa wafanyabiashara na wasambazaji wakubwa ni kati ya Shilingi 2,300 na Shilingi 2,533 kwa kilo moja na kwa upande wa bei ya rejareja katika maeneo mengi nchini ni kati ya Shilingi 2,500 na Shilingi 2,900 kwa kilo na baadhi ya maeneo bei imefikia Shilingi 3,000. Aidha, bei ya juu katika baadhi ya maeneo imetokana na gharama za usafirishaji kutoka sukari inakozalishwa na changamoto za miundombinu ya barabara.

***164.*** **Mheshimiwa *Spika*;** Hadi Aprili 2021, inakadiriwa jumla ya tani 26,871.28 za Sukari zilikuwepo ghalani, ambapo tani 12,214.95 zikiwa kwenye ghala ya wazalishaji Sukari nchini na tani 14,656.33 zilikuwepo katika maghala ya Wafanyabiashara. Aidha, katika kuhakikisha nchi inaendelea kukidhi mahitaji ya Sukari, Serikali kupitia Bodi ya Sukari, ilitoa idhini kwa wazalishaji kuagiza tani 40,000 za sukari ya kuziba

pengo la mahitaji kwa mwaka 2020/2021. Bodi ya sukari imekwishatoa leseni za uagizaji na kiasi hicho kipo katika hatua mbalimbali za uingizwaji.

**h)Kuimarisha Mfumo wa Ukusanyaji wa Taarifa za Masoko**

**Mheshimiwa *Spika;*** Wizara imeendelea kukusanya na kuchambua taarifa za mwenendo wa bei na masoko ya bidhaa zikiwemo; Taarifa za bei za mazao makuu ya chakula (Mahindi, Mchele, Mtama, Uwele, Ulezi, Maharage, Ngano na Viazi Mviringo) kutoka katika masoko makuu ya mikoa Tanzania bara na kuzisambaza taarifa hizo kila siku ya Jumatatu, Jumatano na Ijumaa kwa wadau wakiwemo:- Ofisi ya Rais, Ofisi ya Waziri Mkuu/Usalama wa Chakula, Benki Kuu Tanzania (BOT), Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Shirika la Chakula Duniani – WFP, NMB, GPSA (Wakala wa Ununuzi Serikalini), Wizara ya Kilimo (Kitengo cha Market Intelligence), Wizara ya Mifugo na Uvuvi, na wadau wengine mbalimbali zikiwemo taasisi za Utafiti. Aidha, taarifa hizo hutangazwa na Redio – Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), na kuchapishwa katika magazeti ya *The Guardian* na Mwananchi na pia zinapatikana katika tovuti ya Wizara.

***165.*** **Mheshimiwa *Spika;*** Wizara pia imeendelea kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa za bei za baadhi ya vifaa vya ujenzi ikiwa ni pamoja na nondo na bati na mwenendo wa bei ya sukari. Tarehe 27 – 30 Septemba, 2020, Wizara ilifanya ufuatiliaji na tathmini ya ukusanyaji wa taarifa za bei za mazao na vifaa vya ujenzi mkoani Mbeya kwa kutembelea soko la Mwanjelwa, Soko la SIDO, Igawilo (Uyole) na soko la Mbalizi na kuweza kupata taarifa za bei za mazao na vifaa vya ujenzi, kupata maoni ya kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za masoko pamoja na changamoto za kibiashara katika masoko.

***166.*** **Mheshimiwa *Spika;*** Wizara ilifuatilia na kutathmini mwenendo wa uzalishaji saruji viwandani, ili kubaini hali halisi ya uzalishaji, usambazaji na mwenendo wa bei na jinsi viwanda hivyo vilivyojipanga kukabiliana na changamoto ya uhaba na upandaji holela wa bei ya saruji nchini. Lengo kuu

lilikuwa ni kutambua uwezo wa viwanda vya ndani na hali halisi ya uzalishaji wa saruji na sababu zinazochangia uhaba na mfumuko wa bei ya bidhaa hiyo.

**i) Udhibiti wa Ubora na Viwango vya Bidhaa zinazozalishwa Nchini na zinazozalishwa Nje ya Nchi**

***167.*** **Mheshimiwa Spika**; Kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya leseni 336 za nembo ya ubora ya TBS zilitolewa ambayo ni sawa na asilimia 67.2 ya lengo la kutoa leseni 500 kwa mwaka 2020/2021. Miongoni mwa leseni hizo, leseni 197 zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo wanaozalisha mafuta ya kupaka, chaki, mchele, korosho, unga wa mahindi, sabuni za aina mbalimbali, viungo, mafuta ya nazi, keki, juisi, pombe za nafaka, mkate, pombe isiyotokana na nafaka, pombe kali, mvinyo, nyama za kuku, na nyama za kusindika. Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali na wadau mbalimbali katika dhana ya kuzingatia mifumo ya ubora ili kuzalisha bidhaa zenye ubora unaokubalika.

***168.*** **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia TBS imetoa jumla ya vyeti vya ubora (Certificates of Conformity to Standards - CoCs) 24,760 kwa shehena za bidhaa zitokazo nje ya nchi; sawa na asilimia 63.5 ya matarajio ya kutoa vyeti 39,000.

***169.*** **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia Wakala wa Vipimo imeendelea kufanya kazi ya udhibiti wa bidhaa zilizofungashwa mipakani, kupitia vituo vya ukaguzi vya Sirari (Mara), Mtukula (Kagera), Namanga (Arusha), Holili (Kilimanjaro), Tunduma (Songwe), Tarakea (Kilimanjaro), Horohoro (Tanga) ,Kasumulu (Mbeya), na Kasesya-Rukwa. Baadhi ya bidhaa zilizoingia nchini na kukaguliwa ni pamoja na mafuta ya petroli na mafuta ya kula. Aidha, Wakala wa Vipimo imeendelea kukagua bidhaa zilizofungashwa zinazozalishwa na viwanda vya ndani ili kuhakiki usahihi wa kiasi kilichotamkwa. Baadhi ya bidhaa zilizokaguliwa ni vyakula, vilainishi, saruji, rangi, mitumba, mabati na nondo.

### j) Udhibiti wa Ushindani Usio Haki katika Soko

***170.*** **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia Tume ya Ushindani (FCC) imeshughulikia mashauri 17. Mashauri hayo yanahusu makubaliano yanayofifisha ushindani (2), miunganiko ya kampuni yaliyofanyika bila idhini ya FCC (10), makubaliano ya siri (2), na matumizi mabaya ya nguvu ya soko (3). Katika mashauri yanayohusu makubaliano yanayofifisha ushindani (Anti-Competitive Agreements) katika sekta ndogo ya tumbaku, FCC inaendelea na ufuatiliaji wa karibu wa makubaliano yaliyofikiwa kati ya FCC na kampuni za ununuzi wa tumbaku katika Mkoa wa Tabora. Utekelezaji wa makubaliano hayo umekwishaanza ambapo kampuni za tumbaku zimelipa kiasi cha fedha kwa Katibu Tawala wa Mkoa (RAS) wa Tabora kama zilivyotakiwa kwenye makubaliano hayo. Pamoja na hayo; Wizara kupitia FCC inaendelea kufanya uchunguzi wa shauri yanayohusu makubaliano ya siri (cartel) kwenye sekta ndogo ya chuma na saruji.

***171.*** **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia FCC inaendelea kufanya tafiti katika sekta mbalimbali zenye lengo la kubaini mienendo inayokinzana na Sheria ya Ushindani. Aidha, tafiti katika sekta ndogo ya mbolea imekwishafanyika na kwa sasa tafiti katika tasnia ya famasia (pharmaceutical industry study) imepanga kufanyika ili kubaini masuala yanayofifisha ushindani katika maeneo hayo.

### k) Utaratibu wa Ukaguzi wa Magari nchini

***172.*** **Mheshimiwa Spika;** Wizara imetekeleza agizo la Serikali la kuandaa utaratibu stahili wa kukagua magari yaliyotumika nje ya nchi na bidhaa mbalimbali zinazoingia nchini kwa Mfumo wa *Destination Inspection* (DI) badala ya mfumo wa awali wa *Pre-Shipment Verifacation of conformity* (PvoC). Utaratibu wa kukagua magari kutoka nje ya nchi baada ya kuwasili hapa nchini umeanza tarehe 01 Machi, 2021 ambapo waagizaji wote wa magari wanatakiwa kupeleka maombi yao TBS na sio kwa mawakala.

#### *4.1.7. Maendeleo ya Rasilimali Watu*

***173. Mheshimiwa Spika;*** Wizara ilipokea IKAMA ya watumishi kwa mwaka 2020/2021 kutoka Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora ambayo inatoa mwongozo wa kuajiri baada ya kibali cha kuajiri kutolewa. Aidha, Wizara imepokea muundo mpya ambao utasaidia katika kujaza nafasi za uteuzi zilizoko wazi.

***174. Mheshimiwa Spika,*** Katika kuwajengea uwezo watumishi wake, Wizara imepeleka watumishi ishirini na moja (21) katika vyuo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Kati ya hao, mtumishi mmoja anashiriki Shahada ya Uzamivu (Phd), watumishi kumi na tisa (19) wanashiriki mafunzo ya Shahada ya Uzamili (Masters Degree), na mmoja anashiriki mafunzo ya Diploma ya Utunzaji Kumbukumbu. Aidha, watumishi kumi na sita (16) wameweza kushiriki mafunzo ya muda mfupi katika kozi mbalimbali zilizochangia katika kujenga uwezo na kuongeza ufanisi katika maeneo yao ya kazi.

***175. Mheshimiwa Spika,*** Kwa mwaka 2020/2021, Wizara imewapeleka watumishi wanne (4) katika mafunzo ya muda mfupi ya ujasiriamali ambao wamestaafu katika Utumishi wa Umma, ikiwa ni kuwaandaa na maisha baada ya kustaafu. Aidha, watumishi hao tayari wamekwisha andaliwa nyaraka zao muhimu na kuwasilishwa katika mamlaka husika kwa ajili ya uandaaji wa mafao yao kwa wakati.

***176. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Wizara imefanikiwa kufanya kikao kimoja cha Kamati Maalum ya Maadili ya Wizara kikilenga kupanga mikakati ya kudumisha uadilifu kwa watumishi wa Wizara. Pia kupitia vikao vya idara vinavyofanyika kila mwezi, elimu imetolewa kwa watumishi kuhusu athari za vitendo visivyo na uadilifu kazini vikiwemo vya rushwa lakini pia kusisitiza uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya kiutumishi wakati wa kutoa huduma.

***177. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2020/2021, Wizara imeendelea kutoa huduma ya lishe bora na posho ya usafiri kila mwezi kwa watumishi saba (7) wanaoishi na Virusi vya UKIMWI ambao wamejiweka wazi kwa mujibu wa Mwongozo wa Serikali. Wizara pia iliweza kushiriki katika semina zilizofanyika kuanzia tarehe 25 Novemba 2020 na kufikia kilele siku ya maadhimisho ya siku ya kimataifa ya UKIMWI tarehe 1 Desemba, 2020 iliyofanyika mji wa Moshi Mkoani Kilimanjaro.

***178. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kupambana na kuendelea na jitihada za kupambana na kujikinga maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI (VVU) na Magonjwa Sugu yasiyoambukiza (MSY) kazini. Wizara imeweza kufanya kikao kimoja cha Kamati Maalum ya Masuala ya UKIMWI na Magonjwa Sugu yasiyoambukiza (MSY) kilichofanyika tarehe 4 Machi, 2021. Aidha, Wizara inatoa vifaa tiba na vifaa kinga kwa watumishi wake bure pamoja na elimu inaendelea kutolewa juu ya kujikinga na Virusi vya UKIMWI (VVU) na Magonjwa Sugu yasiyoambukiza (MSY). Katika kuhamasisha watumishi kufanya mazoezi, Wizara iliweza kuratibu Bonanza moja lililofanyika tarehe 23 Januari, 2021 katika viwanja vya *St. John* – Dodoma ambapo watumishi sabini (70) waliweza kushiriki.

### *4.1.8.* Ukaguzi wa Ndani

***179. Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2020/2021, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kulingana na Sheria, miongozo na kanuni zilizowekwa. Katika kuhakikisha kuwa kunakuwepo kwa matumizi sahihi ya rasilimali za serikali, Wizara imefanya ukaguzi wa fedha, rasilimali watu na ununuzi na kuhakikisha kwamba sheria, kanuni na taratibu zinafuatwa na hatimaye Wizara imepata hati safi ya Ukaguzi. Aidha, Kamati ya ukaguzi ya Wizara ilifanya vikao vinne ili kupitia taarifa za hesabu pamoja na ukaguzi na kutoa ushauri unaostahili kwa Afisa Masuuli.

### *4.1.9.* Ununuzi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha

***180.* Mheshimiwa Spika;** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Kitengo cha Ununuzi kiliweza kutekeleza yafuatayo:-

Kusimamia shughuli za ununuzi wa bidhaa na huduma kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi Na.7 ya mwaka 2011 na kanuni zake GN Na, 446 ya mwaka 2013, kama zilivyo fanyiwa marekebisho mwaka 2016 pamoja na miongozo inayotolewa na Mamlaka ya Udhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA); Kuandaa Mpango wa Ununuzi kwa mwaka fedha 2019/2020; Kuwezesha Watumishi watatu (3) kupata mafunzo ya mfumo wa ununuzi kwa njia ya kielektroniki Tanzania Electronic Procurement system(TANePS); Kuratibu vikao vitatu (3) vya Bodi ya Zabuni ya Wizara; Kuandaa taarifa za ununuzi za kila mwezi, robo pamoja na taarifa ya mwaka na kuziwasilishwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA); na Kufanya uhakiki mali za Wizara na kuhuisha taarifa za Daftari la Mali la Wizara kwa mujibu wa muongozo wa mali za Serikali wa mwaka 2019 pamoja na Sheria ya Fedha Na. 6 ya mwaka 2001 na Kanuni zake, GN.132 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2004.

***181. Mheshimiwa Spika;*** Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Kitengo cha Fedha na Uhasibu imeendelea kuimarisha udhibiti wa matumizi ya fedha za umma kwa kuboresha mifumo ya usimamizi wa rasilimali fedha ikiwemo uzingatiaji wa sheria na kanuni za fedha na manunuzi ya umma. Aidha, katika kutekeleza masuala ya uwazi na uwajibikaji (Transparency and Accountability) katika matumizi ya fedha za umma, Wizara imekuwa ikiandaa taarifa za fedha zinazokidhi viwango vya kimataifa katika uandaaji wa taarifa za fedha kwa taasisi za umma (International Public-Sector Accounting Standards) na miongozo mbali mbali itolewayo na Wizara ya Fedha na Mipango. Kutokana na taarifa za fedha zinazokidhi viwango vya kimataifa na miongozo mbali mbali ya Serikali, Wizara kwa miaka mingi imekuwa ikipata hati safi za ukaguzi kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

### *4.1.10. Mawasiliano Serikalini*

***182. Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2020/2021, Kitengo kimeendelea kutoa elimu na kuhabarisha Umma kupitia Vyombo vya Habari ikiwemo Radio, Televisheni, Magazeti,

Majarida, Mitandao ya Kijamii na kupitia Maonesho ya Biashara yanayofanyika nchini. Aidha, Kitengo kinakamilisha Makala Video (Video Documentary) pamoja na kitabu cha picha kinachohusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano katika Sekta ya Viwanda na Biashara. Makala ya Video itarushwa kupitia vyombo mbalimbali vya habari hapa nchini. Pia Kitengo kimeboresha tovuti ya Wizara ili iendane na mahitaji halisi ya habari ya Wizara pamoja na teknolojia ya kisasa.

#### *4.1.11. TEHAMA na Takwimu*

***183. Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2020/2021, Wizara imeendelea Kusimamia na kuratibu matumizi bora, salama na sahihi ya miundombinu na Rasilimali za TEHAMA, kuongezea uwezo watumishi wake katika teknolojia za kisasa; na Kuimarisha ulinzi wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa kufanya tathmini ya ulinzi wa mifumo ya TEHAMA. Aidha, Wizara inaendele na kazi ya uundaji wa kanzidata ya Taifa ya viwanda ambapo itasaidia kupata takwimu za viwanda kwa wakati na hata kurahishisha katika utengenezaji wa sera za viwanda Nchini. Na vile vile, Wizara inaendelea na utengenezaji wa Mfumo wa Dashibodi wa kuchunguza maendeleo na utendaji wa taasisi zote zilizopo chini ya Wizara kielektroniki.

## 5. MIPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2021/2022

***184. Mheshimiwa Spika;*** Sekta ya Viwanda na Biashara ina mchango wa kipekee katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambao una malengo mahsusi 12 na vipaumbele vitano. Kati ya malengo mahsusi 12, malengo sita (ambayo ni 50%) yanahusu Sekta ya Viwanda na Biashara moja kwa moja. Katika vipaumbele vitano, vipaumbele vitatu (60%) vinahusu Sekta ya Viwanda na Biashara. Vipaumbele hivyo ni pamoja na kuchochea uchumi shirikishi na shindani; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza uwekezaji na biashara; kuchochea maendeleo ya watu; na kuendeleza rasilimali watu.

### *5.1.*Malengo Makuu ya Mpango wa Bajeti

***185. Mheshimiwa Spika;*** Wizara ina Malengo Makuu mawili (2) ya utekeleza Bajeti ya 2021/2022. Kwa upande wa Sekta ya Viwanda, Lengo kuu ni Kuchochea ujenzi na maendeleo ya viwanda vinavyokidhi mahitaji ya bidhaa za ndani, kuongeza uwezo wa nchi kushindana katika Soko la kikanda na kidunia. Kwa upande wa Sekta ya Biashara, Lengo kuu ni kusimamia na kuratibu utekelezaji wa BLUEPRINT ili kujenga ushindani na kuendelea kuboresha mazingira ya biashara Nchini ili kuchochea uwekezaji.

### *5.2.*Misingi *ya Kuzingatia katika Kutekeleza Malengo Makuu ya Bajeti*

***186. Mheshimiwa Spika;*** Katika kuandaa vipaumbele vya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2021/2022 tumezingatia misingi ifuatayo:-

a) Viwanda kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya bidhaa ya soko la ndani;

b) Viwanda vinavyozalisha ajira kwa wingi;

c) Viwanda ambavyo vinaipa nafasi Tanzania kushindana katika soko la kanda na kidunia;

d) Viwanda vya kuchakata malighafi itokanayo na maliasili za nchi;

e) Viwanda vinavyoipa nchi uwezo wa kutumia eneo la kijiografia vizuri katika kukuza ushindani, ikiwemo bandari; na

f) Viwanda ambavyo vitaiandaa nchi kuingia mapema katika mapinduzi ya nne ya viwanda.

### *5.3.Vipaumbele kwa Bajeti ya Mwaka 2021/2022*

***187. Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2021/2022, Wizara ina vipaumbele vifuatavyo:

(a) Kuendeleza miundombinu ya msingi na saidizi ya maeneo ya uwekezaji (Industrial Parks) na huduma ya viwanda kwa wawekezaji na wajasiriamali;

(b) Kuratibu na kusimamia uanzishwaji wa maeneo maalum ya kibiashara (trading hubs) hususan kwa maeneo ya mipakani ambapo kuna biashara kubwa. Pia, kuona namna ya kuimarisha eneo maalum la kibiashara la Kariakoo ambalo kihistoria limekuwa likifanya vizuri na kuona namna ya kuliboresha zaidi;

(c) Kusimamia kwa karibu utekelezaji wa miradi ya kielelezo iliyopo katika Mpango wa Maendeleo wa tatu;

(d) Kuweka mkazo na msisitizo katika kukuza na kuchochea viwanda vidogo na vya kati (small and medium industries) vinavyotumia teknolojia rahisi na ya kisasa vilivyojikita vijijini na mijini;

(e) Kuboresha kanzidata (Database) kwa ajili ya kupata takwimu sahihi za viwanda nchini;

(f) Kuweka mkazo katika kuwatambua, kuwawezesha na kuwahudumia wawekezaji katika viwanda vikubwa na vyenye tija kubwa katika uchumi wa nchi (mtaji, ajira, na kodi);

(g) Kuimarisha utafiti na matumizi yake katika maendeleo ya viwanda, ikiwemo kuwa na ushirikiano wa karibu na taasisi za utafiti na elimu ya juu nchini;

(h) Kufufua Viwanda Vilivyobinafsishwa, upanuzi na ukarabati wa viwanda vilivyopo na kuchochea/ kuhamasisha uwekezaji/uanzishwaji wa viwanda vipya;

(i) Uendelezaji na uwekezaji katika maeneo maalum ya uwekezaji na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje;
(j) Uendelezaji wa taasisi za utafiti na maendeleo ya teknolojia ya viwanda na kuvutia na kuchochea matumizi ya teknolojia za kisasa;

(k) Kulinda viwanda na biashara za ndani dhidi ya ushindani usio haki;

(l) Kudhibiti ubora na viwango vya bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini na zile zinazoagizwa kutoka nje;

(m) Kujenga mifumo imara ya soko la ndani na kuhamashisha utafutaji na utumiaji wa fursa nafuu za masoko;

(n) Kuimarisha ushirikiano na OR-TAMISEMI katika maendeleo ya viwanda vidogo vidogo. Kuona uwezekano wa kuwaongeza majukumu maafisa biashara wa Halmashauri ili wawe na majukumu pia ya kusimamia viwanda vidogo vidogo katika maeneo yao kwa kushirikiana na SIDO;

(o) Kupanua na kuboresha mahusiano na ushirikiano na Taasisi za sekta binafsi, tukitambua kuwa, kisera, sekta binafsi ndio wajenzi, wamiliki na waendelezaji wa sekta ya viwanda nchini; na

(p) Kujenga uwezo wa watumishi wa Wizara na taasisi kwa kuwapa fursa za kupata elimu na ujuzi, vitendea kazi na huduma nyinginezo.

### *5.4. Mwelekeo wa Sekta ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2021/2022*

***188. Mheshimiwa Spika;*** Kwa misingi hiyo, mwelekeo wa kisketa ni kuhakikisha kuwa, nyaraka zote za kisekta zinazoongoza uwekezaji wa viwanda, uzalishaji na ufanyaji biashara nchini zinaboreshwa kwa kuzingatia mazingira na matakwa ya nyakati hususan ushindani wenye haki na kuwezesha Watanzania kushiriki kikamilifu katika kuzalisha na kutumia mali, huduma na bidhaa zinazozalishwa nchini. Lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa, mchango wa sekta katika Pato la Taifa unakua, ajira kwa Watanzania zinazalishwa na kulindwa, bidhaa zinazalishwa kwa wingi hususan zile zinazotumika na wananchi walio wengi, uzalishaji wenye tija unahimizwa, kipaumbele kikiwa kutumia rasilimali zilizopo nchini, viwanda vya ndani vinapata ulinzi wenye tija na

shindani, viwanda vipya vinajengwa na kuendelezwa, viwanda vilivyopo vinaendelea kuzalisha kwa malengo yaliyokusudiwa.

***189. Mheshimiwa Spika;*** Katika ujenzi wa viwanda, uendelezaji na ulinzi wa viwanda litakuwa jukumu letu la kipaumbele na kuhakikisha kuwa Taasisi zinazohusika kuendeleza viwanda hivyo zinajengewa uwezo unaotakiwa kumudu majukumu na matakwa ya wadau katika maeneo yote nchini. Suala la kuweka mifumo muhimu ikiwemo miundombinu ya msingi na saidizi pamoja na ujenzi wa soko la ndani vitapewa msukumo wa kipekee ili kuleta tija kwa gharama nafuu kwa wawekezaji wa ndani ya nchi yetu. Mipango ya kuboresha na kurahisisha mazingira ya uwekezaji na biashara itaendelea kuwa ajenda ya kudumu ili kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa nchi yenye mvuto kwa uwekezaji na kufanya biashara.

***190. Mheshimiwa Spika;*** Tunapozungumzia mazingira rafiki ya kufanya biashara tunalenga pia shughuli zote za viwanda na biashara ambazo zinafanywa na wananchi. Hapa kuna tatizo la mamlaka mbalimbali kufungia viwanda na biashara bila kushirikisha Wizara yenye mamlaka juu ya viwanda na biashara. Tatizo hili ni kubwa zaidi katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa ambako viwanda na biashara hufanywa kinyume cha taratibu. Ninapenda kukumbusha, kuwaomba na kuagiza tena Mamlaka zote kuacha mara moja mtindo huo. Adhabu ya kufungia kiwanda au biashara ni ya juu sana na ina athari kubwa kwa uchumi na shughuli za uchumi na jamii na zinaathiri pia mapato ya Serikali. Ni vema wahusika wakazingatia taratibu kwa kuwapa muda wahusika na kuwaelekeza taratibu za kurekebisha masuala yanayohusika badala ya kuwatoza faini kubwa na kufungia shughuli husika.

***191. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imedhamiria kuendeleza jitihada za kujenga imani kwa wafanya biashara kupitia kuweko kwa uwazi na kutabirika kwa mwelekeo wa kisera wa Serikali; Mawasiliano chanya ya mara kwa mara ambapo tunataka tunapokutana na wafanyabiashara tufanye mazungumzo yenye tija ya kubadilisha mikakati ya kukuza biashara na masoko, badala mikutano hiyo kutumika tu kama

jukwaa la kusikiliza malalamiko ya wafanyabiashara; na Kuendelea kuzipitia kanuni za mamlaka za udhibiti zinazoonekana kukwamisha biashara kila inapobidi na kwa kuzingatia matokeo ya kitafiti. Vilevile Wizara itachochea na kuhamasisha tabia ya kujali wateja (customer care) miongoni mwa watendaji wa Serikali wanaohudumia sekta mbalimbali za biashara; na Kuweka mkazo/msisitizo wa pekee katika kutafuta masoko ya bidhaa za Tanzania, hapa ndani ya Nchi na Nje ya Nchi – hususan kwa zile Nchi ambazo bado hatujazifuatilia lakini zina fursa kubwa ya masoko kama vile Nchi za Mashariki ya Kati.

***192. Mheshimiwa Spika;*** maelezo hayo yanalenga kukumbusha dhamira ya Taifa ya kujenga uchumi wa viwanda na nia ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Sita kutekeleza agenda ya viwanda ili kuleta maendeleo endelevu kwa kasi na kuchochea maisha bora kwa Watanzania.

***193. Mheshimiwa Spika;*** baada ya maelezo hayo, naomba sasa nieleze malengo ya vipaumbele kwa mwaka 2021/2022.

***MALENGO YA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA KWA MWAKA 2021/2022***

***5.5. MALENGO MAKUU YA WIZARA***

***194. Mheshimiwa Spika;*** Kwa kuzingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Ilani ya CCM (2020 – 2025) na Mpango Mkakati wa Wizara, Wizara kwa mwaka 2021/2022 itatekeleza yafuatayo:

(a) Kuhamasisha na kuendeleza uwekezaji katika viwanda na Miradi ya kielelezo;

(b) Uendelezaji wa miundombinu ya msingi katika maeneo ya Uwekezaji nchini;

(c) Kuendeleza utafiti na maendeleo ya teknolojia;

(d) Kuboresha mazingira ya biashara nchini;

(e) Kulinda viwanda na biashara za ndani na kuimarisha ushindani;

(f) Kushughulikia masuala ya ubora na viwango nchini;

(g) Kutafuta fursa za masoko na kuwaunganisha na wazalishaji wa ndani;

(h) Kuwawezesha wajasiriamali kwa kuwapa elimu na mitaji;

(i) Kuendeleza biashara; na

(j) Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi.

***5.5.1. Sekta ya Viwanda***

***195. Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2021/2022 Sekta ya Viwanda itatekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuimarisha Utafiti wa masuala ya viwanda nchini;

b) Kuweka mazingira wezeshi hasa miundombinu ya Viwanda nchini;

c) Kuhamasisha maendeleo ya Ujuzi Viwandani;

d) Kuhamasisha uongezaji thamani kwa mazao ya kilimo;

e) Kufanya mapitio ya Mikakati ya Pamba Nguo na Mavazi, Ngozi na bidhaa za Ngozi na Mafuta ya kula;

f) Kufanya tathmini ya hali halisi ya uzalishaji na mahitaji ya bidhaa viwandani Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa miradi ya kimkakati;

g) Kuhamasisha uwekezaji wa Sekta Binafsi katika maeneo maalum ya EPZ/SEZ;

h) Kueneza dhana ya KAIZEN nchini; na

i) Kukusanya Taarifa za Sekta ya Viwanda nchini.

### *5.5.2. Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo*

***196. Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuratibu uanzishwaji na uendelezaji wa Kongano mbalimbali kwa ajili ya wajasiriamali;

b) Kufanya tafiti kwa lengo la kubaini hali ya sasa ya ujasiriamali nchini;

c) Kuimarisha/Kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wajasiriamali wadogo na wa kati;

d) Kuhamasisha ubunifu na uendelezaji wa teknolojia rafiki kwa ajili ya uanzishwaji wa viwanda vidogo na vya kati;

e) Kuhamasisha uboreshaji wa bidhaa za wajasiriamali wadogo na wa kati ili kufikia soko la ndani, kikanda na kimataifa na

f) Kukamilisha marejeo ya sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo (2003) pamoja na mkakati wake

### *5.5.3. Sekta ya Biashara*

***197. Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2021/2022 Wizara kupitia Sekta ya Biashara itatekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kuendeleza majadiliano ya kibiashara kati ya Nchi na Nchi (Bilateral), Kikanda (Regional) na Kimataifa (Multilateral) kwa ajili ya kupanua fursa za masoko na uwekezaji ili kuvutia uwekezaji nchini;

(b) Kuendeleza majadiliano ya biashara kwenye nchi za China, Urusi, Mauritus, Uturuki, Misri, Israel, DRC Congo, Sudani ya Kusini, Vietnam na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na kuingia nazo makubaliano ya biashara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi;

(c) Kuendelea na majadiliano ya kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara kwa Nchi za Afrika (Continental Free Trade Area – CFTA);

(d) Kukamilisha majadiliano ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu linalojumuisha Kanda za COMESA, EAC na SADC;

(e) Kukamilisha majadiliano ya biashara ya huduma kwa sekta sita (6) za kipaumbele katika nchi wanachama wa SADC;

(f) Kutekeleza Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye masuala ya biashara ya bidhaa na huduma;

(g) Kuratibu na kushiriki kwenye majadiliano ya biashara ya kimataifa katika mashirika yaliyo chini ya Umoja wa Mataifa na mengineyo ikiwemo WTO, UNCTAD, CFC na ITC;

(h) Kuhamasisha Jumuiya ya Wafanyabiashara kuhusu fursa za masoko ya upendeleo yatakonayo na majadiliano ya Nchi na Nchi, Kikanda na Kimataifa;

(i) Kukamilisha utungaji wa Sheria ya Kujilinda Kibiashara (Trade Remedies Act)

(j) Kutekeleza Mkataba wa Shirika la Biashara Duniani (WTO) unaohusu uwezeshaji wa Biashara;

(k) Kukamilisha mapitio na kuanza utekelezaji wa Sera mpya ya Taifa ya Biashara;

(l) Kuimarisha kamati za kitaifa za kusimamia urahisishaji wa biashara nchini; na

(m) Kuandaa miradi na program mbalimbali kwa ajili ya kujenga uwezo kwa wataalam na Sekta Binafsi; ***5.5.4. Sekta ya Masoko***

***198. Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Sekta ya Masoko itatekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini;

(b)Kuwaunganisha wazalishaji,wasindikaji na wafanyabiashara na masoko ya ndani na nje ya nchi;

(c) Uhamasishaji wa matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala;

(d) Kuhamasisha na kurahisisha biashara mipakani;

(e) Kuhamasisha na kuwezesha utangazaji wa bidhaa na huduma za Tanzania;

(f) Ukusanyaji, Uchambuzi na Usambazaji wa Taarifa za Masoko;

(g) Kuandaa na kupitia Sera, Sheria na Kanuni mbalimbali kama vile:

• Kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003;

• Marekebisho ya Sheria ya Viwango Na.2 ya 233 mwaka 2009 na Kanuni zake

• Kukamilisha Sera ya Taifa ya Ubora;

• Kuandaa Mkakati wa Kukuza Mauzo Nje;

***5.5.5. Maendeleo ya Rasilimali Watu***

***199. Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Idara ya Utawala na Rasilimali Watu itatekeleza masuala yafuatayo:-

**Maendeleo ya Rasilimali Watu:**

a) Kuajiri watumishi (58) wa kada na ngazi mbalimbali kwa lengo la kuwezesha Idara na Vitengo;

b) Kupandisha vyeo watumishi (124) wa kada mbalimbali;

c) Kupeleka watumishi (11) katika mafunzo ya muda mrefu na watumishi (25) katika mafunzo ya muda mfupi ya nyanja mbalimbali kwa lengo la kuwajengea uwezo, kuongeza ufanisi;

d) Kuandaa watumishi (5) wanaotarajia kustaafu na kukidhi mahitaji ya kimuundo;

e) Kutekeleza Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi – Mwamtuka (OPRAS) kwa:

• Kutoa mafunzo kwa watumishi wapya (58) watakaoajiriwa ya namna ya ujazaji wa fomu za OPRAS,

• Kuhakikisha kuwa Watumishi (204) wanasaini mikataba yao ya kazi kwa wakati, ·

• Kufanya mapitio ya nusu mwaka; na

• Kufanya tathmini ya utendaji kazi wa Watumishi wa mwaka mzima kwa wakati.

f) Kuratibu na kusimamia masuala yote ya uendeshaji wa shughuli za Wizara;

g) Kutoa huduma stahiki kwa viongozi na watumishi wa Wizara kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo katika Utumishi wa Umma; h) Kuandaa programu mbalimbali za michezo kama vile mabonanza na kushiriki katika mashindano ya SHIMIWI kwa lengo la kujenga afya za watumishi, kuongeza ushirikiano na kufahamiana; na

i) Kuhakikisha watumishi (5) watakaohitimisha ajira zao wanalipwa mafao kwa wakati.

***Masuala Mtambuka:***
**a)** ***Rushwa:*** Kuendeleza jitihada za kupambana na kudhibiti rushwa kwa watumishi kwa kuweka mikakati mbalimbali na

kutoa mafunzo juu ya Sheria Kanuni na Taratibu kuhusu uzingatiaji wa maadili, uwajibikaji na utoaji huduma bora katika utumishi wa umma na kuhakikisha zinafuatwa na watumishi wote. Vilevile, Wizara kupitia dawati lake la malalamiko itaendelea kukusanya na kupokea malalamiko na kero kutoka kwa wateja wa ndani na nje ya ofisi kwa lengo la kuzitatua ikiwa ni njia mojawapo ya kudhibiti na kupambana na rushwa mahali pa kazi.

**b)** ***Ukimwi na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza:*** Wizara itaendelea na jitihada za kupambana na maambukizi ya VVU mahala pa kazi kwa kuzingatia Waraka wa Utumishi Na. 2 wa mwaka 2014 kuhusu Kudhibiti Virusi vya UKIMWI, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa Mahali pa Kazi katika Utumishi wa Umma na kuwahudumia watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na waliojiweka wazi. Aidha, Wizara itaendesha Semina kwa watumishi ikiwa ni njia ya uhamasishaji na uelimishaji wa masuala ya UKIMWI pamoja na upimaji afya wa hiari ili kudhibiti UKIMWI na Magonjwa sugu yasiyoambukizwa mahala pa kazi.

**c)** ***Masuala ya Jinsia:*** Wizara kupitia dawati la jinsia itaendelea kuratibu masuala ya kijinsia na kuyahuisha kwenye sera, mipango, mikakati na program za Wizara pamoja na Taasisi zake katika mwaka 2021/2022.

### *5.5.6. TEHAMA na TAKWIMU*

***200. Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Kitengo cha TEHAMA na Takwimu kitatekeleza masuala yafuatayo:-

(a) Kusimamia matumizi bora na sahihi ya miundombinu ya TEHAMA katika kutoa huduma ndani na kwa wateja wa nje;

(b) Kuboresha miundombinu ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi kwa wafanyakazi katika utoaji wa huduma kwa umma;

(c) Kutoa mafunzo kwa watumishi kuhusu matumizi bora na sahihi ya Miundombinu na Rasilimali za TEHAMA; na

(d) Kuimarisha mifumo ya ukusanyaji Takwimu/ taarifa za Viwanda, Biashara na Masoko.

### *5.5.7. Ununuzi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha*

***201. Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Kitengo cha Ununuzi kitaendelea kusimamia shughuli za ununuzi wa bidhaa na huduma kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi Na.7 ya mwaka 2011 na kanuni zake GN Na, 446 ya mwaka 2013, kama zilivyo fanyiwa marekebisho mwaka 2016 pamoja na miongozo inayotolewa na Mamlaka ya Udhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA). Masuala yafuatayo yatatekelezwa:-

a) Kuandaa Mpango wa Ununuzi kwa mwaka 2021/2022;

b) Kufanya ununuzi wa bidhaa na huduma kupitia Mfumo wa Kielektroniki (Tanzania Electronic Procurement system - TANePS);

c) Kuratibu vikao vinne (4) vya Bodi ya Zabuni ya Wizara kwa mwaka 2021/2022;

d) Kuandaa taarifa za ununuzi za kila mwezi, robo pamoja na taarifa ya mwaka na kuziwasilisha Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA); na

e) Kuhakiki mali za Wizara, kuhuisha taarifa za Daftari la Mali la Wizara kwa mujibu wa Muongozo wa Mali za Serikali wa mwaka 2019 pamoja na Sheria ya Fedha Na. 6 ya mwaka 2001 na Kanuni zake, GN.132 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2004.

## *5.6.MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA 2020/2021*

### *5.6.1. Taasisi za Kuendeleza Uwekezaji*

#### *i) Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)*

***202. Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kuanzisha Kilimo shirikishi cha Ufuta na Mawese (Block farming) katika mikoa ya Pwani na Kigoma

(b) Kuzalisha zana ndogondogo za kilimo na Vipuri kwa kushirikiana na Taasisi za Utafiti na KMTC

(c) Kuanzisha Kiwanda cha Mbolea na Upimaji wa afya ya Udongo

(d) Kuanza utekelezaji wa mradi wa Mchuchuma na Liganga

(e) Kukamilisha tafiti za mradi wa Magadi soda na kujenga kiwanda –Engaruka

(f) Kuendelea na Utekelezaji wa Mradi wa Matrekta ya URSUS

(g) Kufanya ukarabati wa kiwanda cha KMTC kwa kujenga foundry na kubadilisha baadhi ya mashine

(h) Kufufua na kuendesha Kiwanda cha Matairi cha Arusha bila kutegemea wawekezaji binafsi.

(i) Kuchimba makaa ya mawe Katewaka-

***ii) Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uzalishaji wa Bidhaa kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi (EPZA)***

***203. Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uzalishaji wa Bidhaa kwa Mauzo Nje ya Nchi (EPZA) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendeleza Maeneo Maalum ya Kiuchumi yenye dhima mahsusi inayozingatia Jiografia na rasilimali zilizopo katika eneo husika (Thematic Approach to Development of SEZs) katika maeneo yaliyolipiwa fidia na kuhamasisha ushiriki wa Serikali za Mikoa na Halmashauri za Miji katika uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Uwekezaji;

(b) Kuweka alama na kuimarisha ulinzi katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi yaliyokwishalipiwa fidia ili yasivamiwe;

(c) Kuainisha na kuhamasisha uwekezaji katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi – SEZ;

(d) Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi iliyo chini ya SEZ - (Monitoring and Evaluation);

(e) Kupitia Sheria zinazosimamia Mamlaka ya EPZ ili kuendana na wakati;

(f) Kuboresha mifumo ya utoaji huduma kwa kutumia TEHAMA; na

(g) Kuimarisha Rasilimali Watu katika Mamlaka ya EPZ.

***5.6.2. Taasisi za Utafiti, Maendeleo ya Teknolojia na Mafunzo***

***i) Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO)***

***204. Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) itatekeleza malengo yafuatayo:

(a) Kuendeleza Mitaa ya Viwanda ya SIDO na kutengeneza Mfumo Unganishi wa shughuli za TEHAMA za Shirika;

(b) Kuhawilisha teknolojia kwa Kuimarisha vituo vya uendelezaji teknolojia (TDCs) na Vituo vya mafunzo na uzalishaji (TPC) vya SIDO;

(c) Kutunisha Mtaji wa Mfuko wa Wafanyabiashara Wananchi (NEDF); na

(d) Kuanzisha kituo kimoja cha kutengeneza vifungashio na kununua kwa wingi na kuimarisha usambazaji wa vifungashio kwa wajasiriamali mikoa yote.

***ii) Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO)***

***205. Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania

(TIRDO) itatekeleza yafuatayo:- (a) Kuendelea kutoa huduma za kitaalam viwandani zenye lengo la kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora bila kuchafua mazingira pia zinazolenga matumizi bora ya nishati;

(b) Kuendelea na mchakato wa kufanya utafiti na kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali wa Sekta ya Ngozi jinsi ya kupunguza uharibifu wa mazingira kwa kuhifadhi na kurejesha taka za ngozi ili kutengeneza bidhaa kama 'Leather boards';

(c) Kuendelea na kukamilisha mchakato wa kupata ithibati (Accreditation) na kuboresha maabara za chakula, Kemia na mazingira ili ziweze kufikia viwango vya kimataifa na kuweza kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani;

(d) Kuendelea kutekeleza miradi mbalimbali yenye lengo la kuleta teknolojia mpya za uzalishaji;

(e) Kuendelea kutekeleza zoezi la kupata ramani ya viwanda nchini (Industrial Mapping) ili kupata kanzidata ya uhakika ya viwanda,

(f) Kuanzisha Kituo cha Taarifa za Viwanda (Industrial Information Centre) na Kituo cha Ubashiri wa Teknolojia za Viwanda (Industrial Technology Forecasting and Foresighting) ili kuweza kupata taarifa za maendeleo na kanzidata za viwanda kwa wakati na kusaidia viwanda kwenye ushindani wa teknolojia za viwanda, na

(g) Kuendelea kukamilisha marejeo ya Sheria ya Bunge Na.5 ya mwaka 1979 iliyoanzisha TIRDO kwa kufuatilia ripoti ya mapitio ya Sheria iliyokwisha wasilishwa Wizara mama na hatimaye kupelekwa Bungeni,

***iii) Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC)***

***206. Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kufanya uchunguzi wa namna bora ya kudhibiti kinyesi cha kuku wanaofugwa kwenye viota (cage) katika eneo finyu kwenye miji na maeneo yanayozunguka miji ili kutunza na kuboresha usafi wa mazingira;

(b) Kubuni na kuunda teknolojia ya kutenganisha maganda na kiini cha mbegu ya chikichi ambayo inahamishika;

(c) Kuunda teknolojia ya Kipandio kinachofaa kupanda mbegu za ufuta, alizeti, pamba na karanga ili kuchangia kuongeza uzalishaji wa mazao yenye kutoa mafuta ya kula nchini;

(d) Kufanya usanifu wa teknolojia ili kufikia hatua bora kabisa (design optimization) na kuziingiza kwenye soko la wadau;

(e) Kufanya tathmini ya mahitaji ya teknolojia katika hali ya uchimbaji madini kwa wachimbaji wadogo;

(f) Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Wajasiriamami wadogo 5 wanaojishughulisha na ubunifu na utengenezaji wa zana za kilimo na teknolojia za vijijini;

(g) Kuanzisha Vituo vya Ukaguzi na Majaribio katika maeneo matatu (3) muhimu ya Bandari na mipakani ambayo ni Bandari ya Dar –es Salaam, Horohoro mkoani Tanga na Tunduma mkoani Songwe;

(h) Kununua vifaa, mitambo, mashine na magari ya kusaidia kufanikisha kazi za ukaguzi na majaribio ya Zana za Kilimo na teknolojia za vijijini; na

(i) Kujenga ufahamu na kusimamia utekelezaji wa Kanuni za Majaribio na Ukaguzi wa zana za Kilimo na teknolojia za vijijini.

(j) Kujenga uwezo wa rasilimali watu kwenye Kada ya utafiti na wafanyakazi wengine wasio watafiti kwa kuwapa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu.

***iv) Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO)***

***207. Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Shirika la Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO) litatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea na uboreshaji wa karakana na ofisi ya usanifu pamoja na miundombinu ya Taasisi kwa ujumla;

(b) Kujenga uwezo wa wafanyakazi wa Taasisi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu ili kuboresha utendaji kazi;

(c) Kuendeleza ubunifu na kutengeneza chasili cha mtambo wa kuchakata na kukausha mazao ya kilimo (Muhogo) na kukausha korosho pamoja na kubangua (drying and scooping) ili kuongeza thamani;

(d) Kubuni na kuendeleza chasili cha mtambo mdogo wa kuchakata miwa na kutengeneza sukari (Mini/ small scale sugar processing technology);

(e) Kuendeleza ubunifu na maboresho katika utengenezaji wa mtambo wa kukamua na kusindika mafuta ya mbegu za alizeti;

(f) Kusanifu na kuendeleza chasili cha mtambo wa kuchakata michikichi ili kupata mafuta ya kula pamoja na mazao yake mbalimbali;

(g) Kuendeleza ubunifu na maboresho ya kutengeneza mtambo wa kuteketeza taka ngumu za hospital (Existing biomedical solid waste incinerator) ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi pamoja na kuweza kutumika katika kuteketeza/ kuchoma damu zisizo salama na madawa ya hospitali yaliyokwisha muda wake kwa kiwango cha nyuzi joto 1500 – 2000 (Ni maombi ya MSD kusanifu “incinerator” hiyo);

(h) Kubuni na kuendeleza chasili cha jokofu la ngazi tatu la kuhifadhi maiti katika hospitali;

(i) Kubuni na kuendeleza chasili cha mtambo wa kuchakata zao la mkonge;

(j) Kuhawilisha teknolojia na kuhamasisha utengenezaji kibiashara wa mitambo iliyobuniwa na Taasisi ukiwemo mtambo wa kusindika mafuta ya kula yatokanayo na mbegu za mchikichi; na

(k) Kujitangaza ili kujenga uelewa kwa umma kuhusu shughuli zinazofanywa na Taasisi ya TEMDO kwa kushiriki kwenye maonesho angalau manne ya teknolojia/biashara (kama vile DITF, Nane nane, Maonesho ya kanda ya SIDO, n.k).

***v) Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)***

***208. Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Chuo Cha Elimu ya Biashara (CBE) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuimarisha na kuendeleza rasirimali watu hasa katika hatua ya shahada za Uzamivu;

(b) Kufanya upembuzi yakinifu katika kuboresha makazi ya watumishi katika eneo la Oysterbay Dar es Salaam;

(c) Kuimarisha na kuboresha mifumo ya TEHAMA;

(d) Kufanya ukarabati mkubwa wa minudombinu ya kufundishia na kujifunzia, Kampasi ya Dar es salaam na Dodoma; na

(e) Ujenzi wa Kampasi ya Mbeya.

***5.6.3. Taasisi za Ushindani na Udhibiti wa Ubora wa Bidhaa na Huduma***

***i) Shirika la Viwango Tanzania (TBS)***

***209. Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) itatekeleza yafuatayo:-

a) Kutayarisha viwango 580 vya kitaifa katika sekta/ nyanja mbalimbali ikiwemo nyanja za uhandisi mitambo (mechanical), kemikali (chemical), uhandisi umeme (electro technical), kemikali (chemicals), sekta nguo na ngozi (textile and leather), madini (mining and minerals), sekta ya kilimo na chakula (food and agriculture), mazingira (environment) pamoja na sekta mtambuka (general techniques).

b) Kutoa leseni ya ubora kwa bidhaa 600 kutoka katika sekta mbalimbali zikiwemo bidhaa za wajasiriamali wadogo (SMEs);

c) Kusajili majengo, maeneo ya uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa za chakula na vipodozi (food and cosmetic premises) 19,530;

d) Kusajili bidhaa za chakula na vipodozi (food and cosmetic products) 6,040;

e) Kukagua na kutoa vibali (Certificate of Conformity – CoCs) 68,000 kwa bidhaa zitokazo nje ya nchi pindi zinapowasili bandarini (Destination Inspection).

f) Kufanya ukaguzi wa ubora na kutoa leseni za ukaguzi 45,000 za magari yaliyotumika (used motor vehicles) yanayoingizwa nchini;

g) Kutoa ripoti 170 za kitaalamu kwa wasafirishaji wa bidhaa nje ya nchi (technical assistance to exporters);

h) Kutoa mafunzo na semina 150 kuhusu viwango na udhibiti wa ubora (Quality Assurance Training) kwa wadau mbalimbali;

i) Kupima sampuli 52,000 za bidhaa mbalimbali;

j) Kufanya ugezi kwa vifaa/mashine mbalimbali vipatavyo 10,000; na

k) Kuanza ujenzi wa Viwango House Dodoma.

***ii) Wakala wa Vipimo (WMA)***

***210. Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo (WMA) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia, kuhakiki na kukagua vipimo vyote vitumikavyo na viingiavyo nchini kwa lengo la kumlinda mlaji;

(b) Kuendelea na ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa kwenye maeneo ya mipakani, bandarini na viwandani kwa lengo la kuhakiki usahihi wa kiasi/ idadi iliyotamkwa (decraled quantity);

(c) Kununua vitendea kazi yakiwemo magari Mawili na vitendea kazi vya kitaalam;

(d) Kuongeza idadi ya Watumishi300 (Maafisa Vipimo 200, Maafisa Vipimo wasaidizi 50 na Madereva 50);

(e) Kuendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu matumizi sahihi ya vipimo; na

(f) Kuwajengea uwezo (Capacity building) watumishi wa Wakala wa Vipimo kwa kuwapeleka mafunzo ndani na nje ya nchi ili kuongeza elimu na ujuzi.

***iii) Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)***

***211. Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) itatekeleza yafuatayo:-

a) Itaendelea kuelemisha umma kuhusu umuhimu wa kusajili shughuli mbalimbali za kibiashara BRELA na mabadiliko mbalimbali ya sheria zinazosimamiwa na BRELA.

b) Itaendelea kuongeza wafanyakazi, kutoa mafunzo kwa watumishi na kuongeza vitendea kazi kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi katika kutoa huduma

c) Itaendelea kuimarisha mifumo na miundombinu ya BRELA na kuhamasisha umma kuhusu matumizi ya mifumo ya TEHAMA ya utoaji huduma inayosimamiwa na BRELA.

d) Itaendelea kuimarisha mahusiano kati yake na Wakurugenzi wa Halmashauri na Maafisa Biashara kwa lengo la kufikisha huduma za BRELA kwa umma katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na kuanzisha Vituo vya Pamoja vya Utoaji wa Huduma za Usajili wa Biashara kwenye Halmashauri zote nchini.

e) Kuimarisha mfumo wa ORS na kurahisisha taratibu za matumizi yake ikiwa ni pamoja na kuwezesha mfumo huo kutumika kutoa leseni za Daraja “B” na “C”.

***iv) Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB)***

***212. Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kusimamia utekelezaji wa mfumo wa stakabadhi kwa waombaji wa leseni za kuendesha ghala kwa mazao mbalimbali kwa kutoa leseni, kufanya ukaguzi na kufuatilia utekelezaji wa kanuni za mfumo wa stakabadhi,

b) Kuwaunganisha wakulima na taasisi za fedha ili kupata huduma za kifedha kwa urahisi kupitia mfumo wa stakabadhi za ghala,

c) Kuviunganisha viwanda vya kusindika mazao kununua kutoka ghala zinazotumia mfumo wa stakabadhi za ghala,

d) Kuweka miongozo kwa kila zao litakalotumia Mfumo wa Stakabadhi za ghala kwa kushirikiana na taasisi nyingine zinazohusika na mnyororo wa thamani wa mazao hayo,

e) Kutoa elimu ya mfumo wa stakabadhi za ghala kwa wadau mbalimbali ili kukuza manufaa ya mfumo huu kwa watumiaji hususan wakulima na wasindikaji wa mazao,

f) Kupanua matumizi ya mfumo wa stakabadhi katika mazao ya nafaka, mbegu za mafuta na mazao mengine. Aidha, mfumo utapanuliwa ili kuingiza mazao yasio ya kilimo kama vile Wanyama hai, Nyama, Ngozi na mbao.

g) Kuandaa Ghala za Mfano za kielektroniki zitakazokuwa katika madaraja mbalimbali kulingana na mahitaji ya watumiaji yatakayopatikana kwa njia ya mtandao

h) Kushirikiana na Mikoa, Halmashauri za Wilaya, Vyama vya Ushirika na Taasisi nyingine kufanikisha udajishaji wa Ghala na kutoa mwongozo kuhusu ujenzi wa ghala za kuhifadhi mazao ya wakulima; na

i) Kuendelea kuhamasisha utekelezaji wa BLUEPRINT katika shughuli za Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala.

***v) Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE)***

***213. Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Mamlaka ya Biashara Tanzania (TANTRADE) itatekeleza yafuatayo:-

a) Kuratibu ukusanyaji wa matarajio ya Mavuno ya Mazao na kuunganisha na masoko kwa kusanifu mfumo shirikishi wa kukusanya takwimu za uzalishaji; kuanzisha consolidation center kwa mazao yasiyo na Bodi na mfumo wa ghala; kutambua wanunuzi wa ndani na madalali; kutambua watoa huduma wa kila zao katika consolidation centers na kuanzisha vikundi vya uzalishaji kwa mazao yasiyo na Bodi ili kufahamu wazalishaji kwa urahisi na kuwaunganisha na soko;

b) Kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kutekeleza mikakati ya kukuza ujasiriamali kupitia Vituo vya Pamoja vya Utoaji wa Huduma za Kibiashara kwenye Halmashauri nchini.

c) Kuanzisha Mfumo wa kusimamia Kilimo cha Mkataba kati ya Wakulima na Wafanyabiashara kwa: kutambua maeneo ya uzalishaji mkubwa wa mazao yasiyo na Bodi na yasiyo na

mifumo maalum ya masoko; wanunuzi wakubwa kwa mazao yanayozalishwa nchini; kuandaa kanuni za biashara za mkataba; kutoa elimu na uhamasishaji wazalishaji na wanunuzi; Kuratibu mikutano mbalimbali ya kuwakutanisha wanunuzi na wazalishaji; na kutambua watoa huduma za fedha 'vifungashio' na teknolojia kwa wazalishaji wa bidhaa nchini;

d) Kuimarisha mfumo wa *Market Intelligence* ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za masoko kwa kukusanya na kutunza Takwimu za Biashara za ndani na nje ya nchi kila wiki; kupanua wigo wa ukusanyaji na usambazaji wa bei za mazao kwenye masoko; kuboresha na kuimamrisha mbinu za kusambaza Taarifa za biashara; kuratibu Semina za kutangaza fursa za biashara katika Masoko ya kimkakati na kuongeza idadi ya wadau wanaopata taarifa za biashara

e) Kukuza Biashara ya Mazao na bidhaa za viwandani zinazozalishwa nchini katika masoko ya Kikanda kwa; kuimarisha tafiti na mifumo ya uchambuzi na usambazaji wa fursa za masoko; kuandaa mfumo wa kutambua na kuingia makubaliano na wanunuzi na kutangaza bidhaa na kukutanisha wazalishaji na wanunuzi kupitia mikutano ya B2B na misafara ya kibiashara;

f) Kuimarisha Ushirikiano wa TanTrade na Ofisi za Ubalozi kwa kuweka mfumo wa mawasiliano kwa kupitia Wizara Mama; kuanzisha Maeneo ya kuoneshea Bidhaa (Display Centers) na upatikanaji wa Taarifa muhimu za bidhaa za Tanzania ; na kuimarisha inteligensia ya masuala ya Biashara kwa Maofisa wa Ubalozi na kubadilishana uzoefu na mikakati ya utatuzi wa changamoto za biashara;

g) Kuimarisha mifumo ya Soko la Ndani kwa kuandaa Mwongozo wa kufanya biashara katika maeneo ya mikusanyiko; kuandaa kanuni za kisheria za kusimamia mifumo ya soko la ndani nchini; kubuni mifumo ya kusimamia na kuratibu uuzaji wa bidhaa katika masoko ya bidhaa, nafaka, madini, minada ya mifugo na uvuvi; kutoa taarifa ya mwaka ya mwenendo wa Sekta ya Biashara nchini; kuanzisha

program za kuhamasisha matumizi ya bidhaa zinazolishwa na viwanda vya Tanzania; kuanzisha program za kupunguza utegemezi wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi; kufanya tafiti za kina za fursa za biashara zilizopo katika maeneo ya uwekezaji wa Serikali kama vile treni ya mwendo kasi, huduma za utalii katika mradi wa bwawa la umeme la Mwalimu Nyerere;

h) Kusimamia Sekta ya Maonesho kwa kuwezesha shughuli za ukuzaji biashara nchini (Trade Promotion Events) kama vile Maonesho na Misafara ya Biashara kwa kuhakikisha shughuli hizo zinafuata taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria;

i) Kuimarisha biashara mipakani kwa kuwezesha wafanyabiashara kukidhi vigezo vya kibiashara, kujenga mazingira rafiki ya biashara na kurahisisha bidhaa kuvuka mipaka mara baada ya ukaguzi; kutoa elimu juu ya matumizi ya utaratibu wa Uasili wa Bidhaa, sheria na taratibu za kufanya biashara mipakani; kuimarisha vikundi vya usimamizi wa biashara mipakani na kuimarisha mfumo wa upokeaji wa maoni na malalamiko mipakani; na

j) Kuimarisha biashara ya Zanzibar kwa kuanzisha nembo za kutangaza na kuendeleza bidhaa za kipaumbele; kuratibu programu za kuongeza thamani wa zao la Mwani; kusimamia mradi wa Dagaa katika eneo la Fungurefu Mkokotoni; kufanya tafiti na upembuzi yakinifu za fursa na biashara; na kutafuta masoko yenye tija kwa bidhaa zinazozalishwa Zanzibar.

***vi) Tume ya Ushindani (FCC)***

***214. Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Tume ya Ushindani (FCC) itatekeleza yafuatayo:

a) Kuboresha hali ya ushindani katika soko (Competition Protection and Promotion improved) kupitia:

i. Kuharakisha uchunguzi na kufanya maamuzi kwenye mashauri manne (4) ya miunganiko ya kampuni

yatakayofanyika bila kuiarifu FCC; mashauri manne (4) katika suala la matumizi mabaya ya nguvu ya soko; mashauri manne (4) katika suala la makubaliano yanayofifisha ushindani; mashauri matatu (3) ya makubaliano baina ya washindani kuhusiana na kupanga bei, kupunguza uzalishaji, kugoma kusambaza bidhaa au huduma; na kufanya utetezi wa maamuzi yake yatakayofikishwa katika Baraza la Ushindani, Mahakama Kuu ya Tanzania na Mahakama ya Rufani.

ii. Kufanya tafiti tatu (3) katika masoko kwenye sekta za kiuchumi zenye lengo la kubaini mienendo inayokinzana na Sheria ya Ushindani; iii. Kutoa elimu na ushawishi juu ya uelewa wa Sheria ya Ushindani katika uchumi wa soko, kwa:

b) Wadau wakuu ambao ni pamoja na Serikali na Taasisi zake, wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu vya umma na binafsi na wafanyabiashara.

c) Kupitia (review) sera, sheria, mipango na taratibu za Serikali na kushauri ya hatua za kuchukua pindi sera, sheria, mipango na taratibu hizo zinapofifisha /kuathiri ushindani katika soko.

i. Kufanya uchunguzi wa malalamiko ya walaji juu ya vitendo hadaifu vya wafanyabiashara nchi nzima na kuyatatua,

ii. Kutoa elimu na ushawishi juu ya sheria ya kumlinda mlaji kwa wadau wote wa soko kupitia semina na vipindi vya vyombo vya habari,

iii. Kufanya Uchunguzi wa bidhaa na huduma zinazohadaa ama kuwadanganya walaji,

iv. Kuandaa Mikataba ya Makabaliano (Memorandum of Understanding) na taasisi za kimkakati katika kuwalinda walaji dhidi ya mienendo potofu na hadaifu sokoni,

v. Kuandaa kanuni mbalimbali baada ya marekebisho ya Sheria ya Ushindani ili kuongeza nguvu ya utekelezaji kisheria.

vi. Kuongeza mapambano dhidi ya bidhaa bandia na pia kuhakikisha kiwango cha bidhaa hizo kinapungua katika soko.

d) Kuongeza ufanisi katika kutoa huduma (Service delivery capacity improved) kwa: -

i. Kuboresha vitendea kazi kwa kununua samani za ofisi na kompyuta,

ii. Kuimarisha mifumo ya utoaji huduma za FCC kwa njia ya kielektroniki,

iii. Kuongeza wafanyakazi mpaka kufikia 85 ikilinganishwa na idadi ya sasa ya Wafanyakazi 73, na iv. Kuimarisha ofisi ya Dodoma kwa kuanza ujenzi wa Jengo la FCC na kuanzisha ofisi ya Kanda mkoa wa Tanga.

***vii) Baraza la Ushindani (FCT)***

***215. Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Baraza la Ushindani (FCT) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kupokea, kusikiliza na kutoa maamuzi ya mashauri ya rufaa yanayowasilishwa katika Baraza ambapo lengo letu ni kutoa maamuzi ya mashauri 70.

(b) Kuimarisha uwezo wa kutekeleza majukumu ya Baraza. Hii ikiwa pamoja na uboreshaji wa mifumo ya Baraza (ikiwemo: case management system; na information management system); na Mafunzo ilikuongeza kasi ya usikilizwaji wa mashauri yanayowasilishwa katika Baraza;

(c) Kuendelea kufanya utafiti wa kisheria na kiuchumi katika ushindani na udhibiti kwa ajili ya kusaidia katika uendeshaji wa mashauri ya Baraza;

(d) Kuongeza uelewa kwa Wadau wengi zaidi na Jamii kwa ujumla juu ya shughuli za Baraza na haki katika ushindani wa soko;

(e) Kuboresha vitendea kazi vya Baraza; na (f) Kushughulikia masuala Mtambuka.

## 6. MAKADIRIO YA MAKUSANYO NA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2021/2022

### *6.1.Makusanyo ya Serikali*

***216. Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2021/2022, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya Shilingi 15,000,000 kutokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni na makusanyo mengine. Kati ya fedha hizo, Shilingi 9,000,000 zitakusanywa katika Fungu 44 na Shilingi 6,000,000 zitakusanywa katika Fungu 60.

### *6.2.Maombi ya Fedha*

***217. Mheshimiwa Spika;*** Kwa mwaka 2021/2022, Wizara ya Viwanda na Biashara inaomba kutengewa jumla ya Shilingi 105,670,459,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 52,582,573,000 ni za Matumizi ya Kawaida na Shilingi 53,087,886,000 ni za Matumizi ya Maendeleo zikiwemo Shilingi 400,000,000 fedha za nje. Aidha, katika Bajeti hiyo, Shilingi 81,398,833,000 ni za Fungu 44 (Viwanda) na Shilingi 24,582,573,000 ni za Fungu 60 (Biashara).

## 7. SHUKRANI

***218. Mheshimiwa Spika;*** Napenda kuwashukuru na kuwatambua Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia kwa njia moja au nyingine katika jitihada za ujenzi wa uchumi wa viwanda. Washirika hao ni nchi rafiki za Austria, Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Sweden, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi. Aidha, tunayashukuru Mashirika ya Kimataifa: ARIPO, Benki ya Dunia, CFC, DANIDA, DFID, EU, FAO, IFAD, JICA, Jumuiya ya Madola, KOICA, SIDA, Taasisi za Umoja wa Mataifa (UNCTAD, UNDP, UNIDO, UNWOMEN), USAID, WIPO, FSDT, TMEA, SADC na WTO. Vilevile, tunazishukuru Wizara, taasisi zote za umma, Sekta Binafsi,

taasisi zisizo za kiserikali (CBOs & FBOs) kwa kutoa ushirkiano unaohitajika katika ujenzi shirikishi wa uchumi wa viwanda. Ni azma yetu kuhakikisha kuwa ushirikiano huo unaendelezwa ili kuleta matokeo yanayokusudiwa kwa nchi na jamii nzima ya Watanzania kwa ujumla.

***219. Mheshimiwa Spika;*** Tunawashukuru sana Wananchi wote na hususan Watanzania ambao kwa uzalendo wao wameendelea kuelewa na kushiriki kutekeleza ujenzi wa uchumi wa viwanda na pia kufuatilia kwa karibu miongozo na jitihada za Serikali katika azma hiyo. Tunawasihi Watanzania wote kuendeleza ari hiyo ambayo ni kichocheo muhimu katika kuiletea nchi manufaa kwa kizazi cha sasa na vijavyo.

## 8. HITIMISHO

***220.* Mheshimiwa Spika;** Tanzania ndiyo nchi yetu Watanzania na hatuna mwingine wa kuijenga bali ni sisi Watanzania wenyewe. Hivyo hatuna budi kutekeleza kwa dhati maamuzi na msimamo makini wa Serikali wa ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini ili tusiwe katika ulimwengu wa watazamaji na wasimuliaji wa kudumu wa maendeleo ya nchi nyingine. Tunatambua kuwa kujenga ushindani katika kujiletea maendeleo ni vita vya kiuchumi visivyoepukika. Hivyo katika kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, tunategemea kuongeza kasi na umakini katika kujenga ushindani uendelevu hususan katika kuendeleza shughuli za viwanda na biashara na kutumia fursa zote za masoko ya ndani na nje ya nchi. Ni dhahiri kuwa hatua ya maendeleo tuliyofikia na tunakoelekea twalazimika kujiimarisha zaidi kiushindani kwani fursa za upendeleo zinaelekea ukingoni au kukoma. Tunapaswa kujizatiti kusimama kwa miguu yetu ili maendeleo ya watu na nchi kwa ujumla iwe ni matokeo halisi ya jitihada za Watanzania wenyewe. Nchi yetu imejaliwa rasilimali nyingi ambazo tunapaswa kuzitumia kwa nidhamu, umakini na uendelevu ili ziendelee kuwanufaisha Watanzania. Kwa kuwa sera, sheria na mikakati ya Serikali imejikita kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji na kwa kuwa tumejipanga na

kuchagua ujenzi wa uchumi wa viwanda, basi hatuna budi kukubali kuwa kazi iendelee.

**9. MAOMBI RASMI YA FEDHA**

***221. Mheshimiwa Spika;*** Naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio ya Wizara ya Viwanda na Biashara ya kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi 15,000,000 na matumizi ya jumla ya Shilingi 105,670,459,000 kwa mwaka 2020/2021.

**10. MWISHO**

***222. Mheshimiwa Spika;*** Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara yenye anuani ifuatayo: *www. mit.go.tz.*

***223. Mheshimiwa Spika;*** Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Waziri wa Viwanda na Biashara kwa wasilisho zuri sana la taarifa yako na limeungwa mkono. *(Makofi)*

Sasa namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ili aweze kuwasilisha Taarifa yao ya Kamati. Karibu Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. DAVID M. KIHENZILE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara Fungu Namba 44 - Viwanda na Fungu Namba 60 - Biashara kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi Fungu 44 na 60 ya mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, uzima na nafasi nyingine kukutana hapa Dodoma katika Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi na Mbili. Kabla ya kuendelea kutoa maoni, nitangulie kuomba kuwa Taarifa yote iingizwe katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira naomba nitumie fursa hii kushukuru kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati hii kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inaeleza namna Kamati yangu ilivyotekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti ya Kanuni 117(1) na (2) na imeainisha mapendekezo kadhaa ambayo Kamati inaamini ni muhimu yafanyiwe kazi kwa wakati wa utekelezaji wa majukumu ya bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Aidha, taarifa hii inalenga pia kuliomba Bunge lako Tukufu kuidhinisha maombi ya fedha kwa ajili ya Wizara ya Viwanda na Biashara Fungu 44 - Viwanda na Fungu 60 - Biashara kwa mwaka wa fedha 2021/ 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maudhui ya taarifa hii yanagawanyika katika maeneo makuu manne yafuatayo; moja, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2020/2021; mbili, matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo; tatu, uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa ajili ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na nne, maoni na ushauri wa kamati unaotokana na chambuzi na ufuatiliaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa majukumu na mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2020/2021 na matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021;

utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021; wakati Bunge lako Tukufu linaidhinisha bajeti ya viwanda na biashara kwa mwaka wa fedha unaoishia 2020/2021 ilizingatia malengo na vipaumbele vya Wizara hii. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ilibainisha hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa melngo hayo. Kamati ilipongeza hatua hizi, hata hivyo iliendelea kusisitiza Serikali katika maeneo yafuatayo:-

Moja, mkakati wa kuendesha sekta ya viwanda nchini, utekelezaji wake haujafanikiwa ilivyotarajiwa hususan katika sekta ya chuma na bidhaa ya chuma ambapo mpaka sasa tuna viwanda 23 vinavyozalisha bidhaa za chuma, lakini malighafi inayotegemewa ni chuma chakavu. Kuna haja ya kuanza utekelezaji wa Liganga na Mchuchuma mara moja ili tuweze kupata malighafi kwa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili; mkakati wa kuhamasisha uendeshaji wa sekta ya mafuta ya kula bado haujafanikiwa. Pamoja na uwepo wa ardhi yenye rutuba inayofaa katika uzalishaji wa malighafi ya mafuta, lakini bado kuna changamoto upatikanaji wa bidhaa ya mafuta ya kula na upandaji holela wa bei ya mafuta hayo. Kuna haja ya kurejea mkakati wetu juu ya uendeshaji wa sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2020/2021; kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) za Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu Toleo la Juni, 2020 katika kutekeleza majukumu yake Kamati ilifanya ziara ya kutembelea baadhi ya miradi iliyotengewa fedha na inayotekelezwa chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa lengo la kujionea hali halisi na hatua zinazofikiwa katika utekelezaji wake. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Bunge liliidhinisha jumla ya shilingi bilioni 29.7 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyopo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Kamati ilipata fursa ya kutembelea na kukagua Mradi wa *Mchuchuma Coal,* Mradi wa *Liganga Vanadium, Titanium,* Mradi wa *Tanzania Mini Tiger Plan Bagamoyo SEZ* na *Benjamin Mkapa EPZA,* Mradi wa *Institutional Support* katika Shirika la Utafiti

wa Maendeleo ya Viwandani *(TIRDO)* na Mradi wa *TAMCO Kibaha Industrial Park.* Maelezo ya miradi hiyo, kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati kutokana na changamoto ya muda, naomba nizungumzie mradi mmoja ambao ni mradi wa *Mchuchuma Coal* pamoja na mradi wa *Liganga Vanadium and Titanium.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Mradi wa *Mchuchuma Coal* pamoja na Mradi wa *Liganga Vanadium and Titanium* iliidhinishiwa shilingi milioni 260 kwa ajili ya utekelezaji wake. Fedha hizi zililenga kufanya uhakiki wa mali za wananchi watakaolipwa fidia kwa kupisha eneo la mradi na kufanya upelembaji na tathmni ya mradi *(MNE)* yaani yote miwili. Mpaka Kamati inafika eneo la mradi hakukuwa na kazi iliyokuwa inaendelea. Kamati ilihoji kuhusu hili na kujulishwa kuwa utekelezaji wa Mradi wa Mchuchuma na Liganga umesimama kwa muda wakati Serikali inafanya majadiliano na mwekezaji ili kutafuta namna bora ya kutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutembelea na kukagua eneo la mradi huu Kamati ilikuwa na ushauri ufuatao; mosi, Serikali iongeze kasi katika majadiliano yanayoendelea na kupata muafaka hara iwezekanavyo ili utekelezaji wa miradi hii muhimu tena ya kielelezo ianze mara moja, ikizingatiwa miradi hii ni miradi ya kichocheo kwa sekta ya viwanda hususan viwanda vya chuma. Pia itachangia uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, katika majadiliano yanayoendelea tunapaswa kuwa makini na kuhakikisha upatikanaji wa mkataba wenye maslahi kwa pande zote mbili, ikiwa mwekezaji aliyeko haafikiani na mapendekezo yetu, tutafute mwekezaji mwingine na tatu, mradi wa ujenzi wa kipande cha barabara kinachounganisha miradi hii miwili, Liganga na Mchuchuma ukamilike kwa kuwa urahisi wa utekelezaji wa miradi hii unategemea ukamilikaji wa barabara hizo kwa ajili ya usafirishaji wa malighafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021; Bunge lako tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi bilioni 81.4 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kutokana na kuidhinishwa kwa fedha hizo, Kamati ilifanya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ikiwa ni sehemu ya kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni ya 117(2), lakini pia kwa lengo la kujiridhisha kama dhamira ya Bunge lako ya kuidhinisha bajeti hii imetimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, uchambuzi wa kamati ulizingatia utekelezaji wa malengo na vipaumbele vya Wizara, ukusanyaji wa mapato na upatikanaji wa fedha ukilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuli; mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ya Viwanda na Biashara Fungu Namba 48 na 60 ilipanga kukusanya jumla ya shilingi milioni 15 kutokana na uuzaji wa nyaraka na zabuni. Hadi kufikia Machi, 2021 Wizara haikuwa imekusanya kiasi chochote. Kamati inaishauri Wizara hii kubaki na jukumu la kuratibu na kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara na kutoweka kipaumbele masuala ya utafutaji wa mapato kwa kuwa jambo hilo tayari linatekelezwa na taasisi ambazo ziko chini yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, upatikanaji wa pesa kutoka Hazina; katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ya Viwanda na Biashara chini ya Fungu 40 - Viwanda na 60 - Biashara ilitengewe kiasi cha fedha kama ilivyoonekana katika jedwali namba 01 na Taarifa ya Kamati. Kamati ilifanya uchambuzi wa mwenendo wa upatikanaji wa fedha ikilinganisha na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge pamoja na kipindi cha utekelezaji. Muhtasari wa uchambuzi huo ni kama inavyoonekana kwenye jedwali namba 2 la Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi wa Kamati kuhusu Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na bajeti

ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ni kwamba; mosi, hakuna mwenendo mzuri wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwani kiuhalisia mpaka kufikia Machi, 2021 utekelezaji wa bajeti ilipaswa kuwa asilimia 75 lakini Wizara ilikuwa imepokea asilimia 55.94 kwa maana ya kuwa utekelezaji umepungua kwa asilimia 19.9. Pili, mwenendo wa upatikanaji wa fedha umeathiri zaidi utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo mpaka kufikia Machi, 2021 kiasi kilichopokelewa kilikuwa shilingi bilioni 6.98 ambayo ni sawa na asilimia 23.2 tu kwa maana ya kuwa asilimia 76.8 ya miradi ya maendeleo haikutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtazamo wa Kamati ni kuwa mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha kwa Wizara ya Viwanda na Biashara unaashiria kukwama kwa utekelezaji wa baadhi ya majukumu yaliyopangwa kwa mwaka huu wa fedha. Wizara hii ikiwa imebeba maono ya Serikali ya ujenzi wa Tanzania ya viwanda kuna haja ya kupea kipaumbele katika kupatiwa bajeti ili utekelezaji wa majukumu yake uende kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati kuhusu bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021; wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya bajeti pamoja na mapendekezo ya maombi ya fedha ya Wizara ya Viwanda na Biashara mwaka 2020/2021, Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo 22. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati. Hata hivyo, kuna maeneo ambayo Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wake na inaendelea kusisitiza juu ya Serikali na utekelezaji wake. Maeneo hayo ni kama yanavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022; wakati wa kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara, Kamati ilipitia maelezo ya Waziri kuhusu malengo waliyojipangia kuyatekeleza kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa lengo la kujiridhisha na tija inayoweza kupatikana katika utekelezaji

wa bajeti ya mwaka 2021/2022 katika Fungu namba 44 na 60. Uchambuzi wa malengo hayo ulibaini yanaendana na majukumu ya msingi ya Wizara na Biashara lakini pia yamezingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa na Ilani ya Uchaguzi ya chama kinachoongoza Serikali ambacho ni Chama cha Mapinduzi. Mfano wa hii umeelezwa hapa chini kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makisio ya maduhuli; kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ya Viwanda na Biashara imepanga kukusanya jumla ya shilingi milioni 15 kutokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni. Uchambuzi wa kamati ulibaini kuwa kiasi kilichopangwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ni sawa kabisa na kilichopangwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha ulioishia 2020/2021 ambacho hakikukusanywa kabisa. Kamati imesisitiza Wizara kubaki na jukumu la kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara, kuachana na habari za makusanyo kwa kuwa jukumu hili tayari linatekelezwa vizuri na taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022; katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara imetengewa jumla ya bilioni 105.7 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shughuli za maendeleo kwa mafungu yote mawili 44 na 60. Muhtasari wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 03 la Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati kuhusiana na mpango wa bajeti wa Wizara ya Viwanda na Biashara umebaini mambo yafuatayo:-

(i) Kiasi cha bajeti kilichoombwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa ajili ya mafungu yote mawili kimeongezeka kwa asilimia 23 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge mwaka wa fedha unaoishia 2020/2021.

(ii) Ongezeko la Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara limesababishwa na ongezeko katika fedha za miradi ya

maendeleo ambayo imeongezeka kwa asilimia 78.8 ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021.

(iii) Ongezeko la fedha za miradi ya maendeleo linatia mashaka kidogo kwenye utekelezaji wake kwa kuwa hata hiyo ya mwaka unaoishia ilitekelezwa kwa asilimia 21 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Kamati kuwa Serikali ione haja ya kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara ili iweze kutekeleza majukumu yake yanayolenga kuimarisha mazingira ya sekta za viwanda na biashara na kuongeza mchango wake katika uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Kipindi cha Miaka Mitano Kuanzia 2021/2022 – 2025/2026 unalenga kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Mpango huu umeainisha maeneo matano ya kipaumbele na kati ya maeneo hayo, matatu yanatekelezwa chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ione haja ya kuiwezesha kikamilifu Wizara ya Viwanda na Biashara ili iweze kutekeleza mpango huu kiukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ambayo Kamati imeona kuna haja kwa Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara kuyatilia mkazo wakati wa utekelezaji wake wa Bajeti ni kama ifuatavyo:-

(i) Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 utajumuisha utekelezaji wa miradi mitatu ya kielelezo na kipaumbele chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara ambayo ni Miradi ya Liganga, Mchuchuma, Magadi Soda. Miradi hii ni ya Muda mrefu na imekuwa ikitajwa katika mipango mbalimbali ikiwepo Mpango wa Pili wa Taifa, lakini utekelezaji wake bado unasuasua. Miradi hii ni kichocheo kwa baadhi ya viwanda nchini hususani viwanda vya chuma kwa kuwa inatarajiwa kuzalisha malighafi ambazo

zingetumiwa na viwanda hivyo. Kamati inaishauri Serikali itoe kipaumbele kwa miradi hii wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo ili walau utekelezaji wake uanze.

(ii) Utekelezaji wa Mradi Kituo cha Biashara cha Kurasini (*Kurasini Logistic Centre*); Mradi wa *Kurasini Logistic Centre* ni moja ya miradi ya kielelezo na unatarajiwa kuchochea ukuwaji wa sekta ya biashara na viwanda. Utekelezaji wa mradi huu umechukua muda mrefu sana takribani miaka saba ambapo kubwa lililofanyika ni ulipaji wa fidia ambapo takribani bilioni 101 zimekwishalipwa. Kamati haioni jitihada za dhati katika kutekeleza mradi huu na madhara ya kuchelewesha utekelezaji wa mradi huu ni kuwa eneo lile lilikwishalipiwa fidia kiasi kikubwa ambacho kinaonekana kama zimefukiwa tu na hutunufaiki na kiasi hicho. Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuanza utekelezaji wa mradi huu ili tuanze kunufaika kama ilivyokusudiwa.

(iii) Mazingira ya kufanyia Biashara; pamoja na hatua nzuri zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali, bado kuna malalamiko kutoka kwa wawekezaji kuhusu mazingira rafiki ya kufanyia biashara na uwekezaji nchini. Baadhi ya wawekezaji wanalaamikia uwepo wa changamoto kama vile mamlaka nyingi za udhibiti, urasimu katika upatikanaji wa vibali vya uhamiaji na mlolongo wa kupata vibali vya uwekezaji. Aidha, taarifa ya Benki ya Dunia inaripoti Tanzania kuwa katika nafasi ya 141 kati ya 190 ya nchi yenye mazingira rahisi ya kufanyia biashara nafasi ambayo si nzuri sana. Na kwa kutambua hivyo Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(a) Kukamilisha mchakati wa kuandaa Muswada wa Sheria ya Uwezeshaji wa Biashara *(Business Facilitation Act)* na Muswada huo uwasilishwe Bungeni haraka ili uweze kusaidia kutatua changamoto hizi.

(b) Kuongeza nguvu/kasi katika utekelezaji wa *blueprint* ili kuondoa changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo wazalishaji na wafanyabishara nchini.

(c) Kuzisisitiza na kuzisimamia sekta zote za Serikali kuhakikisha kwamba, zinatekeleza sehemu yake katika *blueprint.*

(d) Kukamilisha mapitio ya kodi mbalimbali kwa nia ya kuzipunguza kwa kutazama majirani zetu kikanda ili tuweze kushindana nao katika masoko ya ndani na nje.

(e) Kutoa elimu kwa wananchi kuhusu *blueprint* ili kurahisisha utekelezaji wake kwa kuwa kila mtu ana nafasi yake katika kuongeza ufanisi katika kuleta maendeleo.

(iv) Kufungamanisha sekta ya kilimo, uvuvi na mifugo pamoja na ujenzi wa viwanda; miongoni mwa vipaumbele vya mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo ni kuanzisha viwanda vitakavyochakata mazao ya kilimo, uvuvi na ufugaji na kwa kuzingatia asilimia kubwa ya Watanzania wanajihusisha na shughuli hizo, Kamati inashauri Serikali kwamba uhamasishaji wa ujenzi wa viwanda ambavyo vitachakata mazao yatokanayo na shughuli hizi uende sambamba na Wizara husika kuiwezesha na kuihamasisha jamii kushiriki shughuli hizo kwa tija ili tuweze kutoa huduma za malighafi kwenye viwanda hivi. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeongeza ajira za kutosha kwa jamii na kuongeza mapato kwa Serikali.

(v) Sekta ya utalii kuendeshwa kibiashara; sekta ya utalii nchini ina uwezo mkubwa wa kutuletea mapato kuliko ilivyo sasa, hii inatokana na ukweli kwamba sekta hii kwa sasa haifanyi kazi zake kibiashara hususan upande wa kujitangaza. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kulisimamia jambo hili kwa kuifanya sekta ya utalii kufanya kazi zake kibiashara ili kuongeza idadi ya watalii wa ndani na wale watakaokuja nchini ili kuongeza mchango wa mapato yatakayotokana na sekta hii.

(vi) Uwepo wa bidhaa bandia zisizokidhi viwango sokoni unadhihirisha bado kuna ushirikiano mdogo uliopo baina ya Taasisi za Ukaguzi zilizopo katika Vituo vya Mipakani pamoja na gharama kubwa inayotozwa kwa ajili ya ukaguzi,

jambo linalosababisha baadhi ya wafanyabishara kuamua kutumia njia za panya kuingiza bidhaa zao na kupelekea uwepo wa bidhaa hafifu sokoni. Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(a) Serikali kuzisimamia kwa ukaribu mamlaka hizo kuhakikisha zinashirikiana katika kufanya ukaguzi, lakini pia Serikali iangalie namna ya kupunguza gharama zilizopo ili kuweza kuwavutia wafanyabiashara kupitisha bidhaa zao katika vituo halali.

(b) Serikali kuimarisha Shirika la Viwango *(TBS)* pamoja na Tume ya Ushindani *(FCC)* kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Vilevile taasisi hizi mbili zifanye kazi kwa ushirikiano katika kuhakikisha bidhaa zilizopo sokoni zinakidhi viwango lakini pia ni halali na zinaleta ushindani wa usawa sokoni.

(vii) Kiwanda cha Viuwadudu cha Kibaha – *Tanzania Biotech Products Ltd;* kiwanda hiki kilianzishwa kwa lengo la kutokomeza malaria nchini. Mpango wa awali ilikuwa ndani ya miaka mitano Wizara ya Afya ichukue dawa lita milioni tano kila mwaka na kuzipatia Halmashauri zote nchini. Utekelezaji umeshindikana kutokana na kuwa mteja mkubwa ambaye ni Wizara ya Afya ameshindwa kutekeleza makubaliano aliyoingia na kiwanda, hivyo basi tuna kiwanda ambacho kilifanya uwekezaji mkubwa wa dola za Marekani milioni 22 lakini mpaka sasa hakizalishi na pia kama nchi bado tunasumbuliwa na ugonjwa wa malaria. Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(a) Wizara ya Viwanda na Biashara ikae chini na Wizara ya Afya pamoja na TAMISEMI wajadiliane muafaka wa makubaliano ya awali na dawa zianze kutumika ili kiwanda kiendelee kuzalisha.

(b) Kwa kuwa bajeti kubwa inayoelekezwa kupambana na malaria inatokana na fedha za ufadhili na ili ufadhili huo uweze kutumika kwa dawa hii ya Viuadudu ni lazima vibali vya *WHO* vithibitishe ubora wa dawa. Wizara ya

Viwanda na Biashara ihakikishe kiwanda kinakamilisha na kuiwasilisha haraka iwezekanavyo taarifa inayohitajika ili *WHO* kwa ajili ya kuthibitisha dawa hii.

(viii) Mpango wa kulinda Viwanda vya ndani; Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa unalenga kujenga uchumi shindani na viwanda kwa Maendeleo ya watu, kwa kuzingatia hilo tunapaswa kuweka mazingira rafiki yatakayokuza Viwanda vya ndani ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi ikiwa ni pamoja na kutengeneza ajira nyingi zaidi kwa wananchi. Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Serikali ihakikishe inalinda bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani ya nchi kwa kuweka uwiano wa kodi kwenye bidhaa zinazoingizwa kutoka nje utakaoendana na bei za Bidhaa zitakazozalishwa nchini.

(b) Viwanda vya ndani ambavyo vinazalisha na vinauwezo wa kukidhi mahitaji ya soko ni vema Serikali ikatengeneza mazingira ya kuvilinda viwanda hivyo. Aidha, manunuzi ya umma *(Public Procurement)* yatoe kipaumbele kwa viwanda vya ndani.

(c) Serikali iimarishe miundombinu ya umeme, maji na barabara ili kuvipa unafuu viwanda viweze kupunguza gharama za uzalishaji.

(d) Serikali kupitia vyuo vya ufundi iimarishe mafunzo ya taaluma na stadi za Viwandani ili tuweze kukidhi soko la rasilimali watu nchini.

(ix) Utekelezaji wa ukusanyaji kodi kwa njia ya kielektroniki *(Electronic Tax Stamp – ETS);* sote tunatambua nia njema ya Serikali ya kuanzisha Mfumo wa *ETS* lakini utekelezaji wake unalalamikiwa na wafanyabiashara kuwa ni wa gharama kubwa na unaendeshwa na mshauri elekezi kutoka nje ya nchi, malipo yanafanywa kwa njia ya fedha za kigeni na pesa yote inayokusanywa kupitia *ETS* inaenda nje ya nchi. Kamati inaishauri Serikali kusikiliza malalamiko ya wafanyabiashara kuhusu Mfumo wa *ETS*, iyatafakari

malalamiko hayo na kuyashughulikia bila kuathiri sheria zilizopo na kuweka mbele maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; naomba kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Spika, kwa weledi mkubwa, Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na wewe Mwenyekiti na viongozi wote katika kusaidia kuongoza vikao vya bunge hili la Kumi na Mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kushiriki kikamilifu wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni ya bajeti kwa wizara hii mbele ya Bunge lako tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini na kwa ruhusa yako naomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Geofrey Mwambe, aliyekuewa Waziri wa Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Kigahe Exaud Silaoneka, Mbunge, Makatibu Wakuu pamoja na watumishi wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa jinsi walivyoshirikiana na kamati katika kujibu hoja za Wajumbe wa Kamati, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na kufafanua kwa kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Aidha, Nampongeza Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo (Mbunge) kwa kuteuliwa kwa nafasi ya Waziri wa Viwanda na Biashara. Tunamkaribisha kwenye kamati na tunamuahidi ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru aliyekuwa Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila kukwama. Nimpongeze Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuteuliwa kuwa Katibu wa Bunge. Nimshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Ndugu Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Fedha Bwana Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Bi. Zainab Mkamba

na Bi. Mwajuma Ramadhan pamoja na Msaidizi wa Kamati Bi. Grace Mwenye kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, sasa naomba kulishauri Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 44 na 60, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kiasi cha shilingi 105,670,459,000.00 kama alivyofafanua mtoa hoja pamoja na maoni ya Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA, FUNGU 44-VIWANDA NA FUNGU 60-BIASHARA KWA MWAKA 2020/2021 NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI FUNGU 44 & 60 YA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 **UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, uzima na nafasi nyingine ya kukutana hapa Dodoma katika Mkutano huu wa Tatu wa Bunge la Kumi na Mbili.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, naomba nitumie fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu maoni ya Kamati hii kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hii inaeleza namna Kamati yangu ilivyotekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) na (2) na imeanisha mapendekezo kadhaa

ambayo Kamati inaamini ni muhimu yakafanyiwa kazi wakati wa utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Aidha, taarifa hii inalenga pia kuliomba Bunge lako tukufu kuidhinisha maombi ya fedha kwa ajili ya Wizara ya Viwanda na Biashara, **Fungu 44-Viwanda** na **Fungu 60-Biashara** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, Maudhui ya Taarifa hii yanagawanyika katika maeneo makuu manne yafuatayo:-

i) Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2020/2021;

ii) Matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kwa ajili ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2021/2022; na

iv) Maoni na ushauri wa Kamati unaotokana na uchambuzi na ufuatiliaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA MPANGO WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 NA MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021.

### 2.1 Utekelezaji wa Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

**Mheshimiwa Spika**, wakati Bunge lako Tukufu linaidhinisha Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha unaoishia 2020/2021 ilizingatia malengo/vipaumbele vya wizara hii, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ilibainisha hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa malengo hayo. Kamati ilipongeza hatua hizo, hata hivyo iliendelea kuisisitiza Serikali kuongeza kasi katika maeneo yafuatayo: -

i) Mkakati wa kuendeleza Sekta ya Viwanda nchini utekelezaji wake haujafanikiwa ilivyotarajiwa hususani katika Sekta ya Chuma na Bidhaa ya chuma ambapo mpaka sasa tuna viwanda 23 vinavyozalisha bidhaa za chuma lakini malighafi inayotegemewa ni chuma chakavu. Kuna haja ya kuanza utekelezaji wa Mradi wa Liganga na Mchuchuma mara moja ili tuweze kupata malighafi kwa viwanda vyetu;

ii) Bado kuna changamoto ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya kimkakati, mfano Utekelezaji wa Mradi wa Matrekta ya URSUS unasuasua ambapo Mbia katika mradi huu Kamapuni ya URSUS S.A ya Poland ameshindwa kukamilisha utekelezaji wa Mkataba wa mradi huu. Mradi ulipaswa kuwa umekamilika kufikia Juni, 2018 na matrekta 2400 yalipaswa kuwa yamekwishaingizwa nchini lakini ni matrekta 822 tu yaliyopokelewa;

iii) Bado hatujapata tija iliyokusudiwa katika utekelezaji wa lengo la kusimamia na kufuatilia Miradi ya Kimkakati. Mfano miradi ya **Liganga na Mchuchuma, Mradi wa Magadi Soda ya Engaruka, na Mradi wa Kiwanda cha Matairi cha Arusha** bado hakuna jambo lililokamilika katika miradi hiyo; na

iv) Mkakati wa kuhamasisha uendeshaji wa Sekta ya mafuta ya kula bado haujafanikiwa. Pamoja na uwepo wa ardhi yenye rutuba inayofaa katika uzalishaji wa malighafi za Mafuta lakini bado kuna changamoto ya upatikanaji wa bidhaa ya mafuta ya kula na upandaji holela wa bei ya mafuta hayo. Kuna haja ya kurejea mikakati yetu juu ya uendeshaji wa Sekta hii.

### 2.2 **Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

#### 2.2.1 **Mapitio ya Taarifa za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Juni, 2020 katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilifanya ziara ya kutembelea baadhi ya miradi iliyotengewa fedha na inayotekelezwa chini ya

Wizara ya Viwanda na Biashara kwa lengo kujionea hali halisi na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wake.

Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Bunge liliidhinisha jumla ya Shilingi **29,687,886,000** kwa ajili ya kutekeleza Miradi mbalimbali ya Maendeleo iliyopo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Kamati ilipata fursa ya kutembelea na kukagua Mradi wa Mchuchuma *Coal* (**Mradi Namba 3171 Fungu 44**); pamoja na Mradi wa Liganga *Vanadium Titanium* (**Mradi Namba 3161 Fungu 44**); Mradi wa Tanzania *Mini Tiger Plan* Bagamoyo SEZ na Benjamini Mkapa EPZ (Mradi **Namba 6260 Fungu 44**); Mradi wa *Institutional Support* katika Shirika la Utafiti wa Maendeleo ya Viwandani Tanzania *TIRDO* (**Mradi Namba 6260 Fungu 44);** na Mradi wa TAMCO Kibaha Industrial Park (**Mradi Namba 6260, Fungu 44**). Maelezo ya Miradi hiyo ni kama yafuatavyo;-

**a) Mradi wa Mchuchuma Coal (Mradi Namba 3171 Fungu 44); pamoja na Mradi wa Liganga Vanadium Titanium (Mradi Namba 3161 Fungu 44)**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Mradi wa Mchuchuma *Coal* (**Mradi Namba 3171 Fungu 44**); pamoja na Mradi wa Liganga *Vanadium Titanium* (**Mradi Namba 3161 Fungu 44)** iliidhinishiwa Shilingi **260,000,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wake. Fedha hizi zililenga kufanya uhakiki wa mali za wananchi watakaolipwa fidia kwa kupisha eneo la Miradi na Kufanya uperembaji na tathmini ya Miradi (M& E) yote miwili.

**Ø Hali ya Mradi wakati wa Ziara ya Kamati**

Mpaka Kamati inafika eneo ya Mradi hakukuwa na kazi iliyokuwa inandelea. Kamati ilihoji kuhusu hili na kujulishwa kuwa utekelezaji wa mradi wa Mchuchuma na Liganga umesimama kwa muda wakati Serikali inafanya majadiliano na Mwekezaji ili kutafuta namna bora ya kutekeleza mradi huu. Maamuzi ya kufanya majadiliano upya ni baada ya Mkataba wa awali kuonekana na mapungufu ambayo kwa namna moja ama nyingine kusingekuwepo na usawa wa mgawanyo wa faida na Tanzania ndio tungeathirika zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kutembelea na kukagua eneo la Mradi wa Mchuchuma *Coal* (**Mradi Namba 3171 Fungu 44**); pamoja na Mradi wa Liganga *Vanadium Titanium* (**Mradi Namba 3161 Fungu 44**), Kamati ilikuwa na maoni na ushauri ufuatao:-

i) Serikali iongeze kasi katika majadiliano yanayoendelea na kupata muafaka haraka iwezekanavyo ili utekelezaji wa miradi hii muhimu tena ya kielelezo ianze mara moja ikizingatiwa miradi hii ni miradi ya kichochocheo kwa sekta ya Viwanda hususani viwanda vya chuma, pia itachangia katika uzalishaji wa umeme;

ii) Katika majadiliano yanayoendelea tunapaswa kuwa makini na kuhakikisha unapatikana mkataba wenye maslahi ya pande zote mbili. Ikiwa muwekezaji aliyepo haafikiani na mapendekezo yetu tutafute muwekezaji mwingine; na

iii) Mradi wa ujenzi wa kipande cha barabara kinachounganisha miradi hii miwili Liganga na Mchuchuma ukamilike kwa kuwa urahisi wa utekelezaji wa miradi hii unategemea ukamilishaji wa barabara hizo kwa ajili ya usafirishaji wa malighafi.

**b) Mradi wa Tanzania *Mini Tiger Plan* Bagamoyo SEZ na Benjamini Mkapa EPZ (Mradi Namba 6260 Fungu 44)**

**Mheshimiwa Spika,** Bunge lako tukufu liliidhinisha jumla ya Shilingi **5,000,000,000.00** katika mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Tanzania *Mini Tiger Plan* Bagamoyo SEZ na Benjamini Mkapa EPZ (Mradi Namba 6260 Fungu 44). Fedha hii ililenga kutekeleza kazi mbalimbali ikiwemo kufanya upembuzi Yakinifu (Feasibility Study), kuandaa Mpango kabambe wa uendelezaji (Masterplan), Survey na kufanya usanifu wa miundombinu ya ndani (Design of on site Infrastructure) eneo la Bagamoyo Textile; kujenga barabara katika eneo lililojengwa viwanda 11 katika eneo la mradi wa Bagamoyo SEZ; kusimamia uendelezaji wa miundombinu ya mradi wa Bagamoyo Technological Park; kutengeneza na kukarabati miundombinu ya ndani katika

eneo la uwekezaji la Benjamin William Mkapa SEZ; kushiriki katika huduma za kijamii (Corporate Social Responsibilities) kwenye maeneo yaliyozunguka miradi ya Bagamoyo SEZ na Benjamin William Mkapa SEZ.

**Ø Hali ya Mradi wakati wa Ziara ya Kamati**

Hadi kufikia Machi, 2021 ambapo Kamati ilikuwa imetembelea miradi hii hakukuwa na kiasi chochote cha fedha kilichokuwa kimepokelewa hivyo hakukuwa na kazi iliyokuwa imetekelezwa. Kamati ilipata fursa ya kutembelea baadhi ya viwanda vilivyokuwepo katika maeneo hayo ambapo katika eneo la Bagamoyo ilitembelea kiwanda cha TANFROZ Ltd, katika eneo la Benjamin Mkapa ilitembelea Kiwanda cha TOOKU na Kiwanda cha DZ CARD.

**Mheshimiwa Spika,** mara baada ya ziara katika Eneo la Mradi Bagamoyo SEZ, Benjamin Mkapa SEZ ikiwa ni pamoja na kutembelea viwanda hivyo vitatu Kamati ilikuwa na ushauri ufuatao:-

i) Sheria ya EPZA ifanyiwe marekebisho kwa lengo la kuongeza asilimia ya mauzo yanayoweza kufanyika ndani ambapo kwa sasa asilimia 20 tu ndio inauzwa ndani na asilimia 80 inauzwa nje ya nchi. Jambo hili litavutia uwekezaji zaidi katika maeneo ya EPZ na SEZ kwa kuwa Tanzania ina watu wengi na tayari inatazamiwa kama moja ya soko kwa bidhaa zinazozalishwa katika maeneo hayo;

ii) Agizo la EPZA kurudisha baadhi ya maeneo ambayo bado hayajafidiwa litaleta changamoto kwa upande wa eneo la Bagamoyo kwani eneo lile tayari lipo katika mpango wa Mradi wa EPZ – Bagamoyo na kipindi yatakapohitajika tena ili kukamilisha mpango wa awali wa mradi, gharama ya kuyatwaa tena maeneo hayo itakuwa imeongezeka. Hivyo ni bora EPZA ikaruhusiwa kuendelea kuyamiliki, jambo hili liende sambamba na ushirikishwaji wa Sekta Binafsi katika kumiliki maeneo ya EPZA ili kupata wawekezaji watakaolipa fidia; na

iii) Serikali ihakikishe kunakuwa na ubora wa miundombinu inayowekwa katika maeneo haya ya uwekezaji hususani barabara na Umeme ili kuyafanya maeneo hayo yawe rafiki zaidi katika shughuli za uzalishaji.

**c) Mradi wa *Institutional Support* katika Shirika la Utafiti wa Maendeleo ya Viwandani Tanzania *TIRDO* (Mradi Namba 6260 Fungu 44)**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi **Na. 6260 *Institutional Support*** unalenga kuziwezesha Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara kutekeleza majukumu yake, Mradi ulitengewa Shilingi **500,000,000.00** kwa ajili ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO). Fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya TIRDO zililenga kupata ithibati ya maabara ya Kemia na Mazingira ifikapo Juni, 2021 na kuongeza vigezo vya uhakiki kutoka 5 hadi 20 kwa ajili ya maabara ya bidhaa za chakula ifikapo Juni, 2021.

**Ø Hali ya Mradi wakati wa Ziara ya Kamati**

Wakati wa ziara ya Kamati, TIRDO ilikuwa imepokea Pesa iliyokuwa imeidhinishiwa kiasi cha Shilingi **500,000,000.00** na taratibu kwa ajili ya kupatiwa idhibati ya maabara hizo mbili ya Kemia na Mazingira ili ziweze kutekeleza majukumu yake kiukamilifu na kujiamini na waweze kuhudumia wateja wote bila kikwazo zilikuwa zinaendelea. Pamoja na mambo mengine Kamati ilipata fursa ya kutembelea mradi wa usindikaji wa zao la mihogo kwa ajili ya kupata spirit pamoja na starch, pia ilitembelea Kiwanda cha mjasiliamali ambae amepewa eneo la incubation na anazalisha dawa aina ya COVIDOL na BUYEGE ambazo ni dawa kwa ajili ya kupambana na gonjwa la COVID - 19.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kutembelea maeneo hayo na kupatiwa taarifa fupi juu ya kazi mbalimbali zinazoendelea katika eneo la TIRDO ikiwemo kitengo cha kuwalea watafiti/ wagunduzi mbalimbali, Kamati ilikuwa na maoni na ushauri ufuatao;-

i) Shirika linakabiliwa na uchakavu wa majengo hususani maabara zake na vitendea kazi jambo ambalo halitoi taswira/picha nzuri kwa wateja wao hususani viwanda vya wawekezaji kutoka nje. Kamati inashauri Serikali kuliwezesha Shirika hili kupata maabara za kisasa na majengo mapya ili waweze kutanua wigo wao na huduma kwa kuwa wataweza kuhudumia wateja wengi zaidi na wa aina mbalimbali;

ii) Shirika lisaidiane na Wizara ya Viwanda kujitangaza kwa lengo la kupata wawekezaji watakaokuja kununua teknolojia mbalimbali zinazozalishwa na Shirika kupitia wagunduzi wao waliopo katika *incubation*;

iii) Kamati ilijulishwa pia kuwa Shirika halina Wajumbe wa Bodi baada ya wajumbe kumaliza muda wao tangia Novemba 2018, jambo linalopelekea kukwama kwa baadhi ya majukumu kwakuwa Bodi ndio chombo cha juu cha maamuzi katika Shirika. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha Shirika linapata wajumbe wapya wa Baraza kwa lengo la kuliwezesha Shirika kuendelea na utekelezaji wa majukumu yake kama lilivyokusudiwa; na

iv) Shirika pia linakabiliwa na Deni kubwa la ardhi ambalo ni mzigo kwa Taasisi, Kamati inashauri Serikali kuangalia namna ya Kulifutia deni hili kwa kuwa hata hela za kulipa deni hilo zinatoka Serikalini jambo ambalo ni kutoa hela Serikalini na kuirudisha Serikalini.

**d) Mradi wa TAMCO Kibaha Industrial Park (Mradi Namba 6260, Fungu 44);**

**Mheshimiwa Spika**, mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ya Viwanda na Biashara, Fungu **44** iliidhinishiwa shilingi 500,000,000/= kwa ajili ya kutekeleza mradi Na. **6260** – *NDC-Industrial Park (TAMCO*-Kibaha) unaohusisha kuendeleza maeneo maalumu ya Viwanda. Fedha hiyo ililenga kufanya usanifu wa Kilomita 4 za barabara za ndani (Asphalt Concrete Level) iliyopo ndani ya eneo la mradi na kufanya uperembaji na tathmini ya Mradi (M&E).

Ø **Hali ya mradi wakati wa Ziara ya kamati**

Hadi Kamati ilipofika katika eneo la Mradi tarehe 16 machi, 2021 fedha za Maendeleo zilikuwa hazijapokelewa hivyo shughuli zilizokuwa zimepangwa kutekelezwa kwa fedha hizo zilikuwa hazijatekelezwa. Pamoja na kuwa shughuli za maendeleo zilizokusudiwa kutekelezwa zilikuwa hazijaanza, lakini eneo la *TAMCO* – Kibaha ni eneo la Viwanda hivyo, Kamati ilifanikiwa kutembelea Viwanda viwili (2) vilivyopo katika eneo hilo ambavyo ni Kiwanda cha HEISTER BIO SCIENCE AFRIKA LTD na Kiwanda cha TANZANIA BIOTECH PRODUCTS LTD.

**i) Kiwanda cha TANZANIA BIOTECH PRODUCTS LTD**, Kiwanda hiki kinazalisha viuadudu (bio-lavacite) ambavyo vinalengwa kutumika kupambana na ugonjwa wa Malaria kwa kumtokomeza kiluilui wa mbu wa malaria akiwa katika hatua ya lava. Kiwanda kinamilikiwa kwa ubia kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Cuba.

**Mheshimiwa Spika**, kiwanda hiki kilianzishwa kwa lengo la kutekeleza mradi/mpango kwa kutokomeza malaria nchini ndani ya Miaka mitano. Kiwanda kilianza uzalishaji Machi, 2015 na kufikia Machi, 2020, ilipaswa Tanzania kuwa imetokomeza kabisa ugonjwa wa malaria na mteja mkubwa alitegemewa kuwa ni Wizara ya Afya ambae aliingia makubaliano na Kiwanda ya kuchukua dawa lita Milioni Tano (5) kila mwaka.

Ø **Hali ya Kiwanda wakati wa ziara ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** wakati Kamati inafika eneo la Kiwanda hiki, uzalishaji ulikuwa umesimamishwa, hali hiyo ilisababishwa na kukosa soko la uhakika. Jambo lilopelekea kiwanda kukosa hata fedha za kujiendesha ikiwa ni pamoja na kushindwa kulipa mishahara ya wafanyakazi kwa muda wa miezi minne (4).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikuridhishwa na hali waliyoikuta katika kiwanda, Kamati inaishauri Wizara ya Viwanda kukaa

chini na Wizara ya afya na kufanya marejeo ya makubaliano ya awali, zoezi hili lihusishe TAMISEMI kwa kuwa Halmashauri zetu ndio zinazotizamiwa kuchukua dawa hizo. Aidha, Kamati inaisihi Serikali kutafakari nia yake ya kuanzishwa kiwanda hiki kwa kuzingatia kuwa kama nchi tupo miongoni mwa nchi zilizoathirika zaidi na ugonjwa wa Malaria.

**ii) Kiwanda cha HEISTER BIO SCIENCE AFRIKA LTD**

**Mheshimiwa Spika,** Kiwanda hiki kinajihusisha na uzalishaji wa Chanjo za Mifugo za aina 26, Kiwanda kinamilikiwa kwa asilimia mia na kampuni ya kigeni kutoka India. Uwekezaji uliofanyika ni wa gharama ya Bilion 41 na wameshatoa ajira 25 na wanatarajia kuajiri kati ya watu 150 – 200 kiwanda kitakapoanza uzalishaji. Wakati wa ziara ya Kamati walikuwa katika maandalizi ya kufanya majaribio ya mitambo ya uzalishaji na majaribio hayo yatafanyika mwezi Mei, 2021.

**Mheshimiwa Spika**, uwepo wa kiwanda hiki inatarajiwa kutoa ajira, kulipa kodi lakini pia kitarahisisha upatikanaji wa chanjo mbalimbali kwa bei nafuu. Pamoja na matarajio hayo kiwanda kinakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa umeme ambapo kwa sasa hawana umeme wa viwandani na hivyo wanatumia umeme wa majumbani ambao pia sio wa uhakika. Changamoto hizi kwa pamoja zinaathiri kuanza kwa uendeshaji wa kiwanda.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kutoa ushirikiano kwa kiwanda kwa maeneo mawili ambayo ni upatikanaji wa umeme wa viwandani na bila kuathiri sheria za nchi tufanikishe upatikanaji wa vibali vya ajira kwa wataalamu wanaohitajika ili kiwanda kianze uzalishaji haraka iwezekanavyo na tuanze kunufaika.

**e) Ziara ya Kamati katika Kiwanda cha Unlever na kiwanda cha Everwell Cable & Eng Co. Ltd**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilipata fursa ya kutembelea na kukagua shughuli za Viwanda kwa lengo la kubaini mafanikio na changamoto zao ili Kamati iweze kuishauri

Serikali ikiwa na uelewa wa kutosha. Viwanda vilivyotembelewa ni kiwanda cha Uniliver na kiwanda cha Everwell Cable & Eng Co. Ltd.

**a) Kiwanda cha Unlever**

**Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha Uniliver kilichopo Mufindi kinajihusisha na uzalishaji na usambazaji wa majani ya chai. Kiwanda hiki kilielezea changamoto wanazokabiliana nazo katika uendeshaji wa shughuli zake ambazo ni; -

i) Upatikanaji wa maji na umeme usio na uhakika jambo linalopelekea kuathiri uzalishaji na ubora wa chai;

ii) VAT Refund, imekuwa hairejeshwi kwa muda jambo linalopelekea kuongeza gharama za uendeshaji wa kiwanda ikiwa ni pamoja na kupunguza mtaji wa kiwanda; na

iii) Ubovu wa miundombinu ya barabara ambapo kiwanda hiki kipo katika eneo ambalo limezungukwa na viwanda zaidi ya kumi (10). Changamoto yao kubwa ni ukosefu wa lami kwenye barabara ya Nyololo – Mtwango (40.4 km) na Mafinga – Mgololo (77.6 km), jambo linaloathiri usafirishaji wa mazao kutoka shambani na bidhaa viwandani kwenda sokoni.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya ziara ya Kamati katika kiwanda hiki, maoni yafuatayo yalitolewa na wajumbe;-

i) Serikali ishughulikie suala la VAT Refund ambazo zinadaiwa na kiwanda na kuzirudisha kwa wakati kwani zimepunguza mtaji ya kiwanda; na

ii) Serikali iboresha miundombinu inayozunguka maeneo ya kiwanda ikiwemo umeme, maji na barabara, kwani kwa kuboresha miundombinu hiyo haitasaidia kiwanda cha Uniliver pekee, itakuwa imesaidia viwanda vingine vilivyokuwa maeneo hayo hivyo kuongeza uzalishaji kwenye viwanda hivyo na kukuza zaidi pato la Taifa.

**b) Kiwanda Everwell Cable & Eng Co. Ltd**

**Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha Everwell Cable & Eng Co. Ltd kinajihusisha na uzalishaji na usambazaji wa nyaya za Umeme katika matumizi ya ngazi zote (Umeme mdogo na mkubwa, majumbani na viwandani, nguzo za Umeme za zege na uundaji/uboreshaji wa transfoma zenye uwezo na aina tofauti.

Katika uendeshaji wa shughuli kiwanda kinakabiliana na changamoto zifuatazo; -

i) Kutokuwepo kwa umeme wa uhakika ambako kunapelekea uzalishaji kusimama mara kwa mara;

ii) Ucheleweshwaji wa upakuaji wa mizigo bandarini pia kunachangia kupunguza kasi ya uzalishaji kiwandani kwa kuwa malighafi nyingi zinatoka nje ya Nchi;

iii) Upatikanaji wa vibali ya ajira kwa watumishi wa kigeni; na

iv) Kutokuwepo na ushirikiano wa mazungumzo kwa baadhi ya idara, sekta, taasisi na wakala wa serikali endapo mazingira hayo yanahitajika.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya ziara katika kiwanda hiki, Kamati ilikuwa na ushauri ufuatao;-

i) Serikali iongeze juhudi katika kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini hususani upande wa vibali vya ajira kwa wageni. Pale wawekezaji wanapokidhi vigezo vya kisheria vya kupatiwa vibali vya kazi basi wapatiwe vibali hivyo ili kutokwamisha shughuli za uwekezaji nchini;

ii) Serikali iongeze juhudi katika kuweka miundombinu wezeshi ambayo ni umeme, barabara na maji katika maeneo ya viwanda; na

iii) Mamlaka za Serikali zinazohusika katika mambo ya Sekta ya Viwanda na Biashara zifanye kazi kwa ushirikiano na ziwe na mfumo unaozungumza baina ya mamlaka.

### f) Mkutano wa Kamati na Wafanyabiashara

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilipata fursa ya kukutana na wafanyabiashara mbalimbali ikiwepo wafanyabiashara wa Chai, Mbao na Wafanyabiashara chini ya mwamvuli wa Shirikisho la Viwanda Tanzania (*CTI*). Katika majadiliano na wafanyabishara hao walikubaliana mambo yafuatayo:-

i) Shirika la Viwango Tanzania – *TBS* lishirikiane na wafanyabiashara wa mbao kupanga viwango na bei za mbao ili kuleta ushindani sawa sokoni. Kwa sasa mbao zinazozalishwa Viwandani zimewekewa viwango na tozo mbalimbali ikiwepo ya TBS lakini zile zinazozalishwa kienyeji na watu binafsi hazina viwango na tozo ya TBS na mbao zote hizi zinauzwa katika soko moja na kwa bei moja wakati mbao za viwandani zimetumia gharama kubwa kuzalisha. Jambo hili limepelekea baadhi ya viwanda kushindwa kuendelea na uzalishaji wa mbao ambapo kati ya Viwanda 27 vilivyokuwepo ni viwanda 3 tu ndio vinafanya kazi kwa sasa;

ii) Kwa kuwa Serikali imejipanga kuwa na uchumi shindani wa viwanda, ni vyema Serikali ikayaimarisha maeneo yenye Kanda za Viwanda na kuhakikisha inaweka miundombinu wezeshi itakayosaidia kukuza uzalishaji hususan Miundombinu ya maji na umeme wa uhakika pamoja na Barabara;

iii) Serikali iangalie namna ya kurejesha madai ya fedha za VAT pamoja na Ushuru wa Forodha wa 15% kwa sukari ya viwandani. Mfano madai ya wadau chini ya mwamvuli wa *CTI* wanadai VAT kiasi cha **Bilioni 16.03**, na Ushuru wa Forodha wa 15% kwa sukari ya viwandani kiasi cha **Bilioni 31.01**. Ili kurahisisha urejeshwaji wa fedha hizi kwa wakati, Serikali iandae akaunti ya tofauti ambapo hela hizi zitahifadhiwa na mara baada ya uhakiki kukamilika zirejeshwe kwa wahusika;

iv) Gharama kubwa inayotozwa kwa kutumia Mfumo wa ukusanyaji kodi kwa njia ya kielekroniki (Electronic Tax Stamp – ETS) inapunguza mitaji lakini pia inapunguza Akiba ya Fedha za Kigeni (National Forex Reserves). Mfumo huu unatoza gharama kubwa na unaendeshwa na mshauri Elekezi kutoka

nje ya nchi na hivyo malipo kutakiwa kufanywa kwa fedha za kigeni. Aidha, gharama inayotozwa ni kubwa kuliko hata kodi inayokusanywa na Serikali. Serikali iangalie namna ya kumpata mshauri elekezi mwingine atakaetoza gharama nafuu na halisi ambae atatokea nchini au ikiwa amepatikana kutoka nje ya nchi basi ashirikiane na kampuni ya ndani kutoa huduma hiyo;

v) Katika kutatua changamoto ya wingi wa mamlaka za Udhibiti ambazo kuna baadhi zinafanya kazi zinazoendana. Serikali isimamie na kuhakikisha utekelezaji wa Blueprint unaendelea na ifikapo 2025 iwe imetekelezwa kiukamilifu. Vilevile, Serikali ihakikishe Sheria au mamlaka yoyote ya udhibiti inafanyiwa Regulatoty Impact Assessment (RIA) kabla ya kupitishwa na kuanza utekelezaji wake; na

vi) Mchakato mrefu na gharama kubwa za upatikanaji wa Vibali vya ajira kwa wataalamu kutoka nje ya nchi, jambo linalodhohofisha ari ya uwekezaji mpya na urithishaji wa utaalamu/teknolojia. Serikali iangalie namna ya kutoa vibali vya muda wakati mchakato wa uhakiki unaendelea, pia waandae mfumo wa kuomba vibali kwa njia ya mtandao. Vilevile, gharama za vibali ziangaliwe upya na kupunguzwa.

**g) Uzingatiaji wa Usawa wa Kijinsia katika shughuli za Viwanda Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Kamati ilipata fursa ya Kutembelea baadhi ya Viwanda na kubaini kuwa, idadi kubwa ya wanawake wanaoshiriki katika kazi za viwandani wanahusika na shughuli ndogo ndogo katika nafasi za chini ikilinganishwa na wanaume ambao wameshikilia nafasi nyingi za maamuzi.

Ni maoni ya Kamati kuwa, upo umuhimu wa Serikali kwa kushirikiana na wawekezaji kuhamasisha uzingatiaji wa usawa wa kijinsia kwa kuhakikisha wanawake wanapata fursa sawa za nafasi za maamuzi katika shughuli za viwanda nchini, hali ambayo itachochea weledi na ujuzi wa wanawake na hivyo kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya uchumi wa viwanda.

### 2.3 **Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika,** Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Shilingi **81,366,902,000.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Kutokana na kuidhinishwa kwa fedha hizo, Kamati ilifanya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti hii ikiwa ni sehemu ya kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni ya 117(2) lakini pia kwa lengo la kujiridhisha kama dhamira ya Bunge lako ya kuidhinisha bajeti hii limetimia. Aidha, uchambuzi wa Kamati ulizingatia utekelezaji wa malengo/vipaumbele vya Wizara, Ukusanyaji wa mapato na Upatikanaji wa fedha ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa na Bunge.

#### 2.3.1 **Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ya Viwanda na Biashara (**Fungu 44 & 60**) ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi **15,000,000** (Fungu 44 – Viwanda Shilingi **9,000,000.00** na Fungu 60 – Biashara Shilingi **6,000,000.00**) kutokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni. Hadi kufikia Machi, 2021 Wizara haikuwa imekusanya kiasi chochote.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaikumbusha Serikali kuwa, jukumu la wizara hii ni kuratibu na kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara, kwa kutambua jukumu hilo inaishauri wizara kutoweka kipaumbele masuala ya ukusanyaji/utafutaji wa Mapato kwakuwa jambo hilo tayari linatekelezwa na Taasisi zilizopo chini ya Wizara.

#### 2.3.2 **Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.**

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha **2020/2021**, Wizara ya Viwanda na Biashara chini ya mafungu **44 – Viwanda** na **60 – Biashara**, ilitengewa kiasi cha fedha kama inavyoonekana katika Jedwali Namba 01.

**Jedwali Na. 01 Muhtasari wa Mchanganuo wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa Majukumu chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa fungu 44 &60.**

| UFAFANUZI | KIASI CHA FEDHA | % YA BAJETI |
|---|---|---|
| **Jumla** | 81,366,902,000.00 | **100** |
| **Matumizi ya kawaida** | 51,679,016,000.00 | **63.5** |
| **Matumizi ya Maendeleo** | 29,687,886,000.00 | **36.5** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara ya Viwanda na Biashara

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa mwenendo wa upatikanaji wa fedha ikilinganisha bajeti iliyoidhinishwa na Bunge pamoja na kipindi cha utekelezaji. Muhtasari wa Uchambuzi huo ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 02.

**Jedwali Na. 2 Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa na Kiasi cha fedha iliyopokelewa kwa mafungu 44 – Viwanda na 60 – Biashara hadi kufikia Machi, 2021**

| Mchanganuo | Bajeti iliyoidhinishwa | Kiasi kilichopokelewa | % ya Bajeti |
|---|---|---|---|
| **Jumla** | 81,366,902,000.00 | 45,512,707,118.72 | **55.94** |
| **Matumizi ya kawaida** | 51,679,016,000.00 | 38,629,551,706.20 | **74.7** |
| **Matumizi ya Maendeleo** | 29,687,886,000.00 | 6,883,155,412.52 | **23.2** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara ya Viwanda na Biashara

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Kamati kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka fedha **2020/2021**, na kwamba:-

i) Hakuna mwenendo mzuri wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina, kwani kiuhalisia mpaka kufika Machi, 2021 utekelezaji wa Bajeti ulipaswa kuwa asilimia **75** lakini wizara ilikuwa imepokea asilimia **55.94** kwa maana kuwa utekelezaji umepungua kwa asilimia **19.9; na**

ii) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha umeathiri zaidi utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambapo mpaka kufikia Machi, 2021 kiasi kilichopokelewa kilikuwa shilingi **6,883,155,412.52** ambacho ni sawa na asilimia **23.2** tu kwa maana kuwa asilimia **76.8** ya miradi ya Maendeleo haikutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, mtazamo wa Kamati ni kuwa mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha kwa Wizara ya Viwanda na Biashara unaashiria kukwama kwa utekelezaji wa baadhi ya majukumu yaliyopangwa na Wizara kwa mwaka huu wa fedha. Wizara hii ikiwa imebeba maono ya Serikali ya Ujenzi wa Tanzania ya Viwanda, kuna haja ya kupewa kipaumbele katika kupatiwa bajeti ili utekelezaji wa mujukumu yake uende kama ilivyokusudiwa.

## 3.0 **MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA USHAURI YA KAMATI KUHUSU BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Majukumu na Bajeti pamoja na mapendekezo ya Maombi ya Fedha ya Wizara ya Viwanda na Biashara ya Mwaka 2020/2021, Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo Ishirini na Mbili (22). Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati, hata hivyo kuna maeneo ambayo Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wake na inaendelea kuisisitiza Serikali katika maeneo yafuatayo:-

i) Uzingatiaji wa ushauri kuhusu kufanya marejeo ya makubaliano kati ya Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Afya kuchukua dawa ya Viuadudu kila mwaka kutoka katika Kiwanda cha Tanzania Biotech Product Ltd bado haujatekelezwa kwa kasi inayotakiwa. Ni mwaka mzima umeisha tangia agizo hili limetolewa lakini muafa haujapatikana na dawa za kiwanda kile zinakosa mteja mpaka kupelekea kukosa fedha za kujiendesha ikiwa ni pamoja na kushindwa kulipa mishahara ya wafanyakazi wake;

ii) Utekelezaji wa ushauri kuhusu kuhamasisha Uwekezaji kwenye uzalishaji wa bidhaa ambazo mara kwa mara zimekuwa zikikumbana na changamoto ya uhaba kama bidhaa ya mafuta na Sukari bado haujafanikiwa. Tumeendelea kuona bidhaa hizi zikipotea au kupanda bei kiholela; na

iii) Mradi wa Kurasini Logistic Centre bado haujaanza utekelezaji kama ilivyoshauriwa na Kamati. Ukweli ni kuwa tumekwisha lipa fidia ambayo ni fedha nyingi (Bilioni 101) na hakuna kinachofanyika hivyo hatunufaiki na fedha hizo ni kama zimefukiwa tu kwa kuwa hakuna tija inayopatikana hadi sasa.

## 4.0 **UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

### 4.1 **Uchambuzi wa Mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022**

#### 4.1.1 **Uchambuzi wa malengo/mpango**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara, Kamati ilipitia maelezo ya Waziri kuhusu malengo waliyojipangia kuyatekeleza kwa mwaka wa fedha 2021/ 2022 kwa lengo la kujiridhisha na tija inayoweza kupatikana katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2021/2022 katika **Fungu 44 na 60**.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi wa Malengo hayo ni kuwa yameendana na majukumu ya msingi ya Wizara ya Viwanda na Biashara, lakini pia yamezingatia Mpango wa tatu wa Maendeleo wa Taifa na ilani ya uchaguzi ya chama kinachoiongoza Serikali.

**Kwa mfano**, lengo la kuboresha mazingira ya biashara Nchini linaendana na Mpango wa Tatu wa Maendeleo kwa Kipindi cha Miaka Mitano Kuanzia 2021/22-2025/26 pamoja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 katika Aya ya 18

(a)(iii) ukurasa wa 12 wa Ilani ambayo kwa pamoja vimejielekeza kuimarisha mazingira ya Uchumi na Biashara kwa kuendelea kufanya mageuzi kwenye Sheria, Kanuni, tozo na utendaji wa Sekta ya Umma kwa kuzingatia Mwongozo wa kuboresha mazingira ya biashara (*Blueprint*).

### 4.1.2 Makisio ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ya Viwanda na Biashara imepanga kukusanya shilingi **15,000,000.00** kutokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kiasi kilichopangwa kukusanywa na Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ni sawa kabisa na kiasi kilichopangwa kwa mwaka wa fedha unaoishia 2020/21 ambacho hakikukusanywa kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** jukumu la wizara hii ni kuweka mazingira wezeshi ya kufanya Biashara, Kamati imeisisitiza Wizara kubaki na mtazamo huo na kuachana na habari za makusanyo kwa kuwa jukumu hili tayari linatekelezwa vizuri na Taasisi zake.

### 4.1.3 Mpango wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara imetengewa jumla ya Shilingi **105,670,459,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shughuli za maendeleo kwa mafungu yote mawili **Fungu 44 na 60**. Muhtasari wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 03

**Jedwali Na. 03 Mchanganuo wa Maombi ya Fedha kwa Wizara ya Viwanda na Biashara Fungu 44 – Viwanda na 60 – Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

| UFAFANUZI | MGAWANYO | FUNGU 44 | FUNGU 60 |
|---|---|---|---|
| **Matumizi ya Kawaida** | Mishahara | 23,191,574,000 | 22,801,535,000.00 |
| | Matumizi mengineyo | 5,119,373,000 | 1,470,091,000.00 |
| | **Jumla** | **28,310,947,000** | **24,271,626,000.00** |
| **Miradi ya Maendeleo** | Fedha za Ndani | 52,687,886,000 | 0 |
| | Fedha za Nje | 400,000,000.00 | 0 |
| | **Jumla** | **53,087,886,000.00** | **0** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara ya Viwanda na Biashara

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati kuhusiana na mpango wa bajeti wa Wizara ya Viwanda na Biashara umebaini mambo yafuatayo;-

i) Kiasi hicho cha bajeti kinachoombwa kwa mwaka wa fedha 2021/22 kwa ajili ya mafungu yote mawili kimeongezeka kwa asilimia **23** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ya Mwaka wa Fedha unaoishia yani 2020/2021;

ii) Ongezeko la Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara limesababishwa na ongezeko katika fedha za Miradi ya Maendeleo ambayo imeongezeka kwa asilimia **78.8** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021;

iii) Ongezeko la fedha za miradi ya maendeleo linatia mashaka kidogo kwenye utekelezaji wake kwa kuwa hata hiyo ya mwaka unaoishia ilitekelezwa kwa asilimia **21.9** tu.

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa kwa Kipindi cha Miaka Mitano Kuanzia 2021/22-2025/26 unalenga kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali ione haja ya kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara ili iweze kutekeleza majukumu yake yaliyolenga kuimarisha mazingira ya Sekta za Viwanda na Biashara na kuongeza mchango wake katika Uchumi wa Nchi.

## 5.0 **MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa kwa Kipindi cha Miaka Mitano Kuanzia 2021/22-2025/26 unalenga kujenga ***Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu***. Mpango huu umeainisha maeneo matano (5) ya kipaumbele na kati ya maeneo hayo matatu yanatekelezwa chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ione haja ya kuiwezesha kikamilifu Wizara ya Viwanda na Biashara ili iweze kutekeleza mpango huu kiukamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** maeneo mengine ambayo Kamati imeona kuna haja kwa Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara kuyatilia mkazo wakati wa utekelezaji wa Bajeti yake ya Mwaka 2021/2022 ni pamoja na:-

i) **Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati**
**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 utajumuisha utekelezaji wa miradi mitatu ya kielelezo na kipaumbele chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara ambayo ni miradi ya Liganga, Mchuchuma, Magadi Soda. Miradi hii ni ya Muda mrefu na imekuwa ikitajwa katika mipango mbalimbali ikiwepo Mpango wa Pili wa Taifa lakini utekelezaji wake bado unasuasua. Miradi hii ni kichocheo kwa baadhi ya Viwanda nchini hususani Viwanda vya Chuma kwa kuwa inatarajiwa kuzalisha malighafi ambazo zingetumiwa na viwanda hivyo. **Kamati inaishauri Serikali itoe kipaumbele kwa miradi hii wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo ili walau utekelezaji wake uanze.**

ii) **Utekelezaji wa Mradi Kituo cha Biashara cha Kurasini (*Kurasini Logistic Centre*)**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Kurasini Logistic Centre ni moja ya miradi ya kielelezo na unatarajiwa kuchochea ukuwaji wa Sekta ya Biashara na Viwanda. Utekelezaji wa mradi huu umechukua muda mrefu sana takribani miaka saba (7) ambapo kubwa lililofanyika ni ulipaji wa fidia ambapo takribani Bilioni 101 zimekwishalipwa. Kamati haioni jitihada za dhati katika kutekeleza mradi huu na madhara ya kuchelewesha utekelezaji wa mradi huu ni kuwa eneo lile limekwishalipiwa fidia kiasi kikubwa ambacho kinaonekana kama zimefukiwa tu na hutunufaiki na kiasi hicho. **Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuanza utekelezaji wa mradi huu ili tuanze kunufaika kama ilivyokusudiwa.**

iii) **Mazingira ya Kufanyia Biashara**
**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua nzuri zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali, bado kuna malalamiko kutoka kwa

wawekezaji kuhusu Mazingira rafiki ya kufanyia biashara na uwekezaji nchini. Baadhi ya wawekezaji wanalaamikia uwepo wa changamoto kama, mamlaka nyingi za udhibiti; urasimu katika upatikanaji wa vibali vya uhamiaji; na mlolongo wa kupata vibali vya uwekezaji. Aidha, taarifa ya Benki ya Dunia inaripoti Tanzania kuwa katika nafasi ya 141 kati ya 190 ya nchi yenye mazingira rahisi ya kufanyia biashara nafasi ambayo si nzuri sana. **Kwa kutambua hayo Kamati inaishauri Serikali;-**

a) **Kukamilisha mchakati wa kuandaa Muswada wa Sheria ya uwezeshaji wa Biashara (*Business Facilitation Act*) na Muswada huo uwasilishwe Bungeni haraka ili uweze kusaidia kutatua changamoto hizi;**

b) **Kuongeza nguvu/kasi katika utekelezaji wa Blueprint ili kuondoa changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo wazalishaji na wafanyabishara nchini;**

c) **Kuzisisitiza na kuzisimamia Sekta zote za Serikali kuhakikisha zinatekeleza sehemu yake katika Blueprint;**

d) **Kufanya mapitio ya kodi mbalimbali kwa nia ya kuzipunguza kwa kutazama majirani zetu kikanda ili tuweze kushindana nao katika masoko ya ndani na kikanda; na**

e) **Kutoa elimu kwa wananchi kuhusu blueprint ili kurahisisha utekelezaji wake kwa kuwa kila mtu ana nafasi yake katika kuongeza ufanisi na kasi katika kuleta maendeleo.**

iv) **Kufungamanisha Sekta ya Kilimo, Uvuvi na Mifugo pamoja na Ujenzi wa Viwanda**

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa vipaumbele vya mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo ni kuanzisha Viwanda vitakavyochakata mazao ya kilimo, uvuvi na ufugaji, na kwa kuzingatia asilimia kubwa ya watanzania wanajihusisha na shughuli hizo**. Kamati inashauri Serikali kwamba uhamasishaji wa ujenzi wa viwanda ambavyo vitachakata mazao yatokanayo na shughuli hizi uende sambamba na Wizara**

**husika kuiwezesha na kuihamasisha jamii kushiriki shughuli hizo kwa tija ili tuweze kutoa huduma za malighafi kwenye viwanda hivi. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeongeza ajira za kutosha kwa jamii na kuongeza mapato kwa serikali.**

v) **Sekta ya Utalii kuendeshwa kibiashara**

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya utalii nchini ina uwezo mkubwa wa kutuletea mapato kuliko ilivyo sasa, hii inatokana na ukweli kwamba sekta hii kwa sasa haifanyi kazi zake kibiashara hususan upande wa kujitangaza. **Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kulisimamia jambo hili kwa kuifanya sekta ya utalii kufanyakazi zake kibiashara zaidi ili kuongeza idadi ya watalii wa ndani na wale wanaokuja nchini ili kuongeza mchango wa mapato yatakayotokana na sekta hii.**

vi) **Uwepo wa Bidhaa bandia na zisizokidhi viwango sokoni**

**Mheshimiwa Spika,** uwepo wa bidhaa bandia au zisizokidhi viwango sokoni unadhihirisha bado kuna ushirikiano mdogo/ hafifu uliopo baina ya Taasisi za Ukaguzi zilizopo katika Vituo vya Mipakani pamoja na gharama kubwa inayotozwa kwa ajili ya ukaguzi, jambo linalosababisha baadhi ya wafanyabishara kuamua kutumia njia za panya kuingiza bidhaa zao na kupelekea uwepo wa bidhaa hafifu sokoni. **Kamati inaishauri:-**

a) **Serikali kuzisimamia kwa ukaribu Mamlaka hizo kuhakikisha zinashirikiana katika kufanya ukaguzi, lakini pia Serikali iangalie namna ya kupunguza gharama zilizopo ili kuweza kuwavutia wafanyabiashara kupitisha bidhaa zao katika vituo halali.**

b) **Serikali kuimarisha Shirika la Viwango TBS pamoja na Tume ya Ushindani FCC kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi, Vilevile taasisi hizi mbili zifanye kazi kwa ushirikiano katika kuhakikisha bidhaa zilizopo sokoni zinakidhi viwango lakini pia ni halali na zinaleta ushindani wa usawa sokoni**

vii) **Kiwanda cha Viuwadudu cha Kibaha – Tanzania Biotech Products Ltd**

**Mheshimiwa Spika**, kiwanda hiki kilianzishwa kwa lengo la kutokomeza Malaria nchini. Mpango wa awali ilikuwa ndani ya miaka 5 Wizara ya Afya ichukue dawa lita Milioni 5 kila mwaka na kuzipatia Halmashauri zote nchini. Utekelezaji umeshindikana kutokana na kuwa mteja mlengwa (Wizara ya Afya) ameshindwa kutekeleza makubaliano aliyoingia na kiwanda, hivyo basi tuna kiwanda ambacho kilifanyiwa uwekezaji mkubwa wa **Dola za Marekani 22,307,688.20** lakini kwa sasa hakizalishi, pia kama nchi bado tunasumbuliwa sana na ugonjwa wa malaria. **Kamati inaushauri ufuatao;-**

a) **Wizara ya Viwanda na Biashara ikae chini na Wizara ya Afya pamoja na TAMISEMI wajadiliane muafaka wa makubaliano ya awali na dawa ianze kutumika ili kiwanda kiendelee na uzalishaji; na**

b) **Kwa kuwa Bajeti kubwa inayoelekezwa kupambana na malaria inatokana na fedha za ufadhili na ili ufadhili huo uweze kutumika kwa dawa hii ya Viuadudu ni lazima vibali vya WHO vithibitishe ubora wa dawa. Wizara ya Viwanda na Biashara ihakikishe Kiwanda kinakamilisha na kuiwasilisha haraka iwezekanavyo taarifa inayohitajika na WHO kwa ajili ya kuthibitisha dawa hii.**

viii) **Mpango wa kulinda Viwanda vya ndani**

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa kwa kipindi cha Miaka Mitano Kuanzia 2021/22-2025/26 unalenga kujenga ***Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu***, kwa kuzingatia hilo tunapaswa kuweka mazingira rafiki yatakayo kuza Viwanda vya ndani ili kuongeza kazi ya ukuaji wa uchumi ikiwa ni pamoja na kutengeneza ajira nyingi zaidi kwa wananchi. **Kamati inashauri:-**

**a) Serikali ihakikishe inalinda bidhaa zinazozalishwa na Viwanda vya ndani ya nchi kwa kuweka uwiano wa Kodi**

**kwenye Bidhaa zinazoingia kutoka nje ya nchi utakaoendana na bei za Bidhaa zitakazozalishwa nchini;**

**b) Viwanda vya ndani ambavyo vinazalisha na vinauwezo wa kukidhi mahitaji ya soko ni vema Serikali ikatengeneza mazingira ya kuvilinda Viwanda hivyo. Aidha, manunuzi ya umma *(Public procurement)* yatoe kipaumbele kwa viwanda vya ndani;**

**c) Serikali iimarishe miundombinu ya umeme, maji na barabara ili kuvipa unafuu Viwanda viweze kupunguza gharama za uzalishaji;**

**d) Serikali kupitia vyuo vya ufundi iimarishe mafunzo ya taaluma na stadi za Viwandani ili tuweze kukidhi soko la rasilimali watu nchini.**

ix) **Utekelezaji wa Mfumo wa ukusanyaji kodi kwa njia ya kielekroniki (Electronic Tax Stamp – ETS)**

**Mheshimiwa Spika,** sote tunatambua nia njema ya Serikali ya kuanzisha Mfumo wa ETS lakini utekelezaji wake unalalamikiwa na wafanyabiashara kuwa ni wa gharama kubwa na pia unaendeshwa na mshauri elekezi kutoka nje ya nchi, malipo yanafanywa kwa fedha za kigeni na pesa yote inayokusanywa kupitia ETS yote inaenda nje ya nchi. **Kamati inaishauri Serikali kusikiliza malalamiko ya wafanyabiashara kuhusu Mfumo wa ETS, iyatafakari malalamiko hayo na kuyashughulikia bila kuathiri sheria zilizopo na kuweka mbele maslahi ya Taifa.**

## 6.0 **HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza sana kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa weledi mkubwa. Vilevile, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Spika, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza vikao vya Bunge hili la Kumi na Mbili.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kushiriki kikamilifu wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni kuhusu Bajeti ya Wizara hii mbele ya Bunge lako tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini na kwa ruhusa yako naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge (Hansard).

i) Mhe. David Mwakiposa Kihenzile, Mb - **Mwenyekiti**
ii) Mhe. Eric James Shigongo, Mb - **M/Mwenyekiti**
iii) Mhe. Usonge Hamad Juma, Mb
iv) Mhe. Martha Nehemia Gwau, Mb
v) Mhe. Cecil David Mwambe, Mb
vi) Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa, Mb
vii) Mhe. Lucy John Sabu, Mb
viii) Mhe. Hawa Chakoma Mchafu, Mb
ix) Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb
x) Mhe. Haji Makame Mlenge, Mb
xi) Mhe. Issa Ally Mchungahela, Mb
xii) Mhe. Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mb
xiii) Mhe. Khatib Said Haji, Mb
xiv) Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb
xv) Mhe. Maryam Omar Said, Mb
xvi) Mhe. Deodatus Philip Mwanyika, Mb
xvii) Mhe. Zulfa Mmaka Omary, Mb
xviii) Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb
xix) Mhe. Nancy Hassan Nyarusi, Mb
xx) Mhe. Salim Hassan Turky Toufiq, Mb
xxi) Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb
xxii) Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb
xxiii) Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb
xxiv) Mhe. Dkt. James Kimea Alfred, Mb
xxv) Mhe. Daudi Silanga Njalu, Mb

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Geofrey Idelphonce Mwambe, Mb. aliyekuewa Waziri wa Viwanda na Biashara, na Naibu Mhe. Kigahe Exaud Silaoneka, Mb, Makatibu wakuu pamoja na Watumishi wote wa Wizara ya Viwanda kwa jinsi walivyoshirikiana na kamati

katika kujibu hoja za Wajumbe wa Kamati, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha **2020/2021**, na kufafanua kwa kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha **2021/2022.** Aidha, Nampongeza Mhe. Kitila Mkumbo, Mb, kwa kuteuliwa katika nafasi ya Waziri wa Viwanda na Biashara, tunamkaribisha kwenye kamati na tunamuahidi ushirikiano.

**Mheshimiwa Spika,** nimshukuru aliyekuwa Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila kukwama. Aidha, nimpongeze Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc,* kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuteuliwa katika nafasi ya Katibu wa Bunge. Nimshukuru pia Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Athumani Hussein, *ndc.* Mkurugenzi msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi Bw. Michael Chikokoto, makatibu wa Kamati Bi. Zainab Mkamba na Bi Mwajuma Ramadhan pamoja na Msaidizi wa Kamati Bi. Grace Mwenye kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema haya, sasa naomba kulishauri Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu **44** na **60**, kwa Mwaka wa Fedha **2021/2022** kiasi cha shilingi **105,670,459,000.00** kama alivyofafanua mtoa hoja pamoja na maoni ya Kamati hii.
**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

David Mwakiposa Kihenzile, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA**
21 Mei, 2021

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa David Kihenzile, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza kipindi cha saa hizi, sasa nina matagazo mafupi ya wageni walioko Bungeni asubuhi hii.

Kuna wageni waliopo kwenye Jukwaa la Spika ambao kwanza ni wageni 51 wa Profesa Kitila Mkumbo, Mbunge, Waziri wa Viwanda na Biashara ambao ni Watendaji Wakuu 27 wa Wizara na Taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara Ndugu Dotto James. Karibuni sana wageni wetu kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Lakini pia tuna Ndugu Prosista Laswai, mke wake Mheshimiwa Waziri Profesa Kitila. Karibu sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Kuna Madiwani 14 wa Manispaa ya Ubungo wakiongozwa na Mheshimiwa Bakari Kimwanga, karibuni sana Madiwani wetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Lakini pia tuna viongozi tisa wa CCM Wilaya ya Ubungo wakiongozwa na Mwenyekiti wa Wazazi Wilaya ya Ubungo, Ndugu Justin Sangu, Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Ubungo Ndugu Pili Mustapha na Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Ubungo Ndugu Edwin Mrema. *(Makofi)*

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Edson Kigahe, Mbunge, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara ambaye ni mke wake kutoka Mkoani Iringa, Ndugu Rehema Mponzi. Karibu sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa hao ndio ambao wamekuja leo kutembelea. *(Makofi)*

Katibu, tuendelee. Tunaendelea na majadiliano Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana wewe mwenyewe binafsi kwanza asubuhi ya leo kwa kunipa nafasi ya kwanza kabisa kuchangia majadiliano haya kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara, lakini pia nikupongeze kwa kurudi tena hapo mezani na kutuongozea Bunge letu. Pongezi hizi nizipeleke pia kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, watendaji

wote na watumishi wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwanza kabisa kwa hotuba nzuri kabisa, fupi, inayoeleweka, yenye malengo makubwa ya kimkakati, lakini kwa namna ilivyooanisha kati ya Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano wa Maendeleo na ule wa Mwaka Mmoja amechanganya pia humo ndani na Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa maana ya kutaka kuwatekelezea watu na ndio maana tulisema Ilani hii ni bora ukilinganisha na ilani nyingi zilizoko Barani Afrika kwa sababu ina malengo makuu na yanayotekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie hasa kwenye maeneo matano. Eneo la kwanza kabisa ni utaratibu huu unaotumika sasa na Serikali kwa ajili ya kufanya kuhesabu mali zinazozalishwa kwenye viwanda vya vinywaji, almaarufu kama *ETS,* ufinyu wa bajeti ya Wizara hii, lakini pia pamoja na masuala ya *economic drivers* ili tuweze kuisaidia Wizara tuweze pia kuisaidia na nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mkakati ambao nchi yetu imejiwekea tunaweza tukaita ni Wizara mama, na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara tunafahamu mengi na huwa tunayajadili kule ndani, lakini mwishoni lazima tuyalete hapa ili tuweze kuishauri zaidi Serikali na yaingie kwenye taratibu zetu za Kibunge kwa maana ya *Hansard* ili kuweza kulisaidia Taifa letu. Malengo ya kuanzisha viwanda ni mazuri sana, lakini namna ya kufikia utekelezaji wa mambo haya ndio sehemu ambayo kidogo inaleta kutokufanya vizuri kwenye mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nchi yetu imekubali na imechagua viwanda kuwa kama ni sehemu ya *economic drivers.* Ni kati ya vile vitu vikubwa ambavyo tunategemea nchi yetu ikasimame ili kupandisha zaidi uchumi wetu, lakini pia kuwasaidia wananchi. Tunafahamu kuna mikakati mikubwa ya Serikali kwenye masuala ua Liganga na Mchuchuma, lakini haya ndio mambo yatakayokwenda kupandisha uchumi wa Kusini, matumizi mazuri ya Bandari

ya Mtwara pamoja na kubana matumizi kwenye *National Reserve* kwa maana ya pesa tutakayotumia nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano tulipoanza kutekeleza mradi wa *Standard Gauge Railway* kutoka Dar es Salaam kwenda mpaka Kigoma na Tabora mwanzoni kabisa tungefikiria tofauti kwa kuanza kuchimba kile chuma kilichopo Liganga na Mchuchuma ili chuma kile kiweze kutumika kutengeneza reli yetu na kiasi cha pesa kinachobakia kiweze kutumika kufanya mambo mengine kama *economic driver,* lakini kuchagua ni kuanza. Sasa na sisi tulichagua kuanza kutengeneza *SGR,* sasa hebu tuone kwa sababu pia kuna mkakati wa kutengeneza reli ya Kusini itakayoanzia *Mbamba Bay,* itapita Songea, itapita Masasi, itapita maeneo ya Ndanda kuelekea Bandari ya Mtwara ili kuweza kukuza uchumi wa watu wa Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi tuone namna sasa ya kuanza kutekeleza mradi huu wa Liganga na Mchuchuma ambao umeanza kutajwa siku nyingi sisi tukiwa wadogo kabisa huko na huu ni uchumi mkubwa kabisa utakaoweza kuendeleza zaidi maeneo ya Kusini ambayo kwa namna fulani yalikuwa yanaonekana kama yametolewa kwenye mkakati wa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado hapo hapo kwenye suala la *economic drivers.* Ukiangalia kwenye sekta zinazokua vizuri kuna sekta ya ujenzi inakua kwa asilimia 14 na wote tunakubaliana. Kwa mfano tunapokuwa na barabara bora kwa vyovyote vile tutakuwa na biashara nzuri, tutakuwa na barabara nzuri pia zinazoweza kusafirisha mazao kutoka eneo moja kwenda eneo lingine ikasaidia pia kuwakuza wakulima wetu. Suala la umeme pia limekua kwa asilimia nane, lakini pia kuna suala la usafirishaji na lenyewe karibu asilimia 11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukienda kwenye mchango kwenye *GDP* kilimo kinachangia *almost* asilimia 36 kwenye *GDP.* Viwanda vinachangia asilimia 24 kwenye *GDP,* lakini ukija kuangalia kwa ujumla bajeti ya kilimo pamoja na bajeti ya kiwanda ni ndogo sana. Mfano kama ambao

nilisema pale toka mwanzo kwamba Mchuchuma na Liganga awamu iliyopita kwa maana ya bajeti iliyopita wamepelekewa shilingi milioni 120 tu halafu leo tunasema tunataka tuone Mchuchuma na Liganga vinakwenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya majadiliano yanayofanywa na Serikali na hivi vitu vimetajwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, hebu basi fanyeni hima muone namna sasa ya kukuza uchumi wetu kama ambavyo iko China kwa ajili ya viwanda vya chuma, kwa ajili ya kuboresha ile Bandari ya Mtwara ambako uwekezaji mkubwa kabisa pale umefanyika, lakini hatuoni sasa tija ya kutumia ile bandari kwa sababu kimsingi hatuna mizigo mikubwa ya kuweza kupeleka pale. Tunategemea uzalishaji, mzigo pekee mkubwa unaopelekwa Bandari ya Mtwara ni korosho peke yake, kwa nini sasa tusione na kile chuma tunatakiwa tukilete bandarini kwa ajili ya kukisafirisha kwenda nje, lakini pia tutengeneze na viwanda kwenye maeneo hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo pia Wizara ya Viwanda na Biashara wanatakiwa walione, kubadilisha sheria kidogo hasa zaidi kwenye matumizi ya mazao ya shambani na kila mara nimekuwa najaribu kuwaeleza kwenye hili jambo tufungamanishe Wizara ya Viwanda, Wizara ya Biashara pamoja na *TIC* au Wizara ya Uwekezaji. Hivi ni karibu sawa vitu vinavyoingiliana, vitu vinavyofanya kazi kwa kushabihiana, wawe na mahusiano mazuri ili tuweze kupata *definition* ya kila kimoja. Tujue majukumu halisi ya Wizara ya Viwanda na Biashara, wafungamanishe na majukumu halisi ya Wizara ya hawa *TIC,* lakini pia tuangalie kwenye Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nitoe mfano hapa na kila mara nimekuwa nasema hapa ndani ya Bunge kuhusiana na mazao yanayobakia shambani hasa zaidi baada ya mavuno ya korosho. Huwa wanatupa kitu fulani kinaitwa kochoko, wenzetu wa Scotland mwaka jana wametengeneza ile pombe yao inaitwa *Scotish Whisky* wameingiza *almost 4.5 billion Euro* kwa ajili ya kutengeneza

hii pombe. Na sisi tunavyo vifaa vya kutengenezea hivi kwa mfano kochoko. Nia sasa wakulima wale wanunue yale mabibo yanayobakia waweze ku-*extract* tuweze kupata pesa za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilisema nitaliongelea hap ani suala la *ETS.* Hakuna mgogoro kwamba baada ya Serikali kuamua kutumia mfumo huu wa *ETS (Electonic Tax Stamps)* kwa ajili ya kuhesabu bidhaa kwenye viwanda ni kweli imeongeza mapato na imepunguza kabisa wizi. Sasa suala lililopo ni kwamba, wafanyabiashara wanalalamikia kwamba, kazi ya *ETS* ni kuhesabu tu, hii Kampuni ya SIPA, inahesabu chupa moja moja wanaweka pale *label* na kwenda kuiambia Serikali kwamba kiwanda kwa mfano cha Cocacola kimezalisha chupa 500 tunaomba mkazitoze kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa utakuta kwa mfano *juice* ya *mls 200* kodi inayoipata Serikali ni shilingi 1.08, lakini *juice* hiyo hiyo ya *mls 200* fedha anayoipata SIPA kwa kuhesabu kile kichupa kimoja ni shilingi 23. Sasa mtaona hizi gharama zinakwenda kumuongezea mlaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba sana na Katibu Mkuu wa Wizara Mheshimiwa Dotto James ndio alikuwa ni mmoja wa waasisi wa huu utaratibu na yupo huko kwenu, hebu muangalie kwa nini tusitafute kampuni nyingine itakayoweka hizo *stamps,* itakayokuwa inahesabu kwa gharama nafuu zaidi ili mapato yake nayo yalingane. Haileti tija akilini kuona eti Serikali inapata shilingi 1.08 alafu yule aliyefanya kazi ya kuhesabu chupa na kuitaarifu Serikali kwamba nimehesabu hizi chupa inapata shilingi 25 katika *juice* ya *mls 200* sawa sawa na ilivyo kwenye soda, kwenye Cocacola au na Pepsi au na nyingine gharama ni kubwa sana ya kuhesabu kuliko ushuru unaokusanywa na Serikali kwa hili nalo tukaliangalie vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya maendeleo mwaka jana imepata asilimia 23 tu Wizara hii ni kubwa, lakini sio sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuone pia kuhusu masuala ya viwanda vilivyobinafsishwa Mheshimiwa Waziri umeyataja hapa, ninafikiri umekwenda kuyafanyia kazi tuone kiwanda cha Buko cha Korosho pale Masasi kila siku tukiwauliza mnasema kwamba kuna kesi inayoendelea mahakamani, lakini kuna jambo kubwa ambalo tunakwenda sasa hivi kukutana nalo, kuna biashara za korosho zitaanza hivi karibuni na msimu wa korosho unakenda kufunguliwa na suala kubwa sana Waziri la unyaufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakapokuwa unamaliza kutoa hotuba yako na hili utueleze tunaomba sasa kufahamu kinagaubaga na Serikali iseme kwa neno moja je, kuna unyaufu ama la kwenye zao la korosho ili sasa wale wanaokuja kufanya biashara ya korosho, wanaokuja kuhudumia maghala waweze kujua wazi toka wanaanza hii biashara kama ni kweli kuna unyaufu au hakuna kwa sababu imekuwa ikileta mkanganyika mkubwa sana.

Mheshimiwa Waziri niombe pia kukukumbusha suala la *blueprint.* Imetengenezwa *blueprint* na Serikali hii na kila siku tunasema kwamba tunaweza tukatumia *blueprint* ili kuondoa vikwazo vinavyowakuta wafanya biashara kwa hilo nalo ukalifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi uliyonipatia ahsante kwa muda wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Cecil Mwambe, tunaendelea na Mheshimiwa Issa Mchungahela baadaye Mheshimiwa Subira Mgalu na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma wajiandae wabunge wa CCM tutachangia kwa dakika saba saba kwasababu *list* imeongezeka.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ameniweka hai na kuweza kuchangia bajeti hii ya viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kujielekeza kwenye bajeti hii kwa kuangalia baadhi ya vitu mimi sina shaka na mipango, mipango ya Chama chetu cha Mapinduzi lakini mipango pia ya Serikali sina shaka. Tumekuwa na mipango mizuri mingi sana tangu Serikali ilivyoanza kuundwa na mpaka hivi leo, ukiangalia bajeti za kila mwaka utathibitisha hilo. Kwa miaka mitano hii inayokuja mipango yetu imekuwa mikubwa na mizuri sana na kama tunavyojielekeza kwenye bajeti ya uchumi endelevu, lakini uchumi shindani pia hili ni jambo zuri kabisa na ni jambo jema lakini tunahitaji kujielekeza nguvu zetu katika utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tuna shida sehemu katika suala hasa la bajeti kuangalia vipaumbele. Tumekuwa hatujikiti sana katika vipaumbele vya bajeti zetu, tunaongea mambo mazuri, lakini katika utekelezaji nafikiri kumekuwa na changamoto, tuangalie mfano mdogo tu katika bajeti zetu, ukiangalia bajeti ya viwanda kwa mfano bajeti hii ndio mkombozi katika uchumi wa nchi hii kwa sababu kwa kutumia bajeti hii tungeweza kwa namna moja au nyingine kufikia malengo yale ya uchumi endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu gani kama tungeingia kwenye vipaumbele, lakini ukiangalia unakuta miradi ambayo tunajaribu kutaka kuitekeleza ambayo kwa hali halisi ndio miradi ya mkakati unakuta kitu tofauti kwa mfano Mradi wa Liganga na Mchuchuma ambao ni mradi mkakati kwa mwaka 2020/2021 ulitengewa takribani shilingi milioni 120 tu, mwaka 2021/2022 umetengewa shilingi milioni 25. Kwa kweli hatuko *serious* kabisa kama kweli tunataka kufanya yaani kwamba kama miradi hii ni mradi mkakati tofauti tunachoongea na kile tunachokifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia Mradi wa Mchuchuma tumetengewa takribani shilingi milioni 120 peke yake mwaka 2020/2021 lakini mradi huo huo pia tumetengewa takribani shilingi milioni 25 katika msimu wa mwaka 2021/2022 kwa kweli hatupo *serious,* hatupo *serious* kabisa, lakini mradi wa Ziwa Natron wenyewe ulitengewa shilingi milioni 50 peke yake, hali kadhalika kwenye mwaka

2021/2022 ulitengewa shilingi milioni 24 kwa kweli haioneshi kabisa kama sisi tupo *serious* katika huu uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu tukitaka tuendelee kwa umakini kabisa uchumi wa viwanda lazima tufanya *seriousness,* ionekane kabisa kwa sababu ukiangalia kiasi kilichotengwa kwa maendeleo kwa takribani kwa miaka hii miwili haizidi bilioni 30 sasa sijui kama kweli tunataka kutekeleza maendeleo ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuzungumza ni nini; kama tutajielekeza kweli kwenye uchumi wa viwanda kikweli kweli tunaweza tukaendelea vizuri sana na tukawa tumepata tija kubwa na mafanikio makubwa sana katika maendeleo na hatuwezi kujidanganya hatuwezi kuendelea pasipo kuendeleza viwanda, kwa sababu viwanda ndio vyenyewe vinakula *material, material* nyingi sana ambazo sisi tunatengeneza hapa ina maana kwamba kwenye kilimo kwa mfano, lakini kwenye maeneo mengine ya uchumi kwa mfano ya madini na hali kadhalika kwenye maeneo mengine ya uchumi kwa mfano yanayotokana na bahari yaani kwenye uchumi wa *blue* hivi vyote vinatumika na viwanda ndugu zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo bila viwanda hivi vitu vyote tunavyovizungumza haviwezi kufanikiwa na hatutaweza kuviendeleza, kama nilivyojaribu kuangalia kwa mfano tuchukulie mfano tuone muonekano halisi wa kadri jinsi haya mambo yanavyokwenda yanavyoweza yakatupatia tija. Tuna *issue* ya *EPZ* ambaye na yenyewe hatuoni kama tuna u- *seriousness.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EPZ* kwa mfano pale Benjamin William Mkapa Serikali iliwekeza pale shilingi bilioni 36.4 kwa ajili ya kufidia na kuweka miundombinu, lakini ukiangalia pale kilichotokezea tulipata tija kubwa sana kutoka kwenye hiyo shilingi bilioni 36 tuliyowekeza tija tulizozipata pale tulipata uwekezaji wa mtaji yule mwekezaji aliweka mtaji wa shilingi bilioni 134; unaweza ukaona ni fedha nyingi kuliko tulizowekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa shilingi bilioni 36 tuliyowekeza tumepata shilingi bilioni 134 kama uwekezaji wa mtaji, lakini kampuni pia ilifanya mauzo ya shilingi bilioni 385.93 na kampuni hizo pia zilifanya matumizi ya fedha ambazo takribani shilingi bilioni 2019.184 lakini pia Serikali ilipata faida kupitia kodi ya shilingi bilioni 22.67 *on top of that* tulipata ajira ya watu 3,156.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnaweza mkaona kwa jinsi gani tija kubwa ya shilingi bilioni 36 tu imezalisha haya yote haya tumepata Watanzania, kama tungewekeza vya kutosha Benjamin William Mkapa bila shaka mngeweza mkaona tija gani mngepata hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ukiangalia *SEZ* eneo na Bagamoyo Serikali iliwekeza shilingi bilioni 26 peke yake lakini katika kuwekeza shilingi bilioni 26 Serikali ilikuja ikapata tija kubwa sana kulikuwa na tija kwa mfano shilingi bilioni 4.8 ya uwekezaji; mwekezaji aliweka hizo fedha, lakini mwekezaji pia alifanya mauzo ya nje ya shilingi bilioni 56.2 lakini kama haitoshi kampuni pia ilipata kwa kulipa kodi shilingi bilioni 1.305. Kwa hiyo unaweza ukaangalia kwa kiasi kidogo tu cha shilingi bilioni 26 tulizowekeza Bagamoyo tumepata fedha nyingi hizi, lakini cha kushangaza hapo hapo Serikali inadai kujaribu kurudisha baadhi ya maeneo ambayo tungeendelea kuyawekeza ya *SEZ* kwa kweli hatupo *serious* na kama tupo *serious* kwa kweli tunatakiwa tuwekeza kikamilifu kwenye viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, lakini naomba *seriousness* kwenye viwanda ifanyike, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Subira Mgalu baadaye Mheshimiwa Stanslaus Nyongo na Mheshimiwa Ahmed Salum ajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa kuweza kuchangia Wizara hii ya Viwanda na Biashara, nianze kukupongeza kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti, ninaamini utafanya vizuri kama ulivyofanya Bunge la Kumi na Moja, lakini sambamba na hilo nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa uandaaji mzuri wa hotuba ya bajeti na uwasilishaji mzuri wa Mheshimiwa Waziri ambao bajeti yao kwa kweli imeainisha maeneo mbalimbali na ukizingatia sekta hii ya viwanda ndio muhimili mkuu wa kukuza uchumi, kupambana na umaskini na kuzalisha ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri hotuba yake imeainisha maeneo mbalimbali, lakini kubwa imeanza kutoa mwelekeo wa utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan alipotoa hotuba yake ndani ya Bunge ambayo ililenga kuchukua hatua mbalimbali katika kukuza uwekezaji na kufanya marekebisho kadhaa katika sera, sheria na kanuni na kuondoa vifungu ambavyo vitabainika kusababisha vikwazo katika uwekezaji, lakini pia vikwazo kwa wafanyabiashara na ninapongea Mheshimiwa Rais tumeona namna ambavyo anaendeleza mafanikio ya awamu ya tano kwenye sekta hii ya viwanda lakini tumeona pia hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Wizara nyingine katika kuwezesha sekta hii ya biashara na viwanda kuona kwamba inafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano tumeona Mamlaka ya *TRA* imefungua akaunti zote walizofungiwa wafanyabiashara, kwa hiyo, tumeona namna ambavyo wawekezaji nao wameanza kurejesha imani yao na mitaji mbalimbali, lakini mchango wangu utajielekeza kwanza kwenye utekelezaji wa mpango wa kuboresha biashara wa *blueprint* pamoja na mafanikio ya kupunguza tozo zaidi ya

232; lakini ningemuomba Mheshimiwa Waziri kama tunataka mafanikio katika sekta yake hii ambayo itawezesha sekta nyngine ni lazima hatua ya kupunguza muda wa gharama za kupata leseni na vibali ambavyo vimeainishwa kwenye mpango huu wa *blueprint* utekelezeke kwa dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninasema hivyo ukifanya mapitio ya taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwanza hata taarifa ya Kamati niipongeze wamewasilisha vizuri nchi yetu kuwa nafasi ya 141 kwa mwaka 2020 kutoka 131 kwa mwaka 2015 ni wazi imeshuka, lakini ninatambua mpango huu wa *blueprint* umeanza kutekelezwa 2019 lakini ninataka niseme taasisi kwa mfano *TRA*, Baraza la Mazingira Tanzania, Uhamiaji na masuala ya utoaji vibali vina mchango mkubwa katika kuweka mazingira wezeshi ya kibiashara nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano katika ripoti hiyo imeainisha namna gani Mamlaka ya *TRA* imetumia zaidi ya siku 182 mpaka siku 675 kujibu maombi ya vivutio vya kodi wakati sheria ya uwekezaji ya mwaka 1997 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2015 imetamka kifungu 16(2),(3),(4) ndani ya siku 14 *TIC* inapopeleka maombi ya hawa wawekezaji mbalimbali wawekezaji hao wajibiwe, lakini utaona kwenye mamlaka zetu ucheleweshaji ni mkubwa. shilingi bilioni

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia baraza la mazingira uwekezaji wote wa viwanda lazima upatikane mchakato wa uhakiki wa mazingira. Sheria ya *NEMC* ya mwaka 2018 imeitaka baraza hili kuchukua siku 95 kwenye mchakato huo na kutoa vibali, lakini imekuwa ikichukua siku mpaka 133 mpaka siku 200 na kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ni miradi 5,600 kati ya 13,000 ambayo ilipewa vibali vya maingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaamini pia kaka yangu Mheshimiwa Jafo Mheshimiwa Waziri katika Wizara hii anayo nafasi kubwa kama ambavyo alivyokuwa na nafasi za mamlaka nyingine ili kuwezesha kwamba mpango huu

ukamilike na kwa kweli kama watajikita kwenye mpango huu vikwazo vingine vyote ni vyepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nije kwenye changamoto vya wafanyabiashara, wafanyabiashara pamoja na hatua zinazoendelea kuchukuliwa lakini bado wanalalamika utitiri wa kodi katika biashara mbalimbali, kwa mfano Mkoa wetu wa Pwani sisi unaongoza kwa viwanda na ninachukua fursa hii kuupongeza uongozi wa Mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika maeneo mbalimbali kwa mfano Wilaya ya Mkuranga, viwanda vinavyotengeneza *gypsum* kwa mfano kiwanda cha KNAUF kinalalamika tozo kubwa ya karatasi ambayo imewekwa kwa ajili ya malighafi ya kutengeneza bidhaa ya *gypsum,* lakini sambamba na hilo tunavyo viwanda katika eneo la Kibaha, nikupongeze Mheshimiwa Waziri umeainisha namna gani Serikali imeenda kujielekeza eneo letu la *TAMCO,* lakini na mchango wake wa tozo mbalimbali wa zaidi ya shilingi bilioni tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo hayo pia zipo changamoto za masuala ya miundombinu wezeshi kwa mfano suala la nishati, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nishati, ni siku tatu zilizopita alitembelea maeneo yale na kuwatia moyo wenye viwanda na kuwaambia mipango ya Serikali namna gani itawezesha umeme wa uhakika wa maeneo haya usio katika katika, lakini tunaomba hatua hii ifanyiwe haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo sisi wana Pwani tunaomba Serikali kwamba viwanda hivi pamoja na kwamba tunaongoza kwa kuwa na viwanda vingi lakini ajira hata zile ambazo zisizohitaji wataalam vijana wengi wamekuwa wakikosa ajira, lakini pia mazingira kazini ya wafanyakazi, pia ujira wa wafanyakazi hawa. Kwa hiyo tunaomba Serikali ishughulikie hayo naipongeza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kuainisha eneo la uwekezaji la Bagamoyo, lakini pia kwa kuwa Serikali ina mpango wa kuongeza uzalishaji wa sukari naomba niwakaribishe Wilaya ya Rufiji na Wilaya ya Kibiti yapo maeneo ya kimkakati kwa kutumia Bonde la Mto Rufiji na uwezo wa kujenga viwanda hivyo vya sukari, lakini pia niipongeze Serikali yenyewe kwa kutumia mifuko yake ya Hifadhi ya Jamii kuwekeza katika viwanda mbalimbali, lakini katika hili kwa kuwa Serikali imewekeza kwa mfano Serikali imewekeza katika mradi wa Mkulazi *CAG* ametoa maoni kadri muda wa manunuzi wa mashine unavyochelewa, kiwanda hiki cha Mkulazi kinapata hasara. Niiombe Serikali jambo hili lipo ndani ya uwezo wao wajitahidi ili nchi yetu ijitosheleze kwenye uzalishaji wa sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ninatambua mkakati wa uzalishaji wa vifaa tiba. Ripoti ya *CAG* imeainisha namna gani Serikali kupitia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ilivyotumia fedha zaidi shilingi milioni 900 kuanzisha kiwanda hiki katika Mkoa wa Simiyu, lakini mpaka leo zaidi ya siku 500 kibali cha ujenzi wa kiwanda hiki hakijatoka, lakini sambamba na hilo pia kuna Kiwanda cha Chai Mponde kule Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wanataka kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali kwakuwa ndio yenyewe ambayo imeona iwekeze kwenye miradi ya uwekezaji basi ijitahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimepata maombi au utumishi wa wamiliki wa hoteli, kuna hii *hotel levy* mpango wa *blueprint* ulipendekeza kupunguza kwa asilimia mbili, lakini mpaka sasa hivi haijatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaunga mkono hoja, lakini niombe mpango huu utekelezwe mpaka ngazi za Halmashauri, ahsante sana na hongereni na kazi iendelee. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Subira Mgalu. Tunaendelea na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo na

Mheshimiwa Ahmed Salum na Mheshimiwa Njau David, wajiandae.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nashukuru sana kwa kunipatia nafasi, mimi kwanza niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya yeye na watumishi wote katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji aliyekuwa akichangia/aliyemaliza sasa hivi naye amekumbushia suala la Kiwanda cha Vifaa Tiba katika Mkoa wa Simiyu hasa vifaa vinavyotokana na zao la pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni tatizo ni nini, nani kakwamisha kibali hivi kama sisi tunataka nchi iwe ya viwanda sisi wenyewe tena tunakuwa vikwazo maana yake nini. Naiomba Serikali mjitahidi kuhakikisha kwamba kiwanda hiki cha vifaa tiba kinaanza kufanyakazi kwa sababu ndiyo mkombozi wa Watanzania kwa maana vifaa tiba, lakini bado ni mkombozi kwa wakulima wa pamba katika mikoa inayozalisha pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la pamba linalimwa katika mikoa takribani minne, mitano zaidi na bado kuna mikoa mingine zaidi. Mkoa wetu wa Simiyu, Mkoa wa Mwanza, Mkoa wa Shinyanga, Mkoa wa Mara na Mkoa wa Kagera ni wazalishaji wazuri wa pamba, na sisi katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 tumesema kabisa kwamba tutajikita katika kuhakikisha tunasimamia uzalishaji wa mazao na hasa mazao ya biashara pamba ikiwemo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamba ndiyo mkombozi wa wakulima wa maeneo haya, lakini naomba nikuambie uzalishaji wa pamba huu kila siku umekuwa na maneno, umekuwa na kelele kwa sababu zao la pamba limekosa soko la kudumu. Mkulima wa pamba ananyanyasika miaka yote, sisi kwetu pamba imebadilika imekuwa siyo zao tena la

biashara limekuwa zao la kisiasa, *is a political crop* kwa sababu wewe Mbunge, wewe Diwani unapoomba kura inabidi uongelee maslahi ya zao la pamba ndipo upewe kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sisi Wabunge tuliomo humu wa mikoa tunayozalisha pamba tukirudi hivi hivi mimi naomba niwaeleze hatutarudi tena humu Bungeni kwa sababu wakulima wengi wa pamba wanaona kama vile hatuwatetei. Zao la pamba linakwenda kuzalisha nguo, *market* ya nguo iko Tanzania, iko Kenya, iko Uganda nchi zote za Afrika Mashariki wanahitaji nguo na binadamu anapozaliwa leo mpaka kufa kwake anahitaji nguo; ukizaliwa unafunikwa nguo, ukikua unavaa nguo, ukilala unajifunika nguo, ukienda msibani, ukifa tunakuzika umevalishwa nguo. Hakuna *product* iliyokuwa muhimu kutoka baada ya chakula kinachofata ni nguo na *market* hii ya *East Africa* ni kubwa mno. Lakini nguo zinazozalishwa zinaingizwa kutoka nchi za nje na tunalipa kodi kubwa tunatumia fedha za kigeni kupeleka fedha nje na tunalipa kodi hizo na tunaponunua fedha za kigeni tunakwenda kuingiza nguo kwa ajili ya matumizi ambayo ni *basic* kwa mwanadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamba tunayozalisha asilimia 75 tuna *export* hebu ona hiyo miujiza yaani *raw material* inayohitajika kwa bidhaa ambayo ni muhimu *raw material* yake badala yaku-*consume* sisi hata Tanzania kuitumia katika viwanda vyetu vya kuzalisha nguo, bidhaa hiyo tuna *gin* tuna-*process* kwa asilimia 25; asilimia 75 ya *process* yaani kwa maana ya mnyororo wa thamani tunaupeleka nje, halafu tukishaupeleka nje tunakwenda kuzalisha ndiyo tuna *import* tena, haya ni maajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali msimame na miradi ya kimkakati mlijali suala la zao la pamba kuna mkakati wa *CC (Cotton to Cloth)* nimeona imekuwa ni maneno tu hatujui mkakati huu ni wa Wizara ya Kilimo, hatujui mkakati huu ni wa Wizara ya Viwanda, hatujui mkakati huu ni wa nani? Tunaomba Serikali mkae muamue leo kwamba tunakwenda kulipa soko zao letu la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusitegemee wafanyabiashara watutengenezee kiwanda cha nguo, ni lazima Serikali i-*invest* kwa sababu gani, mnyororo wa thamani wa kutoka pamba kwenda nguo hapa katikati kuna viwanda vingi sana kuna uzalishaji wa pamba, kuna kufanya mambo ya ku-*gin,* kuna kutengeneza majora na kutengeneza majora kuna kuhitaji hapo katikati kuna *process* nyingi, hapo kuna utengenezaji wa rangi za nguo, kuna utengenezaji wa *label* za nguo, *pakken material* kwa maana ya *plastic* kuna vitu vingi hapa katikati mjasiriamali mmoja hawezi kutengeneza *value chain* ya pamba mpaka kwenye nguo ni lazima Serikali *intervene,* ni lazima Serikali itengeneze miundombinu wa wajasiriamali kila mmoja katika *value chain* hii ya pamba alenge sehemu moja afanye biashara. Kama ni mtengeneza rangi atengeneze rangi, kama ni mtengeneza vifungo atengeneze vifungo, kama ni mtengeneza uzi atengeneze uzi, kama mtengeneza *label* atengeneze *label, the end of the day* hii *value chain* ikikamilika ndipo unaweza ukatengenezewa shati ukavaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo nguo uliyovaa hapo Mheshimiwa Waziri nguo uliyovaa hapo kifungo ni kiwanda kingine, *label* ni kiwanda kingine hiyo rangi ni kiwanda kingine viatu ni kiwanda kingine. Kila kitu ni kiwanda kingine bila Serikali ku-*intervene* ikatengeneza *value chain* nzima hatuwezi kuwa na *cotton to cloth,* hiyo *strategy* yenu haitafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vitu havihitaji elimu sijui ya namna gani, kwani hamuoni kuna kiwanda kinachotengeneza baiskeli? Baiskeli inatengenezwa na fundi chini ya mti tu, lakini anayetengeneza tairi mwingine, anayetengeneza *rim* mwingine, anayetengeneza *wire,* ni mwingine ni Serikali ndiyo inayotengeneza utaratibu huu kama mnasema sijui mnaanzisha sijui *industrial park* tengenezeni *industrial park* ya tairi, tengeneza ya *spoke,* tengeneza ya kengele, tengeneza ya mpira, tengeneza ya *wire; the end of the day* mtu anakwenda ku-*assemble* baiskeli chini ya mti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wewe leo mnasema leo mfanyabiashara atengeneze kiwanda cha nguo! Mimi nawaeleza haitawezekana mtu akatengeneza eti nguo kamili ukienda hata pale *EPZ* Dar es Salaam kuna watu wanatengeneza nguo wana-*export* wanapeleka Marekani, lakini leo unakuta kifungo kimetoka Malaysia, unakuta sijui majora yametoka India, sijui zipu imetoka sijui wapi, rangi imetoka sijui wapi, ndiyo wanakwenda ku-*assemble* pale wakisha-*assemble* ndiyo wanapeleka wanakwenda kuuza sehemu zingine. Serikali na kama mimi leo ningeongea na Mama Samia Suluhu Hassan - Rais wetu ningemwambia aanzishe Wizara inaitwa *Textile Ministry,* iangalie kutoka pamba mpaka nguo kwa sababu Wizara ya Viwanda na Biashara hamtaweza peke yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba hili mlizingatie bila hivyo sisi wakulima wa pamba tutaendelea kulia na wakati tunazalisha pamba nzuri yenye thamani nzuri ambayo sisi kama Serikali tunaomba muiongezee thamani pamba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani leo pamba tunauza shilingi 1000 tu na bado tukiuza shilingi 1000 mkulima bado analaliwa, mkulima anacheleweshewa fedha, mara tunaanzisha Ushirika, mara sijui tunafanya nini tuna chemka. Tengeneza *demand* ya pamba katika nchi yetu sisi tuweze kuuza pamba yetu na tuongeze thamani ya pamba yetu, tukauze Kenya, tukauze Uganda, tukauze sehemu zingine. *Market* ipo binadamu wote wanahitaji nguo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Stanslaus Nyongo. Tunaendelea na Mheshimiwa Ahmed Salum baadaye Mheshimiwa Njalu Daudi na *Engineer* Ezra wajiandae.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia leo katika

Wizara hii ya Viwanda na Biashara, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwa hotuba nzuri sana yenye malengo mazuri ya kuboresha vivutio vya uwekezaji katika Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nimwambie Mheshimiwa Waziri mwaka 2017 aliyekuwa Waziri wa Viwanda na Biashara wakati huo Mheshimiwa Mwijage kuna kitu walikianzisha kinachoitwa *blueprint*. Chimbuko la *blueprint* lilitokana na muwakilishi wa *World Bank* baada ya kuwa ameongea na aliyekuwa Waziri Mwijage akamwambia bado ninyi Tanzania hamko vizuri kwenye vivutio vya uwekezaji na namna ya kuwekeza ndani ya Jamhuri ya Muungano, walibishana sana. Maana yake ni kwamba Mheshimiwa Waziri wakati ule alienda kufanya utafiti wa kina na kujua kweli Tanzania ni nini kinachofanya wawekezaji wasiweze kuja vizuri kuwekeza ndani ya nchi pamoja na wawekezaji wa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya utafiti mdogo nikaiona Tanzania katika *easy of doing business in Tanzania report* ya *World Bank Group* ya mwaka 2020 Tanzania ni ya 141 nchi ya kwanza kabisa ni New Zealand, nchi ya pili ni Singapore, nchi ya tatu ni Hong Kong kwa maana ya kwamba vivutio vizuri na namna ya uwekezaji mzuri ndani ya nchi hizo ni nchi za kwanza ambazo zinaongoza tatu bora duniani. Lakini Rwanda ni ya 38; angalia Rwanda wako 38 sisi tuko 141. Lakini ukiingia Kenya wenyewe wako wa 56 naongelea hii ripoti ambayo iko ndani ya *World Bank Group*, Uganda wenyewe ni 116, Zambia 85, Malawi 109 na nchi ya mwisho kabisa duniani ni Somalia ya 190.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake nini? Maana yake ni kwamba tafrisi yake hii ni kwamba Mheshimiwa Waziri unaweza ukawa una mipango mizuri sana, lakini *blueprint* ambayo iliandaliwa kama hutoifanyia kazi kwa maana kuondoa vikwazo ambavyo vinafanya uwekezaji visiwekeze vizuri, waone ni shida katika kuwekeza katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utaongea sera nyingi sana, mambo mengi sana, huwezi kufanikisha. Ondoa vikwazo chukua hii

*blueprint* lete hapa tupitishe futa kero zote zinazosumbua uwekezaji na moja katika sababu inayofanya Serikali isilete *blueprint* ndani ya Bunge hili wanaona kwamba *TBS* watawazuia mapato yao, wanaona *NEMC* tukitoa hii tutawapunguzia mapato yao, wanaona sijui mamlaka gani tutawapunguzia. Mamlaka iliyochini ya sheria ya kukusanya kodi ni *TRA* peke yake na siyo hizi zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBS* kazi yake ni kufanya mazingira mazuri mwekezaji aendelee kuwekeza vizuri na aone nchi hii ni bora, *NEMC* ni mamlaka ya kumsaidia mwekezaji aone kwamba nchi hii ni nzuri, lakini hawa nao wamekuwa na *regulate* badala ya kurahisisha uwekezaji wao ndiyo wamekuwa wa kwanza kufanya uwekeaji uwe mgumu ndani ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri utakapokuja kuhitimisha hapa nataka hili la *blueprint* utueleze vizuri tu utalileta lini ili tulifanyie kazi nchi yetu itoke kuwa wa 141 ipande sasa tuwazidi hata Rwanda tuwe katika *top* 20 na wanajua wawekezaji nje ya nchi kule wanatazama Tanzania iko *rank* ya ngapi, shida ni nini, wanatizama, ni kama vile ndege iko juu ya anga, anatizama sehemu bora ya kwenda kuwekeza ni wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji kuna ushindani mkubwa leo, Zambia wanataka wawekezaji, Ghana wanataka wawekezaji, Ghana ni nchi ya 116, Kenya wanataka wawekezaji, Tanzania tunataka wawekezaji, Rwanda wanataka wawekezaji, Uganda wanataka wawekezaji, wote wanavuta kila mmoja anatengeneza mazingira mazuri ya mwekezaji kwenda kuwekeza pale. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hilo namba moja nataka tu utueleze kuhusu *blueprint* haya yote haya kama hutorekebisha *print* mipango yote Mheshimiwa Waziri sidhani kama utafanikisha kwasababu vitakwaza na hii *blueprint* ambayo sisi tumeishauri vizuri Serikali kwenda kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya kimkakati kanda ya ziwa tuna pamba inayoajiri watu milioni 21; ukija

hapa Dodoma inajulikana kwa zabibu, ukienda Singida na Dodoma pia inajulikana kwa mafuta pamoja na Kigoma. Sasa tusipokuwa na mikakati kama Mheshimiwa Nyongo alivyosema, tusipokuwa na mikakati ya makusudi kabisa kwani shida iko wapi Serikali ikiingilia chini ya Shirika letu na *NDC* wakatoa bilioni 50; tukafanya *business plan* tukaona tukiwekeza kiwanda kikubwa ndani ya Mkoa wa Shinyanga, ndani ya Mkoa wa Mwanza ambayo itakwenda kununua pamba yote ya wakulima hapa tukawekeza zaidi ya bilioni 100, 150 baada ya hapo mkatangaza kuuza kama mpango walivyokuwa wakifanya *National Housing* walikuwa wakichora michoro, wanaweka pale, wanatangaza, wenye fedha walikuwa wakileta fedha zao wanajengewa wanapewa nyumba. Kwa hiyo *NDC* wanaweza Mheshimiwa Waziri unaweza ukachukua mpango huu wa Serikali kujenga viwanda vikubwa vitano vya kimkakati ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na baada ya hapo unaiuza tu kwa mwekezaji yeyote kwamba sisi tumejenga hii, faida yake hivi, tumemaliza lete bilioni 150 unauza *NDC* inaendelea kujenga kiwanda kingine Kigoma cha mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo tunakwenda kuwasaidia wakulima ambao wanapata matatizo ya masoko ya kilimo chao kwa mfano Kigoma hawana masoko mazuri ya mawese, ukija Shinyanga hatuna masoko mazuri ya pamba; na ni kweli kabisa pamba ni zao la kisiasa ndani ya mikoa tunayolima sisi pamba. *(Makofi)*

Mimi katika Jimbo la Solwa mpaka wakulima bahati nzuri mimi katika Jimbo la Solwa wakulima wengi wanalima dengu wamechukua zao mbadala la biashara katika Jimbo la Solwa wameona hii pamba hii ni shida wameachana nayo, tumewaachia Mkoa wa Simiyu wao wameendelea na pamba sisi tumeendelea, lakini kwa sababu kubwa hatuna masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija Urafiki kiwanda cha Urafiki ilikuwa ni *joint venture* baina ya Serikali na Serikali ya China leo mashine pale zote zimeuzwa. Mimi nilikuwa kwenye kamati ya viwanda na biashara tumeenda pale wamesema

wameuza kama *scrapper,* mimi sidhani kama imeuzwa *scrapper;* zile mashine ziliuzwa kabisa kwa makusudi kukibomoa kile kiwanda na sasa hivi wanataka kufanya *complex* ya soko la bidhaa zilizozalishwa China kuja kuuzwa *finished product* ndani ya nchi yetu ni hatari na siyo nzuri kwa maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushauri Mheshimiwa Waziri umshauri Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu fanya mazungumzo na Serikali ya Kenya; Wachina hawa ambao wako *Joint Venture* katika kiwanda hiki cha Urafiki waondoke watuachie sisi ili tuone namna bora ya kiwanda hiki tuwekeze kwa namna gani, tuendeleze hiki kiwanda cha pamba, tuendeleze kama kwenye mikakati yako uliyojiwekea hapa, kwamba tuwe na kiwanda ambacho kinaweza kikaunganisha magari au vifaa vya kilimo kupitia JKT na kadhalika. Hayo yatakuja baada ya kwamba China imekubali kutuachia sisi kumiliki Kiwanda cha Urafiki kwa asilimia 100; lakini ukienda pale roho inakuuma sana na mimi siamini kama zile mashine ziliuzwa kama *scrapper.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiunda *task force* utakuta zile mashine ziliuzwa tu nchi fulani hivi wameamua kukivuruga vuruga Kiwanda cha Urafiki kwa maslahi kwamba tutengeneze ajira China sasa badala ya sisi nchi ambayo tunajikongoja kwenye uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TIC* wanafanya vizuri, lakini hawana maamuzi palepale yaani wanakwenda wanakupokea vizuri mno, wanafanyakazi nzuri mno, lakini unapopeleka maombi yako ya usajili wa *certificate* au kupata *approved* au msamaha wa bidhaa kwa ajili ya uwekezaji wa kiwanda mpaka tena iende tena Makao Makuu, ikubaliwe, wakae kikao kiendelee, siku zinaenda tu uone tu namna bora kwamba *TIC* iwe mamlaka kamili. Sasa hivi imepelekwa chini ya Waziri Mkuu, iwe mamlaka kamili kabisa pale unapo-*log document* zako, wawe na mamlaka ya kisheria ya kufanya maamuzi hapo hapo bila kuchelewa ili tuondoke kwenye hii *rank* ya 141 tuende sasa kwenye *top 20* katika uwekezaji duniani. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umemalizika tunaendelea na...

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naunga hoja mkono ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, baadaye atafuatia *Engineer* Ezra na Mheshimiwa Neema Mgaya ajiandae.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, hotuba muhimu sana kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mimi nitaendeleza tu kwa yale ambayo umezungumza kwa sababu mimi ni mkulima na mfugaji, nitazungumzia sana kuhusiana na pamba. Pamba inazalishwa katika Mikoa 17 na pamba inazalishwa katika Wilaya 56; kwa wale ambao hatuna biashara zingine kwenye Wilaya zetu tunategemea mapato kutokana na hilo zao la pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Simiyu inazalisha 60% ya pamba kwenye nchi hii na ndiyo maana Serikali Awamu ya Tano ilipokuja ikaona suala la pamba ikaja na mkakati wa kutengeneza kiwanda cha vifaa tiba pale Wilayani Bariadi. Sasa mkakati huu umekuwa wa muda mrefu takribani tangu mwaka 2016 leo ni miaka minne, Serikali tunakwama wapi? Lakini ukiangalia kwenye hoja za *CAG* katika mradi huo imetumika shilingi milioni 900 kwa ajili ya kumaliza upembuzi na vitu vyote kwenye mradi huo wa Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningeomba tu Serikali kwenye mipango mikubwa hasa kwenye mikakati ya kimkakati kwenye zao la pamba hususan kwenye mkoa wetu wa Simiyu na mikoa mingine 17 ambayo nimeitaja. Mradi huu

utakapokamilika utasaidia sana kwa wakulima wa pamba katika mikoa hiyo na wilaya hizo zinazozalisha na hii itaongeza tija kwenye uzalishaji wa pamba na itaongeza tija kwa wakulima wetu, lakini itaongeza ajira kwa vijana ambao wanamaliza shule, lakini na sisi vijana ambao tunaendelea na biashara zetu tutaendelea kuziendeleza vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Waziri ningekuomba sana suala hili liwe kipaumbele kuhakikisha kwamba taasisi yako ya viwanda na biashara kusudi ambalo linalotarajiwa lifanyike na wananchi tuone kwamba kweli haya yanayozungumzwa na Serikali yanafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyo viwanda vya ushirika, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ilisema tuwe na ushirika, ni jambo jema kuhakikisha tunamkomboa mkulima wetu ambao wanaushirika hawa wakiwa jumuiya ya pamoja wataungana na kukisemea kile ambacho wamekizalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini changamoto inayokuwepo sasa badala ya kwamba ushirika hawa waendelee kujiimarisha hatua inayofuata ushirika anakuwa sasa dalali wa kwenda kuwatumikia wenye viwanda *private* ambapo mimi naamini kabisa wangeanza na hatua ya kwanza tuko na viwanda. Hayati Mwalimu Nyerere alitengeneza nchi hii kimkakati, kila mkoa kulikuwa na kiwanda cha nyuzi, kulikuwa na viwanda vya pamba mfano ukiangalia kwenye mkoa wetu wa Simiyu tuna viwanda takribani viwanda sita vya ushirika lakini hakuna mkakati hata mmoja ambao Serikali inauleta sasa tunaenda kuzalisha kuweza kusimamia kiwanda kimoja cha ushirika tukiboreshe ili kusudi sasa uzalishaji wa pamba washindane na hawa washirika na *private sector.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachofuatia Serikali ni kuja na mawazo, wewe *private sector* fedha zako utapeleka pale kwenye ushirika watakununulia pamba, sasa unajaribu kujiuliza kwa njia ya harakahara.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Njalu naomba ukae. Kuhusu Utaratibu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni ya 68 naomba nisome.

**MWENYEKITI:** Isome.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa majadiliano Bungeni au kwenye Kamati yoyote ya Bunge, Mbunge hataruhusiwa kuzungumzia jambo lolote ambalo yeye mwenyewe ana maslahi binafsi nayo ya kifedha, isipokuwa baada ya kusema jinsi anavyohusika nalo na kutaja kiwango cha maslahi hayo na kwa sababu hiyo itakuwa ni lazima kwa Mbunge yeyote anayetaka kuzungumzia jambo hilo Bungeni au kwenye Kamati yoyote ya Bunge kusema kwanza jinsi anavyohusika na jambo hilo na kutaja kiwango cha maslahi ya kifedha aliyonayo kuhusiana na jambo hilo kabla ya kuanza kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hili, kwa sababu imekuwa ni udamaduni hapa Bungeni lakini imenibidi niseme tena sasa kwa sababu anayezungumza ni rafiki yangu, mosi; yeye ni mkulima wa pamba, pili yeye ni mfanyabiashara wa pamba, ananunua pamba kutoka kwa wakulima na tatu yeye ana *ginneries* za pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu kanuni zetu zinatupa huo utaratibu nilikuwa nashauri tu umpe mwongozo ili kutuwezesha tusiende hatua za mbele zaidi za kikanuni ambazo nadhani ni kali zaidi. Ili vilevile na Wabunge wengine siku nyingine wakiwa wanachangia masuala ambayo wana maslahi nayo binafsi kuanza wa-*declare* baada ya ku-*declare* sasa waendelee na mambo mengine,

tunafundishana tu ili mwenendo mzuri wa Bunge uweze kwenda nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa Mheshimiwa Halima ametoa Kuhusu Utaratibu kwa Mheshimiwa Njalu, lakini nafikiri Mheshimiwa Njalu anaelewa vizuri utaratibu huo na angekuwa na maslahi ya kifedha ambayo yanatakiwa kikanuni angeweza ku-*declareinterest* kwa vile hakusema na haku-*declare* ina maana hana maslahi ya kifedha. Tunaomba tuendelee. *(Makofi)*

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru japokuwa alitaka kunichokoza, unajua ndugu yetu naye ana changamoto zake, nimemsamehe. *(Makofi/ Kicheko)*

Mimi nazungumza kadri ya maslahi ya nchi yetu na ningekuwa nimetaja maslahi yangu binafsi nisingeeleza haya yote kwa sababu lazima ufahamu unapokuwa kwenye biashara ni kuzungumzia masuala yako binafsi, lakini nimezungumza mjadala wa umma, nimezungumza Mikoa 17, Wilaya 56, nimezungumza habari ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni sehemu ambayo nafaidika nisingeelezea hayo, kwa hiyo ni suala la kujifunza na kuendelea naye kuelewa kwamba tunajifunza kitu gani, lakini na mimi nimeshakuwa *senior* humu ni mwaka wa saba niko Bungeni humu sasa, kwa hiyo, suala ambalo lazima ujuwe una *form one* hapa wala siyo njuka. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi zetu za Serikali mfano; *TIRDO* tulitembelea sisi kama kamati tumeona ufanisi wake, lakini bado uwezo hawajajengewa kifedha. Mimi ninaamini kabisa yote tunayoyazungumza haya *TIRDO* tukiijengea uwezo wanauwezo mkubwa sana wa kutengeneza viwanda vidogo vidogo ambavyo vinazalisha alizeti, mpunga na kadhalika. Kwa hiyo, haya yote tukiyachukuwa tunaweza tukapiga hatua na nchi yetu ikaongeza ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niendelee kusema kwamba suala hili ni muhimu sana kwa nchi, lakini vilevile suala hili ni muhimu kwenye kodi kwa sababu unapotengeneza wafanyabiashara ndiyo unazalisha kodi unazalisha walipa kodi wengi nchini hasa sehemu sekta ya viwanda na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningekuomba sana Mheshimiwa Waziri, nadhani Mheshimiwa Waziri ulitembelea kule Katavi uliona kwamba watu wanavyowekeza kwenye viwanda kwenye mikoa hii mipya, kwa hiyo, ni imani ya kwamba shughuli zikienda sambamba itatusaidia sana na wewe Mheshimiwa Waziri na Serikali sehemu kubwa ninyi ni kuhakikisha wafanyabiashara mnawawezesha kwa miundombinu, mnawezesha kila jambo ili kusudi nchi yetu iendelee kufanya mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge lililopita nilishawahi kusema kwamba Waziri wa Viwanda na Biashara, Katibu Mkuu wa Viwanda na Biashara hawa ni sehemu kubwa sana ya kuiwezesha Serikali kukusanya mapato yake makubwa sana bila hata bugudha yoyote ile, lakini kulingana tu na sera sijui mipango au kwa sababu ni kutimiza wajibu, kila mtu akiamka anaamka na analolifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko changamoto nyingine moja kwenye suala la nchi zetu hizi wanazofanya biashara kwa kuingiliana mfano Zambia na Tanzania kuna sheria imepitishwa Zambia asilimia 50 wanataka wao mzigo wabebe Wazambia kupita malori yao, lakini asilimia 20 ibebwe na Watanzania, asilimia 30 iende kwenye *train*. Sasa jambo hili siyo afya sana. Sasa kwenye mjadala huo hatujui umeanzaje mpaka Waziri wa Zambia akafika mahala hakatoa huo waraka wake kwenye nchi zetu za Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeshauri na lenyewe Mheshimiwa Waziri ulichukuwe mjaribu kulifanyia kazi ili kusudi biashara hizi zifanyike vizuri zaidi na watu waendelee kupata mapato kwenye nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Njalu, tunaendelea na Mheshimiwa *Engineer* Ezra, Mheshimiwa Neema Mgaya na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri wetu wa Viwanda na Biashara, Naibu Waziri na watendaji wote maana kazi kubwa wameifanya na hotuba nzuri imesomwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nadhani nina dakika saba tu na vitu ni vingi nadhani niweze kwenda haraka haraka. Jambo langu la kwanza ambalo ninalo tuna hii *issue* ya *Special Economic Zone*, nilikuwa najaribu kupita nimeona tulijiandaa ni karibu kila mkoa uweze kutengeneza kongani kwa ajili ya viwanda, lakini sasa nikawa nawaza jambo moja, nimejaribu kuangalia katika *research* zangu nikawa naona viwanda vingi sana ambavyo vimejengwa katika wakati uliopita vimejengwa Mikoa ya Pwani na Mikoa ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikawaza nikasema kwanini viwanda vingi sana vimejengwa Pwani na Dar es Salaam wakati sikusema labda malighafi nyingi sana ziko pale, lakini kitu ambacho nimekiona viwanda vingi vilivyojengwa ni viwanda vya *process*, unakuta mtu analeta *raw material* kutoka nje ya nchi ana i-*process* akimaliza ku-*process* inakuwa *product* ambayo tunaitaka anaweza kuiuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikawa nawaza sisi wa Mkoa wa Kagera, kilometa 1,400 kutoka bandari ya Dar es Salaam, watu wa Mara Kigoma kilometa 1500, tutakapo jenga viwanda ambapo tunaleta malighafi kutoka nje ya nchi tukaenda kujenga vile viwanda kwetu Kigoma, kwetu

Kagera, sidhani kama tutaweza kuwa *competitve*tuweze kushindana na watu ambao wanajenga vile viwanda maeneo ya Pwani. Kwa sababu hakuna mfanyabiashara ambaye hatakuwa tayari kuja ku-*invest* Kagera na Kigoma *at is the same incentive*ambayo na mtu wa Dar es Salaam anapata na mtu wa Pwani anapata yeye aongeze kilometa zile aende kule aweke kiwanda, halafu kesho wakati wa kuuza mtu yule akashindane na mtu aliopo Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeshaongeza *cost of transportation container* moja mpaka ulifikishe Kagera la *forty feets* ni milioni sita, ufikishe Kigoma ni milioni sita, kuja na kurudi kama ile *product* utakayouza Dar es Salaam ni milioni sita unaongea *forty feets* imeshaongeza milioni 12, wakati aliopo Dar es Salaam ka-*clear* kwa 350,000, mzigo unaingia sokoni. Sasa nilichokuwa naomba kwa Wizara ya Viwanda tujaribu kuweka mkakati maalumu wa kuona na sisi maeneo yetu ya huku tuweze kuweka uwekezaji yaani tuweze kuweka vivutio kwa ajili ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama na sisi tunasema watu wakawekeze Kagera, wakawekeze Kigoma, wakawekeze mikoa mingine ya pembeni huku tuwe na *incentive* ambayo Serikali inatoa, waone kuna unafuu fulani kwao ili hata kama tukiwaambia wakaweke viwanda kule waweze kuja kuweka viwanda *unless otherwise* sasa viwanda hivi vitaendelea kubaki Dar es Salaam na Pwani tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu kimoja cha muhimu ambacho ninacho, mimi nina *declear* kwamba niko kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara tulitembelea Ubungo pale *EPZA,* kuna watu pale wanazalisha *jeans* wanapeleka Marekani, lakini kitu ambacho niliona wakati wa ziara wanatoa *material* kutoka Pakistan wanaleta *garments* kabisa ambayo iko tayari kwa ajili ya kushona kinachofanyika pale ni kama fundi cherehani wanashona tu zile nguo, alafu wana *export* kwamba zimetoka hapa alafu wanapeleka Marekani, maana analeta *under Special*

*Economic Zone* halipi kodi anamaliza pale tena ana *export* halipi kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilichokuwa naomba ni kitu kimoja, amemaliza kuongea Mheshimiwa Nyongo hapa, mimi natoka Kanda ya ziwa katika Jimbo langu la Biharamulo tunalima pamba pia, wakulima wa pamba wako wengi sana hapa ni aibu kuona pamba inatolewa hapa, tuna *export* pamba inaenda nje ya nchi, wale jamaa wanaenda wana *process* wanatangeneza *garments* za kutengenezea *jeans* Pakistan halafu the *same* pamba ambayo tulipeleka sisi inatoka Pakistan inakuja Ubungo inashona, inamaliza kushona inapeleka Marekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa nasema ni nini, viwanda hivi vya kimkakati ambavyo tunavyovipanga, tupange viwanda vya kimkakati ambavyo vitatumia *raw materials* ambazo ziko kwenye sehemu zetu. Sidhani kama kile kitu kinachofanyika Pakistan kinashindwa kufanyika hapa, maana tuna viwanda vingi ambavyo vina *process* vitu hapa na tumeonesha kwamba tunaweza kufanya vitu ambavyo vinafanyika nje vikaweza kufanyikia hapa. Nilichokuwa naomba kwa upande wa Wizara ya Viwanda sasa, maana ninyi ndiyo *custodian* wa suala la biashara na vitu vingine hapa, muende mkatusaidie mkae na *TIC,* mtusaidie, wawekezaji wanapokuja washaurini wawekezaji kwa sababu tayari tuna *client* anayetengeneza *jeans* hapa na ana *export jeans* nyingi sana. Sasa kwa sababu tuna *client* anaye *export jeans* hapa na pamba tunayo tutafute wawekezaji wa kwenda kuweka viwanda Kanda ya Ziwa tunapolima pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakishaweka viwanda Kanda ya ziwa tutowe pamba sisi kwanza tukishatengeneza vile tutapata mashudu kwenye pamba, tutapata mafuta haya tunayo *import* kutoka nje, kutakuwa na *advantage* nyingi. Yule mtu akishamaliza kutengeneza *garment* tutoe pale tulete Ubungo pale tukamuuzie. Najua ipo shida maana katika maongezi na mtu mmoja aliniambia hatuna *capacity* hiyo, hakuna mtu ambaye yuko tayari kulima pamba hapa

kwa shilingi 1,000; akakope pesa benki alafu pesa ifie kule wauze *assets* zake. Lakini kama soko liko pale Ubungo tuna hakika kwamba watu watalima pamba na kinachotakiwa anayekuja kuwekeza kwenye kile kiwanda hakishakuwa na shamba lake yeye mwenyewe la kulima pamba ni kwamba hata kile kiwanda chake hakitakufa, maana tumekuwa na shida moja sana Watanzania, unakuta mimi nimwekeza kwenye kiwanda, unapowekeza kwenye kiwanda hata kwa wenzetu wanachokifanya huwezi kutengeneza *excavator* tunaona *caterpillar* yale barabarani, kuna anaye muuzia *engine,* kuna anayemuuzia vitu vingine, kuna anayemuuzia *ticks*, inakuwa *combination* kiasi kwamba kabla ya kiwanda chako wewe kufa unayetengeneza *caterpillar* kuna *stakeholders* wengi sana huku nyuma yako wana *feel* uchungu kabla ya wewe kuweza kuathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa shida yetu sisi utakuja kukuta kiwanda unacho wewe tu, *raw material* unatoa nje kwa hiyo hata kesho kiwanda kinakufa hakuna mtu anayeumia hapa, lakini tukiweza kutengeneza viwanda ambavyo ni *feeders* wa viwanda vingine ambavyo vipo hapa nina hakika hata vile viwanda vikubwa havitaweza kufa kwa sababu tayari kuna mtu ananufaika navyo pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu kingine ambacho ninacho kwenda kwa Serikali, kuna jambo moja ambalo nimekuwa najiuliza sana, mimi nimekuwa nafanya kazi ya *sales* naweza ni-*declare interest*, kitu kimoja ambacho watu tumehusika na maunzo sehemu nyingi tulipo, lazima usimame katikati, unasimama katikati kwa *client* na unasimama katikati kwa kampuni, unaangalia maslahi *both sides*. Sasa sehemu kubwa sana ya viwanda wafanyabiashara wamekuwa wanaachwa kama yatima, ninachoomba kwa Serikali hasa kupitia Wizara ya Viwanda wa Biashara tunapolia humu tukawa tunasema viwanda, viwanda, kazi yenu nyie kubwa ni mambo ya viwanda na wafanyabiashara. Simameni na wafanyabiashara maana mfanyabiashara anapokufa hebu *feel* kwamba kuna kitu mimi nimepoteza kwenye sehemu yangu ya kazi maana hawa watu wanakuwa wanalia kodi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka kipindi cha nyuma niliwahi kuelezea hapa tulivyoenda pale Ubungo mtu mmoja amefunga kiwanda anapeleka Uganda, wakati tunaongea pale tunaambiwa *TRA.* Sasa nikawa najiuliza hivi *TRA* ni nani? Maana mimi nakumbuka wakati nafanya kazi nilikuwa nagombana sana na wahasibu unaleta mteja pale mhasibu akija naye anakubalikia wakati unatafuta mteja mhasibu hayupo, lakini siku unamfikisha pale anasisimama anataka hiki anataka hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mimi nikuombe Mheshimiwa Waziri hii kazi ya kutafuta wateja ni yako tunachotaka utuhakikishie kwamba unapoangaika kutafuta wateja huyu *TRA* wanajua unatumia nguvu kuwatafuta, sasa msimalize kuwapata watu wanajenga viwanda hapa, kesho mtu mwingine anaweka kikwazo hivi viwanda vinafungwa itakuwa ni aibu kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina hakika *direction* yetu ni nzuri, tumemsikiliza Rais hapa alivyosema, kwa hiyo, nina hakika tukiji-*tune* katika kuhakikisha tunajenga mazingira mazuri ya kuwasikiliza wafanyabiashara, haiwezekani mtu akaweka bilioni 250 hapa halafu wewe huwezi kwenda kukaa naye mezani ukamuuliza ana matatizo gani? Akaweka bilioni 300 hapa huwezi kwenda kukaa naye mezani ukajua anamatatizo gani? Hizo atazipeleka Uganda, atazipeleka Kenya, atazipeleka Zambia na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani baada ya hayo kwa sababu ya muda nilitaka niongee *issue* ya Liganga na Mchuchuma lakini wenzangu wameshaongea ni sehemu ambayo itatusaidia sana sana, maana kama unaagiza mzigo China, ukiomba *quotation* ya *product* yoyote ya chuma China hawawezi kukupa *quotation* ya *thirty days* kwenda nje, sana sana ya siku kumi/siku saba kwa sababu bei ya chuma inabadilika kila wakati. Sasa suala la Linganga na Mchuchuma tulichukulie *serious* ni sehemu itakayotunyanyua sisi hapa maana *product* za chuma hata tunavyoziagiza huko nje ni *very expensive* na bei zinapanda kila siku. Nyote ni mashahidi kama kuna mtu anafanya biashara hapa

tumesikia China juzi wameongeza *13 percent* kwenye *export* zote. Kwa hiyo, kama hata kuna mzigo ulikuwa umeagiza China leo umeongezeka kwa asilimia 13 kwa sababu bei ya chuma ilivyo *fractuate. (Makofi)*

Kwa hiyo, niombe suala la Liganga na Mchuchuma Serikali ilichukulie *serious* ili sasa liweze kututoa hapa, tuunze chuma hapa kwa majirani zetu kama sisi tutashindwa kutumia hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo naomba niunge mkono hoja, ahsante sana.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana *Engineer* Ezra. Tunaendelea na Mheshimiwa Neema Mgaya, Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma na Mheshimiwa Felista Njau pamoja na Mheshimiwa Tabasam Hamis, ajiandae.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake nzima ya Wizara hii ya Viwanda na Biashara kwa kazi nzuri wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitazungumzia maeneo matatu, nitazungumzia katika Mamlaka ya Viwango *(TBS)*, lakini vilevile, nitanzungumzia Liganga na Mchuchuma na nitamaliza kwa kuzungumzia malighafi ya parachichi katika kuchochea uwazishwaji wa viwanda vya kuchakata zao hili muhimu la parachichi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Viwango *(TBS)* ninavyojua mimi kazi yake ni kuangalia afya za wananchi wa Tanzania kuwa salama kutokana na bidhaa zinazoingizwa ndani ya nchi. Hivi karibuni kumekuwa na mabadiliko ya bidhaa zinazoingia ndani ya nchi kama magari yale ambayo *used* yanayoingia ndani ya nchi yakabadilishiwa mfumo wa ukaguzi kutoka kwenye ile *system* ya zamani ya *pre-arrival inspection* kuja kwenye *destination inspection.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani *TBS* waliingia mikataba na makampuni ya Japan pamoja na Dubai katika ukaguzi wa magari haya na kazi ilikuwa inafanyika vizuri sana, lakini vilevile *TBS* haikuingia gharama yoyote katika ukaguzi huu wa magari zaidi ya kupokea *percent* ambayo waliokuwa wanapewa na makampuni yale na katika ukaguzi wa magari haya magari yalikuwa yanakaguliwa katika dola 150 mpaka 300 kwa gari moja inategemea na ukubwa wa gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile ndani ya miaka 10 *TBS* iliweza kupata *USD* milioni 10 kama *percent* waliokuwa wanapewa na yale makampuni. Mimi najiuliza kwa kuwa kazi ya *TBS* ni kuangalia na kulinda afya za Watanzania kutokana na hizi bidhaa zinaingia ndani ya nchi. Leo imeamua kubadilisha mfumo wa ukaguzi wa magari haya yawe yanakaguliwa hapa nchini, mashaka ambayo niliyonayo, kazi ile ni ngumu na ni nzito. Lakini vievile inatakiwa tujiandae vizuri kuhakikisha kwamba tunaweza kuthibiti uingizwaji wa magari mabovu ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Nina wasiwasi na miundombinu ambayo inatumika kukagua magari haya, mfano kule Japan katika kampuni hizo tano walikuwa na uwezo wa kukagua magari 2,000 ndani ya mwezi mmoja, lakini nimefuatilia hapa Tanzania gari moja inakaguliwa ndani ya masaa mawili na kuna meli ambazo zinabeba magari zaidi ya 2,000, mashaka yangu hakutakuwa na mrundikano wa magari pale bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile unapoileta gari hapa, mteja ameshanunua gari ameshaileta hapa Tanzania, inakaguliwa na *TBS* itakaposema hii gari ni mbovu hii gari itakwenda wapi? nina wasiwasi nchi yetu isijekwenda kuwa *dumping country*. Lakini vilevile huyu Mtanzania ambaye amejikwamua mwenyewe ameona gari mtandano kuna hawa watu wanaitwa Wapalestina wanauza magari mpaka dola 500 mpaka dola 1,000 bila kujali iko kwenye ubora gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtantanzia wa watu amejikwamua amenunua gari ameileta imefika bandarini

hapa anaambiwa aikarabati ili iweze kukidhi viwango zaidi ya ile pesa aliyoinunulia, hatuoni kwamba tunakwenda kuwanyanyasa wananchi wetu wanyonge ambao yeye amependa kujikwamua aweze kuwa na usafiri wake wa kumpeleka kazini na kwenye shughuli zake. Leo anaambiwa kwamba hii gari haina ubora unabidi ugharamie kuikarabati na ataingia gharama kubwa. Wakati zamani zile kampuni zinazouza magari kwa mfano kama hawa wanaojiita *Beforward* ukinunua gari kwa *Beforward* yeye kule anaponunua kwenye mnada anaiangalia kabla hajaileta Tanzania ataipeleka kwenye zile kampuni za kuangalia ubora wa gari; akiipelekea kwenye ile kampuni akiona kama kuna changamoto zozote za kurekebisha ile gari *Beforward* ilikuwa inafanya yenyewe kwa niaba ya mnunuzi aliyenunua.

Sasa leo kubadilisha mfumo ule ina maana sasa tunamuongezea gharama mnunuzi ambaye ni mwananchi mnyonge Mtanzania. Mimi nilikuwa naomba suala hili mliangalie kwa umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile Serikali imekwenda kuwekeza bilioni 20 kwa ajili ya kutengeneza miundombinu hii ya ukaguzi wa magari, wakati bilioni 20 hii si mngetuletea sisi Njombe, Mbeya kule, Rukwa maeneo tunayolima parachichi tukaweza kufungua viwanda vya kuchakata zao la parachichi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Liganga na Mchuchuma; naiomba sana Serikali sana iongeze kasi ya majadiliano yanayoendelea ili mradi huu uanze mara moja. Sisi wananchi wa Mkoa wa Njombe na wananchi wa Nyanda za Juu Kusini na Kusini kwa ujumla pamoja na Watanzania wote mradi huu utakwenda kuwa ni kichocheo kikubwa sana kwa uchumi wa mtu mmoja mmoja lakini vilevile Tanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumekuwa tukizungumza miaka mingi sana ndani ya Mbunge tangu mwaka 2010 tunazungumzia Liganga na Mchuchuma. Nilifikiri kipindi kile tumeanza kutengeneza *standard gauge* mradi

huu ungekuwa tayari umeshaanza kufanya kazi ili *raw materials* za chuma ziweze kutumika katika vile vifaa ambavyo vinatengeneza reli, lakini vilevile tuna miradi mingi inayoendelea madaraja hii malighafi ya chuma ingeweza kutumika katika kutengeneza *standard gauge* pamoja na reli zingine ambazo zinaendelea na ambazo zinatakiwa kutengenezwa na madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukizungumizia makaa ya mawe juzi hapa nilimuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri wana mkakati gani kuhakikisha kwamba *NDC* kuachia baadhi ya vitalu ili wananchi waweze kuchimba makaa hayo kwa sababu kuna uhitaji mkubwa sana wa makaa haya ya mawe. Na Serikali ilikubali kwamba wananchi sasa waanze mchakato wa kuomba ili waweze kupewa vitalu hivyo. Sikupata nafasi ya kushukuru, nashukuru kwa majibu hayo na wananchi wa Ludewa pamoja na Njombe na wadau wengine wa maeneo mbalimbali ambao wanajishughulisha na biashara hizi za wachimbaji wadogo wadogo wapo tayari na wataanza kuleta maombi hayo ili muweze kuyafanyia utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitojisikia vizuri kama nitamaliza kuchangia bila kugusa malighafi ya zao la parachichi. Kama tunavyojua malighafi ya parachichi inalimwa mikoa mingi takribani mikoa 12, jirani yangu hapa anatoka Jimbo la Hai naye ameniambia Hai wanalima sana zao la parachichi. Hebu hii Wizara sasa iangalie ni namna gani inakwenda kuwakomboa vijana katika suala zima la ajira katika kuhakikisha kwamba wanaleta wawekezaji wengi ndani ya nchi ili waweze kuanzisha viwanda hivi vya kuchakata parachichi kama ni takribani mikoa 12 ina maana tuna uwezo wa kuanzisha viwanda vingi sana vya kuchakata zao hili la parachichi na hii itakwenda mkombozi kwa Taifa letu kwa sababu vijana wetu watakwenda kupata ajira, lakini vilevile tutawasaidia wakulima hawa wa zao la parachichi kuweza kuboresha malighafi hii iwe na thamani zaidi baada ya ku-*export* parachichi kama parachichi, sasa tuanza ku-*export* mchuzi wa parachichi, lakini vilevile majani, mbegu

zile zote zifanye kazi na wananchi wetu waweze kupata mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda nakuomba sana ukae na Waziri wa Kilimo muone namna bora ya kuweza kulipeleka mbele zao hili la parachichi. Ulimwenguni wanajua zao hili la parachichi inaitwa *green gold,* kwa hiyo, ni wakati sasa kuhakikisha kwamba mnaweka kipaumbele na mnaweka mkakati mahususi na mnaweka jitihada kubwa katika kuhakikisha kwamba mnapeleka zao hili mbele hili kuweza kumkwamua mkulima mmoja mmoja na vilevile kuweza kuchochea uchumi na kuongeza mapato ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ndio njia za kuweza kuongeza mapato,...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** ...siyo kwenda kuongeza mapato kwa *TBS. TBS* haina kazi ya kuongeza mapato, kazi yake ni kuangalia afya ya Mtanzania, kuzuia bidhaa ambazo zitakwenda kuathiri afya ya Mtanzania sio kazi ya *TBS* kuongeza mapato. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Neema nakushukuru sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mie niweze kuchangia, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kukuteuwa Profesa Mkumbo kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara, mimi binafsi naamini kwamba umefanya vizuri sana kwenye Wizara ya Maji, wakati ukiwa mtendaji. Imani yetu sisi wafanyabiashara kwenye kipindi chako hiki kwenye hii Wizara ya Viwanda na Biashara na kwa kuwa ni bajeti yako

ya kwanza hatutakupiga mishale mikubwa sana, utegemee mwakani ndio utakutana nayo kama hutabadilisha haya mambo huko Wizara ya Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ningependa kumshauri Mheshimiwa Waziri afanyie kazi kwamba Serikali iongee lugha moja, shida ambayo uwa nazungumza mara nyingi kwamba yaani ukiangalia katika mfumo Wizara ya Viwanda na Biashara ni kama hauna kazi yoyote, kwa sababu watu wengi hawaoni umuhimu wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa sababu kila tatizo utakalokumbana nalo kwenye biashara lina Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukikumbana na mazingira lina Wizara yake, ukikumbana na kodi lina Wizara yake, ukikumbana na Halmashauri lina Wizara yake. Sasa nikuombe, mnapoenda kukutana kwenye *cabinet* lazima ulilie *power* ya Wizara yako. Nakupa mfano Mheshimiwa Waziri, sasa hivi kuna mjumbe mmoja hapa amechangia, mnahamasisha watu wawekeze viwanda, lakini hivi viwanda mngekuwa mnazungumza lugha moja mngekuwa mnavipanga kiwilaya hata kimikoa. Ni kweli kwamba ni nani atakayefuata *juice* Geita akaiuze Dar es Salaam wakati *juice* hiyo hiyo inatengenezwa tena Dar es Salaam?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba mnatoa vitu ambavyo hamjapanga maeneo sahihi kwamba hiki kikae huku na hiki kikae huku. Lakini nikupe mfano tu sasa hivi kuna shida ya mnafungua *refinery;* nakupa biashara moja tu, *refinery* imejengwa Mwanza, imejengwa Geita, imejengwa hapa na ukiangalia kiuhalisia dhahabu nyingi inatoka Geita; kwa nini msingetengeza tu kama *zone* ya dhahabu mtalii yeyote au mnunuzi akija ukitaka dhahabu nenda Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unafungua *refinery* Geita, unafungua *refinery* Mwanza, sijui mtu wa Mwanza atatoa wapi hiyo dhahabu ya kutengeneza! Kwa sababu sisi watu Geita hatutakubali itoke dhahabu Geita ipelekwe Mwanza halafu Manispaa ya Mwanza ikakusanye *levy* yetu ambayo ingetengenezewa huku. Kwa hiyo ni vizuri

mzungumze lugha moja na ukalilie madaraka kabisa kwenye *cabinet* kwamba na wewe ni waziri ambaye unaweza kujitosheleza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Taarifa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma taarifa tusikilize ya Mheshimiwa Almas.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kumpa taarifa mzungumzaji wa sasa hivi kwamba ilitokea hiyo tumbaku inalimwa Tabora, Viwanda vya Tumbaku vyote viko Morogoro. Tatizo kubwa sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea ndio maana nimemwambia Profesa tunakupa mwaka mmoja ukajaribu kurekebisha haya mambo tuwe na *zone,* kila kitu kipatikane mkoa fulani. Na hili la Mheshimiwa Waziri najua Serikali ilikuwa na nia nzuri sana ya kutaifisha viwanda na ninashukuru sana kwa sababu pia Katibu Mkuu wa sasa alikuwa Katibu Mkuu wa Fedha na Mheshimiwa Rais amekurudisha kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara na hili ujisifu, tunahitaji viwanda vifanye kazi, hakuna Wizara inayojisifu kuua viwanda, kuua taaluma unayoisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupa mfano Mheshimiwa Waziri mimi nina maslahi na kiwanda fulani kule Tanga kiwanda cha *furniture,* wakati Serikali inabinafsisha kazi ya mwekezaji ni kutengeneza, kazi ya kulinda masoko ni kazi yenu Serikali msikwepe majukumu. Huwezi ukanipa mimi kiwanda nikiendeshe kinatengeneza *furniture,* mteja mkubwa niliyemlenga ni Serikali, ninyi wenyewe mmetukimbia mnanunua vya Kichina, sasa lazima uzalishaji uwe wa kubambanya, lakini wewe unataka nizalishe kwa asilimia 100 hii kitu haiwezekani ni kazi yenu ninyi Serikali kulinda viwanda vya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mkumbo ninatamani sana kukuomba ukatembelee Kiwanda cha *Play and Panel* pale Tanga kimefungwa kikiwa na malighafi eti kinazalisha asilimia 20. Twende Moshi pale *Kiliwood* imefungwa na *Kiliwood* iliuzwa na Serikali na ninyi wenyewe kwenye mkataba mkasema *material* mtamgawia ninyi kutoka kwenye mashamba yenu. Lakini mashamba yale *material* mnawagawia walanguzi mwenye kiwanda mnampa asilimia moja, sio sawa ni wakati tunaona sasa Serikali inafungua akaunti ilizozifunga hii ni hatua nzuri fungueni na viwanda. Hao mliowanyang'anya viwanda wengine wana uwezo, mliwasababisha kufunga viwanda ni ninyi kutokulinda soko la ndani. Huwezi ukanishindanisha mimi mzawa ambaye ninakopa CRDB mkopo asilimia 14 ukanishindanisha na mtu wa nje ana mkopo asilimia mbili, ni hesabu za *design* gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina kuamini sana Profesa, ninakuomba utembelee hivi viwanda niko tayari hata kesho tufuatane mimi na wewe ukaone uonevu huo uliotokea huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Kiwanda cha Moproco pale Morogoro lazima tuwaambie ukweli, sijui ni hesabu za *design* gani na ndio maana mimi nikisema hapa mnanilaumu kwamba nawalaumu maprofesa, sitakulenga sana profesa kwa sababu wewe ni rafiki yangu. Kiwanda cha Moproco ni kiwanda cha mafuta ya alizeti, alizeti inapatikana miezi mitatu tu, mtu anataka kuzalisha mwaka mzima unatoa wapi hiyo alizeti? Ni jukumu la Serikali kuwahamasisha watu walime alizeti ili mtu azalishe miezi 12. Sasa ninyi mkikuta amefunga kipindi ambacho hakuna *material* mnamnyang'anya kiwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri dhambi hii ya kupora vitu vya watu isikuangukie mikononi mwako, kama Serikali imeanza kufungua akaunti kaa na Katibu wako mfungue hivyo viwanda, wapeni muda kama ni mwaka mmoja, kama ni miezi sita, wakope hela mambo yaendelee tumeshambiwa

kazi iendelee halafu bado umeshikilia viwanda vya kazi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine Mheshimiwa Waziri nikuombe sisi kule kwetu jimboni kwangu tutalima mananasi yanaliwa tu shilingi 200/shilingi 300, ukiingia kwenye *internet* Dubai kule nanasi linauzwa mpaka dola 15; ni kazi yenu Serikali kututafutia masoko. *(Makofi)*

Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri uje uone mananasi tunayoyauza kwa mafungu kama mafenesi, njoo uone ili uone namna wataalam wako wakazunguke huko duniani tupate masoko tuweze kuuza bidhaa zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho Profesa nimesema wewe ni rafiki yangu lakini nikuombe sana mimi sio kwamba nadharau maprofesa, lakini vitendo vya maprofesa wakati mwingine ndio vinatufanya tulaumu hata kama mtatusema namna gani. *(Makofi)*

Naomba nitoe mfano mdogo tu wakati wa Marehemu Hayati Magufuli najua Marais wetu wanatupenda sana Watanzania wote, Mheshimiwa Rais aliunda tume ya kuchunguza *corona,* ikachunguza ile hatoe jibu kwa Watanzania, ikaja *corona* ya mapapai, ya mbuzi, ya maembe, na tukaona mpaka Mabunge ya Ulaya yanamsifu Rais Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa sasa watu mkaanza kuchachamaa mitandaoni Mama yetu Samia naye ameunda tume, tume ya Mama Samia miezi mitatu baadaye tuchomwe sindano mnataka kumaliza sisi ambao sio wanasayansi.

Sasa niwaombe sana wasomi wetu muwe makini, lazima muwe makini hatuwezi na Profesa miezi mitatu kasema *corona* ya mapapai huyohuyo miezi mitatu baadaye *corona* ya kuchoma sindano na ninamuomba mama sana atumie busara maprofesa hawa kama watamchanganya tuko huku kitaa tumsaidie. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi chanjo zinasemwa tunachanjwa tupunguze nguvu za kiume na sisi bado tunataka kuzaa, Serikali inasema tuzae maprofesa mnatuchanganya. Mama achana na hawa ma-*professor* wametufikisha pabaya. Wazungu wenyewe walisifu Tume ya Marehemu Magufuli akasema mapapai na mbuzi. Mbunge lilijadili Bunge la Ulaya tunaona mitandaoni miezi mitatu baadaye tunang'ang'anizwa kuvaa mabarakoa, maprofesa hao hao. Sasa niwaambie na sisi Chama cha Waganga tutakaa na sisi tutoe taarifa yetu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Musukuma. Tunaendelea na Mheshimiwa Felista Njau, baadaye Mheshimiwa Hamis Tabasam na Mheshimiwa Condester Sichalwe na Mheshimiwa Muharami Mkenge wajiandae.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu ambayo kimsingi inagusa jamii kubwa ya Watanzania.

Kwanza kabisa kabla ya kwenda mbele ni lazima tuangalie huku nyuma tulifanya vizuri kiasi gani au vibaya kiasi gani ili tuweze kujisahihisha. Nikisema hivyo ninakwenda moja kwa moja kwenye mpango wa utekelezaji wa bajeti wa miaka ya fedha ya mwaka 2016/2017 ambayo bajeti ya Wizara hii ilikuwa ni asilimia 44; mwaka 2017/2018 ilikuwa ni asilimia 9.51 mwaka 2018/2019 ilikuwa ni asilimia 6.5; ukijumlisha kwa wastani wake miaka hii minne mfululizo unakuja kupata asilimia 20 tu ya bajeti katika sekta muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwendaje mbele katika kauli hii ya nchi ya viwanda huku tukiweka asilimia 20 miaka minne mfululizo. Hatuwezi kwenda kwa sababu mwisho wa siku mipango hii ni lazima itekelezwe, pesa ni lazima ziwepo ili maendeleo yawepo. Kwa tathmini hii ya mpango *target* yetu ni nini? Mpango wa Pili tulikwama wapi leo

tunakwendaje mbele? N lazima tu-*refer* tulikotoka ili tuangalie tulikwama wapi twenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema haya kwa sababu hapo nyuma wakati wa kauli mbiu ya nchi yetu ya viwanda ilivyopamba moto, kuna Waziri alisimama kwenye matamko yake akasema tutakwenda kujenga viwanda 100 kila mkoa; alikuwa ni Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Jafo, akasema tutakwenda kujenga viwanda, hizi kauli hizi zisiwe mapambio zikawaponza Watanzania wakatuona huku tunapiga mapambio tu, haiwezekani. Hizi kauli ziende na vitendo, na alivyosema hivi nilikumbuka Kiwanda cha *Tanganyika Packers* nikasema kiwanda hiki kikifufuliwa wananchi wa Jimbo la Kawe na Dar es Salaam wanakwenda kupata ajira nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikasema kiwanda hiki kimebeba jina la Kawe maana ya Kawe ni njia ya kupita ngo'mbe *(cow way)* ni Kawe nikasema kiwanda hiki kikifufuliwa tutakwenda kupata ajira nyingi kwa sababu viwanda vingi vimekufa. Siweze kurejea haya kwa sababu viongozi na Wabunge wengi wameongea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawezaje kufikia malengo wakati sekta ya kilimo tumeiacha nyuma, hawa ni mapacha ni lazima tuangalie kilimo tunatengaje bajeti yake inatekelezwa vipi hili twende mbele kwa sababu kama hatuna *raw material* hatuwezi kwenda na viwanda. Na ukiangalia kwa miaka mitano mfulululizo sekta ya kilimo wametengewa asilimia 17 tu; tunakwendaje kwa namna hiyo? Hatuwezi kwenda kwa sababu hawa ni mapacha bila *raw materials* viwanda haviwezi kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema hayo najielekeza kwenye nafasi yetu ya kidunia ambayo wengi wameiongelea ya 141 kati ya nchi 190; tunakwenda hivyo tulikuwa tumejiwekea malengo kama Tanzania twende kwenye *double digit position,* hatuwezi kwenda kama malengo yetu hatuwezi kuyatekeleza vizuri wakati tunapanga. Nikisema

hayo ninaangalia mazingra ya biashara na viwanda kwa Tanzania ni rafiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwama kwa sababu mazingira si rafiki, Tanzania kuna utitiri mkubwa wa kodi, ukileta uwekezaji anaaanza kujiuliza wazawa wameshindwa kuwekeza kwa sababu ya utitiri wa kodi. Nikianza kutaja hatutamaliza, ukitaka kufungua kiwanda au kuanzisha biashara ni lazima uende ukasajili *BRELA* kule ni pesa, ni lazima ulipe kodi ya zuio, hiyo ni pesa; ni lazima ulipe kadiri unavyopata hiyo ni pesa; ni lazima ulipe gharama za *OSHA* hiyo ni pesa; ni lazima ulipe kodi ya ujuzi hiyo ni pesa; bado Manispaa wanakusubiri ulipe leseni hiyo ni pesa; gharama za Zimamoto, ada za Mamlaka ya Chakula; hiyo ni pesa na gharama lukuki ambazo ziko hapa. Mlundikano huu wa kodi, mwananchi wa kawaida mwenye mtaji wa kawaida hawezi kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda namna hiyo Mheshimiwa Waziri nikuombe wakati unakuja na mkakati wako, una-*wind up* hapa, utueleze ni mkakati gani ulionao ili kuwezesha Watanzania waweze kuwekeza. Tusiimbe tu nchi ya viwanda kwa mdomo, tukatekeleze kwa vitendo kwa sababu...

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji anayezungumza anasema kwamba Serikali haijajenga viwanda kwa maana kauli ilipamba tu moto, lakini viwanda vingi havijaanzishwa. Nataka nimpe taarifa kwamba kutokana na *Tanzania National Business Portal,* ripoti inayozungumzia kwamba toka Awamu ya Tano ilipoingia madarakani, viwanda 4,877 vimejengwa. Kati ya viwanda hivyo, viwanda 201 ni viwanda vikubwa, viwanda 460 ni

viwanda vidogo, viwanda 3,406 na viwanda 4,401 ni viwanda vidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimpe taarifa kwamba Serikali ya Awamu ya Tano na Awamu ya Sita imefanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba mazingira ya viwanda yanakuepo na viwanda vingi vimeshajengwa nchini. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felista unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sipokei taarifa hiyo kwa sababu sizungumzii viwanda vinavyofichwa chumbani, nazungumzia viwanda vyenye tija kwa wananchi, nazungumzia viwanda ambavyo vilikuwepo na hatujaviona. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felista, viwanda vipi vinafichwa chumbani? Naomba uondoe hilo neno.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema huwezi kuwa na *blender* useme una kiwanda; huwezi kuwa na cherehani moja unaajiri watu wangapi?

**MWENYEKITI:** Basi tumia lugha nyingine, lakini siyo ya chumbani.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *blender* hata ndani si unajua. Kwa hiyo…

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Naomba nimpe Mheshimiwa dada yangu taarifa kwamba hivi tunavyozungumza bajeti iliyoko mezani kwake hapo zimeshatengwa shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya kufufua kiwanda kikubwa sana cha *Kilimanjaro Machine Tools,* kiwanda ambacho kilikufa miaka mingi, sasa kimeshatengewa hela. Kiwanda hiki kinatengeneza viwanda vingine vidogo vidogo, kazi yake ni kuunda vyuma na fedha imeshatengenezwa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba kumpa taarifa kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inaendeleza kujenga viwanda vikubwa vikubwa kama hiki ambavyo havipatikani kwingine duniani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felista.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kaka yangu Mheshimiwa Mafuwe, alikuwa anataka kuchangia kwa sababu hayuko kwenye *list.* Mimi niendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba maneno haya siyasemi mimi; kupitia Ripoti ya *CAG* anasema kwamba kumekuwa na utekelezaji mdogo wa bajeti ya maendeleo kwa viwanda vidogo vidogo katika ngazi zote za Serikali; mfano, kwa miaka minne ya nyuma mfululizo, Wizara ya Viwanda na Biashara imetumia asilimia 16 tu ya fedha za maendeleo zilizopelekwa kwa ajili ya maendeleo ya viwanda vidogo vidogo. Maneno haya si ya kwangu, ni maneno ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali *(CAG). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema hivyo ninasema tujielekeze kwenye ukweli, tunavyopanga hapa tuweke bajeti na ile bajeti iende na ikatekelezwe. Sisemi mapambio ya kuweza kumfurahisha mtu. Watanzania huko nje wanalia, akina mama huko nje wanalia kwa sababu hata akiwa na biashara yake ule utitiri wa kodi kwa miaka mitano iliyopita hii Watanzania wengi biashara zao zimefungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi mtakuwa ni mashahidi, hamuwezi kusema lakini mnajua kwenye

majimbo yenu kilio cha Watanzania ni kikubwa kuliko tunavyofikiri. Twende tukarekebishe kwa sababu kazi ya Bunge ni kuielekeza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kuielekeza Serikali ikaangalie utitiri huu wa kodi, ipunguze ili wananchi wetu wapate nafuu na waweze kuwekeza. Nia yetu ni njema kwa sababu Tanzania yetu ni moja, tunahitaji maendeleo, hatuhitaji malumbano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hapa hatuhitaji ahadi, tunahitaji utekelezaji. Utekelezaji ni jambo la msingi kwa sababu baada ya kutoka hapa tutakuwa na dhambi ya kujibu kwa Mwenyezi Mungu. Wale watu wenye imani kila siku unamwambia mtoto wako utanyonya kesho kama mtoto wa kuku halafu mwisho wa siku Watanzania wanakosa imani na Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende tukatekeleze vile tulivyovipangilia ili tuweze kufikia azma ya Serikali ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo, ninakushukuru sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Felista. Tunaendelea na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao. Mheshimiwa Condester Sichalwe, Mheshimiwa Muharami Mkenge na Mheshimiwa Juma Usonge wajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema. Naomba kuchangia mchango wangu katika bajeti ya Viwanda na Biashara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu nazungumzia suala la viwanda vya kuchakata pamba katika nchi hii. Mikoa inayolima pamba katika nchi hii ni mikoa 17, lakini Wilaya 54 zinalima zao la pamba kwa ukubwa kabisa. Katika Ilani yetu ya uchaguzi tumeainisha kwamba tutatengeneza tani milioni

moja katika nchi hii ndani ya miaka mitano kuanzia mwaka 2021 na kuendelea mpaka mwaka 2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kufikisha tani milioni moja kama hujajiandaa kuwa na viwanda. Ushauri yangu kwa Serikali katika Wizara ya Viwanda na Biashara; Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ni miongoni mwa wasomi wakubwa wenye heshima katika nchi hii, mimi binafsi nakukubali na ninashangaa maono haya Mheshimiwa Rais aliyapataje ya kukufikiria kwamba Profesa Mkumbo anaweza akawa sababu ya kubadilisha maisha ya Watanzania, akakuweka katika hii Wizara. Sasa itendee haki hii Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, Mheshimiwa Profesa Mkumbo, Waziri wa Viwanda na Biashara, andaa andiko, mimi najua wewe ni mwandishi mkubwa katika nchi hii, andaa andiko kwa ajili ya kuweka mashine za kuchakata pamba. Hizi mashine zilizopo katika vyama vyetu vya ushirika vya Nyanza, Shirecu, Musoma, Kagera kule Biharamulo, Tabora na Singida; hivi viwanda haviwezi sasa hivi kuchakata pamba kwa sababu mashine hizi zilikuwa za kizamani. Hizi mashine zimetoka India, kuna mashine zimefungwa kule Nyakalilo mwaka 1959, mashine zimefungwa pale katika *ginnery* ya kwetu Nyamililo, hizi ni mashine zimewekwa pale mwaka 1967.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashine zimekuja kufungwa *Buyagu Ginnery,* hizi ni mashine za mwaka 1972. Lakini kuna mashine mpya ambayo imefungwa pale *Manawa Ginnery* katika Wilaya ya Misungwi, hii ndiyo mashine mpya peke yake katika Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashine zilizoko *Nasa Ginnery,* ukienda *Nyambichi Ginnery* Kwimba; hizi mashine zimechoka. Nenda Bariadi, hizi mashine zilizoko kule zimechoka; nenda Maswa, kiwanda kilichoko Maswa sasa hivi ni gofu. Majengo yapo na haya majengo ni imara; andaa andiko la kuweka mashine za kisasa ambazo gharama zake ni ndogo, ni dola 50,000 mpaka dola 70,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashine hizi zikishachakata pamba andika andiko Mheshimiwa Profesa Mkumbo, kila Halmashauri ambako pamba inalimwa wawe na viwanda vya nyuzi. Lazima utenganishe kiwanda cha kuchakata pamba na kiwanda cha nyuzi. Hizi viwanda vya nyuzi vikiwa katika Halmashauri husika, huko hawa Wakuu wetu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri na sisi Wabunge, tutahakikisha hili zao la pamba linatoa ajira kubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya hapo nyuzi zitauzwa katika viwanda vikubwa. Tutakuwa tuna viwanda vikubwa katika makao makuu ya mikoa ambako pamba inazalishwa. Kule watatengeneza majora halafu yale majora yatashuka chini tena kwa ajili ya hao washonaji watakaokuwa wanashona nguo hizi. Kwa hiyo, watashona nguo na tutazalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Mkumbo aende akajifunze Thailand. Thailand hawalimi pamba kama Tanzania, lakini leo ndiyo nchi ya kwanza duniani kwa kuzalisha nguo za watoto na nguo za akina mama. Pamba inatoka Tanzania, hatuwezi kukubali katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Mkumbo kaa ufikiri uwasaidie Watanzania na utapata heshima kubwa; ukibadilisha mapinduzi ya zao la kilimo na viwanda katika nchi hii utapata heshima kubwa sana. Na kule unakokwenda kutengeneza walipakodi, utakwenda kuwatengenezea kule katika kilimo. Mazao ya kilimo yakipata uchakataji mzuri katika nchi hii tutaiokoa nchi hii na ajira itapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema tunatengeneza ajira milioni nane; nini milioni nane, tutatengeneza ajira milioni 17. Kwa sababu tukiwa na viwanda sisi nchini, tujiondoe kuuza robota. Na usifikiri kutengeneza viwanda vikubwa, kuna viwanda vinakuja katika kontena la *20 feets* au *40 feets,* kontena dogo tu, kontena lile dogo linakaa hata makao

makuu ya kata. Watalima pamba na watachakata robota. Uwe na viwanda vya kuchakata robota 35 mpaka 100, basi inatosha. Utaibadilisha nchi hii kuhusiana na suala la pamba. Kila Mbunge anayesimama hapa anazungumzia jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, kuna jambo ambalo linaonekana katika nchi hii halileti afya, suala la biashara ya Zanzibar na Tanzania. Hili jambo lazima liangaliwe kwa nguvu kubwa. Haiwezekani nchi inaitwa Tanzania Bara, Tanzania Visiwani tunaunda Tanzania, leo mzigo ukija ukaupitishia Zanzibar unaonekana umefanya jambo haramu katika nchi hii, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tengenezeni sera nzuri ya biashara katika nchi hii. Wazanzibari waone wana haki ya Muungano kuuza vitu hapa na sisi Watanzania tuone tuna haki ya kuuza bidhaa zetu Zanzibar. Haiwezekani kitu kama hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Wazanzibari hawatufurahii sisi kwa sababu tumefunga mpaka, yaani inaonekana kama mzigo unatoka Zambia au Uganda, haiwezekani kitu kama hiki. Kwa hiyo tengenezeni sera nzuri ya biashara, kwamba mzigo utakaoshuka Zanzibar kuja Tanzania Bara ni asilimia tano au kumi ulipiwe ushuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo biashara zetu za mipakani za sheria za Afrika Mashariki, hizi biashara zilizoko tumetengeneza majengo. Ukienda katika mpaka wa Burundi na Tanzania kule Kobelo, leo tunagongwa Kobelo, unagonga Kabanga, ukienda Rusumo, hali kadhalika. Ukienda katika mpaka wa Tanzania kule Misenyi, Mtukula, ukienda mpaka wetu sisi wa Sirari leo ule mlango wa Sirari unaonekana ukipitia Sirari unakuja wewe unakuwa kama unafanya biashara haramu, haiwezekani kitu kama hiki katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalieni hii biashara ya mipakani, Tanzania imeshuka katika biashara ya kuagiza

mizigo nje ya nchi. Wekeni hizi kodi kwa sababu wewe ndiyo una haki ya kutengeneza walipa kodi wapya na wewe ndiyo una haki ya kulinda walipa kodi na wafanyabiashara katika nchi hii. Hii dhamana umeichukua wewe umepewa na Mheshimiwa Samia Suluhu kuhakikisha wafanyabiashara wanakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nchi, Rais akija wa aina hii biashara inakufa, akija Rais wa aina nyingine biashara inapanda, haiwezekani katika nchi hii. Tengenezeni sera ya biashara wafanyabiashara tufanye biashara kwa amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na-*declare* mimi ni mfanyabiashara, lakini biashara nyingine tumeziacha katika nchi hii. Leo kuna biashara mfano kama sasa hivi nilitoa ushauri mimi, kuna biashara ya mifugo, hii biashara ya mifugo ni kubwa sana katika nchi hii. Leo mifugo wetu, ng'ombe wananunuliwa na watu wa Comoro, wanakuja kununua ng'ombe Kahama, Sengerema na Kwimba. Wale ng'ombe wanapelekwa Comoro wanalishwa miezi miwili wanakwenda kuuzwa Ufaransa, haya ni mambo ya ajabu sana. Kwa nini sisi tusitafute soko la ng'ombe Ufaransa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna soko kubwa kule Ghuba, wenzetu wanakwenda katika ibada ya Hijja sasa hivi. Hii ibada ya Hijja Mheshimiwa Profesa Mkumbo, ni kwamba mnatakiwa mkatafute soko hili la mbuzi na ng'ombe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mbuzi anauzwa mpaka dola 200, 300 Saudi Arabia, wakati huyu mbuzi anauzwa kwenye masoko Kongwa, Sengerema na sehemu nyingine kwa shilingi 50,000, shilingi 70,000, anauzwa Saudi Arabia dola 300; sasa haya ni maajabu makubwa sana. Ng'ombe anauzwa shilingi 700,000, anakwenda kuuzwa dola 2,000 au 1,500 Jiddah. Sasa hili ni jambo ambalo hii ni kazi yako Mheshimiwa Profesa Mkumbo; hakikisha hii minada kwenye haya masoko yetu tuuze sisi wenyewe katika hizi nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala la kuweka viwanda vya nyama. Viwanda vya nyama katika nchi hii ni vichache kulinganisha na idadi ya ng'ombe tulionao. Tanzania leo ni nchi ya pili kwa mifugo ikitoka Botswana...*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tabasam kwa mchango wako mzuri, muda wako umemalizika.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Lakini kama umenikatia kidogo hivi maana yake bado nilikuwa naendelea kuserereka, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. *(Kicheko)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Muharami Mkenge, baadaye Mheshimiwa Juma Usonge na Mheshimiwa Joseph Kamonga wajiandae.

Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe hayupo? Tuendelee na Mheshimiwa Muharami

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo.

**MWENYEKITI:** Aah yupo eeh, haya.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa na mimi kwanza nianze kwa kupongeza wasilisho kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Na mimi naomba kutoa mchango wangu katika maeneo matatu kama muda utakuwa rafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza kabisa nataka kutoa mchango wangu kwa kuishauri Serikali ni kwa namna gani iweze kutusaidia wananchi wa Tanzania

kuendesha biashara zake, lakini kwa kuangalia na kasi halisi ya teknolojia ambayo iko duniani ili iweze kutusaidia kuendana na mataifa mengine na kukimbizana sawasawa na wenzetu ambavyo wanakimbizana huko kwenye mataifa ambayo yameendelea ambayo yanatumia teknolojia katika kufanya vizuri kwenye biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili ni kuomba ni kwa namna gani Serikali inaweza kuwekeza nguvu kubwa kwenye maeneo ya mipaka maana kuna fursa nyingi sana ikiwa ni pamoja na kufungua viwanda kwenye maeneo ya mipaka, lakini pia hata kuboresha mazingira mazuri ya biashara kwa sababu panapatikana ajira nyingi, kuanzia vijana, wazee, watu waliosoma na ambao hawajasoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na eneo la tatu, nitataka kuchangia na kuishauri Serikali kwamba vijijini akina mama wengi wameonekana ndio ambao wanatengeneza pombe za kienyeji na pombe hizi za kienyeji kwa kule vijijini zimeonekana zikipendwa sana. Basi kwa nini Serikali isitafute namna nzuri ya kuwasaidia akina mama hawa kuboresha ujuzi wao ili itusaidie kutoku-*import* pombe nyingi kutoka mataifa ya nje, tutumie ujuzi wa akina mama hawa ili kuendelea kutengeneza pombe zetu hapahapa kwa watu ambao ni watumiaji wa pombe waendelee kutumia vitu vyetu halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye teknolojia za biashara ambazo ziko duniani, naomba kuanza na namna gani ambavyo toka dunia ilivyokuwa imeanza kuna mifumo mbalimbali ambayo ilikuwepo ya biashara. Mfumo wa kwanza wa biashara uliokuwepo ni mfumo wa *barter trade. Barter trade* ilikuwa inafanyika katika mfumo kwamba kulikuwa hakuna *means of exchange,* kwa hiyo, biashara zilikuwa zinafanyika kwa kubadilishana bidhaa na bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya hapo, mfumo huo ulikuja ukapita baada ya dunia kuendelea tukaja kwenye *metal* au *coin* ambapo vito au dhahabu vilitumika

kama *means of exchange.* Baada ya hapo dunia ikaondoka tukaingia kwenye *paper (cash) ch currency,* maana yake hapa tunaangalia *Tanzanian Shilling, Kenyan Shilling, Zambian Kwacha, Nigerian Naira, Pula* na pesa mbalimbali kutoka kwenye mataifa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo tunaendelea tuko kwenye huu mfumo, lakini tukaja kwenye mfumo mwingine ambao tunaita *credit card* ambao hata sasa hivi bado tunatumia, kwamba watu hawataki kubebeshana pesa nyingi, lakini mtu unapokuwa na kadi unaweza ukafanya *transaction* mahali popote pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa nne uliofuata ambao sasa dunia ipo na ndipo mahali ambapo dunia inatengeneza pesa nyingi sana, ndipo mahali ambapo hata matajiri wengi ambao wamepata kutokea katika kipindi cha miaka 15, ninapowaongelea Bill Gates, Alibaba, wametokana na mfumo huu wa teknolojia ambao umegawanyika katika *phases* mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naongelea *fourth industrial revolution* ambayo ndani yake kuna *block chain technology.* Kwenye *block chain technology* kuna teknolojia nyingi; watu wa sheria wanaweza wakaitumia *block chain technology,* watu wa ardhi wanaweza wakaitumia *block chain technology,* lakini hapa nataka niongelee kwenye mambo ya fedha namna gani *block chain technology* inatumika, na zaidi ya hapo nataka kuongelea kwenye *digital currency.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwenye *digital currency,* hii ni teknolojia ambayo ni kubwa sana lakini kwa bahati mbaya tafsiri ambazo tunazipata sanasana kwenye Nchi kama Tanzania na nyingine za Afrika, tunashindwa kuitafsiri vizuri teknolojia hii. Na hakuna namna tunaweza tukaizuia teknolojia hii isije kufanya kazi, na tayari huko duniani kuna watu ambao wametokea matajiri wengi sana kwa kupitia *block chain technology* ambayo ndani kuna *digital currency.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwenye *digital currency* nataka kuziongelea baadhi ya *currencies.* Mfano naziongelea *bitcoin, ethereum, theta, bitcoin cash, litecoin* na *ripple,* na zipo *coin* mbalimbali. Lakini hapa nataka kuiongelea zaidi *coin* ya *bitcoin. Coin* hii mpaka sasa Tanzania hatufahamu kwa upana namna *bitcoin* inavyofanya kazi, na Watanzania wengi wamekuwa wakiendelea kupoteza fedha zao kwa sababu wanadanganywa, hawajui. Lakini kama Serikali ingekuwa imeamua kulivalia njuga jambo hili wakaamua kuwekeza kwenye elimu kuna vijana wengi wa Kitanzania ambao wanaulewa mkubwa na wimbi kubwa sana la vijana ambao wapo wengine wanafanya na wanatengeneza hela, lakini pia Serikali inapoteza mapato yake kwa kiasi kikubwa sana kupitia hili eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano leo nikiongelea, jana bei ya *bitcoin* ilikuwa milioni 92 za Kitanzania, nachukulia mfano mtu kwa mfano *South Africa* kuna *ATM* ya *bitcoin,* Kenya kuna *ATM* ya *bitcoin* lakini sasa hivi tuchukulie mtu anatuma hela kutoka *South Africa* anamtumia Mtanzania aliopo hapa, hakuna namna yoyote ambayo *BOT* wanafuatilia *transactions* hizi kwa sababu mambo yote yanafanyika *online,* mambo yote yanafanyika kwenye *internet.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hata ilipotokea wakati ambapo Serikali iliamua kuzifunga zile *bureau* nyingi ambazo zilikuwa zipo Arusha na sehemu zingine, *bureau* nyingi ziliamua kuhamia kwenye *online* kwa mfano Serikali haijui kuna kitu kinaitwa *remitano*, Serikali haijui *local bitcoin,* Serikali haijui kuna kitu kinaitwa *e-wallet* huko kwote Watanzania wapo ambao wanatengeneza hela na wanatengeneza hela wakati mwingine naweza kusema hata hela zinaingia nchini kinyume na taratibu kwa sababu hakuna *connection* kati ya teknolojia, Serikali na taasisi za fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ombi langu kwa sababu ya ku-*serve* muda, Serikali tuamue kujifunza hata kwa nchi za wenzetu, tunaweza kujiuliza *South Africa* wanafanyaje mpaka wana *ATM* ya *bitcoin,* Kenya wanafanyaje mpaka

wana *ATM* ya *bitcoin?* Kwa nini wanaweka zile ATM, wananufaika na nini.

**MWENYEKITI:** Malizia sentensi yako ya mwisho.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa hiyo kwa kumalizia ni kwamba tunaiomba Serikali iwekeze sana mahali hapa kwa sababu wimbi kubwa la vijana ambao wanatumia teknolojia wanaweza wakapata ajira kwa kupitia mahali hapa na Watanzania wengi wasiendelee kupotoshwa na kuibiwa kama ambavyo lilikuja hata wimbi la *D9* watu wengi wakaibiwa ni kwa sababu Serikali ilikuwa haijaweka mikono yake namna gani ikusanye mapato na namna gani iwalinde Watanzania hawa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Condester. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Muharami na baadaye Mheshimiwa Juma Usonge, Mheshimiwa Joseph Kamonga na Mheshimiwa Lucy Mayenga wajiandae.

Mheshimiwa Muharami hayupo? Tuendelee na Mheshimiwa Juma Usonge baadaye Mheshimiwa Joseph Kamonga.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kuchangia kwenye hotuba hii ya Wizara ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujalia leo hii tupo wazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita zaidi, mara nyingi sana Wabunge wote waliosimama hapa wanazungumzia suala la vijana na mimi kama rika ya vijana bado ninayo haki ya kuzungumzia suala la vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii, imebeba taswira kubwa na dhana kubwa sana ya kumkomboa kijana wa Kitanzania sasa hivi. Ukweli usiopingika idadi kubwa sana ya vijana wa Tanzania ndiyo ambao wanajishughulisha na shughuli mbalimbali, lakini ndiyo wanaochangia pato kubwa sana la Taifa hili la Tanzania. Ripoti ya dunia kwenye Benki Kuu inaonyesha kwamba Tanzania kila mwaka vijana milioni moja wanaingia kwenye suala la ajira, lakini vijana 200,000 tu ndiyo wanufaikaji wa ajira, lakini vijana 800,000 ndiyo ambao hawapati ajira mpaka muda huu tuliouzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ukizungumza kama miaka mitano ijayo bado tunatengeneza wimbi kubwa sana la vijana ambao watakuwa hawana ajira. Sasa wazo langu, kwenye Wizara hii, lazima tuweke mipango mikakati namna gani tunaweza tukawasidia vijana kwenye Wizara hii. Isiwe Wizara hii kazi yake kubwa sana, kazi yake kufanya mipango mikakati kwa ajili ya kuvutia wawekezaji, lakini hatuangili vijana namna gani tunaweza tukawasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo mipango mahsusi ya kuweza kuwasaidia vijana, tunao vijana wa vyuo vikuu wanamaliza vyuo vikuu, lakini mwisho wa siku wanabakia hawana ajira, ni vijana tu wachache ambao wananufaika na ajira, lakini vijana wengi hawanufaiki na ajira. Kama Wizara imejipanga vipi na namna gani kuwasaidia vijana hawa ambao wanahitimu vyuo vikuu? Kwa nini tusitengeneze *exemption at least* miaka kama mitatu, minne tukawapa mikopo ya fedha ilimradi wakaanzisha makampuni wao wenyewe binafsi kama vijana ambao wamehitimu vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wapo wanafunzi ambao wamemaliza kada ya sheria, wanaweza wakaendesha kampuni zao za kisheria tukawa tuna mawakala wa-*law* wakawa wanatetea wananchi, leo hii Tanzania tunaweza tukajikuta hata mtu wa kawaida mkulima anawakili wake wa kuweza kumtetea kwenye mahakama. Leo hii tunaweza tukawa na mvuvi, lakini pia akawa na wakili

wake wa kuweza kumtetea kwenyea mahakama endapo kutatokea matatizo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado hatujaona fursa ya kuweza kuwasaidia vijana wanaohitimu chuo kikuu, lakini wapo wanafunzi ambao wanamaliza kwenye kada ya *IT* ndiyo hawa hawa mwisho wa siku wanaweza wakaanzisha makampuni makubwa ya kufungua masuala ya *website*, ya kufungua masuala ya *computer technician* na mambo mengine kadhaa wa kadhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kufungua kwa kampuni hizi nazo zitawasaidia wao wenyewe vijana kupata ajira, lakini pia wapo ambao tayari hawakufikia *level* za vyuo vikuu nao watapata kufanya angalau ajira, japo kufanya usafi kwenye maofisi na kazi nyingine ndogo ndogo. Lakini bado hatujaenda kuwaangalia kuwasaidia vijana, Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwenye ukurasa wa nane hii ambayo tayari tunaizungumzia ya mwaka 2020/2025 imezungumzia kwamba namna gani Serikali inaweza ikatengeneza ajira kwa vijana milioni nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado hatujaangalia mkakati wa kuwasaidia vijana, bado kwenye Wizara hii hatujakaa kabisa. Tusiwe na dhana ya kuweza kuvutia wawekezaji, lakini pia tuwe na dhana ya kuwasaidia vijana wetu ndani ya Tanzania. Najua bado hatujawa na fedha na *capital* na wala hatujawa na wimbi kubwa sana la wawekezaji kuja ndani ya nchi. Lakini namna gani tunawasaidia vijana, kwa mfano wapo vijana ambao wamemaliza masuala ya *business administration* ndiyo hawa hawa wanaweza wakaandika ripoti tofauti tofauti kwa ajili ya *investment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anaweza akaja mwekezaji, lakini akatafuta ripoti tunao vijana ambao tumeshawapa *exemption* ya kodi na tulishawapa fedha kwa ajili ya kujikwamu, lakini vipi wanaweza kutengeneza ripoti tofauti tofauti wakaja wazungu, wakaja ma-*investor* wakachukua ripoti baadaye zikawa *applicable.* Bado hatujawa tukafikiria

lazima Wizara ya Viwanda na Biashara ifikirie namna gani sasa ya kutengeneza fedha kwa ajili ya kuwasaidia vijana kwa ajili ya kujikwamua na huu unyonge na umaskini ili uweze kuisaidia familia zao la sivyo hatuwezi kuwasaidia vijana kwa namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutabaki tuna *propaganda* za kisiasa tuna wasaidia vijana tunatengeneza, tunaandaa ajira kila mwaka, tutaandaa *manifesto*, tutaandaa Ilani, tutaandaa ripoti tofauti tofauti namna gani ya kuwasaidia vijana, lakini bado hatujawa *practical* kwa ajili ya kuwasaidia vijana, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri nakuomba sana wafikirie vijana bado vijana wanateseka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo usishangae kumuona kijana ambaye amehitimu chuo kikuu anaendesha boda boda, usishangae kumuona kijana wa chuo kikuu yupo kwenye michezo ya ku-*bet,* usishangae leo kumuona kijana yupo kondakta ni muhitimu wa chuo kikuu. Serikali imetumia fedha nyingi sana kwa ajili ya kumsaidia kijana ili aweze kufika chuo kikuu, lakini mwisho wa siku akimaliza miaka yake mitano au miaka mitatu ya kuhitimu *degree* anabakia mitaani anaendesha bodaboda. Unadhani kijana kama huyu mwisho wa siku tumemsaidia nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukae kama wizara kuweza kuwasaidia, ingawa tunasisitiza siku zote sisi hapa Bungeni kwamba Serikali itenge fedha kwenye Halmashauri asilimia kumi kwa ajili ya kuwasaidia vijana, sawa inafanya hivyo, lakini kwa nini tusitenge angalau asilimia kadhaa ambayo inatoka kwenye Wizara hii kuwasaidia vijana kuanzisha makampuni au kuanzisha shughuli yoyote ya kibiashara? Bado hatujakaa tukafirikia Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Juma.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kamonga, Mheshimiwa Lucy Mayenga na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia bajeti hii muhimu ya Viwanda na Biashara, lakini vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, bajeti yake imekaa vizuri na inaleta matumaini na pia niipongeze Kamati ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Kihenzile kwa sababu walifanya ziara jimboni kwangu kuangalia miradi mikubwa ile ya Mchuchuma na Liganga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli bajeti inaleta matumaini, tunamuomba tu Mheshimwa Waziri aendelee kuisamimia ili iweze kutekelezwa. Na bahati nzuri nimekaa naye jana kwa muda mrefu kidogo akiwa na Naibu wake na wiki iliyopita baada ya kumuomba aweze kutembelea Jimboni Ludewa aliridhia kwamba atakwenda baada ya kuwasilisha bajeti hii ili aweze kuzungumza na wananchi. Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana na wananchi wa Ludewa wanakusubiri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hali kadhalika siku chache zilizopita Waheshimiwa Madiwani wa Jimbo la Ludewa walikuwepo hapa Bungeni na waliweza kukutana na Mheshimiwa Biteko, nako walileta mawazo yao mbalimbali Mheshimiwa Waziri aliweza kufafanua vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niwashukuru pia Waheshimiwa Wabunge mbalimbali ambao nao wamekuwa wakiona kwamba miradi hii ya Mchuchuma na Liganga ni muhimu sana na ni kitovu kwa uchumi wa nchi yetu. Wabunge wengi sana wamechangia juu ya miradi hii, kwa hiyo, wanaonesha kwamba wanaona umuhimu wa miradi hii. Kwa hiyo naomba sana Serikali iweze kuwa sikivu iwasikilize

Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia umuhimu wa miradi hii maana na sauti za Wabunge ni sauti za wananchi moja kwa moja.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Ludewa wanapoona miradi inazinduliwa maeneo mengine wanajisikia wanyonge sana, wanasononeka, wanafadhaika, lakini kwa mpango huu wanakuwa wana imani kwamba miradi hii sasa itakwenda kutekelezwa, hasa hasa suala la fidia kwa wananchi wa Mchuchuma pale vijiji vya Nkomang'ombe, Kipangala, Iwela wanadai fidia na wamesubiria kwa muda mrefu sana. Wananchi wa Kijiji cha Amani na Mundindi wamesubiria fidia hizi tokea mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini kwa fedha hizi zilizotengwa Mheshimiwa Waziri atakwenda kuwalipa fidia wananchi wale mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mzee mmoja alikuwa anaitwa Mzee Machupa, mwaka 2017 aliwahi kuwaeleza wananchi wa *NDC* kwamba hizi fidia Serikali inashindwa kutulipa wanataka ije ijenge makaburi yetu, tutakufa tutaziacha hizi fedha, bahati mbaya mzee yule Mwenyezi Mungu amemchukua bila kulipwa zile fedha. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naomba sana utekelezaji wa jambo hili na kukumbusha ile ziara ya Ludewa kwenda kuzungumza na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na vilevile tutambue kwamba katika madini haya tunazungumzia tu makaa ya mawe na chuma, kwenye chuma cha Liganga ambacho kinaonekana kwamba kuna mashapo ya chuma ambayo ni tani milioni 126, kwa eneo la kilometa 10 tu ambao walijaribu kufanya uchunguzi. Lakini kwa eneo lote linakadiriwa na tani milioni 700 mpaka milioni 1,400 za chuma ambazo ndani yake kuna madini mengine ya *titanium*, ya *vanadium* na madini haya ni muhimu sana kwa sababu mengine yanatumika kutengeneza vitu vya thamani sana, kama *laptop*, *computers* na ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuna madini mengine ambayo yanathamani kubwa, kwa hiyo, hii ni utajiri mkubwa kwa nchi yetu, ni Serikali haina sababu ya kutoanza miradi hii. *(Makofi)*

Vilevile miradi hii naomba Serikali izidi kuwasiliana, Wizara za Serikali, kwa sababu uwekezaji huu tunavyosema kwamba ni mradi kielelezo, miundombinu nayo inapaswa iendane na miradi hii. Bahati mbaya sana nilisoma bajeti ya Wizara ya Ujenzi nikaona uwanja wa ndege wa Njombe haumo kwenye mpango, wakati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri mama Samia Suluhu Hassan alivyokwenda kwenye...

**MHE. NEEMA W. MGAYA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Neema Mgaya.

**TAARIFA**

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nilikuwa napenda kumpa taarifa kaka yangu Joseph Kamonga, Mbunge wa Ludewa, nilikuwa napenda kumwambia kaka yangu Joseph kwamba Serikali pia itueleze imejiandaa vipi kwenye mradi huu wa Liganga na Mchuchuma kuwatayarisha wananchi wetu wa Ludewa kuupokea mradi ule, kuwapa elimu namna gani ambayo wananchi wataweza kwenda kunufaika na fursa mbalimbali zitakazotokana na mradi huu wa Liganga na Mchuchuma. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hii kwa sababu ananikumbusha *NDC* walianzisha mradi wa kuelimisha jamii unaitwa *PAKA*. Mradi ule haupo tena, nina imani Mheshimiwa Waziri atatoa taarifa na atasema bajeti iliyotengwa kwa ajili ya kuwapa elimu wananchi wa Jimbo la Ludewa na maeneo jirani ili waweze kujiandaa na miradi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo uwanja wa ndege nayo ni sehemu ya uwekezaji, bahati mbaya Wizara ya Ujenzi nimeona wameondoa wakati ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi na wananchi wa Njombe kiasili ni wafanyabiashara kwa hiyo uwanja ule ni muhimu sana na unaendana na miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph. Tunaendelea na Mheshimiwa Lucy Mayenga baadaye Mheshimiwa Mwita Getere na Mheshimiwa Haji Mlenge ujiandae.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kabisa kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Mama yetu mama Samia Suluhu kwa kweli kwa jinsi alivyoweza kubadilisha taswira ya biashara katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokaa, watu wanapokaa kila kona kuzungumzia masuala ya kipato au kuweza kulalamikia kipato, hakuna njia yoyote inayoweza kusaidia wananchi hawa wakaja kuridhika zaidi ya biashara. Ninasema hivyo kwa sababu biashara zote duniani utakuta inagusa kilimo, biashara zote duniani utakuta inagusa mambo ya Liganga, Mchuchuma, biashara zote duniani kuna sehemu ambapo mwananchi atafaidika kwa njia moja au nyingine.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ambacho wasiwasi wangu, ambacho nakiona ni kwamba mitazamo ambayo wanakuwa nayo viongozi wetu wakubwa na hasa niseme Marais wetu na hawa viongozi wengine wakubwa Waziri Mkuu, Makamu wa Rais wakikaa kuongea na wafanyabiashara, wakikaa kuongea kisiasa, ni vitu havifanani

kabisa na mawazo ambayo yapo huku chini kwa watendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachokiona ni tatizo la sisi Watanzania hasa huku kwenye watendaji tubadilishe *mindset* na siyo kitu kingine. Tumekaa kwa muda mrefu sana tunazungumzia changamoto zilizopo kwenye biashara, baada ya hizi changamoto wakasema tuje na kitu kinaitwa *blueprint,* lakini *blueprint* hii ni karatasi, *blueprint* hii ni kitu ambacho kimeandikwa, kinataka mtu aje sasa aseme kwamba hiki tutakitekeleza kwa aina gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine hata kwenye kuchukua hizi hatua tuwe basi tunachukua hizi hatua haraka haraka, niwapeni mfano, kwa mfano, sheria zetu sisi hapa Tanzania kwa muda mrefu hazifungamani, yaani sheria za kodi na sheria za kibiashara zipo tofauti sana. Mtu akija hapa kwa mfano mtu akitoka popote una mtaji wako hata wa dola laki moja, dola laki mbili, ukisema nataka kwenda kufanya biashara fulani, yaani mchakato jinsi utakavyokuwa na jinsi utakavyosumbuliwa kwenye hicho ambacho unakifanya mpaka unakata tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini yote haya viongozi na watendaji Serikalini huko wanayajua kwa nini hawachukui hatua? Ndiyo maana ninasema kwamba viongozi wanaweza wakawa na mawazo mazuri sana, lakini huku chini lazima tubadilike.

Mheshimiwa mwenyekiti, nitoe tu mfano wa mambo kama mawili, matatu hapa Tanzania kuna viwanda viwili tu vya mabati, viwanda hivi ndivyo ambavyo vinafanya kazi ya kuzalisha mabati hapa Tanzania, lakini wafanyabiashara ambao wana mawazo au wanamitaji ya kufanya biashara hii wapo wengi sana. Sasa kinachofanyika ni kwamba kunakuwa na kama kautaratibu kaku-*monopoly* biashara, mtu anakuja anakaa anakwenda kuongea na watu anaowajua mwenyewe huko akienda kuongea nao ninyi ambao mnataka kufanya hiyo biashara kila mkijitahidi kufanya mnashindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndiyo maana nimesema tubadilishe *mindset*, sasa matokeo yake wafanyabiashara hivi sasa wameamua badala ya kuzalisha bidhaa hapa Tanzania wanaamua kwenda Kenya na Uganda kwa sababu kule walipi kitu, wanakuja wanaingiza hapa Tanzania ndiyo wanafanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivi tunavyokaa kupiga makelele viwanda vitawezaje kuanzishwa kwa utaratibu huu. Kodi hizi kwa nini haziwi na mwingiliano yaani kwamba tukisema kwamba tunamfutia kodi hii, *import duty,* tukisema tunafuta *import duty* tunaacha *VAT* tufanye haya mambo kwa sababu ya kuweza kusaidia watu waanzishe viwanda na mambo mengine yaendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, mtu leo hii ukisema kwamba mimi nataka nifanye biashara, mfano labda kama dawa za minyoo, dawa za mifugo, nataka niingize hapa Tanzania, ukiwa na kiwanda hapa Tanzania ile dawa ni ghali kuliko ambayo inatoka nje kwa sababu ya changamoto ya kodi, sasa mtu anafikiria mimi namtaji wangu hakuna mfanyabiashara ambaye hataki faida. Mimi ninamtaji wangu nasema nataka nifanye biashara ya aina fulani halafu nikipiga mahesabu naona kwamba kuanzisha kiwanda hapa Tanzania, najiona kwamba kiwanda kile sawa kuna faida kitaingiza, kitaajiri watu na kadhalika, lakini faida yangu itakuwa ndogo tofauti na ile faida ambayo utaipata kwa kuagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana changamoto licha ya kwamba sijui kuna mazingira biashara, jamani wawekezaji mje mfungue viwanda, siyo rahisi mtu kuja kuanzisha kiwanda hapa Tanzania kwa mazingira haya yaliyopo ya hizi sheria, kanuni, taratibu na haya masuala ya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile sheria hizi hizi leo mimi nimekaa nataka nianzishe kwa mfano labda kiwanda, mimi naomba niwaulize Wizara hii ya Viwanda na Biashara hivi hivi viwanda tu vilivyopo wanavitembelea

kwenda kuangalia kinachozalishwa? Kwa sababu huku chini kwa wananachi mwananchi leo hii, Mheshimiwa Subira amesema pale kwamba kuna viwanda vingi sana kwenye Mkoa wa Pwani, kuna viwanda vya *tiles* na kadhalika. Lakini zile bidhaa ambazo zinazalishwa kwenye hivi viwanda wakati hawa wawekezaji wanakuja, walikuwa wanaamini kwamba watumiaji wa bidhaa hizi mtu analenga soko la lile eneo ambalo anaanzisha ile biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kinachofanyika kwenye Wizara hii ya Viwanda na Biashara hawaendi kukagua hizo bidhaa, wala kwenda kuangalia nini kinaendelea kwenye uzalishaji, wala kwenda kuthibitisha kwamba hiki kinachozalishwa kina ubora, hivi mnafanya nini ofisini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotokea sasa watu wanakuja wanaanzisha biashara, wakianzisha biashara, mtu anaanzisha biashara *let's say* kiwanda cha *tiles,* wanunuzi wanakosekana kwa sababu mnunuzi anaangalia *quality*, akishaangalia *quality* anasema hivi hapa nilipo nikinunua *box* moja la bidhaa *labda let's say* ya *tiles* za Tanzania na *tiles* za China nikiongeza shilingi 10,000 tu, napata hii ya China ambayo fundi anamthibitishia kwamba bora ununue hii itadumu zaidi kuliko hii ambayo inatengenezwa Tanzania. *What is this*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Wizara ya Viwanda na Biashara haiendi kuangalia ubora wa bidhaa ambazo zinazalishwa? Hii ni hatari kubwa sana kwa sababu mwisho wa siku hivi viwanda vita-*collapse,* watu watakaa wanasema karibuni tutawahamasisha kwa njia nyingi sana, Mheshimiwa Mama Samia ameweka mazingira mazuri sana. Lakini kama sisi wenyewe hatutakuwa *serious* kwenda kuangalia mambo ambayo yanafanyika huko, tusikae mwishowe Mbunge mmoja hapa ameelezea, hapa Tanzania tatizo letu ni kama vile kila mtu yaani kwamba elimu ni huyu, wa elimu ndio kinamuhusu peke yake, huyu mwingine wa maji kinamuhusu peke yake, kwenye viwanda huku mambo ya fedha, mambo

ya kodi ni mwingine yaani hatushirikiani, hakuna *co-ordination*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo tukiendelea kuyafanya namna hii tutakuwa tunaongea, viongozi wetu watakuwa wanahubiri haya mambo sana, wananchi wetu watakuwa wanalalamika kwamba pesa hatuna mifukoni, wakati sisi ambao tuko kwenye nafasi hizi za kufanya utendaji huu wa kuthibitisha na ni vitu vya kukaa tu na watu tukawasikiliza na kuthibitisha. Mwisho wake tumekaa hapa tukazungumza sheria ya *TIC*, na namshukuru sana Mheshimiwa Rais pia ali-*mention* hili, mtu anakuja na mtaji wake anasema kwamba, mimi nimekuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana tunamkaribisha mwekezaji, tunamuambia kwamba ukija Tanzania utaingiza wafanyakazi moja, mbili, tatu na kadhalika, lakini huku unampa unamnyang'anya kwa mlango wa nyuma. Sheria ya *TIC* na yenyewe pia kwanza ni ya muda mrefu sana mwaka 1972 inatakiwa kubadilishwa, lakini mpaka leo ni mambo yale ya Serikali mambo yanakwenda hivi na nini tunatumia muda mrefu sana. Mtu anakuja na mtaji wake, mimi nina mtaji wangu wa dola 500,000 au dola 1,000,000 nimekuja hapa Tanzania baada ya kufika hapa nakaa naanza kuwekeza kwenye masuala labda pengine kwenye biashara fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba kwa mimi kwa pesa yangu namuamini dada yangu Esther huyu akinisimamia hapa, yaani hatakuwa na mambo ya ajabu ajabu, namuamini aidha ndugu yangu au ni mtendaji wangu. Halafu sheria inakuambia kwamba umeshafika umeshawekeza mtaji wako, lakini inabidi kwa kweli hapa kwasababu kuna mtanzania mwingine ana elimu kama hiyo kwa nini huyu asifanye. Mwisho, vitu vingine mtu anaangalia kwamba, yeye na huyu mtu wana historia gani, wana ukaribu gani, wako pamoja kwa kiasi gani, uaminifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwentekiti, mwisho, lakini naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana Mheshimiwa Lucy. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwita Getere, baadaye Mheshimiwa Haji Mlenge, Mheshimiwa Stella Fiyao na Mheshimiwa Abdallah Chikota wajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie hii Wizara ya Viwanda na Biashara. Nakushukuru wewe mwenyewe kwa kumuomba Mwenyezi Mungu amekuleta hapa Bungeni, lakini umekaa maeneo yako yale yale kama ulivyo kawaida, tunakuombea uendelee vizuri. Nashukuru Wizara yangu Wizara ya Viwanda ambayo mimi ni mwanakamati, namshukuru Profesa na *crew* yake yote Naibu Waziri na Katibu, kazi zinaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea ni kwamba naomba nchi yetu hii Mungu anaipenda sana na nadhani tuendelee kumuomba Mungu atuepushe na haya magonjwa mabaya yanayokuja na mimi naamini kama tutaendelea kumuomba Mungu hali itaendelea kuwa nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Na niombe tu kwenye mikutano yetu yote tunayokuwa tunakuwa nayo tuwe tunaanza na yale mambo yetu ambayo ni ya Mungu kwa mfano, Bunge letu huwa tunaanza kuomba Mungu kwanza ndio tunaingia, hata kwenye mikutano tuombe kwa kuomba kwamba *Asalaam Aleykum,* Tumsifu Yesu Kristo, Bwana Asifiwe, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kazi Iendelee. Kwa hiyo nadhani hili nalo ni jambo kumtanguliza Mungu kila tunapokuwa tunafanya shughuli zote ambazo tunataka kuzifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie kwenye Wizara hii kwenye upande wa Mchuchuma na Liganga. Mimi kama mwanakamati nilivyoona ile hali na wakati sisi humu tunajipa matumaini kwamba Mchuchuma na Liganga itakuwepo, mimi kwangu naona kama hatutatafuta mwekezaji mwenye uwezo wa kuendesha ule mradi itakuwa ni majina tu tunaita kila siku mpaka tunafia humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili Liganga na Mchuchuma iwepo lazima tutafute mwekezaji mwenye uwezo wa kuendesha ule mradi, maana Serikali haiwezi kuendesha ule mradi. Kama Serikali haiwezi kuendesha ule mradi, tutafute mwekezaji mwenye uwezo wa kuendesha ule mradi na mwekezaji mwenyewe tukishampata mikataba yake tuisome wazi ionekane kwamba, anashughulika na miradi miwili mradi wa madini na mradi wa chuma aelewe mapema kutoka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru...

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa.

**T A A R I F A**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa kaka yangu kwa mchango wake mzuri kwanza wa Liganga na Mchuchuma. Ningependa kumpa taarifa kwamba, kwanza huo mradi umechukua muda mrefu takribani miaka 20, lakini Serikali imeingia ubia na mwekezaji Mchina, amekaa zaidi ya miaka nane, ameshindwa kufanya chochote, wako kwenye hatua ya kulipa fidia, mbaya zaidi wanaenda ku-*review* mkataba na mwekezaji yule yule.

Sasa taarifa yangu nakupa kwa nini wasimfukuze na naungana na wewe watafute mwekezaji anayeweza kwenda kuwekeza kwenye Liganga na Mchuchuma ili tuweze kupata faida katika Taifa letu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, taarifa yake naikubali nadhani dada yangu sasa hivi yuko vizuri sana, kwa hiyo, naikubali taarifa yake. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua tusiwe tunazungumza mambo humu Bungeni kama kujifurahisha. Nchi yetu inahitaji kupata viwanda ule mradi ni mradi mkubwa sana, mkubwa sana. Kwa mwekezaji aliyopo kama ana-*tender* nyingi maana yake anataka afanye mradi mmoja yeye kwa mradi mmoja huo hataki ku-*separate* mambo ya madini na chuma. Kwa hiyo, mimi nione kama ni kazi, kwa hiyo, nimesema tutafute, kama yeye yupo, kama mikataba yake inaeleweka, tuilete hapa Bungeni tuione, tuizungumze humu Bungeni tuione kama anaweza kuifanya ile kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama hawezi kama alivyosema Mheshimiwa Ester tumuondoe, tutafute mwekezaji mwingine mwenye uwezo. Sasa siku hizi nako nimesikia Tanzania kuna matatizo, tunaweka makandarasi, tunawaondoa, sijui ni kienyeji sijui ndio ujanja wao, wanarudi nyuma kinyume nyume kutudai tunalipa mabilioni. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Taarifa.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa muangalie tena mambo haya yanavyokwenda ili tuwe tunaweka hii mikataba na mambo mapya tusiwe tunaingia tena kudaiwa mabilioni ya watu wanaokuwa wanaweka mikataba...

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita subiri kidogo, Taarifa Mheshimiwa Mhagama.

**T A A R I F A**

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kukupongeza kwa kurudi katika nafasi yako, naomba nimpe taarifa mzungumzaji mzuri sana Mheshimiwa Getere kwamba *commitment* ya Serikali ya kuendeleza mradi wa Liganga na Mchuchuma haupo tu kwenye kuingia

mkataba na mwekezaji, bali pia kujenga mazingira ya kuanza kutekeleza mradi huo kitu ambacho hakijafanyika mpaka leo kwamba ilipaswa tuwe na reli ya Kusini ambayo itasafirisha chuma, tulipaswa tumalize barabara ya Madaba – Mkiu kwa ajili ya kusafirisha makaa ya mawe na chuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja yake ni ya msingi na hata mazingira yetu ambayo tulitakiwa tuwe tumeyafanya hatujafanya. Kwa hiyo, hata wakisaini mkataba wa kuchimba kile chuma hawana baraba raya kusafirisha wala reli ya kubeba chuma. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashukuru leo naona kila *point* ninayokwenda mtu anaichangia namshukuru sana kwa *point* hizo ambazo ameenda nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa Liganga na Mchuchuma, kulipa fidia lazima wananchi wa maeneo yale waambiwe, mwenye fedha ya kuwalipa wale wananchi ni nani ni mwekezaji au ni Serikali? Kama ni Serikali itoe maandalizi ya kulipa fidia kwa wananchi, kama ni mwekezaji tuwaambie wananchi kwamba sisi fidia hatutalipa mpaka mwekezaji atakayekuja hapa ndio atalipa ili wananchi wale wajue kinachoendelea pale. Sio wanakaa wanasubiri fidia, fidia, fidia kumbe inasubiri mwekezaji na mwekezaji anaweza kuja mwaka 2030 tumeshatoka humu Bungeni kwa hiyo, wawaambie wananchi kwamba nani anapaswa kulipa hiyo fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihame hapo niende kwenye viwanda vya Wilaya ya Bunda. Wilaya ya Bunda inaenda kuwa maskini kama ilivyokuwa huko nyuma kwamba sisi tulikuwa maskini kwenye Wilaya ya Bunda. Viwanda vilivyokuwepo Bunda kulikuwa na Kiwanda cha *Kibara Ginnery,* kuna *S & C Ginnery*, kuna *Mount* Meru *Ginnery*, kuna *Olam Ginnery*, kuna *Mara Lint Ginnery*, kuna *Ushasi Ginnery*, vyote vinaenda kufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilikuwa viwanda vya pamba na Wilaya ya Bunda ndio inazalisha pamba nyingi kwa maeneo yote ya Mkoa wa Mara. Ndio eneo bora viwanda vimekufa, *Kibara Ginnery* imekufa, Ushasi msimu wa mwaka 2019/2020 Serikali tulilazimisha watu wanunue pamba kwa bei ambayo ni kubwa, wakasema yale makampuni yakinunua watapata *refund* kutoka Serikalini, hawakurudishiwa. Makampuni yamekufa, Olam ilikuwa inafanya kazi imefungwa, *S & C* inakwenda kufungwa, viwanda vingine *Ushasi Ginnery* imefungwa miaka mingi, *Mara Lint* imekufa, Bunda inaenda kuwa maskini ya mwisho katika Mkoa wa Mara na katika maeneo yote ya Tanzania. Kwa hiyo tuombe sasa Waziri…

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa ya mwisho hiyo Mheshimiwa Ester.

**TAARIFA**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa kaka yangu Boni mbali na mchango wake huo mzuri wa *ginnery*, lakini pia Mkoa wa Mara tuna kiwanda pale Musoma cha *MUTEX,* Serikali bado inashindwa ku-*invest* ili wakulima wetu wa pamba, mbali tu ya Mkoa wa Mara na maeneo mengine wawe wana uhakika wa soko. Lini pia Serikali itaenda kuwekeza fedha kwenye kile Kiwanda cha *MUTEX*. Nilikuwa nampa kaka yangu taarifa Mheshimiwa Boni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante namshukuru sana Mheshimiwa Ester yuko sasa hivi nadhani amebadilika yuko vizuri sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumza haya mambo, hatuwezi kuwa na Wilaya kubwa ambayo inazalisha pamba kwa wingi halafu viwanda vyote vimekufa. Kwa hiyo, Wizara ya Viwanda na Wizara ya KIlimo nadhani wakutane

sasa waende waangalie vile viwanda msimu wa mwaka huu haijulikani pamba itauzwa wapi! Kwa hiyo, waende wakutane waone kiwanda kipi kama ni *Mara Lint* kama ni Kiwanda cha *S & C* wawalipe fedha waliyolipa ambayo wanadai Serikali, kama ni Olam wawalipe waliyokuwa wanalipa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna viwanda vya mafuta, mimi hii nchi sijui ina miujiza mimi sielewi. Kama leo tuna alizeti ambayo tukiamrisha mwaka kesho au msimu unaokuja, kwa miezi mitatu tunauwezo wa kupata mafuta mengi na yakabaki ziada tukauza nje hatushughuliki nayo! Tunashughulika na michikichi iive baada ya miaka miwili, mitatu ndio ipatikane tunaendelea kuagiza mafuta kutoka nje.

Naomba Serikali tuwe tuna sehemu mbili, tuwe na *long term* kwa maana ya kupata viwanda vya mafuta na mazao ya mafuta kwa maana ya michikichi ambayo ni *long term* tutakuwa nayo, tuwe na *short term* ambayo ni alizeti ambayo leo Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda wakikubaliana kwamba wanatoa mbegu bora, wanasimamia masoko inapatikana kwa wakati na mafuta yanapatikana kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Getere. Tunaendelea na Mheshimiwa Haji Mlenge, Mheshimiwa Stella Fiyao ajiandae na Mheshimiwa Abdallah Chikota pamoja na Mheshimiwa Patrick Alois Ndakidemi.

**MHE. HAJI MAKAME MLENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuweza kupata fursa nikawa miongoni mwa wachangiaji wa Wizara hii ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kuniwezesha kufika hapa nikiwa katika hali ya uzima na pili niweze kuishukuru Serikali kwa kuweza

kufanya kazi zake vizuri na baadaye kuweza kupata tija. Wizara hii inakazi kubwa ambayo inaifanya nchi hii iweze kutimiza yale malengo yake, ambayo yamejiwekea kwenye Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya nchi. Niseme kwamba nchi hii kwanza niwape shukurani kwa kuwezesha kuyatimiza yale ambayo wameahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja hapa Waziri wa Nishati alizungumzia kuhusu vinasaba kusema suala hili analihamisha kwa mwekezaji mmoja tu na baadaye kulipeleka kwa Serikali kwamba hili suala limeweza kutimia. Lakini pia kusema kwamba yale ambayo tulikuwa tunafanya uchunguzi wa magari *(inspection)* ambayo tulikuwa tunafanya nje leo tunaifanya hapa.

Mimi kwangu niseme hilo ni jambo jema kwa sababu Watanzania wengi wataweza kupata ajira. Ushauri wangu tu hapa niseme kwamba Wizara iweze kusimamia Watanzania wale wasije wakapata hasara kwa sababu ya kuweza kuleta kufanya uchunguzi katika nchi yao. Iwe ni tija lakini pia waweze kusomeshwa, kutolewe elimu watu waweze kupata elimu na wajue nini kinaweza kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niondoke hapo nije kwenye mfumo wa ukusanyaji kodi kwa njia ya *electronic - ETS* ambayo mwenzangu ameshaizungumza kwa hiyo, sitakaa sana kulizungumzia suala hili. Lakini tu niseme kwamba Wizara iweze kukaa na kujadili upya kuliangalia suala hili kwa kina kwa sababu wenye Viwanda ni suala ambalo wanalilalamikia na kama kitu kinalalamikiwa ni vizuri kikaangaiiwa tija inapatikana vipi? Hasa kwa sababu fedha zake ni za kigeni lakini pia fedha zile hazizunguki ndani ya Tanzania. Kwa hiyo, ningeomba Wizara wakaweza kuliangalia suala hili kwa umakini mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende tu pale ambapo hasa nimekusudia kusema maneno yangu leo hii. Niseme kwamba twende kuboresha huduma kwa sababu naamini huduma ni njia moja ya kuweza kufanikisha yale malengo yetu ambayo tumejiwekea. Huduma itakapokuwa haifikii

pale ambapo tunapataka kwa hivyo, hii mipango yetu tunaweza tusifikie katika malengo ambayo tumejiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema kwamba tuweze kwenda kuboresha huduma; kwa sababu Wizara hii ya Viwanda na Biashara ndio ambayo inaweza kuangalia namna nzuri ya kuweza kuendeleza viwanda, lakini wakishaangalia namna hiyo nzuri ya kuweza kuendeleza viwanda wanaoshughulikia ni wengi. Kwa hiyo, ningemshauri Mheshimiwa Waziri kwamba wakae wadau wote ambao wataweza kuifanya biashara iende vizuri. Kwa mfano, hapo nyuma nilikuwa nikikaa kwenye *tv* namuona tu pengine Waziri kutoka Mazingira anaenda kufunga kiwanda, hii hapa tutakuwa hatuna huduma bora, ni vizuri tukafanya pale tukakaa pamoja na Wizara zote zinazohusika katika kuendeleza masuala ya kibiashara, ili tuweze kufika katika yale malengo ambayo tumekusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kwa mfano *TRA* katika safari zetu ambazo tumepita, mimi ni mmoja ya Wajumbe kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara. Katika safari zetu tulikopita, kila mahali ukikutana na wafanyabiashara, ukikutana na wenye viwanda wanailalamikia *TRA*. Mwenzangu amesema hawa *TRA* ni nani, lakini katika sehemu moja tu ndipo ambapo tumefika pale watu wakaizungumza vizuri *TRA.* Lakini ukija ukimuangalia yule ambaye amezungumza vizuri *TRA,* amezungumza kwamba ameanza kwa Katibu Mkuu, akaja kwa Kamishna baadaye watendaji wakapewa maelekezo mahsusi, lakini wenyewe hawawezi kufanya kazi ile kuonesha namna ya huduma bora. Na tukikosa huduma bora hatuwezi kufanya biashara ile ambayo tumeilenga katika Mpango wetu wa Tatu wa Maendeleo. Kwa hiyo, niseme twende kuboresha huduma ili huduma yetu iwe bora zaidi, sasa hivi iko bora lakini iwe bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la *VAT;* nalo limekuwa ni kikwazo kwa wafanyabiashara na wenye viwanda kwa sababu tunawacheleweshea kurejesha fedha zao ambazo fedha hizi ziko kisheria. Lakini kuchelewa

kurejesha fedha zao maana yake unaenda kuwakwamisha na unapowakwamisha wafanyabiashara, unapowakwamisha wenye viwanda maana yake unawakwamisha Watanzania. Kwa hiyo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. HAJI MAKAME MLENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tukaliangalia vizuri...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. HAJI MAKAME MLENGE:** Mheshimiwa Mwenyekit, naomba dakika moja kuweza kuhitimisha suala langu.

**MWENYEKITI:** Malizia tu sentensi yako.

**MHE. HAJI MAKAME MLENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante niondoke hapo, niseme tu ushauri wangu...

**MWENYEKITI:** Usiondoke yaani wewe malizia sentensi yako.

**MHE. HAJI MAKAME MLENGE:** Ushauri wangu kwenye hili, ushauri wangu wale wenye viwanda pamoja na Serikali kufanya kiurafiki zaidi kwa sababu inaonekana kwamba mfanyabiashara anavutia kwake, Serikali inavutia kwake, maana yake hapa hatuwezi tukaenda tukatengeneza nchi ya viwanda. Ili tutengeneze nchi ya viwanda wafanyabiashara waone kama kulipa kodi ni haki yao ya kimsingi, lakini Serikali kukaa na wafanyabiashara na wakaona kwamba wafanyabiashara tunafikisha pale malengo ambayo Serikali inaitaka hili ni jambo zuri. Kwa hivyo, ningeliomba Serikali yangu ikaifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Haji nakushukuru. Mheshimiwa Stella Fiyao.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Nashukuru sana kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika wizara muhimu ya Viwanda na Biashara na niseme tu wizara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kwa kuanza na Ripoti ya Benki ya Dunia iliyotolewa mwaka 2020 ambayo ripoti hiyo imeitaja Tanzania kuwa imeshika nafasi ya 141 kati ya nchi 190 kwa urahisi wa kufanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka sita mfululizo sasa Tanzania imeweza kushika nafasi mbalimbali kama ifuatavyo ambavyo nitakwenda kuzitaja. Kwa mwaka 2015 Tanzania iliweza kushika nafasi ya 131 kati ya nchi 190; lakini kwa mwaka 2016 Tanzania imeweza kushika nafasi ya 139 kati ya nchi 190; kwa mwaka 2017 Tanzania ilifika nafasi ya 132 kati ya nchi 190; kwa mwaka 2018 Tanzania imeweza kushika nafasi ya 137 kati ya nchi 190; kwa mwaka 2019 imeshika nafasi ya 144 kati ya nchi 190 na kwa mwaka 2020 Tanzania imeweza kushika nafasi ya 141 kati ya nchi 190. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja nafasi hizo ambazo Tanzania imeshika lakini bado hatujafikia lengo la Tanzania kushika nafasi ya tarakimu mbili. maana yake lengo letu tulikuwa tushike walau kutoka 99 kushuka chini mpaka moja, lakini hatujaweza kufikia lengo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini hatujaweza kufikia lengo hili? Hii yote inatokana na mazingira magumu yaliyojitokeza ndani ya miaka mitano ya wafanyabiashara wetu kufanya biashara. Ndani ya miaka mitano wafanyabiashara wamefanyabiashara kabika mazingira magumu sana na mazingira hayo yamepelekea wengi kufunga biashara zao. Lakini hata wengine waliotamani kufungua biashara wameshindwa kufungua bisahara kutokana na masharti magumu yaliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hiyo imeathiri sana, ninaweza kuzungumzia hasa wa mikoa iliyoko mpakani. Mimi ninatokea Mkoa wa Songwe ambao uko mpakani mwa Tanzania na Zambia. Ukifika pale Tunduma ni mpakani, sasa hivi asilimia kubwa wamefunga maduka yao kutokana na changamoto kubwa ya biashara. Na hii yote inatokana na mlundikano mkubwa wa kodi ambao wafanyabiashara wengi wameshindwa kuumudu badala yake wamekimbia na kwenda kuwekeza kwenye nchi jirani ya Zambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukienda upande wa Zambia, asilimia 60 ya wafanyabiashara wakubwa walioko Zambia ni Watanzania. Ukienda jioni pale Nakonde, Black maduka makubwa yote yanamilikiwa na Watanzania na Watanzania wamekwenda kuwekeza kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna sababu ya kufanya mabadiliko sana na siku zote nimeendelea kusema kinachopelekea yote hayo ni mlundikano mkubwa wa kodi, tuna sababu kubwa sana na siku zote tumeendelea kusema kufanya marekebisho ya kodi, ya Sheria za Kodi. Marekebisho hayo tukiyafanya wafanya biashara wetu wataweza kufanya biashara kwa uhuru. Sasa hivi tunapata faida gani kama Watanzania wanakwenda kuwekeza nchi jirani, lakini huduma zote wanakuja kuzipata Tanzania. Tukizungumzia barabara wanakuja kunufaika Tanzania, tukizungumzia maji, afya wanakuja kunufaika Tanzania, lakini wakati huo wamekwenda kuwekeza katika nchi jirani ambapo Tanzania hatupati faida yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Zambia kule mfanyabiashara ataulipia mzigo wake wakati wa kuujumua. Atafanya biashara kwa uhuru hata bughudhiwa na jambo lolote, lakini ukija Tanzania mlundikano wa kodi unawakimbiza wafanyabiashara wetu. Siwezi kutaja kodi moja moja, lakini nitasema tu kwa ufupi. Ukija Tanzania mfanyabiashara ili afanye biashara yake kwanza jambo la kwanza atatakiwa kuisajili biashara yake, na kwenye suala zima la kuisajili biashara sio bure, kunatakiwa fedha. Akishaisajili anatakiwa kulipia kodi *TRA*, huyo huyo mfanyabiashara mmoja. Lakini

baada ya hapo kuna kodi ya zuio anatakiwa kuilipia huyu huyu mfanyabiashara. Baada ya hapo ya kodi ya zuio, kuna kodi nyingine nyingi ambazo zingine ni kodi yaani anatoa kodi kadri anavyopata wateja anatakiwa kulipia kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna gharama za *OSHA* huyu huyu mfanyabiashara anatakiwa kulipia; kuna leseni za biashara kwenye Manispaa na Halmashauri zetu huyu mfanyabisahara anatakiwa kulipia; kuna Zimamoto kuna mambo mengi ya kodi mlundikano umekuwa ni mkubwa wa kodi na mlundikano huu unasababisha wafanyabiashara wetu wanashindwa kuwekeza kwenye Taifa letu na badala yake wanakwenda kuwekeza kwenye mataifa jirani. Ni dhahiri kwamba hata mataifa yetu jirani na yenyewe kwenye ushindani wa kibiashara. Kwa hiyo, yanatafuta kila njia kuhakikisha kwamba yanawashawishi Watanzania kwenda kuwekeza huko kwao, tuna sababu ya kufanya marekebisho ya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukienda kununua *tv* ya shilingi 500,000 ukimuomba mwenye duka akupunguzie anakuambia wazi kabisa bei yangu halisi ni shilingi 425,000, ukitaka nikuuzie 425,000 sitakupa *receipt*. Maana yake hapo kodi katika hiyo *tv* moja ya shilingi 500,000 ni shilingi 75,000.

Sasa Mtanzania yupi ambaye atakubali kutoa shilingi 500,000 asikubali kutoa shilingi 425,000 kwa hiyo watu wanakubali kununua vitu bila *receipt* ili kukwepa hiyo shilingi 75,000 kwasababu anajua itamsaidia katika masuala mengine. Na badala yake tumeendelea kuzikosa hizo kodi. Ni lazima tukubali kufanya marekebisho ya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumzie wawekezaji, wawekezaji wanapokuja kuwekeza kwenye Taifa letu kumekuwa na mzunguko mkubwa sana na usumbufu mkubwa wao kupatiwa vibali vya uwekezaji na nafasi hiyo imepelekea wengine kukata tamaa, mwekezaji anafuatilia kibali mpaka miaka miwili, mitatu anaendelea kufuatilia kibali cha uwekezaji, mwisho wa siku anaamua

kukata tamaa anakwenda kuwekeza kwenye mataifa mengine ambapo anaona kuna uwalau hakuna usumbufu. Lakini usumbufu huu umesababisha mianya ya rushwa, badala yake kumekuwa na mianya mikubwa ya rushwa mtu anajikuta mpaka anapatia hicho kibali lazima atoe rushwa. Sasa tunajitengenezea sisi wenyewe mianya ya rushwa kwa wawekezaji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la viwanda. Katika suala zima la viwanda *NSSSF* waliamua sijui nizungumzieje hapa, yaani Mifuko ya Hifadhi ya Jamii waliamua kujiwekeza katika suala zima la ufufuaji wa viwanda. Na waliweza kutoa takribani shilingi bilioni 339 kwa ajili ya kufufua viwanda 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua, Serikali ina mkakati gani ama imeweka malengo gani kuhakikisha fedha hizi zinarudi ili kutokuwatesa wastaafu wetu. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anakuja atuambie jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo mwisho ni suala la teknolojia. Ninaamini kabisa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia maana yake kengele imeshapiga malizia sentensi yako.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aaah, ni refu sana. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Abdallah Chikota baadaye Mheshimiwa Patrick Alois ajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niungane na wenzangu kwa kukupongeza kuteuliwa tena kuwa

mwenyekiti na hatuna mashaka na wewe, tunaomba Mwenyezi Mungu akupe afya njema na hekima ili uendelee ku-*chair* katika kiti chako hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia nimpongeza Mheshimiwa Waziri Profesa Kitila Mkumbo kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na Naibu wake, lakini pia na watendaji wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Dotto James pamoja na Wakurugenzi wa taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mchango wangu utaanza na kujikita na jinsi tunavyoshughulikia matatizo ya wawekezaji na kipekee nichukue nafasi hii kukushukuru na kukupongeza Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo jinsi ulivyoshughulikia mgogoro wa kiwanda cha Dangote, hongera sana. Umechukua hatua za haraka, umefika *site,* ndugu zangu Dangote ni taasisi kubwa, isingefaa kwa kipindi kirefu iendelee kuachwa vilevile mgogoro unaendelea wakati Dangote ni taasisi kubwa, wakati mgogoro ule unaendelea hapa Tanzania, *delegation* ya Benki ya Dunia ilitoka Washington kwenda kuonana na Dangote kule Nigeria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu huku tuone jinsi ukubwa wa taasisi ya Dangote. Kwa hiyo anapopatwa na tatizo naomba tulikimbilie kama ulivyofanya Mheshimiwa Waziri na uendelee kusikiliza matatizo ya kiwanda kile, kwa sababu kiwanda kile kuna ajira rasmi kwa Watanzania zaidi ya 500. Lakini kuna ajira zisizo rasmi zaidi ya 2,000, lakini kuna *fleet* ya magari pale zaidi ya 1,000. Sasa fanya lori moja lina wafanyakazi wawili ina maana kuna ajira 2,000 pale zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hivyo tu, kwamba kwa sisi Wana Mtwara kuna vijana wetu wengi, kuna akina mama, wanapata ajira pale na wanapata mkate wao wa kila siku kutoka katika kiwanda cha Dangote. Mheshimiwa Waziri, pale bado kiwandani kuna changamoto nyingi na naomba utenge muda mkawasikilize. Mimi nitazitaja chache tu, changamoto ya kwanza ni bei ambayo *TPDC* wanaiuzia

Dangote ile gesi asilia. Lakini vilevile kuna changamoto ya meli kwa sababu wana mpango wa kusafirisha saruji sasa kwa kutumia Bandari yetu ya Mtwara, kwa hiyo, tuwasikilize kwa hilo, lakini kuna gharama za bandarini nazo tuziangalie vilevile ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Tume ya Madini sasa hivi imekuja na hoja nyingine kwamba wana-*categorize* Kiwanda cha Dangote kama *mining company* na kutaka kodi nyingi walipe. Kwa hiyo, nalo Mheshimiwa Waziri ukalifanyie kazi. *(Makofi)*

Suala la pili, ni kuhusu soko la korosho, Mheshimiwa Waziri naipongeza Serikali kwa jinsi inavyochukulia kwa unyeti suala la korosho, lakini naomba iongeze nguvu zaidi. Itafute masoko mapya ya korosho. Tusiende na India kila mwaka, twende na masoko mapya na yapo mengi Vietnam, Japan na maeneo mengine.

Kwa hiyo, naomba sana kwamba tutumie taasisi yetu ya *TMX* ili kuhakikisha tunawapata wanunuzi wapya wa korosho, lakini vilevile tuhakikishe sasa kwamba korosho ambazo zinatoka mipakani kwa mfano kule kwetu mpaka wa Msumbuji Jimbo la Cabo Delgado wanaleta korosho zao Tanzania. Lakini mwaka juzi ilitokea sintofahamu tukazuia korosho zile zisiiingie kwamba ni chafu. Korosho za Jimbo la Cabo Delgado zina ubora kama korosho za Mtwara. Kama kahawa yetu inaingia Uganda kwa nini tusiruhusu korosho za Msumbiji ziingie kwetu.

Kwa hiyo, naomba zile korosho za Msumbiji ziingie ili ziongeze uzalishaji wetu kwa sababu Kaskazini mwa Msumbuji yanayoendelea mnayafahamu na wenzetu kule hakuna soko rasmi kama lilivyo sisi la korosho kwetu. Mheshimiwa Waziri ruhusu korosho kutoka Msumbiji ziingie nchini bila ya kuwa na vikwazo vyovyote kwa sababu wafanya biashara wetu wadogo wanafanya biashara hiyo lakini wakulima wa Msumbiji wanaingiza korosho kusiwe na vikwazo ambavyo sivyo vya lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, niungane na wenzangu kuzungumzia Mradi wa Mchuchuma na Liganga. Ni mradi wa muda mrefu, basi sasa hivi utekelezwe na ukitekelezwa mradi huu tunatimiza ile dhana ya *Mtwara corridor. (Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Profesa Patrick A. Ndakidemi, baadaye Mheshimiwa Priscus Tarimo ajiandae.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, na mimi nianze kumpongeza sana Waziri wa Viwanda na Biashara pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kuwasilisha hotuba zao za bajeti na ile ya Kamati ya Kudumu ya Bunge vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita kwenye kuangalia mchango wa Mkoa wa Kilimanjaro kwenye sekta ya viwanda na biashara. Historia inaonesha kwamba Mkoa wa Kilimanjaro kwa muda mrefu umekuwa na historia ya kuwa na viwanda vikubwa ambavyo vimeshachangia sana kwenye kulipatia Taifa letu kipato kikubwa na mkoa wetu pamoja na watu ajira za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Moshi Vijijini kiwanda ambacho kinafanya kazi vizuri sana sasa hivi ni kiwanda cha *TPC* ambacho kinaajiri watu kwa wingi sana na kinachangia kikamilifu kwenye pato la Mkoa wa Kilimanjaro na Taifa kwa ujumla. Kuna viwanda ambavyo vimefungwa havifanyi kazi na viwanda hivi ambavyo vimefungwa vimeshasababisha matatizo makubwa sana

kwenye mkoa wetu wa Kilimanjaro kiuchumi na kijamii kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, orodha ya viwanda ambavyo vimefungwa kule Kilimanjaro na vimetuletea matatizo makubwa sana ni kama ifuatavyo; kiwanda cha kwanza ni kiwanda ambacho kiko jimboni kwangu, Kiwanda cha Kukoboa Mpunga kilichoko Kijiji cha Chekereni, Kata ya Mabogini; hiki ni kiwanda cha kukoboa Mpunga. Kiwanda cha pili, ambacho kipo jimboni kwangu ni kiwanda cha viatu cha Uru Kaskazini kinaitwa Kiwanda cha Viatu cha Msuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vingine ambavyo ni vya *Moshi DC* vya jirani yangu ni *Kibo Match Corporation Limited*, kiwanda cha kutengeneza viberiti; kuna *Kiliwood Product* ambacho hata Mheshimiwa Musukuma amekitaja, kuna *Kibo Papers Limited*, kuna Kiwanda cha Maguni Moshi, kuna Kiwanda cha *Twiga Chemicals* ambacho kinazalisha bidhaa za kilimo na vipo vingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya viwanda hivi kufa, mimi niseme tu sababu zingine ni za ajabu ajabu na sikubaliani nazo sana. Mojawapo ni kwamba wawekezaji ambao walipewa viwanda hivi hawakuwa na nia thabiti ya kuviendeleza hivi viwanda kwa maana nyingine hawakuweza kwenye kuendeleza hivi viwanda. Sababu ya pili ni kwamba teknolojia zimebadilika na hao wenye hivi viwanda hawakuwekeza kwenye teknolojia mpya na sababu ya tatu, ambayo ninayoomba Serikali iliangalie hili, ni kuruhusu bidhaa za nje. Nitatoa mfano, Kiwanda cha Magunia kilishindwa kuzalisha kwasababu Serikali iliruhusu kuingiza *jute bags* ambazo zilikuwa na bei rahisi na yule mtu wa magunia akashindwa kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na viwanda hivi kufa, niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano na ya Sita kwa juhudi kubwa ya kuanzisha tena upya viwanda kule Kilimanjaro. Kuanzia mwezi Disemba, 2017 mpaka mwezi Machi, 2020 Mkoa wa Kilimanjaro ulikuwa na viwanda 113

vipya ambavyo vilianzishwa kwa juhudi ya Serikali. Katika viwanda hivi, viwanda 80 vilikuwa viwanda vidogo sana, viwanda 26 vilikuwa viwanda vidogo, viwanda vinne vilikuwa vya kati na viwanda vitatu vilikuwa ni viwanda vikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa viwanda, ninaushauri kwa Serikali kwamba kwanza kabisa tufufue tuwe na programu maalum ya kufufua viwanda ambavyo nitavielezea hapa chini kwasababu vinatija kubwa sana kwa mkoa wetu wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naiomba Serikali ihamasishe wawekezaji hasa wazawa wa Kilimanjaro najua mko huko mliko, rudini nyumbani mje tuijenge Kilimanjaro yetu, tuweke viwanda ili hadhi ya mkoa wetu iwe kama zamani. Nasema haya kwa sababu Mkoa wa Kilimanjaro kuna miundombinu rafiki sana ya kufanya biashara na kuwekeza viwanda. Viwanda muhimu vyenye tija ambavyo vimeshafungwa ni kama vifuatavyo; cha kwanza, kinaitwa Kiwanda cha Kukoboa Mpunga cha Kilimanjaro ambacho kipo Mabogini. Kiwanda hiki Serikali iliwapa *KNCU* (Chama cha Wakulima wa Kahawa) nafikiri hapa kulikuwa na kosa kidogo badala ya kuwapa *CHAWAMPU* (Chama cha Wakulima wa Mpunga) kule Mabogini ili wakiendeshe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuanzia Septemba, 2014 kiwanda hiki hakijawahi kufanya kazi. Mimi naishauri Serikali nakuomba waziri kwasababu kiwanda kimesharudishwa Serikalini kupitia kwa Msajili wa Hazina naomba ikiwezekana tuwape *CHAWAMPU* wale watu wa Mabogini ndio wanaolima mpunga tuwawezeshe ili waweze kuendesha kiwanda chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha pili, Kiwanda cha Viatu Msuni, hiki pia kipo jimboni kwangu na kinamilikiwa na Kata ya Uru Kaskazini, kilifunguliwa miaka ya 1970 na Baba yetu wa Taifa Mwalimu Nyerere kwa sasa kimekufa. Tunaiomba Serikali, Mheshimiwa Waziri upeleke wataalam wa

*TRDO* pale wakawape utaalam namna ya kufufua hiki kiwanda ili tuunge juhudi za hawa watu wanaokimiliki. Ni kata tu inamiliki hiki kiwanda. Tunaomba sana, tuwaunge mkono wana Kata ya Uru Kaskazini ili kiwanda hiki kifufuliwe.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kingine ni Kiwanda cha Magunia ambacho kipo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Patrick, muda wako umeisha.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi baada ya kusema hayo nimeshayapeleka kwa maandishi naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kutokana na muda, mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Priscus Tarimo, baadaye Naibu Waziri atafuatiwa na Waziri mwenyewe kwa ajili ya ku-*wind up.* Karibu Mheshimiwa Priscus.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa nafasi ya kuweza kuchangia lakini pia nianze kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa uwasilishaji mzuri na uandaaji mzuri wa bajeti ya Wizara yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaenda haraka haraka ili niweze kuongelea mambo mengi zaidi. Nianze kwa kuunganishwa kwa *TBS* na *TFDA* pamoja na marekebisho ambayo yametajwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwenye ukurasa wa 18. Nia ya kuunganisha taasisi hizi za *TBS* na *TFDA* ilikuwa nzuri sana ili kuboresha utendaji. Lakini badala yake imeleta vikwazo, shida katika utendaji. *TBS* sasa imekuwa ndiyo mamlaka ya ku-*standardize* na ku-*regulate* majukumu ambayo kikawaida yasingetakiwa yafanyike na taasisi moja.

Badala yake sasa kumesababisha kuwepo kwa bidhaa *fake* sokoni, hasa bidhaa zinazotoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaweza kutoa mfano; kwa mfano, maziwa ya watoto wachanga, sheria inasema yale ambayo yameshakubaliwa sasa ambayo yamepiwa yanaonekana yana vigezo yawe na maelezo kwa Kiswahili kwa maana ya kwamba *ingredients* na vitu kama hivyo. Lakini sasa hivi ukitoka tu hapo nje ukienda *supermarket* yamejaa maziwa ambayo hayana vigezo na yapo sokoni.

Kwa hiyo, *TBS* ilipounganishwa na *TFDA,* badala ya kuleta kheri imeleta tatizo. Ni vizuri sheria ile iliyopitishwa basi iweze kutofautisha majukumu ndani ya *TBS* kwamba yale ya ku-*standardize* yasimamiwaje na haya ya ku-*regulate* yaweje kwa sababu ya kuiunganisha...

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Neema.

**T A A R I F A**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, ningependa kumpa Taarifa mzungumzaji hiki anachokisema cha jukumu la kuangalia ubora na usalama wa chakula ilivyoondolewa kutoka *TFDA* kwenda *TBS* inahatarisha sana maisha ya Watanzania. Unakuta wengi wetu tunanunua labda boksi ya *juice* ya machungwa tukijua kwamba lile ni chungwa halisi, lakini kihalisia ndani yake kunakuwa na *concentrate,* ladha na rangi. Kitu ambacho ni hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kumpa taarifa kwamba *TBS* na Wizara lazima iangalie namna gani ya kuandaa kanuni zitakazomlinda mlaji na kutoendelea kuweka maisha ya Mtanzania rehani. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea na ni ufafanuzi mzuri wa hiki nilichokuwa nasema kwamba haya majukumu yalivyopelekwa pamoja yameleta matatizo badala ya kuleta heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye viwanda. Wakati viwanda, hasa vile vilivyokuwa vinamilikiwa na Serikali vinabinafsishwa kulikuwa kuna taasisi mbili zinahusika; viwanda vilivyopitishwa kwenye *LAT* na vile vilivyopitishwa kwenye *PSRC.* Vile vilivyopitishwa kwenye *LAT* ni vile ambavyo vilikuwa *liquidated.* Yaani vilikuwa vinauzwa, na ile ilikuwa ni *discretion* ya mnunuaji afanye nini. Lakini vile vilivyopitishwa *PSCR* ilikuwa ili viweze kuboreshwa, viongezewe mtaji, teknolojia, vitoe ajira na vilipe kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Moshi Mjini vipo viwanda vingi amevitaja Mheshimiwa Ndakidemi sasa hivi. Kiwanda cha *Kibo Match, Kibo Paper* na viwanda vingine. Vile vilibinafsishwa ili viendelezwe, lakini vimefungwa havifanyi chochote. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ahsante.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata dakika tano bado.

**MWENYEKITI:** Zimeisha, kengele ya pili imelia. Naomba sasa nimkaribishe...

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Viwanda na Biashara na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kuwasilisha vizuri hotuba ya bajeti na ripoti ya Kamati. Pia niwapongeze sana wataalamu na wadau kwa kazi kubwa wanazofanya kwenye kuipeleka nchi yetu kwenye Tanzania ya viwanda, ndoto iloyobebwa kikamilifu na Serikali ya Awamu ya Tano na Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkoa wa Kilimanjaro ulikuwa una historia ya kuwa na viwanda vingi ambavyo vilichangia sana kwenye ajira na mapato ya mkoa na Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vingi vya zamani vilivyokuwa na majina makubwa kimkoa na kitaifa kwa sasa vimefungwa. Baadhi ya viwanda maarufu ambavyo havifanyi kazi ni *Kilimanjaro Machine Tools Manufacturers Ltd., Twiga Chemicals Ltd.* cha kuzalisha madawa ya kilimo, *Kiliwood Products Ltd.* cha kuzalisha bidhaa za mbao, *Kibo Paper Ltd*. cha kuzalisha karatasi, *Tanzania Packaging Manufacturers (1998) Ltd.* cha kuzalisha magunia, Kiwanda cha Viatu Msuni kilichofunguliwa miaka ya 1970 na Baba wa Taifa, *Kibo Match Ltd.* cha viberiti na *Kilimanjaro Paddy Hulling Co. Ltd.* cha kukoboa mpunga kilichopo Chekereni, Kata ya Mabogini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufa kwa viwanda hivi kwa kiasi kikubwa kumesababishwa na baadhi ya wawekezaji kutokuwa na nia thabiti ya kuviendeleza, kubadilika kwa teknolojia za uzalishaji na ushindani wa bidhaa kutoka nje kama vile mifuko ya *jute* iliyoua soko la magunia ya katani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vipya mkoani Kilimanjaro kama ilivyo kwenye mikoa mingine hapa Tanzania. Kuanzia Disemba, 2017 hadi kufikia Machi, 2020 mkoa wa Kilimanjaro ulikuwa na viwanda vipya 113; kati ya hivi, viwanda 80 ni vidogo sana, viwanda 26 ni vidogo,

viwanda vinne ni vya kati, na viwanda vitatu ni vikubwa. Viwanda hivi vinachangia kikamilifu kwenye pato la mkoa na Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa viwanda katika kujenga uchumi wa nchi yetu na kutoa ajira, ninaishauri Serikali iwe na programu maalumu ya kufufua viwanda vya zamani vilivyowahi kutoa mchango mkubwa wa kiuchumi na iendelee kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vipya mkoani Kilimanjaro kwani kuna miundombinu rafiki na hii itaboresha uchumi wa mkoa na Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda muhimu vyenye tija na ninavyopendekeza vifufuliwe ni kwanza Kiwanda cha Kukoboa Mpunga cha Kilimanjaro *(Kilimanjaro Paddy Hulling Company Ltd.)* kilichopo Kata ya Mabogini. Serikali ilikabidhi kiwanda hiki kwa Chama Kikuu cha Ushirika *(KNCU)* kinachojishughulisha na biashara ya kahawa na tokea mwezi wa Septemba, 2014 kimekuwa hakifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili lilikuwa kosa kubwa sana na *KNCU,* walishindwa kukiendesha, na ulikuwepo mgogoro mkubwa sana wa umiliki wa kiwanda hicho na Umoja wa Wakulima wa Mpunga wa *CHAWAMPU* ambao ni wakereketwa wa mpunga. Msajili wa Hazina amekirudisha kiwanda hiki Serikalini toka mwezi Oktoba, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali iwasiliane na wadau mbalimbali ikiwemo *CHAWAMPU* ili apatikane mwekezaji atakayekifufua na kukiendesha kiwanda hiki kwa tija. Kiwanda hiki kimezungukwa na wakulima wa mpunga wanaozalisha mara mbili kwa mwaka.

Pili ni Kiwanda cha Viatu Msuni kilichopo Kata ya Uru Kaskazini; kiwanda hiki kinamilikiwa na Kamati ya Maendeleo Kata ya Uru Kaskazini *(WDC).* Kina uwezo wa kuzalisha bidhaa mbalimbali za ngozi. Ninaiomba Serikali itume wataalamu wa *TiRDO* kwenye kiwanda hiki ili ushauri wa kitaalamu upatikane na kiwanda hiki kifufuliwe na kuunga juhudi za wana ushirika huu kwenye kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni Kiwanda cha Magunia; kiwanda hiki kinamilikiwa na *Mohamed Enterprises Ltd.* Kiwanda hiki hakijafanya kazi toka kinunuliwe miaka 14 iliyopita (2006). Tunaishauri Serikali ifuatilie utekelezaji wa mwekezaji wa kuanzisha uzalishaji wa magunia. Ikibainika kuwa safari ya uzalishaji kama bado ni ndefu, Serikali ichukue hatua stahiki kwa manufaa ya Taifa.

Nne, ni Kiwanda cha Madawa ya Kilimo cha *Twiga Chemicals;* kiwanda hiki kinamilikiwa na *Twiga Chemicals Ltd.* na bado miundombinu yake ni mizuri. Kwa kuwa kiwanda hiki kimerudishwa Serikalini kupitia kwa Msajili wa Hazina toka Oktoba, 2018, ninaishauri Serikali iharakishe kumtafuta mwekezaji ili dawa za kilimo zizalishwe hapa nchini na kuokoa fedha zetu za kigeni ambazo hutumika kuagiza madawa ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano niKiwanda cha bidhaa za Mbao *(Kiliwood Products Ltd.);* kiwanda hiki kilikuwa kinamilikiwa na *Hans Industries* na kwa kuwa alishindwa kukifufua, kupitia kwa Msajili wa Hazina kimerudishwa Serikalini. Ninaishauri Serikali iharakishe kumtafuta mwekezeji ili uzalishaji urejee na kuliwezesha Taifa kuzalisha bidhaa za mbao na kuachana na utaratibu wa kuagiza bidhaa kutoka nje. Malighafi za mbao zinapatikana kwa wingi hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita ni *Kilimanjaro Machine Tools;* kiwanda hiki kinamilikiwa na Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC).* Kiwanda hiki kinaweza kutoa mchango mkubwa sana kwenye kuzalisha vipuri vya mashine za aina mbalimbali na kuokoa matumizi ya fedha za kigeni za kuagiza vipuri kutoka nje ya Tanzania. Ninaiomba Serikali iisaidie *NDC* kwenye kuingia ubia na wadau mbalimbali na kukifufua kiwanda hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkoa wa Kilimanjaro una fursa nyingi sana za kuanzisha viwanda vipya. Mkoa huu una fursa kubwa za kilimo cha mboga, kahawa, ndizi, mahindi, maharage, mpunga, matunda na maziwa. Bidhaa hizi

zinaweza kutumika kuanzisha viwanda vidogo vidogo na kuongeza thamani ya mazao yetu yanayozalishwa mkoani Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha hili ninaishauri Serikali ianzishe programu maalumu itakayowashirikisha wadau muhimu wa viwanda kama vile *TiRDO, SIDO, TCCIA, VETA* na *CTI* ili watoe mafunzo ya kuhamasisha ujasiriamali wa viwanda mkoani Kilimanjaro. Mkazo uwe kwenye kusindika matunda, mbogamboga, maziwa, unga wa mahindi, michele na maharage. Kuna uwezekano mkubwa sana wa kuanzisha viwanda vya usindikaji wa kahawa na kutengeneza *juice* au mivinyo ya ndizi mbivu. Serikali ikiweka mazingira wezeshi, wajasiriamali wengi wa Kitanzania watatumia fursa hii kutengeneza ajira na kuingizia mkoa na Taifa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuna umuhimu mkubwa wa Kiwanda cha Samaki kujengwa Wilayani Ukerewe ili kutumia malighafi (samaki) wanaozalishwa kwa wingi Wilayani Ukerewe. Kwa kufanya hivyo itasaidia matumizi sahihi na yenye ufanisi ya rasilimali zinazozalishwa(samaki) na itazalisha ajira kwa watu wetu na hivyo kukuza uchumi wao.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuchangia kwa maandishi ili kuweza kufafanua baadhi ya mambo kwenye mchango wangu kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *ETS;* kazi yake kubwa ni kuhesabu, viwanda vilifunga mashine hizi kwa maelekezo ya Serikali, lakini tija yake haifanani na gharama halisi pamoja na mengine mengi, lakini mkataba wa Kampuni ya SIPA haukuwa wazi sana hasa kwenye suala la bei ya uchapishaji wa *stamp* hizo. Mkataba huu ulikuwa wa miaka mitano, muda umekwisha, kuna haja sasa ya Serikali kupitia upya mkataba huo ili kuweza kuangalia upya gharama zake.

Hivi sasa kwa mfano gharama ya kuhesabu chupa moja ya *juice* ya *mls 200* ni shilingi 23, wakati Serikali kodi yake ni shilingi 1.8 tu hivyo utaona mwenye kuhesabu anapata pesa nyingi zaidi kuliko Serikali, na hii ni kuongeza tu gharama kwa wazalishaji na hatimaye bei kwa walaji, sawa na vinjwaji baridi na vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *VAT Refund;* kwa nini Serkali hairudishi kwa wawekezaji na wafanyabiashara *VAT* hasa kwenye viwanda vikubwa, hii pia inachangia sana kukwamisha mitaji na kudorora kwa uzalishaji kwenye viwanda. Serikali inadaiwa sasa walau kiasi cha shilingi bilioni 10 katika *VAT,* pia kuna suala la *industrial sugar,* karibu miaka mitano sasa pesa hiyo haijarudi na kusababisha viwanda vingi kuendelea kukosa *operating capital,* kwa mfano viwanda vya vinywaji baridi, CocaCola na Pepsi, Serikali ibadilishe utaratibu wa kushikilia pesa hi kwa sababu imekuwa mziogo mkubwa sana kwa wenye viwanda.

Kuhusu suala la unyaufu; Serikali kupitia Wizara itoe msimamo ili kuondoa athari zinazoweza kujitokeza wakati wa msimu wa ununuzi wa korosho. Unyaufu umekuwa ni tatizo kubwa na bado mpaka sasa Serikali haijawa na msimamo wa pamoja kuhusu suala hili, mwaka jana wafanyabiashara wa maghala wamepata hasara kwenye uendeshaji wa maghala kwa sababu Serikali imechukua pesa toka kwa wafanyabiashara hao na kuwa hasara kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Liganga na Mchuchuma inafaa kuwekewa nguvu zaidi ili kuweza kuendeleza migodi hiyo, pia lazima kuwa na mfumo ulio wazi kwenye jambo hili, lazima sasa Liganga na Mchuchuma zianze uzalishaji ili kuchangamsha uchumi wa Ukanda wa Kusini Bandari ya Mtwara na reli ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu biashara ya korosho; katika Ilani ya CCM 2020 - 2025 kuhusu eneo la viawanda vya korosho, ibara ya 34 sehemu ya (c) iliahidi kuanzisha *Cooperative Seed Fund,* huu ni mfano wa *REA,* Mfuko wa Maji na *Road Fund,* kwenye mpango huu CCM ilidhamiria

pamoja na mambo mengine kuanzisha viwanda 33 vya kubangua korosho, pamoja na kufufua viwanda vingine vilivyokufa na kufanya ubanguaji kufikia asilimia 50, tani 550,000 kufikia mwaka 2025, vipi bajeti ya Wizara hii imeweza kujibu hii ilani na mkakati uliopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri sasa jambo hili liwe katika utekelezaji, kuna hasara kubwa sana inapatikana kwenye korosho, hadi sasa korosho ghafi na mazao yake yanauzwa ni pamoja na ajira, nchi inapata hasara kubwa sana, maganda ya korosho ni uchumi, sawa na mabibo, kochoko ndiko ambako *wine* na mvinyo zinakotokea, kwa mfano Scotland ambako ndiko unakotengenezwa mvinyo wa Scotish Whiscky, wanaliingizia Taifa lao Euro bilioni 4.5 kwa mwaka jana peke yake. Wizara ione namna ya kushirikiana na Wizara ya Katiba na kuamua kubadilisha Sheria ya Vileo *(Liquer and Intoxication Act* ya 1978) ili wananchi sasa waweze kuzalisha gongo kitaalamu na kuweza kujipatia pesa za kigeni lakini pia ni sehemu ya uchumi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vyetu vinashindwa kwenda kwa faida kwa kuwa na mamlaka nyingi za usimamizi zinazofanya kazi zinazofanana kama vile *OSHA, TBS, TFDA NEMC* na zingine mfano wa hizi. Kwa nini mamlaka hizi zisiunganishwe zikafanya kazi chini ya taasisi moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji Serikali yote iongee kwa pamoja kwani ni Serikali ni moja, mfano kuna mazao ya kimkakati, je, vipo viwanda vya kimkakati vinavyokwenda sambamba na mazao hayo ya kimkakati?

Je, Wizara ya Miundombinu inayo miundombinu inayolingana na viwanda, au mazao hayo ya kimkakati, miundombinu ya barabara, bandari na uchukuzi kwa ujumla wake? Je, ni rafiki sawa na mikakati ya Wizara ya Viwanda? Je, Wizara ya Mazingira nayo inaitambua mikakati ya Wizara ya Viwanda na Biashara, kwani kwa uzoefu unaonesha

Wizara ya Mazingira inaongoza kukwamisha uwekezaji nchini kwa hoja ya uharibifu wa mazingira.

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mchuchuma na Liganga; je, Mradi wa Mchuchuma na Liganga utaanza lini? Mbona umetengewa fedha chache sana Mchuchuma na Liganga.

Kuhusu diplomasia ya uchumi *(economic diplomacy)* taarifa mbalimbali za biashara na viwanda ziende katika Balozi zetu ili waweze kuwajibu haraka wawekezaji huko huko Ubalozini.

Katika Balozi zetu tupeleke *trade attaches* na tuwape *link* kila Balozi ili wawasiliane na Wizara ya Viwanda kupata taarifa muhimu kwa ajili ya masoko ya korosho, chai, pamba parachichi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, parachichi Njombe; parachichi inahitaji muuzaji wa kuuza nje aje na *accreditation registration* na *registration* hii hufanyika kwa gharama kubwa sana. Wizara ina mpango gani wa kusaidia wakulima wa Njombe wa zao la parachichi.

Kuhusu mahindi; zao la mahindi Wizara iweke mkakati wa masoko ya uhakika, hivi sasa bei ya mahindi kwa debe ni shilingi 4000; pembejeo ni gharama sana, Wizara isaidie bei ya mbolea na pembejeo ishuke.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza hotuba nzuri ya Waziri wa Viwanda na Biashara, nampongeza yeye mwenyewe Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na uongozi mzima wa Wizara kwa kazi nzuri na ubunifu katika kutekeleza Sera na Ilani ya chama tawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosikitisha sana ni Wizara hii inayobeba dira ya Taifa letu kwa sehemu kubwa

kutokupewa kipaumbele cha kufikishiwa fedha zilizoidhinishwa kwenye bajeti ya maendeleo. Kwa mwaka 2020/2021 ilipata chini ya asilimia 50 ya bajeti na hivyo kushindwa kutekeleza miradi ambayo ingewezesha kujenga misingi bora ya kuwezesha wananchi wajasiriamali kuanzisha shughuli za uzalishaji na kutengeneza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa majengo/mabanda ya kuwapangishia wajasiriamali wadogo wadogo na wa kati ni falsafa nzuri kwani inawezesha pia kuwafikishia wajasiriamali hawa huduma na mafunzo mbalimbali, na pia kuwasimamia wale wanaopewa mikopo na *SIDO* kutumia mikopo hiyo vizuri. *This be* Serikali ikubali kutenga fedha nyingi zaidi kwa utekelezaji wa mkakati huu na kwa Mfuko *SIDO* wa kuwezesha wajasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika ya *TIRDO, CAMARTEC, TEMDO* yanafanya ubunifu mzuri na unaozingatia uwezekano wa kupeleka kwenye soko letu teknolojia sahihi kwa mazingira yetu na kwa bei nafuu. Hata hivyo taasisi hizi hazipati bajeti za kutosha kujitangaza na kupeleka taarifa sokoni kwa walengwa ili wazijue na wazinunue. Kwa namna hii zinapoteza tija. Wapewe rasilimali fedha na watu wa kueneza kile walichobuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mashirika mengi yaliyo chini ya Wizara hii hayana bodi. Hii inapunguza kiwango cha utawala bora. Tuiombe mamlaka husika ifanye uteuzi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa *blueprints* unastahili kuongozwa na Wizara hii licha ya kwamba Wizara nyingine zina maeneo yao. *Blueprint* inatekelezwa kwa kasi ndogo, lakini kuna haja ya kufanya tathmini mpya kuhusu kero mpya zilizoibuka kwa wafanyabiashara na wawekezaji. Kero zilizoorodheshwa miaka mitatu iliyopita zimepitwa na uhalisia wa sasa.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia maandiko nichangie bajeti ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nibainishe kwanza muhimu ya kuzingatia kwanza tunao mpango wa muda mrefu wa kufufua viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo havifanyi kazi vizuri au vimekufa kabisa. Naomba na kushauri Serikali ifanye tathimini ni kiwanda gani kinaweza kufufuka na kuzalisha kwa tija kubwa. Viwanda ambavyo haviwezi kufufuka tuachane navyo au maeneo hayo kama yana miundombinu wezeshi na saidizi basi maeneo hayo yatumike kwa viwanda vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijikite katika kujenga uchumi shindani kwa kutanguliza lengo kuu ikiwa ni kutengeneza ajira, ikifuatiwa na kuzalisha bidhaa na mwisho kwa umuhimu huo kukusanya mapato. Ni katika mfuatano na umuhimu huo ujenzi wa uchumi wa viwanda shindani utaweza kufikiwa. Kwa maana rahisi shughuli yoyote inayoweza kutengeneza ajira, maslahi ya kukusanya kodi yasitukwamishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga viwanda tubainishe ni viwanda gani tusijihusishe navyo hasa pale penye uwekezaji wa umma ili kuepuka kupoteza rasilimali adimu za wananchi. Pia ni muhimu Serikali kuchangamsha *re-export business* na biashara hapa nchini ili kutengeneza ajira na kukusanya mapato lakini muhimu kulinda viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifanye utafiti ili kujua ni kwa namna gani korosho na pamba izalishwayo nchini inaweze kuongezwa thamani hapa nchini na bidhaa zake kuwa shindani hapa nchini au na kuingia kwenye masoko ya nje na kufanya vizuri. Hoja hapa ni kuzalisha kwa tija na kuingia kwenye masoko mazuri ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ichukue jitihada zaidi kuelimisha wananchi na hasa Wabunge juu ya dhima ya mipango mitatu ya miaka mitano mitano. Hii italeta uelewa wa pamoja hali itakayoongeza kasi ya kutekeleza dira ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wenzangu na Watanzania wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuijalia nchi yetu baraka katika ustawi wa kijamii, kichumi, kisiasa, kidiplomasia mbele ya mataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuapishwa kushika hatamu ya kuliongeza Taifa letu, Mwenyezi Mungu amlinde na kubariki kutuongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini naungana na Watanzania wote kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano katika uongozi wa Mheshimiwa Hayati John Pombe Magufuli, Rais wa Serikali yetu ya Awamu ya Tano, viongozi wake waandamizi, watendaji na wadau mbalimbali kwa jinsi walivyosimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2015/2021 hususan sekta ya viwanda kama mhimili mojawapo uliotufikisha uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kwa namna ya pekee naomba kumwombea Mheshimiwa Hayati John Pombe Magufuli aliyekuwa Rais wa Seikali ya Awamu ya Tano, Mheshimiwa Khatib Said, Mbunge wa Jimbo la Konde, Wahshimiwa Wabunge wenzetu na Watanzania wote waliotangulia mbele ya haki, Mwenyezi Mungu awapokee katika ufalme wake wa mbinguni, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nitoe mchango wangu kupitia mapendekezo ya bajeti ya Wizara hii, kwanza tunaiomba Serikali ifanye tathimini ya viwanda 100 kila Hamashauri zilizoanzishwa na Serikali ya Awamu ya Tano kupitia Wizara ya TAMISEMI, kwani uwepo wa viwanda 100 ulikuwa chachu ya ajira kwa kila Halmashauri, japo kuna haja kubwa ya kuwa na Maafisa Biashara watakaosimamia, kushauri na kuratibu uendeshaji wa viwanda hivi ili kulinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifanye mapitio ya mchakato wa uanzishwaji viwanda na biashara kwa kuondoa vikwazo, urasimu na vigezo ambavyo siyo rafiki katika uanzishwaji wa viwanda hapa nchini kwa kuwa suala la uwekezeji lina ushindani mkubwa sana duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali ijitahidi kupeleka fedha zote zinazoombwa kwenye bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara ili kuleta ufanisi mkubwa katika sekta hii kushikilia uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwe mstari wa mbele kusimamia suala la ubora wa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini kwa ajili ya kulinda afya ya watumiaji na kukidhi ushindani, bei, ubora na soko la ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isimamie suala la kuhamasisha matumizi sahihi ya *blueprint* kama dira katika kuhamasisha wawekezaji hali itakayochochea uanzishwaji wa viwanda kulinda uwepo wa Tanzania kudumu katika kundi la nchi za uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja hoja asilimia mia moja, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa fursa hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Wizara hii ni miongoni mwa Wizara muhimu katika kuendesha uchumi wa nchi yetu.

Pili, natoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuiwasilisha katika Bunge lako Tukufu kwa ufasaha na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia maeneo yafuatayo; kwanza ni kuhusu mazingira ya kibiashara katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa juhudi kubwa inayochukua katika azma yake ya kuelekea kwenye suala la biashara. Ni azma nzuri ambayo itatuvusha katika kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lolote linahitaji matayarisho ya kufanikisha jambo hili. Matayarisho hayo ni kuliwezesha jambo hilo kufanikiwa. Bado katika nchi yetu hatujaweza kufanikisha kutayarisha mazingira bora ya kibiashara. Wafanyabiashara wengi hasa wawekezaji wanapata usumbufu namna ya kupata hudumu hasa ya usajili wa biashara zao. Bado kuna mzunguko wa kupata ruhusa ya kufanya au kuwekeza biashara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali ni kuendelea kwa kasi kubwa kutengeneza mazingira yatakayowavutia wawekezaji wa nje na ndani.

Pili ni kuhusu uhusiano kati ya biashara na kilimo; ni jambo muhimu na ni lazima katika kuleta maendeleo ya kiuchumi katika nchi. Viwanda vyovyote haviwezi kutekeleza malengo yake bila ya kilimo. Kilimo ndio kitakachotoa malighafi ya kuendeleza kiwanda.

Ushauri wangu katika jambo hili kwa Serikali ni kutengeneza mazingira ya kupunguza bei za pembejeo za kilimo ili wakulima waweze kuzalisha mazao ambayo yatapelekwa viwandani kuweza kuendesha viwanda kwa kuzalisha mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mono hoja.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano na ya Sita kwa kazi nzuri katika Mpango wa Pili wa kuimarisha uchumi wa viwanda ambapo viwanda vingi vimejengwa kati ya mwaka 2015 - 2020 vikiwemo viwanda vidogo, vya kati na vikubwa. Tuna imani kwa dhamira ya Rais wetu wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kazi iendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kubwa ataendelea kuweka mkazo mkubwa kwenye ujenzi wa viwanda hasa viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana nchini Tanzania. Tunaunga mkono viwanda kwa sababu vinasaidia kuongeza thamani ya mazao yanayopatikana hapa nchini mfano; pamba, alizeti, katani na kadhalika, lakini pia kuboresha bei ya mazao kwa wakulima, kwani inaondoa gharama za usafirishaji kwenda nje ya nchi ambapo fedha inakwenda kumlipa mkulima, lakini pia ajira za wananchi za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo nina mambo machache ya kuishauri Serikali, Simiyu ni mkoa unaoongoza kwa kilimo cha pamba, kutokana na ubunifu wa viongozi wa Simiyu, wakiongozwa na Mheshimiwa Anthony Mtaka na wasaidizi wake waliweza kubuni na kuishawishi Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, *NHIF, WCF* pamoja na Benki ya Uwezeshaji *(TIB), TBS, TIRDO, TMDA* kuanzishwa kwa kiwanda cha vifaatiba vitokanavyo na pamba; zaidi ya bidhaa 19 vikiwemo taulo za kike. Mkoa na Wilaya ya Bariadi ilitoa eneo lililoko kwenye maeneo yanayofikika na miundombinu ya maji, umeme, mawasiliano na barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliunda kampuni na Bodi ya Wakurugenzi, Serikali iliteua wataalamu waanzilishi wa kiwanda hicho na Serikali iligharamia safari za wataalamu kwenda nje kujifunza teknolojia stahiki kwa ajili ya kiwanda hicho na upembuzi yakinifu ulishafanyika, na gharama zote zilizokwisha kutumika ni shilingi milioni 915.98. Michakato yote ilianza toka mwaka 2016/2017 mpaka sasa hamna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa mkoa wa Simiyu tungependa kufahamu maelezo ya kina kwa nini kiwanda hicho na ujenzi wake haujaanza?

**MWENYEKITI:** Nimkaribishe Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Exaud Kigahe kwa dakika 10 ili aweze ku-*wind up.*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya ya kufanya kazi ya kujadili na kupitisha Bajeti za Wizara mbalimbali hapa Bungeni. Lakini pia kwa namna ya pekee, naomba niwashukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, wewe Mwenyekiti na Wenyeviti wenzako wenza, Wabunge kwa namna ambavyo mnatuongoza katika Bunge hili kwa weledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ya bajeti ya Wizara na Viwanda na Biashara iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Mbunge wa Jimbo la Ubungo ambaye ndiye Waziri wa Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Naomba pia Wabunge wenzangu wote tuunga mkono bajeti hii ambayo imezingatia miongozo mikuu ya Kitaifa hususan Dira ya Taifa, Ilani ya Chama cha Mapinduzi na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea baadhi ya hoja kidogo kulingana na muda. Lakini, hoja nyingine nitamuachia Mheshimiwa Waziri ambaye ndiye mwenye Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niongelee kuhusu ukaguzi wa bidhaa *(destination inspection)* hususan imeongelewa kuhusu magari hasa yaliyotumika. Utakumbuka kuwa ukaguzi huu sio mara ya kwanza sasa kufanyika katika nchi yetu, umeshakuwa unafanyika huku nyuma, lakini kutokana na baadhi ya changamoto ndiyo tulibadilisha baadaye kuanza kuwa na ile *pre-verification of conformity to standards (PVOC)* kwa maana ya kukagua nje bidhaa hizo kabla ya kuingia nchini na hasa magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuona changamoto ambazo tumekuwa tukizipata na Waheshimiwa Wabunge wanajua, kwanza kulikuwa kuna ukosefu mkubwa

sana wa ufanisi katika ukaguzi wa magari yao huko nje. Kwanza tozo iliyokuwa inatozwa kodi zile zilikuwa nyingi, muagizaji alikuwa anatakiwa kulipa takribani dola 150 kwa ajili ya ukaguzi ule. Lakini zaidi ya hapo, usumbufu zaidi anapotuma kule, walikuwa wanatuma hela zaidi ya dola 100 kwa hiyo, unatuma dola 150 ya ukaguzi lakini pia unatuma na dola 100 kwa ajili ya *handling* ya yale makampuni ambayo yanafanya kazi ya ukaguzi kule. Kwa hiyo, unakuta mtu anatuma dola 250 badala ya dola 150. Kwa hiyo, gharama kubwa ya ukaguzi na upimaji ilikuwa ni moja ya changamoto ambazo zilikuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mawakala wengi kutokuwa na ofisi na hivyo kuwa na changamoto kidogo kwenye ukaguzi huo. *TBS* sasa imeanza kukagua magari hapa nchini kuanzia mwezi Machi, 2021 na hakika kazi hii inaenda vizuri na nikutaarifu tu na Bunge lako kwamba kazi ya ukaguzi wa magari yaliyotumika nje unaenda vizuri na baadhi ya changamoto za kawaida ambazo ndizo tunategemea kwa mfano sasa tunapokagua pale baadhi ya magari ambayo hayakidhi viwango yanapewa muda wa kwenda kutengenezwa, halafu yanarudishwa kupata ile *certificate* ya *TRA.* Tumeshapata eneo la UDA pale ambapo magari yale ambayo yanahitaji kutengenezwa yanakaa pale yakishatengenezwa taarifa zile zinarudishwa *TBS, TBS* wanapeleka *TRA* wanapata ile *certificate* ya ukaguzi wanaendelea. Nina uhakika asilimia 80 ya magari yaliyokuja sasa yako vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na utaratibu uliokuwepo sasa hivi ni kwamba *TBS* wanashirikiana na wameshatoa maelekezo kwa kampuni yanayouza magari kule nje kuhakikisha kwamba wanaleta magari yenye ubora. Kwa hiyo, na sisi tunatoa rai kwa waagizaji wote wa magari kutoka nje watumie kampuni ambazo zinafahamika. Wasiagize kwenye kampuni ambazo hazifahamiki kwa sababu zile kampuni zimeshapewa maelekezo ya namna ya ubora ambao tunautaka sisi kama nchi kwenye magari ambayo yanaingizwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili suala la ukaguzi wa magari au bidhaa za kutoka nje, lengo kubwa ni kuhakikisha tunakuwa na bidhaa zenye ubora na hivyo tukishamaliza hili tutajiimarisha tayari zaidi ya shilingi bilioni 60 zimeshatengewa kwa ajili ya kuweka mitambo ambayo itafanya ukaguzi wa magari lakini baadaye kukagua bidhaa nyingine ambazo zinaingizwa kutoka nje. Kwa hiyo, lengo ni kuona kwamba bidhaa nyingi zinakaguliwa sasa nchini ili kuepuka baadhi ya kampuni huko nje kutumia udanganyifu lakini pia na wafanyabiashara wengine kuingiza bidhaa ambazo hazina ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wameongelea kuhusu *Electronic Tax System.* Huu ni mfumo ambao ulianzishwa kwa ajili ya kukusanya kodi kwa njia za kielektroniki. Lengo kubwa la mfumo huu lilikuwa ni kukusanya kodi ya Serikali. Makampuni au wafanyabiashara wengi hasa wenye viwanda walikuwa na *questionable integrity.* Ndiyo maana Serikali ikaona sasa ili kuondoka na tatizo hili la kutokuwa waadilifu kwa wafanyabisahara *integrity* kati ya Serikali na wafanyabiashara ilikuwa chini. Kwa hiyo, tukaanzisha mfumo hu una ufanisi wa mufumo huu umekuwa ni mkubwa ambao kimsingi umdhibiti udanganyifu uliokuwepo unafanywa na wafanyabiashara wasio waaminifu ambao walikuwa hawaripoti taarifa kamili ili waweze kulipa kodi stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo kutokana na mfumo huu yameongezeka, lakini tukubali kwamba katika kufanya kazi yoyote au katika ufanyaji kazi huo kuna changamoto na changamoto kama ambavyo Waheshimiwa wameongelea ni kuhusiana na ile kampuni ambayo inafanya kazi hii kuchukua mapato mengi zaidi kuliko ambavyo Serikali inakusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikutaarifu tu kwamba Serikali sasa inafanyia kazi hili na kwa sababu tulikuwa tumekubaliana, tumeingia mkataba na ile kampuni, kwa hiyo, cha muhimu tunaona namna gani tutakavyofanya ili kuhakikisha baada ya mkataba ule kuisha basi tuweze ku-

*review* ile kampuni, lakini pia ikiwezekana tufanye sisi wenyewe hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala unyaufu wa korosho; niliongelee kidogo hili. Ni kweli kuna changamoto hiyo lakini tumeshakubaliana kwamba sasa tunaenda kufanya utafiti ambao utaangalia namna gani tuweze viwango vya unyaufu katika korosho. Utafiti huo utaongozwa na *TARI* kwa kushirikiana pia na shirika letu la *Tanzania Bureau of Standards,* lakini pia na Bodi ya Korosho na Chuo Kikuu cha Sokoine, lakini pia na wadau wengine kwa maana ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Vyama Vikuu, TAMISEMI lakini pia na waendesha maghala. Kwa hiyo, hilo pia tuanenda kuliangalia ili tuweze kuona namna gani sasa ya kutatua changamoto hii ya unyaufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo pia kuhusu vifaatiba na dawa za binadamu. Limeongelewa kuhusu viwanda vya vifaatiba na dawa; tuna viwanda zaidi ya 14 sasa; kati ya hivyo, viwanda 12 vinatengeza dawa za binadamu lakini viwanda viwili vinatengeneza vifaatiba na vingine viwili vinatengeneza dawa za kinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Kamati ya Kitaifa ambayo inaendelea na upembuzi yakinifu kuhusiana na uanzishwaji wa kiwanda cha vifaatiba katika Mkoa wa Simiyu. Kamati hiyo, iko katika hatua mbalimbali za kuona namna gani ya kuanzisha kiwanda hicho ikiwemo maoni ya hawa Waheshimiwa Wabunge ambayo leo wameyatoa nayo yataingizwa kwenye Kamati hiyo ya Kitaifa ili tuweze kuwa na uhakika sasa wa kuanzisha kiwanda hicho katika Mkoa wa Simiyu. Kusudi ni lile lile kuhakikisha tunatumia malighafi zilizoko nchini kwa maana ya pamba angalau zianze sasa kutumika katika viwanda vyetu vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba tena kuwasihi Waheshimiwa Wabunge kuunga mkono hoja bajeti hii iliyobeba ajenda kubwa ya Kitaifa na hasa ujenzi wa Tanzania ya viwanda. Hakika, kazi hii ni kubwa na sote tuunge mkono ili iweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa nimkaribishe Profesa Kitila Mkumbo, Waziri wa Viwanda na Biashara ili aweze kuhitimisha hoja yake. Karibu na una dakika 20.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge ambazo wamezitoa katika hoja yangu niliyowasilisha asubuhi.

Kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru sana wewe mwenyewe kwa jinsi ambavyo umeweza kuongoza mjadala huu vizuri sana na kuweza kuniongoza pia katika uwasilishaji wangu. Niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri sana katika kuboresha hoja yangu. Lakini kwa nia njema ya kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara.

Nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu vizuri sana baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge ambazo wamezitoa hapa. Tumepokea michango mingi, michango 20 ya kuchangiwa hapa moja kwa moja na michango miwili kwa njia ya maandishi. Niwaahidi tu kwamba...

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge waliochangia kwa maandishi naambiwa wako kumi, niwaahidi Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kauli na kwa maandishi tutajibu hoja zote hizi bila kuacha hoja hata moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, naomba tu kusema kwamba hoja zote ambazo zimetolewa ni za msingi. Zile ambazo ni ushauri, tunazipokea na tutazifanyia kazi zaidi katika kuboresha utendaji wa kazi kama Wizara. Yale ambayo yanahitaji uboreshaji wa kisheria na kimiongozo, tutayafanyia

kazi. Baada ya kusema hayo, naomba uniruhusu nipitie baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, nianze na hoja inayohusu miradi ya makaa ya mawe wa Mchuchuma na chuma cha Liganga. Kama mnavyofahamu, wote tumepitisha Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano hivi karibuni katika Bunge hili hili. Mradi huu ni moja ya miradi 17 ya miradi ya kielelezo ambayo Serikali imepanga kuitekeleza. Ni mradi ambao unaendelea. Ulikuwepo katika Mpango wa Maendeleo uliopita na Waheshimiwa wengi wamehoji kwa nini mradi huu umechelewa. Kwa kweli umechelewa, Serikali haipingi hilo, lakini muhimu ni kujibu hasa kwanini umechelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tukubaliane katika hatua ya utekelezaji ya miradi mikubwa kama hii kuna hatua nyingi, tunafahamu *feasibility study* ya mradi huu ilikamilika mwaka 2012, ni kwa *feasibility study* hii ndiyo tukagundua kwamba tunazo tani milioni 428 za makaa ya mawe katika eneo la Mchuchuma na tunazo tani milioni 126 za chuma katika eneo la Liganga. Hiyo ilikuwa ni hatua ya kwanza ya *feasibility study.* Lakini baadaye, ikaja ikagundulika kwamba pale sio tu kwamba tuna mawe na chuma, tunayo pia madini ya maana sana duniani, madini ya *titanium* na *vanadium.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maandalizi ya mradi pia kama Waheshimiwa Wabunge walivyoeleza, upo ujenzi wa barabara, kilometa 221 pamoja na ujenzi wa reli. Hii nayo ni hatua muhimu. Lakini hatua ya tatu ni kufanya tathmini ya mazingira; athari za mazingira katika utekelezaji wa mradi huo, hili limefanyika. Kwa hiyo, kusema kwamba hakuna kitu ambacho kimefanyika sio sahihi. Yapo mambo ambayo yamefanyika na kwa kweli, zile shughuli za msingi za Serikali imezifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya nne ambayo ni ya msingi ilikuwa ni kutafuta mwekezaji. Mradi huu *investment cost* yake ni zaidi ya dola milioni tatu. Kwa hiyo, ni mradi ambao ilikuwa lazima kutafuta mwekezaji ili kushirikiana na

Serikali kupitia Shirika la *NDC* kuweza kutekeleza. Kwa unyeti wa mradi wenyewe na ukubwa wa mradi wenyewe, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wameeleza, ni mradi muhimu sana kwa maendeleo ya nchi hii. Ni mradi ambao unabeba rasilimali za msingi na muhimu za Taifa. Kwa hiyo, lazima Serikali yoyote duniani na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ingetaka kujiridhisha kuhusu faida ambazo Serikali na nchi hii itazipata sio tu leo. Miaka mingi ijayo, unazungumzia tani milioni 428 za makaa ya mawe na tani milioni 126 za chuma. Unazungumzia uwepo wa madini ya *titanium and vanadium, some of the most precious minerals in the world. (Makofi)*

Kwa hiyo, ni mradi ambao lazima ujiridhishe; mwekezaji akapatikana, tukafanya majadiliano, lakini hatukufikia mwisho kwa sababu mwekezaji alitaka masharti ambayo hayakubaliki kwa nchi, kwa sababu mengi ya masharti yanapingana na sheria zetu, hasa sheria ambazo Waheshimiwa Wabunge tumezipitisha hivi karibuni za mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira hayo ingekuwa ni vigumu Serikali kusema aah, twende tuanze kutekeleza mradi. Bahati nzuri mwekezaji anaelekea kukubali masharti mengi ya Serikali na taarifa ambazo ninazo kutoka kwa *Government Negotiating Team,* bahati mbaya ni kwamba wawekezaji wameshindwa kuja kwa sababu ya mazingira ya sasa ya *pandemic,* lakini mazungumzo yanarudi na masharti mengi anaelekea kukubaliana na akishakubali masharti ya Serikali ambayo tunajiridhisha kwamba ni muhimu kulinda maslahi ya nchi, mradi utaanza kutekelezwa ili mradi uwe na manufaa, sio tu kwa kizazi cha leo sisi hapa, lakini kwa miaka mingi ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, isije pakatokea hapa wakataka kutafuta hili Bunge la Kumi na Mbili waliokuwepo ni akina nani ambao walikwenda kuiuza nchi? Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge Serikali inatambua umuhimu wa mradi huu kama ambavyo nyie mnatambua na Serikali ipo

*committed* kuutekeleza na ndio maana upo katika *documents* zetu zote za ajenda za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo ningetaka kuitolea maelezo ni suala la *blueprint*. Waheshimiwa Wabunge wameongea kwa uchungu kuhusu *blueprint.* Kwanza niwakumbushe, *blueprint* tumeipitisha kama nchi tarehe 01 Julai, 2019, maandalizi yakaanza katika mwaka 2019/2020, mwaka 2020/2021 tukafanya mambo ya kawaida yakiwemo kuondoa baadhi ya tozo, ada na adhabu ambazo zilikuwa zinakwaza biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukatengeneza taasisi za utekelezaji wa *blueprint.* Tukasema tutengeneze *action plan,* tukatengeneza *action plan* imekamilika na *action plan* hii ukiisoma inaanza utekelezaji wake rasmi mwaka 2021/2022 na ndio maana moja ya kitu ambacho tumepata, tumepata *Euro* milioni 11.5 kutoka Jumuiya ya Ulaya kwa ajili ya kutekeleza mradi huu. Na moja ya hatua kubwa sana ni kwamba, tunakwenda kufungua *One Stop Centres* kwenye kila Halmashauri, kwa sababu tathmini inaonesha kwamba, tumefanya mengi katika ngazi ya kitaifa, Serikali Kuu, lakini kwenye *local government* wanaendelea ku-*behave business as usual.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio likaandikwa andiko, tumepata fedha *Euro* milioni 11.5 zaidi ya shilingi bilioni 50, hizi zote zinakwenda kwenye ngazi ya *local government.* Moja ya kazi ya kufanya ni kutengeneza ki-*TIC* kingine kule ambacho kitakuwa na *One Stop Centre* ili mwekezaji akienda apate huduma zote palepale haraka iwezekanavyo, kwa hiyo, ni hatua kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunaendelea na maboresho ya sheria na baadhi ya sheria Waheshimiwa Wabunge mmezipitisha wenyewe hapa ikiwemo *Arbitration Act* ambayo imepita mwaka jana. Hii inakuwa ni moja ya utekelezaji wa *blueprint,* lakini mwaka huu tunafanya marejeo ya sheria kadhaa ambazo zitakuja hapa Bungeni kupitia

*Miscellaneous Amendment* na zingine kama ni sheria za kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumefanya mazungumzo na Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu suala zima la *work permit* ambalo mmelizungumza hapa. Hili nalo tunalifanyia kazi, yale maeneo ambayo yanahitaji mabadiliko ya sheria yanakuja hapa na tumeshaelewana kwamba, kwa kweli ile Sheria ya *Work Permit* lazima tuipitie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala la maagizo ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan aliyatoa hapa na ameyarudia tena juzi, nadhani kwenye moja ya hotuba zake kwamba hizi taasisi nyingi ambazo zinafanya kazi katika nchi yetu, hizi katika ku-*regulate business* lazima zifanyiwe marejeo na alitumia neno ziwe *reviewed,* maana yake lazima tuzipitie na sisi wenyewe katika Wizara yangu tuna taasisi 15 na moja ya kazi ambayo nimeeleza tunaenda kuifanya katika Wizara yetu ni kupitia hizi taasisi kuona kama kuna muingiliano wa majukumu, ili tuweze kuyaweka vizuri.

Kwa hiyo, tunakwenda kufanya mapitio ya taasisi mbalimbali katika nchi hii ambayo tunadhani yanakwaza biashara, ili tuyaweke vizuri. Hili ni agizo ambalo tunalitekeleza halihitaji sheria yoyote kwa sababu tunalifanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumeboresha mifumo ya *electronic.* Mifumo mingi ya *electronic* ambayo tunaiona kwa sasa ndani ya *BRELA* na *TBS* ni matunda ya utekelezaji wa *blueprint.* Mifumo mingi ambayo mnaiona kupitia *TRA* na Wizara ya Fedha na Mipango ni matunda ya utekelezaji wa *blueprint.* Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge inawezekana hatua hazitoshi, lakini sio sahihi sana kusema kwamba hakuna kitu ambacho kimefanyika. Tunafanya mambo mengi, lakini pia, hatupo nyuma ya wakati kwa sababu ndio kwanza *action plan* imekamilika na utekelezaji unakwenda kuanza katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho katika hili, mambo mengi ni *mindset change,* aliongea Mheshimiwa

Mbunge Lucy pale. Mengine hayahitaji sheria, hata mimi ninapozungumza na watendaji wangu na wakuu wa taasisi mbalimbali nawaambia pengine tulikosea kutafsiri, hizi bodi zinaitwa *regulatory authorities* tukatafsiri kwamba ni mamlaka za udhibiti. Sasa udhibiti kiingereza chake ni *control,* ninawaambia hapana, tunapaswa ku-*facilitate* sio kudhibiti. Kwa hiyo, mambo mengi ambayo tunayafanya mengine kwa kweli, ni kubadilisha mtazamo tu mtu akae pale akijua kwamba anakwenda kuwezesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, ndani ya Wizara ya Viwanda na Biashara tumesema tutakwenda kusimamia kitu kinaitwa *service charters.* Taasisi zetu zote zina mikataba ya huduma kwa wateja na mle ndani tumeainisha huduma hii ichukue muda gani, tunakwenda kusimamia kuhakikisha kwamba huduma zinatolewa mapema iwezekanavyo. Muhimu zaidi nasisitiza kwamba ni kubadilisha mtazamo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ni viwanda vilivyobinafsishwa. Waheshimiwa Wabunge viwanda hivi vipo katika maeneo makubwa matatu, vipo viwanda ambavyo vilitelekezwa; kwa nia njema Serikali ilivibinafsosha tukaingia mikataba na wawekezaji wakavichukua, wakavitelekeza. Yamekuwa mapori, wengine wamebadilisha viwanda hivi kuwa sehemu ya kufugia ng'ombe, wameweka mifugo yamekuwa maghala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mikataba na hawa watu na tulisema wataviendeleza viwanda hivi kwa mujibu wa tulivyokubaliana. Tulipofika hapo Serikali isingekaa kimya na wenyewe kule tulipoenda kuzungumzanao wakasema aa aa, kwa kweli tulikosea chukueni viwanda vyenu; tungefanyaje kwa hiyo, hatujapora wamevirudisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kundi la pili wapo wawekezaji ambao tuliona kwamba hawajaishi vile mkataba ulivyotaka. Tukafanyanao mazungumzo, tukakubaliana wakakiri kwamba tulifanya makosa, wamevunja masharti hapa na hapa, wakakubali kujirekebisha. Hawa tunawarudishia viwanda kwa masharti mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wapo ambao wamekubali kwamba kweli tulivunja masharti makubwa na kwa kweli, hatuna uwezo wa kuendelea kufanya hii kazi. Wamevirudisha viwanda 22 hivi ndivyo ambavyo tumevitangaza tunavitafutia wawekezaji wapya na moja ya kipaumbele ambacho tangu niteuliwe nimekipa kikubwa sana ni kusimamia zoezi hili ili viwanda hivi vipate wawekezaji vianze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la mwisho ni viwanda ambavyo kwa kweli tumeshindwa kukubaliana kati ya Serikali na mwekezaji. Yeye anaving'ang'ania anadhani kwamba, yupo sahihi na sisi tunaamini kwamba hayupo sahihi. Sasa nchi hii ni nchi ya utawala wa sheria, katika mazingira hayo tutakwenda kwenye vyombo vya sheria ili tupate haki ama Serikali ama mwekezaji. Hii ndio hatua ambayo tunakwenda nayo katika suala la viwanda ambavyo vimebinafsishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitolee maelezo mafupi kuhusu suala hili la *EPZA* na *SEZ;* Waheshimiwa Wabunge wameongea hapa. Nimeeleza katika hotuba yangu kwamba, moja ya hatua ambayo tunakwenda kufanya, tunakwenda kufanya tathmini ya kina kuhusu mafanikio na changamoto za uwekezaji katika maeneo maalum ya kiuchumi. Hii tathmini itatupa wapi tumefanikiwa, wapi kuna changamoto, nini turekebishe, lakini kwa ujumla wake tathmini ya ndani ambayo tumeifanya uwekezaji katika maeneo haya umekuwa na mafanikio makubwa sana. Mpaka dakika hii tunazungumzia uwekezaji wa dola bilioni 2.5 ni uwekezaji mkubwa, lakini tukifanya tathmini itatupa zaidi tuelekee wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimtoe wasiwasi ndugu yangu Mheshimiwa Getere kuhusu uwekezaji pale Bunda anasema wananchi wake wanakwenda kuwa masikini, hapana. Mwaka huu tumeiagiza *EPZA* inakwenda kujenga *shades* kwenye eneo ambalo tumelitenga lile ili viwanda vianze kujengwa pale. Kwa hiyo, Mheshimiwa Getere hapana, watu wako hawatakuwa masikini, tunakwenda

kuwekeza pale, tutaweka *shades* na eneo lile utafiti wa awali unaonesha kwamba ni eneo *potential* sana, litapata wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwenye hoja hizi nizungumzie kidogo kuhusu mkakati wa *C2C,* mkakati wa nguo na mavazi. Waheshimiwa Wabunge wameongea kwa uchungu. Ni kweli karibu nusu ya nchi hii ni wakulima wa pamba, ni zao muhimu. Haikubaliki kama ulivyosema kwamba tuna-*export* asilimia 30; asilimia 70 ya pamba ambayo tunazalisha hapa. Kumbukeni Waheshimiwa Wabunge mwaka 1992 tulikuwa na viwanda vya nguo 32, lakini mpaka sasa hivi tunazungumza tuna viwanda 12 vya nguo; viwanda nane vya pamba viwanda vingine vilivyobaki vinne vya *polister.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na viwanda hivi katikati viliyumba, laki ni kwa kufuatia mkakati wa *C2C* vingi vimeanza kufanya kazi na juzi nimetoka Morogoro kutembelea baadhi ya viwanda vinafanya kazi vizuri. Muhimu ni kwamba huu mkakati ambao tumeuhuisha, wengi mnafahamu, tumeuhuisha mkakati wetu kwamba sasa unakwenda kutekelezwa kwa miaka mingine kumi, baada ya kuonesha mafanikio makubwa tuna mkakati mwingine mwaka 2021 mpaka mwaka 2031 ili kuhakikisha kwamba viwanda hivi vinasimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini muhimu san ani lile wazo ambalo Mheshimiwa Tabasam amelitoa, ni wazo zuri sana lazima tugawanye. Mchakato wa kutengeneza nguo una hatua karibu sita, lazima tuwe na viwanda vikubwa ambavyo vinapokea kutoka kwenye viwanda vidogo. Tuwe na viwanda ambavyo kazi yao ni ku-*feed* viwanda vikubwa, unaweza ukawa na viwanda vikubwa vitano tu nchi nzima ambavyo kazi yao ni kumalizia mpaka nguo, lakini viwanda vingine vinachakata kuanzia kwenye kuchambua pamba mpaka kutengeneza uzi na uzi ukaenda kwenye viwanda vikubwa. Tupeni nafasi tutekeleze mkakati huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe kwa kweli mkakati huu ni mzuri sana na ni moja ya kipaumbele katika utekelezaji wangu, ukiona kwenye ile hotuba yangu, ni namba mbili. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge niwaombe mnipitishie hii bajeti mapema iwezekanavyo, ili mimi kazi hii nianze mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie; kuna Waheshimiwa wamesema hapa hatutembelei viwanda, tunakaa tu ofisini. Waheshimiwa Wabunge mimi nimeapishwa tarehe 9 Aprili, 2021 kama mwezi mmoja umepita, nimeshatembelea tunavyozungumza tayari viwanda vitano. Cha mwisho nimetembelea juzi kiwanda kikubwa sana cha *21st Century* pale Morogoro cha nguo, kikubwa kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshakutana na wadau mara tano, nikiwa hapa Bungeni ndani ya mwezi mmoja tangu niteuliwe. Kwa hiyo, kutembea ni sehemu yetu, kutembelea viwanda, lazima tutembelee viwanda, tukutane na wadau, tuone changamoto zao, tuone mafanikio yao, Mheshimiwa Naibu Waziri kila siku yupo barabarani. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge hili tunalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la bidhaa la ubora; moja ya taasisi yenye mafanikio makubwa katika nchi hii, na ni vizuri Waheshimiwa tujivunie vitu vyetu, ni *TBS.* wanafanya kazi kubwa sana kudhibiti ubora wa bidhaa zinazozalishwa ndani ya viwanda vyetu, lakini pia vinavyoingia kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana na mimi nimekutana na wafanyabiashara wengine wanalalamika, ukiwauliza nini, unakuta kwamba ana *product* yake ambayo ni *inferior* imekwama *test* ya kawaida ndani ya *TBS,* wana maabara tisa za kisasa kabisa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tusiwe na shaka tunazo taasisi ambazo zinafanya kazi, wanafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea ushauri wenu kwa maana ya kuboresha na ushauri wa Mheshimiwa pale amezungumzia suala la *labeling* kuhusu vyakula, wataliangalia kama kuna upungufu tulirekebishe tuimarishe zaidi, lakini kwa ujumla wake nirudie tena, *TBS* kwa maana ya Shirika letu la Viwango, linafanya kazi nzuri. Ni moja ya mashirika ambayo yanaheshimika sana hapa Barani Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo nimtoe wasiwasi tu Mheshimiwa ambaye alizungumzia kuhusu Zanzibar na Tanzania Bara. Tumeshakaa, tumekutana na ndio maana tumekubaliana kwa mfano kwa *Zanzibar Bureau of Statistics (ZBS)* wamekubaliana na *TBS* wakipima Zanzibar wakakubaliana kwamba, ni kiwango vizuri hapa Tanzania Bara hakuna haja ya kupima tena. Kwa hiyo, limeshawekwa vizuri, tunafanya mazungumzo ya mara kwa mara kati ya sisi na wenzetu Wazanzibari kuhakikisha kwamba hizi kero ndogo ndogo za muungano ziondoke kwa sababu, sisi ni nchi moja, hilo ndio jambo la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge tena waridhie ili bajeti yetu ipite tuanze utekelezaji wa kazi. Ninawasalimu tena kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Toa hoja.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo. Hoja imeungwa mkono.

Katibu, tuendelee.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**MWENYEKITI:** Kamati ya Matumizi

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitabu cha Pili, Matumizi ya Kawaida. Fungu 44 – Wizara ya Viwanda na Biashara. Inapatikana Ukurasa wa 285.

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 44 – WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management......*Sh. 13,831,730,400

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa nimeletewa majina hapa ya kutoka vyama. Kuna Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Neema Mwandabila na Mheshimiwa Ahmed Salim ambao wamekusudia kushika shilingi. Kwa hiyo, nitaanza na Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nitangulize kabisa kusema nisiporidhika na majibu ya Waziri nitashika shilingi. Kwanza ni-*declare* mimi natoka Mkoa ambao unalima pamba, Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao hili limekuwa na changamoto kubwa mbali ya mbegu, mbali ya bei, mbali ya soko la ndani na nje. Sasa tulikuwa na tuna viwanda kadhaa na Mheshimiwa Waziri wewe umejibu vya kuchakata, ni *process.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukienda tu Bunda tuna *ginnery* tano, unakuta inayofanya kazi ni moja. Nenda Nyamibiti - Sumve, *ginnery* imekufa, nenda Manonga - Igunga *ginnery* imekufa, nenda Manawa *ginnery* imekufa kule Misungwi, nenda Kamsama - Sengerema kwa Mheshimiwa Tabasam imekufa, nenda *Chato ginnery,* nenda Kiwanda cha *Taboratex,* nenda *Mutex* Musoma. Sasa hivi vyote vilikuwa vinafanya kazi, lakini leo hii havifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vingekuwa vinafanya kazi leo hii wakulima wa Kanda ya Ziwa na maeneo mengine wangekuwa na uhakika wa soko la ndani. Sasa huyu mkulima wa pamba apate changamoto kwenye mbegu, apate changamoto kwenye bei, apate changamoto tena kwenye soko ambalo mwanzoni alikuwa ana uhakika akimaliza kulima pamba yake ataipeleka wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini Serikali msiamue kuvifufua viwanda hivi kwa kutoa mitaji ya kutosha, aidha kupitia Benki ya *TIB* au kupitia Benki ya Kilimo?

Ninahitaji maelezo ya kina na nisiporidhika nitashika shilingi na nitawaomba Wabunge wenzangu waniunge mkono zao la pamba likiwekewa mkakati lina mchango mkubwa sana katika pato la Taifa letu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja anayoisema Mheshimiwa Ester ni hoja *valid* na Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Kilimo pamoja na Tanzania *Agricultural Development Bank,* mwaka jana tumefanya *survey* ya kuzi-*evaluate* hizo *ginnery* alizozitaja nyingi ziko chini ya ushirika. *Ginnery* ya Manawa sasa hivi

tunavyoongea tumesha-*commision supplier* wa awali aliyeleta teknolojia kwa ajili ya kufanya *assessment* na kuweza kuangalia namna gani tunaweza kui-*revive* lakini ameitaja *ginnery* ya Chato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ginnery* ya Chato mwaka jana tumeipatia fedha za shilingi bilioni tatu imenunua pamba zote na wamelipa mkopo na wame-*make profit* ya *over four hundred million shillings* kama Chama cha Ushirika. *(Makofi)*

Tumeifufua *ginnery* ya Kaku ya Kahama tumeifanyia *pilot* na sasa hivi *ginnery* ambazo ziko chini ya Chama Kikuu cha Ushirika cha Nyanza zinafanyiwa *incomprehensive study* na tunashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu tukishirikiana na Mifuko ya Hifadhi na *Tanzania Agricultural Development Bank* kuangalia namna gani tunaweza kuzifanya hizi *ginnery. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge *ginnery* nyingi zimekufa kwa sababu ya *management,* kwa hiyo, hatuwezi kupeleka fedha sehemu ambayo hakuna *commercial mind* wala hakuna uongozi mzuri. Tumefanya *pilot* na tumeona mafanikio na mwaka huu tunaongeza inaingia *ginnery* mpya ya *MDCU,* ambacho kupitia Chama cha Ushirika cha Mbogwe na wenyewe wataenda kununua pamba na tutawapatia mtaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Ester asishike shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwenye *issue* ya *ginnery tuna-resolve,* tuwahakikishie wakazi wa Mara na Mbunge wa Bunda Vijijini amekuwa *very aggressive* kuhusu *ginnery* zake na yeye zilizoko kwake. Mheshimiwa Tabasam ameongelea kuhusu *ginnery* za Sengerema, zote hizi ziko kwenye *map* ya kuzihakikisha zinarudi barabarani lakini tutazirudisha zikiwa na uongozi sahihi, kwa sababu tunazipelekea mitaji zifanye biashara kama wanavyofanya biashara wengine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya umeridhika na maelezo ya Naibu Waziri wa Kilimo?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tulijadili, Mheshimiwa Waziri atoe majibu ya kutosha ili wakulima wa pamba wawe na uhakika wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja na Wabunge wenzangu waniunge mkono.

**MWENYEKITI:** Wabunge hawajatimia kumi hawa, hawajatimia Mheshimiwa Ester Bulaya tunaendelea.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wametimia.

**MWENYEKITI:** Hawajatimia.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hesabu.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetimia tupo kumi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hawajatimia jamani naomba tuendelee.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetimia, tumetimia.

**MWENYEKITI:** Katibu tuendelee, tumeshamaliza hilo, limekwisha.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe.

**MWENYEKITI:** Hapana wewe ni mtoa hoja unatakiwa uungwe mkono na Wabunge kumi kwa hiyo, hiyo imeshapita hiyo.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo kumi.

**MWENYEKITI:** Hapana.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahaaaa! Tupo kumi, moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi.

**MWENYEKITI:** Wakati nilipohoji hamkutimia tisa na yeye mtoa hoja hawezi kuhesabika, tunaomba tuendelee. *(Makofi)*

Tunaendelea na mwingine Mheshimiwa Neema Mwandabila. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, acheni uonevu. *(Kicheko)*

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante mimi ningependa kupata ufafanuzi. Ooh *my God.*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sema sema sema!! Endelea.

**MWENYEKITI:** Naomba utulivu jamani nimeshazungumza hilo tumeshalimaliza tunaendelea na kazi nyingine.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wameshafukuzwa hao kwenye chama chao.

**MWENYEKITI:** Tafadhali ninaomba, Mheshimiwa Neema endelea.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuhoji baadhi ya mambo kwa Wizara hii ambayo Kitaifa tunategemea ndio Wizara ya msingi ya kuweza kututoa hapa tulipo kuweza kupata Tanzania yenye uchumi ambao ni mzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imekuwa inakuja na mipango mbalimbali na sera mbalimbali, wamekuwa wakitekeleza sera ya viwanda endelevu. Lakini kwa ufuatiliaji ambao umekuwepo tumekuwa tunaona viwanda vingi vinaanzishwa, lakini viwanda vingi pia vinakufa, na katika kufa kwa viwanda hivi hatujapata taarifa kamili ambayo inaonesha ni kitu gani ambacho kinafanya viwanda vya Tanzania badala ya kuendelea vife.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baadhi ya mambo ambayo yanapelekea viwanda kufa Tanzania ni pamoja na mlolongo wa kodi katika kuanzia kwa malighafi, lakini pamoja na kwa vipuri vinavyoingizwa lakini pamoja na kwa bidhaa zinazokuwa zimeanzishwa, kitu ambacho kinafanya zile bidhaa za Tanzania ziwe za gharama ya juu kuliko gharama ambazo zinakuwa zinaingizwa Tanzania na mwisho wa siku unakuta viwanda hivi vinakufa watu wamewekeza fedha nyingi kama ni Serikali iliweka fedha nyingi ambayo ni ya Watanzania inakuwa haija-*mature.* Lakini pia hata kama ni Mtanzania huyu anakuwa amepoteza fedha zake nyingi kwa kuanzisha kiwanda ambacho mwisho wa siku kinakufa na anafilisika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia hizi fedha zote zinazokuwa zinalala chini, mwisho wa siku Taifa linakuwa linaendelea kudumaa. Kwa mfano mchache tu wa viwanda ambavyo vimeweza kufa tunaweza tukaona mfano *STAMICO* kwetu kule Songwe, Ileje, makaa ya mawe yapo lakini shirika halifanyi kazi vizuri. Tunaona kuna Mbeya *Textile* ilishakufa kitambo lakini majengo yapo na ni mazuri ambayo yanahitaji kuendelezwa, lakini tunaona Kiwanda cha *Hill Soap* kilishakufa lakini kuna kiwanda cha...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba uzungumzie hoja yako mahsusi.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni nini kauli ya Serikali katika kuokoa fedha za Watanzania ambazo zinakuwa zinalala katika viwanda hivi badala ya kuendelezwa fedha inakuwa imekaa

pale, mfano mzuri upo Liganga fedha nyingi zinakaa pale mambo hayafanyiki kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Ahsante, umeeleweka naomba Mheshimiwa Waziri utoe ufafanuzi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya awali, ni kweli vipo viwanda ambavyo vilifanya kazi baadaye vikafa na sababu za kufa ni mbalimbali ikiwepo suala la menejimenti. Lakini pia ni muhimu Waheshimiwa Wabunge tukasisitiza kwamba vipo viwanda vingi ambavyo vinafanya kazi nzuri, lakini hoja msingi aliyoitoa ya msingi ni kwamba tunafanya nini? Serikali tunachukua hatua nyingi za kuhakikisha kwamba viwanda vinafanya kazi kwa mfano, kupitia *Finance Act, 2019* hapa Bungeni tulipitisha kodi hapa ya kudhibiti uingizaji wa vitenge kutoka nje ili kulinda viwanda vyetu vya kutengeneza vitenge hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na natua hiyo imesaidia sana na ndio maana unaona kwamba kuna baadhi ya viwanda sasa ambavyo vilikuwa vimeshachoka sasa vimefufuka na vinafanya kazi.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tutaendelea kuchukua hatua zozote zile ambazo ni za muhimu, kuhakikisha kwamba viwanda vinafanya kazi. Zile hatua ambazo zipo ndani ya Serikali kwa mfano, kodi Bunge ndio mahali sahihi tunatoa ushauri Serikali inachukua hatua. Kwa upande wetu tunahakikisha kwamba tunapata wawekezaji ambao wana uwezo, ili waweze kuviendesha viwanda hivi vizuri. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, mimi niweze kusema bado siioni *commitment* ya Serikali katika suala hili. Kwa sababu tunapoongelea maendeleo ya Taifa kwanza niseme nachukua shilingi ili tuweze kuijadili hii hoja kama Taifa kwa

sababu haiwezekaniki Serikali inaweka fedha nyingi, watu wanaweka fedha nyingi chini, lakini ile dhamira kabisa ya ku-*stabilize* soko, dhamira ya kuona bidhaa za humu zinakuwa zinauzika haipo, kiasi kwamba ukisema unatoa bidhaa yako leo hapa Tanzania uende ukauze Kenya unakuta vitu vya Kenya ni bei rahisi.

Sasa ni nini kauli ya Serikali kuhakikisha bidhaa zetu zinaweza ku-*compete* katika soko la nje? Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi wa ziada.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda Mheshimiwa angetupa mfano kwaababu, akisema bidhaa za Tanzania haziuziki! Bidhaa za Tanzania zinauzika. Changamoto ambayo tunayo kwa mfano kwa upande wa viwanda, ni baadhi ya viwanda kukosa *raw materials* kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema hapa vinafanya kazi miezi mitatu vikaishiwa, lakini bidhaa ambazo zinazalishwa zinauzwa labda kama angetupa mfano ni bidhaa gani ambayo imezalishwa haina mauzo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema umemuelewa Profesa?

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme ninamuelewa sana na mfano wa bidhaa ambazo hauwezi ukaiuza nje mfano, ni sukari, sukari sehemu zingine unakuta...

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bei rahisi hapa haiuziki, lakini nguo ya Tanzania zinagharama kubwa kuliko nguo zinazokuwa zimeingizwa Tanzania.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema kama haujaridhika ungetoa hoja tu, kwa sababu umeshazungumza mara mbili na hujatoa hoja mara ya kwanza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme natoa hoja.

**MWENYEKITI:** Umeshapitwa na muda.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *okey* sawa nashukuru ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante tunaendelea na Mheshimiwa Salum Ahmed.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi taarifa unampa nani sasa?

**MHE. RASHID A. SHANGAZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupa wewe hapo.

**MWENYEKITI:** Ahaaa! Utanipaje mimi taarifa. Mheshimiwa Ahmed naomba uendelee unanipa taarifa ipi? *(Kicheko)*

**MHE. RASHID A. SHANGAZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, jina tuliloleta ni la Cosato Chumi sio la Ahmed Salum.

**MWENYEKITI:** Basi hiyo sio taarifa yaani ungetoa tu maelezo.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maelezo hayo ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya ninamuomba Mheshimiwa Cosato Chumi. *(Kicheko)*

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa maelezo na kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza vizuri sana Mheshimiwa Waziri hususan suala zima la mpango wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa biashara hii *blueprint.* Lakini tumewasikiliza Wabunge wengi pamoja na maelezo ya Waziri, kesi yetu ya kutoka hiyo nafasi ya 141 kwenda kwenye *digit* mbili bado ni ndogo kwa maana hiyo *blueprint* bado haijaweza kuwa *operation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndio maana pamoja na hatua ambazo Mheshimiwa Waziri umezieleza hatuendi kwa kasi ambayo tunatarajia, maana kama mwekezaji anaangalia Tanzania ya141, anaangalia Kenya ya 56, Rwanda ya 38; kwa vyovyote hiyo dhana ya uchumi wa viwanda hatuwezi tukai-*achieve.* Kwa hiyo, pamoja na maelezo hayo uliyosema yapo mambo ni ya kikanuni tu. Kwa hiyo mimi ninataka maelezo na kama sitaridhika nitashika shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Profesa.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo Mheshimiwa Cosato Chumi analiongea ni la msingi, taarifa hii ambayo anairejea ambayo ina vigezo 11 ambavyo tunapimwa na Benki ya Dunia, kupitia mpango wake wa *easy of doing business.*

Ni kweli kwamba sasa tupo 141, lakini Waheshimiwa Wabunge msisahau kwamba kabla ya hapo ripoti ya mwaka 2019 tulikuwa 144; kwa hiyo, tumepiga hatua kidogo, lakini tumepiga hatua. Lakini ripoti ambayo tunaizungumza hii, *data* zake ni za mwaka 2019, zikaja kupatikana taarifa mwaka 2020; kwa hiyo, sisi tunaamini kwa hatua ambazo tumezifanya zingine zilikuwa zinafanyika wakati wanachukua hizi *data.* Kwa hatua ambazo tumezifanya ripoti ya mwaka huu tunaamini tutakuwa tumepiga hatua zaidi, lakini tumeweka utaratibu mzuri ndani ya Serikali kwa kushirikiana na sekta ambazo zinahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka mkakati kwamba tusogee twende angalau kwenye *double digit* na ni moja ya mambo ambayo *nimeya-present* kwenye bajeti yangu. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Cosato Chumi, aniachie hii shilingi, nipate mshahara ili tukafanye hii kazi tusogee, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anasema kwamba baada ya mwaka mmoja tumeenda nafasi tatu, itatuchukua miaka 15 kuingia kwenye hizo *digit* mbili, kwa hiyo, mimi ninaomba kutoa hoja tujadili jambo hili ili kuonesha kwamba sisi kama Wabunge tupo *serious* kiasi gani katika masuala mazima ya kuelekea uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Haya, hoja imeungwa mkono. Wangapi wanataka kuchangia labda watatu niwape tu, Mheshimiwa Lucy, Mheshimiwa Salum na Mheshimiwa Mwambe.

**MBUNGE FULANI:** Una pendelea.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, maneno ya upendeleo hayapo, wakati anatoa hoja mtu wenu mlikuwa watu tisa tu, mtoa hoja hahusiki Kanuni ya 63 inaeleza wazi. Mheshimiwa Lucy.

**MHE. LUCY T. MAYENGA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mimi ninaomba kuunga mkono hoja hii kwasababu, hali ya mazingira ya biashara na ufanyaji biashara, changamoto zilizokuwepo na ambazo zimekuwepo kwa muda mrefu zilikuwa zinajulikana na zinajulikana. Hatua hii ya kuingia 141 kutoka 144 mimi nina wasiwasi kwa sababu nikupe mfano mmoja, Tanzania tunatumia shilingi bilioni 16 kuagiza magunia ya kuwekea korosho. Magunia ya kuwekea

korosho *item* moja tu lakini kuna watu ambao wamejaribu kufungua viwanda hapa Tanzania. Kiwanda cha kutengeneza gunia hapa Tanzania bei ya gunia ni kubwa kuliko zile gunia ambazo zinatoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile mazingira ya biashara ile ya kumgusa mtu mmoja mmoja kwa mfano, nchi ya China wanasema kwamba mtu ambaye anakiwanda cha kutengeneza *item* fulani kazi yake ni kutengeneza tu, anayekuja kununua naye anakuwa kazi yake ni kuuza mwisho vinakwenda kwa mlaji. Tanzania hapa mtu anakuja tunamkaribisha mwekezaji anafungua kiwanda cha kutengeneza *item* fulani, yeye mwenyewe anafungua duka Kariakoo, Mtanzania anafaidika vipi kwenye vitu kama hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana tunalalamika fedha haionekani, nilikuwa ninaomba Serikali kama hivi Mheshimiwa Waziri, ninaimani naye sana, ninajua uwezo wake kwenye hili asimame mguu sawa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy naomba utoe hoja, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sio wamalize.

**MWENYEKITI:** Ahaa! Bado wawili haya wapili, nimemtaja achangie wa pili Mheshimiwa Salum, halafu Mheshimiwa Mwambe amalizie.

**MHE. AHMED A. SALUM**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana mimi naunga hoja mkono ya ndugu yangu Cosato na nia hapa ni njema tu kuboresha, ili Mheshimiwa Waziri aweze kufanya kazi yake vizuri wala hatuna nia mbaya kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitizama katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 12 na 13, katika hizi tozo 232 alizozitoa ni sahihi kabisa, lakini ungeenda zaidi kwasababu,

hoja kubwa ya *blueprint* ni mambo mawili tu, kwenye *blueprint* yenyewe, ni kwamba kufanyia marekebisho sheria na kanuni katika mamlaka za udhibiti zinazoingiliana na kukinzana kupitia Wizara mbalimbali, hiyo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini namba mbili ni muingiliano wa majukumu baina ya Taasisi na na Wizara mbalimbali katika *blueprint* mambo mawili makubwa tu haya. Sasa Mheshimiwa Waziri leo ni miaka minne hii *blueprint* imeanza wewe hujawa Mbunge wala Waziri umeikuta na mwekezaji anapotoka nje hawezi akasubiri tu, tunasubiri mwaka wa kwanza unaenda, mwaka wa pili, mwaka wa tatu, mwaka wa nne tunahitaji wawekezaji wa ndani na nje haraka iwekekanavyo.

Sasa katika hotuba yako Mheshimiwa Waziri, hujatuonesha jedwali kwamba ni kanuni zipi ambazo umezirekebisha, ni kanuni zipi ambazo unakwenda kuzifanyika haraka iwezekanavyo na unatupa *time frame* kwamba lini natarajia kuleta marekebisho haya, ili Serikali iweze kuwa katika hatua bora, katika *rank* bora ya dunia katika uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Rwanda leo ya 38 kweli Rwanda juzi tu walikuwa na vita hapa leo wanatupita! Tumewafundisha wao kazi, tumewarekebisha wao na Wizara, eti wao leo wamekuwa wa 38 sisi tumekuwa wa 141.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ahmed, tunaendelea na Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nisaidie na mimi kidogo kwenye hili suala, mwishoni tutasikia Mheshimiwa Cosato anasema nini.

Kimsingi mazingira ya biashara Tanzania sio mazuri kwenye hili jambo na ndio maana kukaja na *blueprint,* kumekuwa na misukosuko mingi *and business is not easy in Tanzania.* Sasa sisi kama nchi tusione aibu wakati fulani kujifunza kwa majirani zetu, kwa nini tusiende ku-*copy* kule

walikofanikiwa hizo *models* zao tukazileta Tanzania kama majaribio lakini twende mbele kwa sababu, wawekezaji hawatusubiri kama ambavyo hapa wamesema na utakumbuka hotuba ya Mheshimiwa Rais ameongelea kuhusu suala la urasimu ulioko *TIC,* lakini urasimu pia ulioko Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na taasisi mbalimbali zilizoko huko ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Waziri tulizoea kusikia haya maneno kwa sababu hili jambo ni kubwa, tulizoea kusikia maneno ya mchakato, upembuzi yakinifu, utaratibu, miundombinu, mikakati, kwenye Wizara zile ambazo hazigusi mambo moja kwa moja. Sasa wawekezaji wanakuja wakiwa na fedha zao na mabenki yamewaahidi kwamba tutawapa fedha za kwenda kuwekeza Tanzania.

Ni lini, ndilo jambo unaloulizwa hapa *implementation* ya *blueprint* itaanza? Mimi nimekuwa Mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara na sasa hivi ni mara ya pili nimesikia hilo neno wakati wa Mheshimiwa Mwijage, nimesikia hilo neno, wakati ule Mheshimiwa Waziri mwingine na sasa hivi umekuja wewe Waziri Kitila. Unasifiwa hapa kwa utendaji wako wa kazi mzuri na ni Profesa, tunaamini wewe ni muarobaini, sasa simama tuambie *blueprint* itaanza kufanya kazi lini kwenye mazingira ya biashara ya Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo tu hapa waliuliza kuhusu suala la unyaufu wa korosho na baada ya miezi miwili kutakuwa na utaratibu wa biashara ya korosho unaendelea. Mheshimiwa Waziri anasema kuna unyaufu tunakwenda sasa kufanya mijadala ili muone namna ya kutatua hili jambo.

Sasa tuelezeni kinagaubaga Watanzania na wawekezaji wanataka kufahamu tarehe ngapi mtaanza kufanya kazi na *blueprint* kwa uhakika ili kila mtu ajue nini anatakiwa kufanya kwenye mazingira ya biashara Tanzania? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kujibu hoja za Waheshimiwa watatu, moja ni ya Mheshimiwa Lucy kuhusu mazingira ya biashara na ameniasa nisimame imara na ninamuahidi kwamba nitasimama imara sana kuhakikisha kwamba haya mambo ambayo anayasema...

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Ngoja Mheshimiwa amalize, halafu utaratibu baadaye. Mheshimiwa naomba uendelee.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa hiyo nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba yale maoni ambayo ameyatoa nitasimama imara kuhakikisha kwamba mazingira ya biashara yanaendelea kuboreka hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ahmed Salum ameuliza kuhusu hatua ambazo tunazichukua kama ambavyo nimeleeza. Labda nitoe mfano mmoja kwa mfano mwaka huu tumepanga ndani ya Bunge hili tulete Sheria Mpya ya Uwekezaji *(Investment Act)* tunaleta hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa upande wa Mheshimiwa Cecil Mwambe nimwambie tu kwamba kama nilivyosema kwenye *action plan* ya mwaka huu imepangwa kwamba *action plan* hiyo ianze kutekelezwa tarehe 1 Julai, 2021 maana yake mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo moja la mwisho tafiti zinaonesha kwamba kuna vigezo vingi vya kuvutia uwekezaji na kuboresha mazingira ya biashara karibu 10; lakini kigezo namba moja duniani kote ni mazingira mazuri ya kisiasa. Namba mbili utashi wa kisiasa, nadhani kama kuna kipindi tumepata *the highest level of political commitment* ni kipindi hiki. Mheshimiwa Rais ameshatoa *commitment* ya juu sana kuhusu kuboresha mazingira.

Naombeni mumpe nafasi mtupe nafsi wasaidizi wake tusimamie naamini Mheshimiwa Cosato Chumi kwenye kipindi kijacho cha bajeti kama hii hali yetu ya *easy of doing business* itakuwa ni bora zaidi kuliko ilivyo sasa. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cosato hitimisha hoja yako.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhitimisha hoja yangu kwanza nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao walisimama kuniunga mkono hoja yangu na waliochangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumza hapa katika *East Africa* sisi tumewazidi Burundi na *South Sudan* tu, katika *SADC* tumewazidi Angola, hata Zimbabwe wenye matatizo ya *political* hiyo anayosema Mheshimiwa Waziri wametuzidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa kauli aliyomalizia Mheshimiwa Waziri akiwa kama Rais wangu wa *DARUSO* nikiwa *first year* kwamba kuna *high level* ya *political commitment* kutoka kwa Mheshimiwa Rais, ninarejesha shilingi lakini nikimpa tahadhari kwamba hiyo *political commitment* bila watendaji kuchangamka *is going to be nothing. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurejesha shilingi. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit* … …Sh. 477,616,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit* … … Sh. 1,134,064,000
Kifungu 1004 - *Government Communication* … Sh. 155,588,000
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit* … … … … … Sh. 164,552,000
Kifungu 1006 - *Legal Service Unit* … … … … … Sh. 255,592,000

Kifungu 1007 - *Management Information System* ........................................ Sh. 347,708,000
Kifungu 1008 - *Procurement management Unit* ...............................................Sh. 270,557,000
Kifungu 2001 - *Industry* ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 6,241,254,600
Kifungu 2002 – *Small and Medium Enterprises Division* ......................................Sh. 5,462,085,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

**FUNGU 60 – BIASHARA NA UWEKEZAJI**

Kifungu 3001 – *Commerce Division* ... ... ... ... Sh. 1,360,618,000
Kifungu 4002 – *Commodity Market Development Division*...................................Sh. 22,911,008,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MATUMIZI YA MAENDELEO**

**FUNGU 44 – WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.......Sh. 1,450,000,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit* ... ... Sh. 32,099,472,137
Kifungu 2001 – *Industry* ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 16,438,413,863
Kifungu 2002 – *Small and Medium Enterprises Division* .....................................Sh. 3,100,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yaje.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Namkaribisha mtoa hoja sasa aweze kutoa taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwamba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2021/2022 – Wizara ya Viwanda na Biashara yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, baada ya kuhoji na kwamba bajeti hii imepitishwa na Bunge hili nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Profesa Kitila Mkumbo na Naibu Waziri wake na timu yenu yote kwa kuweza kutengeneza bajeti nzuri ambayo naamini Wabunge wameridhika nayo na ninaamini kwamba yale ambayo mmekusudia na mmedhamiria yatakwenda kufanyiwa kazi vizuri.

Lakini niwapongeze sana Profesa pamoja na timu yako kwa kuvipa kipaumbele katika vipaumbele vyako kilimo,

ufugaji na uvuvi ambavyo hivyo ndiyo vyenye malighafi nyingi Tanzania hii na ninaamini sasa wenzetu wa Wizara ya Kilimo kama na wao wataweza kuweka mazingira rafiki kwenye uwekezaji kwenye maeneo hayo ya kilimo, uvuvi na ufugaji basi nafikiri viwanda ambavyo tumekusudia kuviboresha, kuvianzisha na vingine vilivyokufa kuvifufua tutaweza. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo niwatakie kila la kheri katika utekelezaji wa bajeti hii ninaamini kwamba Mwenyezi Mungu atawasimamia ili muweze kufanikisha yale ambayo tumefikiria na kuamua kwamba tutayafanya. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo niwapongeze pia Wabunge wote waliotoa mchango naamini Serikali itaweza kuchukua yale muhimu yote na kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile shughuli zetu zimemalizikia hapo basi ninaomba niahirishe sasa shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu, tarehe 24 Mei, 2021 saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 7.50 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 24 Mei, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*